TESSA
Teacher Education in Sub-Saharan Africa

The Open University

Rasilimali za Msingi

# Kujua kusoma na kuandika




**Kusoma na Kuandika kwa madhumuni mbalimbali**
**Kutumia Sauti za Kijumuia Darasani Kwako**
**Uhamasishaji wa mawasiliano katika lugha ya ziada**

Rasilimali za Msingi

# Kujua kusoma na kuandika

Nyenzo za TESSA zimeundwa na kuendelezwa na wataalamu wanaofanya kazi nchi mbalimbali za Kiafrika. Zimetolewa kwa kupitia leseni bunifu ya pamoja na zinaweza kutumika na kurekebishwa kwa mahitaji yako ipasavyo, kuendana na hali halisi kama inavyohitajika.

## Yaliyomo


Namba ya moduli 1 **Kusoma na Kuandika kwa madhumuni mbalimbali**

- Sehemu ya 1 Kuhamasisha na kutathmini usomaji na uandishi
- Sehemu ya 2 Kuchochea hamasa katika usomaji wa hadithi
- Sehemu ya 3 Njia za Usomaji na upokeaji wa taarifa za matini
- Sehemu ya 4 Njia za kuwasilisha mtazamo wako
- Sehemu ya 5 Njia za kuwa msomaji na mwandishi makinifu

Namba ya moduli 2 **Kutumia Sauti za Kijumuia Darasani Kwako**

- Sehemu ya 1 Kuchunguza hadithi
- Sehemu ya 2 Njia za kukusanya na kutenda hadithi
- Sehemu ya 3 Kutumia michezo ya jadi katika kujifunza
- Sehemu ya 4 Utumizi wa hadithi na ushairi
- Sehemu ya 5 Kubadilisha hadithi simulizi, mashairi na michezo kuwa vitabu

Namba ya moduli 3 **Uhamasishaji wa mawasiliano katika lugha ya ziada**

- Sehemu ya 1 Kuandaa mazingira asilia kwa ajili ya mazoezi ya lugha
- Sehemu ya 2 Njia zijengazo ufasaha na usahihi
- Sehemu ya 3 Kuunda Fursa za Mawasiliano
- Sehemu ya 4 Namna ya kujenga juu ya ujuzi wa lugha ya nyumbani
- Sehemu ya 5 Kusaidia ujifunzaji wa lugha ya ziada

Rasilimali za Msingi

# Kujua kusoma na kuandika

## **Namba ya moduli 1** Kusoma na Kuandika kwa madhumuni mbalimbali

**Sehemu ya 1** Kuhamasisha na kutathmini usomaji  na uandishi

**Sehemu ya 2** Kuchochea hamasa katika usomaji  wa hadithi

**Sehemu ya 3** Njia za Usomaji na upokeaji wa taarifa  za matini

**Sehemu ya 4** Njia za kuwasilisha mtazamo wako

**Sehemu ya 5** Njia za kuwa msomaji na mwandishi makinifu

**KISWAHILI**

*TESSA (Teacher Education in Sub-Saharan Africa) inalenga kuboresha utekelezaji darasani wa walimu wa msingi na walimu wa sayansi wa sekondari barani Afrika kupitia matoleo ya Rasilimali Huria za Elimu (OERs) ili kuunga mkono walimu kuunda njia zinazowalenga wanafunzi na kuwashirikisha. OER ya TESSA huwapa walimu kitabu cha kurejea pamoja na vitabu vya shule. Zinatoa shughuli kwa walimu kujaribu madarasani pamoja na wanafunzi wao, pamoja na masomo ya utafiti inayoonyesha jinsi walimu wengine wamefunza mada hiyo, na rasilimali husishi za kuwaunga mkono walimu katika kukuza mipango ya masomo yao na ufahamu wa somo.*

OER ya TESSA imeandikwa kwa ushirikiano wa waandishi wafrika pamoja na wa kimataifa *ili kushughulikia mtalaa na muktadha. Zinapatikana kwa matumizi ya mtandaoni na chapa (*http://www.tessafrica.net*). OER Msingi zinapatikana katika matoleona lugha kadhaa (Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili). Mara ya kwanza, OER ilitolewa kwa Kiingereza na kupatikana Afrika nzima. OER hizi zimebadilishwa na washirika wa TESSA ili kufaa Ghana, Nijeria, Zambia, Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania na Afrika Kusini, na kutafsiriwa na washirika nchini Sudani (Kiarabu), togo (Kifaransa) na Tanzania (Kiswahili) OER ya Sayansi ya Sekondari zinapatikana kwa Kiingereza na zimebadilishwa ili kufaa Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania. Tunakaribisha maoni kutoka kwa wale wanaosoma na kutumia rasilimali hizi. Leseni ya uundaji wa ubunifu huwawezesha watumiaji kuchukua na kujanibisha OER zaidi ili kutimiza mahitaji na muktadha wa kindani.*

*TESSA inaongozwa na Open University, Uingereza, na inafadhiliwa kwa sasa na ruzuku za ufadhili kutoka kwa Wakfu wa Allan and Nesta Ferguson, Wakfu wa William and Flora Hewlett na Open University Alumni. Orodha kamili ya wafadhili inapatikana kwenye tovuti ya TESSA (*http://www.tessafrica.net*).*

*Pamoja na rasilimali kuu za mafundisho za kuunga mkono mafunzo katika masomo maalum, ni chaguo za rasilimali za ziada ikiwa ni pamoja na sauti, rasilimali kuu ambazo zinafafanua utendakazi, vitabu na zana maalum.*

**TESSA Programme**
**The Open University**
**Walton Hall**
**Milton Keynes, MK7 6AA**
**United Kingdom**

**tessa@open.ac.uk**

Copyright © 2017 The Open University
Except for third party materials and otherwise stated, this content is made available under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 licence: http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/. Every effort has been made to contact copyright holders. We will be pleased to include any necessary acknowledgement at the first opportunity.

***TESSA_SwPA_LIT_M1 August 2017***

*This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 License*

# Contents

Sehemu ya 1: Kuhamasisha na kutathmini usomaji na uandishi 5
Somo la 1 5
Somo la 2 7
Somo la 3 8
Nyenzo-rejea ya 1: Kitu ambacho waandishi na wasomaji wafanisi wanatakiwa kukijua 10
Msimbo wa maandishi 10
Nyenzo-rejea ya 2: Mifano ya nyimbo na mashairi 11
Nyenzo-rejea ya 3: Maswali ya mfano ya kuuliza kuhusu bidhaa za dukani 14
Nyenzo-rejea ya 4: Kujiandaa kwa matembezi ya kijumuiya – kipindi hicho wanafunzi watagundua chapa za kimazingira 15
Sehemu ya 2: Kuchochea hamasa katika usomaji wa hadithi 17
Somo la 1 17
Somo la 2 19
Somo la 3 20
Nyenzo-rejea ya 1: Kitu ambacho waandishi na wasomaji wafanisi wanatakiwa kukijua 22
Nyenzo-rejea ya 2: Maswali ya kutumia wakati wa usomaji wa kitabu – usomaji wa kwanza, wa pili na wa tatu 23
Nyenzo-rejea 3: Hadithi 24
Nyenzo-rejea 4: Usomaji kimya endelevu 25
Sehemu ya 3: Njia za Usomaji na upokeaji wa taarifa za matini 28
Somo la 1 28
Somo la 2 30
Somo la 3 31
Nyenzo-rejea ya 1: Matini kuhusu takataka 33
Nyenzo-rejea ya 2: Maswali ya utangulizi 35
Nyenzo-rejea 3: Mabango mazuri 36
Nyenzo-rejea 4: Chati ya pai 37
Nyenzo rejea 5: Matini kuhusu mbuyu 39
Sehemu ya 4: Njia za kuwasilisha mtazamo wako 42
Somo la 1 42
Somo la 2 43
Somo la 3 45
Nyenzo-rejea ya 1: Mtoto ‘aliyetengwa’ 47
Nyenzo-rejea ya 2: Michezo inayohimiza uelewa wa ulemavu wa viungo 47

Nyenzo-rejea ya 3: Muundo wa hotuba za mdahalo 48
Nyenzo-rejea ya 4: Sheria na taratibu za kuendesha mdahalo 49
Nyenzo-rejea ya 5: Mfano wa barua- iliyoandikwa na darasa la mwalimu Mariam 51
Nyenzo-rejea ya 6: Vifungu vya utoaji hoja 52
Sehemu ya 5: Njia za kuwa msomaji na mwandishi makinifu 54
Somo la 1 54
Somo la 2 56
Somo la 3 57
Nyenzo-rejea ya 1: Uulizaji wa maswali – kuwahimiza wanafunzi kufikiri kwa umakinifu kuhusu hadithi 59
Nyenzo-rejea ya 2: Vidokezo vya barua ya mwandishi 59
Nyenzo-rejea ya 3: Usomaji makinifu wa matangazo 60
Nyenzo-rejea ya 4: Kutengeneza matangazo 62

# Sehemu ya 1: Kuhamasisha na kutathmini usomaji na uandishi

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuhamasisha ujifunzaji kusoma na kuandika na kutathmini maendeleo?

**Maneno muhimu:** kujua kusoma na kuandika katika hatua za mwanzo; nyimbo; mashairi; chapa za kimazingira; tathmini; kazi ya kikundi; usomaji wa ushirika.

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- kutumia nyimbo na mashairi kufundisha wanafunzi wa kiwango cha mwanzo kusoma;
- kutumia 'chapa za kimazingira' na bidhaa za dukani kufundishia usomaji, uandishi na uchoraji;
- kutalii njia za kuhamasisha ujifunzaji kwa kutumia kazi ya kikundi;
- kukuza uwezo wako wa kutathmini ujifunzaji.

## Utangulizi

Msomaji na mwandishi mfanisi anatakiwa ajue na aweze kufanya nini? Kama mwalimu, unatakiwa uweze kujibu swali hili ili uweze kuwaongoza wanafunzi wako. Kujifunza kusoma na kuandika kwa ufanisi kunahitaji mazoezi. Hivyo, ni muhimu kutumia mikabala na shughuli mbalimbali ambazo zitawafanya wanafunzi wafurahie. Ni muhimu kutathmini maendeleo ya wanafunzi na kujiuliza mwenyewe kama unakidhi matakwa yao. Sehemu hii inatalii mawazo haya kwani inaangalia ujifunzaji kusoma na kuandika katika hatua za awali.

## Somo la 1

Kujifunza kusoma na kuandika ni kazi ngumu! Kwa sababu unataka wanafunzi wazingatie masomo ya kusoma na kuandika, ni muhimu ufanye darasa lako –na shughuli ambazo zinahamasisha ujifunzaji kusoma na kuandika –liwe la kusisimua kadiri iwezekanavyo.

**Nyenzo Rejea 1: Wanachotakiwa kukijua wale wasomaji na waandishi wafanisi** inaeleza kwamba wanafunzi wanahitaji kujua jinsi ya kuhusisha sauti na herufi, herufi na maneno, maneno na sentensi. Nyimbo na mashairi ambayo wanafunzi wanayajua vizuri –na ambayo wanaweza kuyaimba na kuyaghani kwa kuonesha vitendo –yanawasaidia kujenga mahusiano haya. Pia kushirikishana na wanafunzi wako katika usomaji wa kitabu cha hadithi chenye chapa kubwa kunajenga mahusiano. Unapokuwa unasoma, acha kuwaonesha kila picha na waulize wanafikiri kitu gani kitatokea au kitafuata baadaye. Unapokuwa umemaliza, tumia hiki kitabu kwa shughuli za ugunduzi wa herufi na maneno ambazo utawaambiwa wanafunzi wenyewe waonesha na wasome herufi na maneno fulani. Kumbuka kuwapatia wanafunzi fursa nyingi ili wazungumzie kuhusu hadithi hii –wahusika, kilichotokea, wanavyojisikia kuhusiana na hadithi n.k.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kuwapatia wanafunzi utangulizi kuhusu usomaji

Bibi Nomsa Dlamini anafundisha wanafunzi wa darasa la 1 wa Nkandla, Afrika Kusini, kusoma na kuandika KiisiZulu. Nomsa huwasomea vitabu vya hadithi, kutoka kwenye baadhi ya vitabu alivyoandika na kufafanua mwenyewe kwa sababu vipo vitabu vichache vya KiisiZulu.

Mwanzoni mwa mwaka, anahakikisha kwamba kila mwanafunzi anaelewa jinsi kitabu kilivyotungwa –jalada, jina la kitabu, hadithi ilivyojengwa –kwa sababu anajua kuwa baadhi yao hawakuwahi kushika kitabu kabla ya kuanza shule. Amegundua kwamba utabiri wa shughuli, ambapo wanafunziwanapendekeza kile kitakachofuata katika hadithi, una umuhimu na huchangamsha wanafunzi wake.

Nomsa amegundua kwamba wanafunzi wanahitaji mazoezi mengi ili kuwafanya wajiamini katika usomaji. Hutengeneza nakala nyingi za machapisho ya mashairi au nyimbo za KiZulu ambazo wanazijua vizuri na nyingine ambazo anajua kuwa ni mahsusi kwa ajili ya ufundishaji wa ugunduzi wa herufi-sauti. Wanafunzi huzisema au huziimba na kuonesha vitendo kuhusiana na nyimbo na mashairi hayo (angalia **Nyenzo Rejea 1: Mifano ya nyimbo na mashairi** ). La muhimu zaidi, aliwaambia wanafunzi wenyewe waguse na kusoma herufi na maneno. Baadhi ya wanafunzi waliona kuwa kazi hii ni ngumu hivyo alinukuu majina yao na herufi au maneno waliyoona yanawapa shida. Aliandaa kadi zenye picha, herufi na maneno ili kuzitumia kwa njia nyingine na wanafunzi hawa, ama kwa mmojammoja au katika vikundi vidogovidogo, wakati wanafunzi wengine wakiwa wanafanya shughuli nyingine. Nomsa anafarijika kuona kuwa zoezi hili lilisaidia katika kuwafanya wanafunzi hawa wajiamini na kusonga mbele.

## Shughuli ya 1: Kutumia nyimbo na mashairi katika kufundisha usomaji

Waambia wanafunzi:

Wachague wimbo au shairi wanalolipenda;

wauimbe/waghani;waangalie kwa makini, unaposema maneno na kuyaandika ubaoni (au kwenye karatasi /ubao ili uweze kuyatumia tena);wasome wimbo/shairi ulilonalo (fanya hivi mara nyingi); waoneshe kwa kugusa herufi fulani (mojamoja) au maneno au alama za uandishi (herufi kubwa, kituo, alama ya kuuliza); waamue vitendo mtakavyofanya mkiwa mnaimba wimbo/kughani shairi ; wafanye vitendo hivi mkiwa mnaimba tena wimbo/kughani tena shairi; wakae kwenye vikundi vya wannewanne na mpeane zamu za kusomeana wimbo huu/shairi hili.

Zunguka darasani, ukiangalia wanafunzi wanaopata matatizo katika usomaji.

Malizia kwa kuliambia darasa zima liimbe tena wimbo au lighani tena shairi, na kuonesha vitendo.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Somo la 2

Baadhi ya wanafunzi wanakulia katika nyumba ambazo zina utajiri wa chapa na maumbo: maboksi ya bidhaa za dukani, pakiti na makopo, vitabu kwa ajili ya watoto na watu wazima, magazeti hata kompyuta/ngamizi. Wengine wana vifaa hivi kwa uchache nyumbani kwao. Changamoto yako kama mwalimu ni kulipatia darasa lako mazingira yenye utajiri wa chapa . Njia moja ya kufanya hivi ni kukusanya vifaa vyovyote popote vinapopatikana. Vifaa vya kufungashia (maboksi ya mbao, pakiti na makopo) mara nyingi vinaandikwa sana na hata wanafunzi wadogo mara nyingi hutambua maneno muhimu kwa zile bidhaa ambazo zinatumika sana nyumbani. Kwa wasomaji wazoevu, magazeti ambayo wanajumuiya wameshamaliza kuyasoma yanaweza kutumiwa kwa shughuli nyingi darasani.

Sehemu hii inatalii njia za kutumia chapa kama hizi katika kusaidia kujifunza kusoma.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutumia orodha ya vitu vya dukani kwa shughuli za kujifunza kusoma na kuandika

Precious Muhaji hufundisha Kiingereza kwa wanafunzi 45 wa Darasa la 4 lililopo Lushoto katika Milima ya Usambara. Hawajazoea sana Kiingereza lakini wanatambua herufi na baadhi ya maneno ya Kiswahili yaliyopo kwenye vifaa vya kuhifadhia bidhaa ndogondogo za nyumbani.

Precious alimwomba jirani yake maboksi/makasha, pakiti na makopo matupu. Alivileta vitu hivi shuleni ili kuvitumia katika shughuli za kujifunza kusoma na kuandika.

Mchezo unaopendwa na wanafunzi wake ni mchezo wa ‘ugunduzi wa maneno’. Precious alilipanga darasa katika vikundi tisa vya wanafunzi watanowatano na kukipa kila kikundi boksi, pakiti au kopo lilelile. Aliwaambia wanafunzi waandike namba kuanzia 1 mpaka 5 na kisha aliuliza maswali matano (angalia **Nyenzo Rejea 3: Maswali ya mfano ya kuuliza kuhusu vitu vya nyumbani** ). Wanafunzi walilinganisha majibu wenyewe na waliamua kuhusu jibu la kikundi. Precious alijadili yale maswali na darasa zima. ‘Mshindi’ alikuwa ni kikundi kilichomaliza cha kwanza na kuweza kutoa majibu sahihi zaidi.

Wakati mwingine Precious alikikaribisha kila kikundi ili kiweze kuuliza swali linalohusiana na ugunduzi wa neno.

Ili kuwahamasisha wanafunzi wafikiri kwa makini, wakati mwingine aliuliza swali kuhusu mchoro wa kifaa kinachohifadhia bidhaa na ujumbe uliopo kwenye tangazo.

Precious aligundua kuwa wanafunzi wengine hawakushiriki, hivyo wakati mwingine walipocheza mchezo huu, alimwambia kila mwanafunzi aandike maneno manne kutoka kwenye kontena la kuhifadhia bidhaa za dukani kabla ya kurudi kwenye viti vyao vya kawaida. Wakiwa wamesharudi kwenye viti vyao alimwambia kila mmoja amsomee mwenzake orodha yake. Aligundua wanafunzi sita ambao walihitaji msaada zaidi na alifanya nao kazi baada ya saa za shule kwa nusu saa, kwa kutumia vitu vilevile na kuwapatia muda wa kufanya mazoezi ya kubainisha herufi na maneno.

Precious aligundua kuwa kuzoea herufi na maneno katika vifaa vya kuhifadhia bidhaa huwasaidia wanafunzi kubainisha herufi na maneno haya katika matini nyingine walizozisoma, kama vile hadithi. Kwa kunakili maneno kutoka katika vitu hivyo, wanafunzi pia hujifunza kuandika herufi na maneno kwa kujiamini zaidi na kwa usahihi zaidi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 2: Kutumia orodha ya bidhaa za dukani kwa shughuli za usomaji na uandishi

Leta makopo/mikebe, pakiti au maboksi ya kutosha darasani ili kila kikundi cha wanafunzi watanowatano au sitasita kipate kitu kimojawapo cha kukifanyia kazi au liambie darasa lako likusaidie katika ukusanyaji wa vitu hivi.

Andika maswali ubaoni kuhusu maneno na picha zinazoonekana kwenye pakiti, kopo au boksi (angalia Nyenzo Rejea 3 ). Ama waambie wanafunzi wayasome au uwasomee.

Ama chezesha mchezo wa ugunguzi wa maneno katika vikundi (angalia **Uchunguzi Kifani 2**) au waambie wanafunzi waandike majibu wenyewe. Panga muda wa ziada wa mazoezi na wa kutoa msaada zaidi kwa ajili ya wanafunzi ambao hawawezi shughuli hii.

Katika somo linalofuata, waambie wanafunzi wafanye kazi katika vikundi vilevile wabuni maandishi na taarifa zinazoonekana kwa ajili ya kifaa cha kweli au picha ya bidhaa za dukani.

Kiambie kila kikundi kioneshe na kuzungumzia kuhusu ubunifu/mchoro wao kwa wanafunzi wote darasani.

Wanafunzi wamejifunza nini kwa kusoma orodha ya bidhaa za dukani na kwa kuchora na kuonesha vifaa vyao wenyewe vya kuhifadhia bidhaa hizo? Linganisha mawazo yako na mapendekezo yaliyopo katika Nyenzo Rejea 3 .

## Somo la 3

Kusoma na kuandika kunaweza kusisimua na kuchangamsha sana, lakini baadhi ya wanafunzi wanajenga mtizamo hasi kuhusiana na shughuli hizi. Sababu inaweza kuwa ni kwa vile wanagundua kuwa kusoma na kuandika ni kugumu, labda kwa sababu wanaweza kuchoshwa na kazi za usomaji na uandishi ambazo zinafuata ruwaza zilezile daima, au labda hawaoni thamani kubwa katika usomaji na uandishi. Moja ya changamoto zako kama mwalimu ni kuamsha ari ya wanafunzi katika usomaji na uandishi na kuwafanya wahamasike.

**Uchunguzi Kifani 3** na **Shughuli Muhimu** vinapendekeza shughuli ambazo zinaweza kuwasaidia wanafunzi wafurahie na wajiamini zaidi katika usomaji na uandishi.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kusoma alama zinazopakana jirani na eneo lako na kuandika maelezo kuhusiana na alama hizo

Bwana Richard Limbunga hufundisha Kiswahili Darasa la 5 jijini Dar es Salaam. Dar es Salaam ni eneo lenye watu wengi na mifano mingi ya chapa za kimazingira kuzunguka shule –mifano mingi zaidi ni ya Kiswahili lakini pia kuna mifano kutoka katika lugha mbalimbali za asili.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Ili kuongeza kipato watu wameanzisha ‘biashara za uani’ kama vile maduka ya bidhaa ndogondogo za dukani, sehemu za kunyolea, warepeaji magari na vibanda vya simu. Sehemu zote hizi zina alama na baadhi pia zina matangazo ya kibiashara kwa ajili ya bidhaa mbalimbali. Hizi ni shule, kliniki, sehemu na kumbi za kuabudia, ambazo nyingi yazo zina alama na mbao za matangazo. Katika barabara kuu, kuna alama sehemu nyingi, zikiwemo Chuo Kikuu maarufu cha Dar es Salaam.

Bwana Limbunga alipanga safari kuzunguka Dar es Salaam ambayo ingewapatia wanafunzi fursa ya kusoma na kutengeneza kitini na michoro kuhusu mifano mbalimbali ya chapa na maumbo yanayoonekana. Pia aliandaa orodha ya maswali ili kuongozo uchunguzi wao.

Bwana Limbunga anao wanafunzi 58 katika darasa lake, wakiwemo kumi ambao wamewasili

hivi karibuni kutoka Burundi. Aliamua kuwaomba wastaafu wawili wanaojua lugha nyingi wamsaidie katika shughuli hii. Mmoja anaongea Kirundi, lugha ya wanafunzi kutoka Burundi. Vikundi vitatu vya darasa lile vilikwenda safari.

Marafiki wa Bwana Limbunga walishiriki katika mjadala darasani na kwenye shughuli zilizofuata za usomaji na uandishi. Kufikia mwishoni mwa wiki, watu wale watatu walikubali kuwa wanafunzi wamejua zaidi jinsi taarifa inavyoweza kuwasilishwa kwa njia mbalimbali na kwa lugha mbalimbali na baadhi walionekana wamefurahia zaidi usomaji na uandishi kuliko hapo awali.

## Shughuli muhimu: Kusoma Alama

Kabla ya somo, soma **Nyenzo Rejea 4: Kujiandaa kwa matembezi ya kijumuiya** ili kupanga matembezi na kuandaa maswali yako. Andika maswali ubaoni.

Ili kuanza somo, waambie wanafunzi kuhusu matembezi na, kama wanaweza, waambie wanakili yale maswali kutoka kwenye ubao. Kama hawawezi, andaa orodha ya maswali kwa kila kiongozi wa kikundi kwa ajili ya kuwauliza katika matembezi.

Wachukue kwa ajili ya matembezi yaliyopangwa mpaka kwenye jumuiya yenu mnayokaa.

Wakiwa wanatembea, lazima watoe au waandike majibu ya maswali na wachore mifano ya chapa au picha wanazoziona.

Baada ya muda, waambie wanafunzi kwenye vikundi washirikishane kile walichokiona, walichokiandika na walichokichora. Liambie darasa zima liripoti na lirekodi pointi muhimu ubaoni.

Kiambie kila kikundi kichore, kiandike jina na kichore alama, ilani au tangazo wanalofikiri ni muhimu kuwapo katika jumuiya zao. Wasaidie katika maneno yoyote magumu. Watoto wadogo wanaweza kuhitaji kufanya kazi kwenye vikundi vidogo vyenye mtu mzima wa kuwasaidia.

Kiambie kila kikundi kioneshe mchoro wao darasani kisha kieleze uteuzi wa lugha, maumbo na taarifa.

Onesha michoro hii darasani ili wanafunzi wote waisome.

# Nyenzo-rejea ya 1: Kitu ambacho waandishi na wasomaji wafanisi wanatakiwa kukijua

**Usuli/ welewa wa somo wa mwalimu**

**Lugha wanayotarajiwa kujifunzia usomaji na uandishi**

Kama wanafunzi wanatakiwa wajifunzie kusoma na kuandika katika lugha ambayo si lugha ya nyumbani, hali hii itafanya kazi iwe ngumu zaidi. Katika hali hii, walimu wanatakiwa waanze na kazi za kuongea na uundaji wa msamiati katika lugha hii ya nyongeza, kwa kutumia vitendo na picha. Pindi tu watakapokuwa na uelewa wa baadhi ya yanayosemwa wanaweza kutarajiwa kutumia uelewa huo kwa usomaji na uandishi.

## Msimbo wa maandishi

Wanafunzi wanahitaji kuelewa jinsi herufi kwenye ukurasa unavyowakilisha sauti fulani na jinsi zinavyoungana katika kuwasilisha maana kwa njia ya maneno. Hii ndiyo sababu ya umuhimu wa walimu kwa kiasi fulani kuzingatia 'foniksi' – herufi inayowakilisha sauti fulani – wanapowafundisha wasomaji wa kiwango cha mwanzo. Kwa kuchukua mfano toka katika lugha ya Kiswahili, kama mwalimu ungeweza kutumia picha ya mbwa pamoja na herufi tofauti za m b w a na kisha neno m b w a chini yake. Kwanza waulize wanafunzi wanaona nini katika picha (mbwa), kisha onesha kila herufi na kuitamka; kisha tamka neno zima. Baadaye pima welewa wa wanafunzi kwa kuonesha herufi ambazo hazijaunganishwa na kuwaambia waunde manenokwa kutumia kila moja ya sauti. Baadaye, waambie wakuambie maneno mengine yanayoanza na sauti m. Pia wapatie mifano yako mwenyewe.

**Kanuni za uandishi**

Wanafunzi wanahitaji kuelewa jinsi maneno yanavyoungana kuunda maana katika sentensi, aya, na matini ndefu (mf.kitabu kizima cha hadithi) na jinsi matini zinavyoandikwa kwa njia nyingi na kwa madhumuni mbalimbali (mf. Mapishi ni tofauti na jinsi hadithi inavyoandikwa). Katika miaka ya mwanzo, wanafunzi wanaanza kujifunza jinsi uandishi unavyopangiliwa, lakini hili ni jambo wanalojifunza zaidi katika masomo yao. Wanafunzi wanatakiwa wasome kitabu chote ili waweze kuona jinsi maneno yalivyoungana na jinsi hadithi au dai linavyoendelezwa. Hii ndiyo maana hakutoshi kushughulikia sauti tu.

*Jinsi ya kusoma michoro, pichavivuli, vielelezo na jinsi ya kutengeneza mahusiano baina ya maumbo haya na maneno ya maandishi*

Wanafunzi wanahitaji kufundishwa jinsi kugundua yale yaliyopo katika michoro, pichavivuli na vielelezo. Unaweza kuwasaidia kwa kuwauliza maswali kama vile 'babu ameshika nini?' 'Kiboko ana nini mgongoni mwake?'

**Kuhusu dunia na jinsi inavyojiendesha**

Kadiri mwalimu anavyowasaidia wanafunzi kupanua maarifa yao ya jumla ya dunia na jinsi inavyofanya kazi, ndivyo hivyo inavyowarahisishia wanafunzi kusoma kuhusu kile kigeni na kile wasichokijua kwa sababu wanaweza kuunganisha kati ya kile ambacho tayari wana uzoevu nacho au wameshajifunza na hii taarifa mpya.

Zaidi ya yote, ni muhimu wanafunzi wafurahie kusoma na kuandika – hata wanapokutana na changamoto.

## Nyenzo-rejea ya 2: Mifano ya nyimbo na mashairi

**Nyenzo Rejea ya mwalimu kwa upangaji au kurekebisha kwa ajili ya kutumia na wanafunzi**

**Mfano wa wimbo wa Kiswahili**

Wimbo wa kubembelezea mtoto wa ‘Kua’, unahusu mzazi anayekazania kumwambia mtoto wake mdogo akue. Zingatia mdafao wa marudio ya herufi na sauti zilezile.

Unaimbwa hivi:

‘Kua mwanangu, kua. Kua ili nikupe mawaidha ili kwamba niweze kukupa kundi la ng’ombe na mbuzi, ili upate maziwa. Kua mwanangu, kua. Kua ili uwe mkubwa. Kua upesi kama mgomba kwa sababu mnazi unachelewa. ‘Kua mwanangu, kua.

Katika unaweza kuusikia wimbo huu.

Vyanzo vya asili: [BBC Radio 3 On Your Stree], Website

**Shairi la Kiswahili lililotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza ambalo linafurahisha likighanwa harakaharaka**

***Siagi ya Manjano* na Mary Ann Hoberman**

Siagi ya manjano jeli ya zambarau jemu nyekundu mkate mweusi

Ipakaze kwa wingi

Iseme kwa haraka

Siagi ya manjano jeli ya zambarau jemu nyekundu mkate mweusi

Ipakaze kwa wingi sana

Iseme kwa haraka sana

Siagi ya manjano jeli ya zambarau jemu nyekundu mkate mweusi

Sasa irudie

Ukiwa unaila

Siagi ya manjano jeli ya zambarau jemu nyekundu mkate mweusi

Usiongee mdomo ukiwa umejaa!

**Shairi la vitendo**

Mimi ni chombo kidogo cha sukari, kifupi na imara

Huu ni mpini wangu, huu ni mdomo wangu

Ninapopata joto

Hapo ninapayuka

Nipindue

Nimwage.

**Wimbo wa mnyama dunia – wimbo kutoka Kongo**

Angalizo: Wimbo huu unahusu harakati na sauti za kiitikio zinawakilisha harakati za viumbe.

MSIMULIAJI: Samaki huenda

KIITIKIO: Hip!

MSIMULIAJI: Ndege huenda

KIITIKIO: Viss! MSIMULIAJI: Nyani huenda KIITIKIO: Nyan!

SAMAKI: Ninaanzia kushoto,

Ninageuka kulia.

Mimi ni samaki

Anayeponyoka majini,

Anayeteleza,

Anayenengua,

Anayechupa!

MSIMULIAJI: Kila kitu kinaishi,

Kila kitu hucheza dansi,

Kila ktu huimba.

KIITIKIO: Hip!

Viss!

Nyan!

NDEGE: Ndege huruka mbali,

Huruka, huruka, huruka,

Huenda, hurudi, hupita,

Hupanda, huelea, hutua.

Mimi ni ndege!

MSIMULIAJI: Kila kitu huishi,

Kila kitu hucheza dansi,

Kila kitu huimba.

KIITIKIO: Hip!

Viss!

Nyan!

NYANI: Nyani! Kutoka tawi

hadi tawi

Hukimbia, huchupa, huruka,

Akiwa na mkewe na mtoto,

Mdomo ukiwa umejaa chakula, mkia hewani,

Huyu ni nyani!

Huyu ni nyani!

MSIMULIAJI: Kila kitu huishi,

Kila kitu hucheza dansi,

Kila ktu huimba.

KIITIKIO: Hip!

Viss!

Nyan!

*Vyanzo vya asili: [Siagi ya manjano – Shairi/wimbo wa jadi; Kiingereza Kipya cha Mafanikio, Darasa la 6, Kitabu cha Kusoma], [Oxford University Press]*

*[ Wimbo wa mnyama dunia – Wimbo wa jadi kutoka Kongo], [Ushairi wa Kiafrika kwa Shule, Longman]*

## Nyenzo-rejea ya 3: Maswali ya mfano ya kuuliza kuhusu bidhaa za dukani

**Nyenzo Rejea ya mwalimu kwa kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

1. Ndani ya kopo/pakiti/boksi mna nini?
2. Unajuaje hivi?
3. Ni neno au maneno gani yameandikwa kwa herufi kubwa zaidi yaherufi zote?
4. Unafikiri kwa nini hili neno au haya maneno yameandikwa kwa herufi kubwa kuliko herufi zote?
5. Maneno mangapi yanaanza kwa herufi kubwa?
6. Maneno gani yameandikwa zaidi kwenye kifaa hiki cha kuhifadhia bidhaa kisha kuandikwa mara moja?
7. Neno lipi hutumika sana?
8. Nini uzito wa bidhaa hii (gramu/kilogramu)?
9. Maneno na picha zote zinakuambia nini kuhusiana na bidhaa hii?

**Maswali yanayohamasisha kufikiri kwa makini**

- Unakubaliana au unapingana na kile unachoambiwa na maneno na picha hizi?
- Kama ungekuwa na fedha, ungependa kununua bidhaa hii? Kwa nini ndiyo?, au kwa nini hapana?

Angalizo 1: Baadhi ya bidhaa zina maneno ambayo yako kwenye lugha zaidi ya moja. Kama hivi ndivyo kwa baadhi ya bidhaa unazotumia, ungeweza kuwauliza wanafunzi ni lugha gani ambazo zimekuwa zikitumika na kwa nini wanafikiri lugha hizi zilikuwa zikitumika.

Angalizo 2: Maswali haya ya mfano ni ya jumla sana. Kuna maswali mengine mengi ungeweza kuuliza, kama kuna picha za watu kwenye bidhaa, je, ni wanaume au wanawake, je ni vijana au wazee? Kwa nini watu hawa wawepo kwenye pakiti/kopo/boksi?

Wanafunzi wanaweza kujifunza nini kutokana na kutumia orodha ya bidhaa za dukani

1. Wasomaji wa kiwango cha mwanzo wanaweza kutumia maneno yaliyopo kwenye orodha ya bidhaa za dukani ili kupata ujasiri na stadi katika kutambua muundo wa herufi kubwa na ndogo wa alfabeti na katika kuunganisha maumbo ya herufi na sauti.
2. Kwa kunakili herufi na maneno kutoka kwenye kitu hicho, mwandishi wa kiwango cha mwanzo, anaweza kupata ujasiri na stadi za kuandika herufi na maneno haya kwa usahihi.

3. Wasomaji wa ngazi ya juu wangeweza kusoma 'ujumbe' uliopo kwenye kitu hicho na kutafakari maana yake. Wangeweza kuanza kuwa wasomaji makinifu.
4. Kwa kufanya kazi ya kubuni baadhi ya orodha ya bidhaa za dukani katika vikundi, wanafunzi wangeweza kufaidika kutokana na mawazo ya wenzao, kujifunza vitu vinavyohusika katika kuchora bidhaa, kutumia fikra zao na kufanya mazoezi ya kuandika na kusoma.
5. Baadhi ya wanafunzi wanaona ni vigumu kuzungumza darasani kwa sababu hawajui wazungumzie nini. Ukiwa na kielelezo cha kitu kwa ajili ya kuelezea darasani kinawapa wanafunzi mada ya kuzungumzia.
6. Kila kielelezo cha kikundi kinawapatia wanafunzi wengine vitu vingine vya kusoma.
7. Ungeweza kutengeneza kadi za kusomeshea zenye herufi/maneno ambayo baadhi ya wanafunzi wanayaona ni magumu kuyasoma. Weka picha ya kuwasaidia kwenye kila kadi. Tumia kadi hizi kwa ajili ya mazoezi ya kusoma ya mwanafunzi mmojammoja au kwa kikundi kidogo kwa muda muafaka.

## Nyenzo-rejea ya 4: Kujiandaa kwa matembezi ya kijumuiya – kipindi hicho wanafunzi watagundua chapa za kimazingira

**Nyenzo Rejea ya mwalimu kwa kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

**Hatua 1:** Kama darasa lako ni kubwa sana, unaweza kuwaomba watu wazima kutoka kwenye jumuiya wakusaidie kufanya matembezi na vikundi vya wanafunzi. Kama unawaomba, kutana nao kabla ya matembezi kuwaeleza kile unachotaka wao wafanye. Lazima wajue ni maswali gani utawauliza wanafunzi na ni mifano gani ya chapa za kimazingira unataka wanafunzi wazigundue. Wanaweza pia kuwa na mapendekezo ya kukupa.

**Hatua 2:** Panga shughuli kwa kutembelea mazingira yote yanayoizunguka shule yako. Kwa baadhi yenu eneo hili linaweza kuwa ni kijiji, kwa wengine sehemu ya jiji lenye shughuli nyingi. (Angalizo: Kama shule yako ipo sehemu ambayo imejitenga, unaweza kuhitaji kusaidiana na wanajumuiya ili kupanga usafiri wa wanafunzi kwenda sehemu ambayo wanaweza kuona chapa mbalimbali za kimazingira). Angalia kila mfano wa chapa ya kimazingira unaoweza kuwavutia wanafunzi na panga njia ambayo wewe na wanafunzi mtapitia wakati wa matembezi. Aina za chapa na maumbo/picha, kwa hakika, itatofautiana sana kutoka kwa eneo jirani moja na jingine lakini zinaweza kujumuisha majina (mf.shule, kliniki, msikiti, kanisa, ukumbi wa jumuiya, duka, mto, mtaa); alama (mf. Alama ya SIMAMA); matangazo kwenye mabango makubwa au kwenye kuta za maduka; taarifa za kijumuiya (mf. mabango ya uchaguzi au taarifa kuhusu mikutano au matukio ya kijamii au michezo).

**Hatua 3:** Andaa orodha ya maswali watakayoyajibu wanafunzi. Haya yanaweza kujumuisha:

- Alama au jina hili linatuambia nini?
- Unafikiri kwa nini limewekwa hapa?
- Limeandikwa kwa lugha gani?
- Unafikiri kwa nini limeandikwa kwa lugha hii?
- Unapata taarifa gani kutokana na mchoro au picha kivuli hii unayoiona?

- Ni alama ipi ambayo ni rahisi kuisoma? Kwa nini?
- Unapenda alama ipi? Kwa nini?
- Unawezaje kuboresha baadhi ya alama hizi?
- Ni majina gani mengine, alama, matangazo, mabango, taarifa ambazo ungependa kuwa nazo katika mazingira ya hapa jirani? Kwa nini ungependa kuwa nazo hizi?

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 2: Kuchochea hamasa katika usomaji wa hadithi

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuwahamasisha wanafunzi wapende kusoma hadithi na vitabu?

**Maneno muhimu:** usomaji wa kushirikishana; majibu ya ubunifu; kusoma kimya; mianzo na miisho; kuchochea hamasa.

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- kutumia njia ya kushirikishana katika usomaji wa hadithi kwenye ufundishaji wako ili kusaidia wasomaji wanaoendelea;
- kutumia shughuli zinazolenga mianzo na miisho mbadala katika usomaji;
- kutalii njia mbalimbali za kukuza Usomaji Kimya Endelevu katika darasa lako.

## Utangulizi

Inawezekana zaidi kwa wanafunzi kujifunza kusoma kwa ufanisi kama wanafurahia kusoma na kuandika mara nyingi iwezekanavyo. Ukiwauliza rafiki zako wanafurahia nini katika kusoma, majibu yao yanaweza kutofautiana kuanzia kwenye kurasa za magazeti ya michezo mpaka kwenye mapishi, riwaya za mapenzi, hadithi za upelelezi au wasifu –au wanaweza wasisome kabisa! Kama walivyo rafiki zako, wanafunzi mbalimbali wanaweza kufurahia kusoma aina tofauti za matini. Watavutiwa na kile wanachosoma kwa njia mbalimbali. Kazi yako ni kuwahamasisha wanafunzi wote katika darasa lako wasome kwa ufanisi na wafurahie usomaji.

Sehemu hii inalenga kuwasaidia wanafunzi wapate raha katika usomaji na wavutiwe na hadithi.

## Somo la 1

Aina ya hadithi na shughuli za usomaji wa hadithi ambazo wanafunzi wanazifurahia huenda zikatofautiana kufuatana na umri wao na ujuzi wao wa lugha iliyotumika katika hadithi hiyo. Wanafunzi wadogo zaidi na wanafunzi ambao ndio wameanza kujifunza lugha ya ziada wanafurahia wakisomewa hadithi mara kadhaa –hasa kama wana fursa ya kushiriki katika usomaji. Kwa kusoma hadithi mara nyingi na kuwatia moyo wanafunzi wasome sehemu za hiyo hadithi pamoja na wewe, unawasaidia wazoee maneno mapya na wajiamini kama wasomaji.

Lengo la **Shughuli 1** ni kuandaa na kufundisha somo la kushirikishana katika usomaji. Madhumuni ya shughuli hii ni kuongeza kujiamini kwako na ujuzi kama msomaji, na kuwafanya wanafunzi wapende kusoma vitabu.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutumia uzoevu wa hadithi za utotoni ili kuandaa shughuli za darasani

Wakati Jane Dlomo alipofikiri kuhusu enzi za utoto wake huko Rasi ya Mashariki ya Afrika Kusini, alikumbuka ni kwa kiasi gani alivyofurahia hadithi za bibi yake. Vitu viwili vilimjia akilini: kwanza kabisa, jinsi gani alivyofurahia kusikiliza hadithi zilezile na tena zaidi na zaidi na pili, jinsi gani yeye na kaka na dada zake walivyofurahia kujumuika kwenye hadithi. Wakati mwingine bibi yake aliuliza, 'Mnafikiri kulitokea nini baadaye?' Wakati mwingine aliwataka watoto kuonesha vitendo.

Jane aliamua masomo yake ya usomaji kwa Darasa la 4 nne yawe karibu na jinsi alivyofanya bibi yake katika hadithi. Pia aliamua kuwajaribishia shughuli ambazo zingewahusisha wanafunzi washirikiane naye katika usomaji.

Alipomwambia rafiki yake Thandi kuhusu uamuzi wake, Thandi alipendekeza kuwa washirikiane kupata vitabu vya hadithi vinavyofaa, kufanya mazoezi ya kusomeana hadithi kwa sauti na katika kufikiria njia za kuwashirikisha wanafunzi katika usomaji. Walimu wote wawili waligundua kuwa kushirikishana katika maandalizi kuliwasaidia katika kujiamini zaidi darasani. (angalia **Nyenzo-rejea 1: Maandalizi kwa ajili ya usomaji wa kushirikishana** ).

**Nyenzo-rejea Muhimu: Kutumia usimulizi** wa hadithi darasani inakupa mawazo zaidi.

## Shughuli ya 1: Kushiriki kwa pamoja raha iliyo katika kitabu kizuri cha hadithi

Soma **Nyenzo-rejea 1** na fuata hatua zifuatazo hapa chini: Andaa kazi ya mazoezi mengine kwa baadhi ya wanafunzi ili wayafanye wakati mnapofanya usomaji wa kushirikishana kikundi cha wanafunzi 15 au 20.

Toa maelezo ya usuli kuhusu mada ya hadithi kabla ya kuisoma hiyo hadithi.

Unaposoma, waoneshe wanafunzi vielelezo na waulize maswali kuhusiana na vielelezo hivyo. Tumia sauti yako na vitendo ili kuvuta usikivu wa wanafunzi.

Waalike wanafunzi wajiunge katika usomaji kwa kurudia maneno au sentensi kadhaa ulizoandika ubaoni na kwa kuonesha vitendo.

Mwishoni, jadilini hadithi hii na wanafunzi wako. (Angalia **Nyenzo-rejea 2: Maswali ya kutumia katika usomaji wa vitabu**.)

Ulijisikiaje kuhusu usomaji wako wa hadithi? Je, wanafunzi waliifurahia hadithi? Unajuaje? Unaweza kufanya nini ili kuboresha stadi zako za usomaji?

## Somo la 2

Bruno Bettelheim (1976), mtaalamu wa saikolojia ya watoto, anaamini kwamba kama watoto watakutana na ‘maajabu’ katika hadithi, kwa hakika watapenda kujifunza kusoma. Anatoa hoja kuwa kama watoto anaamini hasa kwamba kuweza kusoma kutafungua dunia yenye uzoevu na welewa wa ajabu, watafanya jitihada kubwa kujifunza kusoma na wataendelea kusoma.

Kusoma pamoja hadithi za kufurahisha na wanafunzi ni njia moja ya mwalimu ya kufanya usomaji uwe ni jambo lenye mvuto. Kitu kingine ni kuchochea udadisi na ubunifu kwa kuwahimiza watafute miisho mbadala ya hadithi (na wakati mwingine mianzo) na kushirikishana mianzo na miisho hii na wanadarasa wenzao. **Uchunguzi kifani 2** na **Shughuli 2** vinaeleza jinsi unavyoweza kuwasaidia wanafunzi wako wawe watunzi wa hadithi kwa ajili ya wenzao.

### Uchunguzi kifani ya 2: Usomaji wa hadithi; uandishi wa miisho mipya ya hadithi

Bibi Miriam Pharouk hufundisha Kiingereza Darasa la 6 katika shule ya Tanga. Siku moja aliwaambia wanafunzi wake wafikirie hadithi ambazo wameshasoma naye na wamwambie ni mwisho upi wa hadithi waliupenda sana na upi waliuona si mzuri au haukuwaridhisha. Aligundua kuwa walikuwa na hadithi tofautitofauti walizozipenda. Hata hivyo, kulikuwa na hadithi moja ambayo wanafunzi wengi hawakuipenda kwa sababu hawakujua kilichotokea kwa wahusika watatu ambao ‘walitoweka’ kwenye hadithi. Miriam aliwaambia wapendekeze nini kinaweza kuwa kiliwatokea wahusika hawa na aliandika mawazo yao ubaoni. Baadaye aliwaambia

wanafunzi wamchague mhusika mmoja kati ya hawa watatu na waandike sehemu ya mwisho ya mhusika huyu katika hadithi hii. Aliwahimiza wanafunzi kutumia mawazo yao wenyewe, na pia yale yaliyoandikwa ubaoni, na waingize michoro kwenye uandishi wao. Kisha alisoma tena ile hadithi ili kuwakumbusha mandhari, wahusika na matukio makuu.

Ingawa Miriam aliwaambia wanafunzi kila mtu aandike mwenyewe, pia aliwahimiza kusaidiana kwa mawazo, msamiati na muenelezo wa maneno. Alizunguka darasani huku wanafunzi wakiwa wanaandika na kuchora, akitoa msaada palipohitajika. Alifarijika alipogundua kuwa wengi wa wanafunzi wake wanapenda kwa dhati wazo la kuwa watunzi na la kuiandikia hadhira halisi (wanadarasa wenzao). Aling’amua kuwa walikuwa waangalifu sana katika kufanya kazi yao kwa sababu wanadarasa wenzao wangesoma kazi zao.

Katika somo lililofuata, wakati wanafunzi wanasoma mwisho wa hadithi ya mwenzao, mwalimu aligundua kuwa wengi wa ‘wasomaji wake waliokuwa wanasitasita’ walikuwa makini kusoma kile ambacho wanadarasa wenzao walikuwa wamekiandika na kuona kile walichokuwa wamekichora.

## Shughuli ya 2: Uandishi wa mianzo na miisho mipya ya hadithi

Andika kwenye ubao wako hadithi fupi katika **Nyenzo-rejea 3: Hadithi** . Futa kichwa cha hadithi na sentensi mbili za mwisho.

Soma hiyo hadithi wewe na wanafunzi wako. Jadilini maneno yoyote magumu.

Waambie wajibu maswali kama yaliyoko kwenye **Nyenzo-rejea 3**.

Panga darasa katika vikundi vya wannewanne –wawili waandike mwanzo wa hiyo hadithi na wawili waandike mwisho wa hiyo hadithi. Wanafunzi wawiliwawili wachore mchoro wa kufafanua sehemu yao ya hadithi. (Zoezi hili linaweza kuchukua zaidi ya kipindi kimoja.)

Kiambie kila kikundi kisome hadithi yao yote na kuonesha michoro yao kwa darasa zima. Jadilianeni na wanafunzi kitu wanachokipenda katika hadithi za wenzao.

Mwishoni, wasomee wanafunzi wote kichwa cha hadithi ya awali na zile sentensi mbili za mwisho. (Huenda wakashangaa kwamba inahusu soka!)

Tafuta hadithi nyingine ili kurudia zoezi hili.Shughuli hii ilifanikiwa vizuri kwa kiasi gani? Wanafunzi walizipokeaje hadithi za wenzao?

## Somo la 3

Walimu lazima wawe mifano mizuri kwa wanafunzi wao. Wanafunzi wako wanaweza kuhamasika zaidi katika usomaji kama wanakuona wewe ukisoma. Kila siku jaribu kutenga muda (angalau mara tatu kwa wiki) kwa ajili yako na wanafunzi wako wa kusoma kimya darasani. Unaweza kuchukua mfano huu kutegemeana na umri wa wanafunzi wako. Kwa mfano, wanafunzi wenye umri mdogo wangeweza kuangalia kitabu cha picha na wenzao au kumsikiliza mtu akiwasomea katika vikundi vidogo.

Usomaji Kimya Endelevu au Usomaji wa Kina (Sustained Silent Reading) huwasaidia wanafunzi wazoee kujitegemea katika usomaji na kwa kasi yao wenyewe (ambayo inaweza kuwa ya haraka sana au taratibu sana kuliko baadhi ya wanadarasa wenzao). Mlengo ni kwenye hadithi yote (au sura yote kama hadithi ni ndefu sana) na kwenye miitikio binafsi ya wanafunzi kuhusiana na kile wanachosoma. Usomaji Kimya Endelevu unaweza kufanywa kutumia kitabu cha kusoma darasani, idadi mbalimbali ya vitabu ambavyo wanafunzi wamevichagua katika maktaba ya darasa au ya shule, au kwa kutumia magazeti (kama wanafunzi wanaweza kuyatumia) – angalia **Nyenzo-rejea 4: Usomaji Kimya Endelevu** .

**Uchunguzi kifani 3** na **Shughuli Muhimu** zinaonesha njia za kutathmini maendeleo ya wanafunzi kama wasomaji. (Angalia pia **Nyenzo-rejea Muhimu: Kutathmini ujifunzaji** .)

# Uchunguzi kifani ya 3: Uzoevu wa walimu kuhusu Usomaji Kimya Endelevu

Chama cha Usomaji Tanzania kilipanga warsha iliyofanyikia Dar es Salaam, ili kuwapatia walimu utangulizi kuhusu Usomaji Kimya Endelevu. Ilielezwa kuwa moja ya malengo makuu ya Usomaji Kimya Endelevu ni kujenga 'utamaduni wa kusoma' miongoni mwa wanafunzi.

Walimu walialikwa kushiriki katika Usomaji Kimya Endelevu na kisha kutafakari uzoevu wao. Kila mwalimu alichagua kitabu au gazeti na kusoma kimya kwa dakika 20. Baada ya kusoma, walikuwa na dakika kumi za mjadala na wenzao watatu kuhusu kile walichokisoma na jinsi walivyoipokea ile matini. Waliporudisha vitabu na magazeti yao waliandika majina yao kwenye kitabu cha rejesta na, pembeni mwa majina yao, waliandika maoni mafupi kuhusu matini hiyo.

Walimu hawa waliamua kuwa Usomaji Kimya Endelevu ni muhimu kwa ajili ya kujenga umakinikaji na nidhamu ya mtu, kwa kujifunza msamiati mpya na mawazo mapya na kutoa maudhui ya kujadiliana na wanafunzi. Walifikiri kuwa wanafunzi wataifurahia shughuli hii na kuona fahari watakapokuwa wamemaliza kukisoma kitabu. Baadhi ya walimu waliamua kujaribu kuendesha zoezi hili kwa kutumia kikundi kidogo kimojakimoja na kuzunguka darasani kwa sababu walikuwa na vitabu vichache tu darasani.

## Shughuli muhimu: Usomaji kimya endelevu

Kusanya vitabu vinavyosisimua, magazeti na hadithi ambazo zinalingana na kiwango cha wanafunzi wako. Washirikishe wanafunzi na jumuiya katika kukusanya matini zinazofaa au tumia vitabu ambavyo wanafunzi wametengeneza darasani (angalia **Nyenzo-rejea 4** ). Tenga dakika 15–20 kila siku au mara tatu kwa wiki kwa ajili ya Usomaji Kimya Endelevu. Waambie wanafunzi wachague matini ya kusoma kwa ukimya. Jisomee mwenyewe wakati wanafunzi wakiwa wanasoma. Mwishoni, kama hawakumaliza kusoma vitabu vyao, waambie watumie alama zilizopo kitabuni ili watakaposoma tena iwe rahisi kujua walipoishia.

Mwambie kila mwanafunzi atoe au achangie kwenye rekodi ya usomaji (angalia **Nyenzo-rejea 4**).

Kila wiki, watake wanafunzi, katika vikundi vidogo, waambiane kuhusu walichokuwa wanakisoma.

Zungukia vikundi kusikiliza wanayosema wanafunzi. Kagua rekodi zao za usomaji.

Je, wanafunzi wamefurahia shughuli hii na wanasonga mbele katika usomaji wao?

Unawezaje kusaidia zaidi?

# Nyenzo-rejea ya 1: Kitu ambacho waandishi na wasomaji wafanisi wanatakiwa kukijua


**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Chagua hadithi yenye wahusika na matukio ambayo unafikiri yatawasisimua wanafunzi wako.

Fikiria maelezo ya usuli ambayo wanafunzi watayahitaji ili waelewe na wafurahie hadithi. Amua jinsi utakavyoyatoa kabla ya kuanza usomaji wa hadithi. Kwa mfano, wanafunzi wenye umri mdogo katika baadhi ya sehemu za Afrika watamfahamu kiboko, lakini wengine wanaweza wasielewe, hivyo kabla ya kusoma hadithi ya Kiboko Mkali utatakiwa uchunguze wanafunzi wanajua nini kwa njia ya kuwauliza maswali kama haya:

Maswali ya kujua maarifa waliyo nayo

- Kiboko anafananaje?
- Je, kiboko anaweza kukuogopesha? Kwa nini ni 'ndiyo' , au kwa nini ni 'hapana'?
- Unaweza kumwona kiboko wapi?
- Kiboko anakula nini? Swali la kwanza linalotabirika
- Hadithi hii inaitwa Kiboko Mkali. Angalia mchoro kwenye jalada la mbele. (Mchoro unaonesha kiboko akijaribu kujikinga kwa majani ya jamii ya mchikichi.) Unafikiri hadithi itahusu nini?




*Imechukuliwa kutoka: Dixie Elementary Magnet School, Book Jackets; Website*

Angalizo: Wakati maswali haya yanarejelea hadithi ya Kiboko Mkali, maswali hayahaya yanaweza kuwahusu wanyama, watu, mahali au shughuli zinazohusiana na hadithi yoyote ile.

Fanya mazoezi ya kusoma hadithi kwa sauti kabla ya kuitumia kwenye darasa lako. Fikiria jinsi ya kuigiza sauti za wahusika na vitendo utakavyoweza kuvitumia ili hadithi ionekane kama ya kweli. Kama kwenye hadithi kuna michoro, amua namna ya kuitumia utakapokuwa unasoma hadithi hii darasani kwako.

Angalia sehemu za hadithi ambazo wanafunzi wanaweza kushiriki mara tu watakapoifahamu hadithi hii. Kwa mfano, katika hadithi moja, Tembo Eddie alijaribu kuigiza vitendo vya wanyama wengine au vitendo vya binadamu na kila mara ashindwapo hulia 'Wah! Wah! Wah! Boo! Hoo! Hoo! Natamani ningejua kitu ambacho ninaweza kufanya!' Unaweza kuandika kiitikio kama hiki ubaoni kwako ili wanafunzi waweze kufuatilia.

Tafuta mahali kwenye hadithi ambapo unaweza kuwauliza wanafunzi baadhi ya maswali ya utabiri kama vile: 'Unafikiri Eddie atafanya nini baadaye?' au 'Kiboko Mkali atatatuaje tatizo lake?'

## Nyenzo-rejea ya 2: Maswali ya kutumia wakati wa usomaji wa kitabu – usomaji wa kwanza, wa pili na wa tatu

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Hapa pana maswali machache unayoweza kuuliza kabla ya kusoma hadithi na wanafunzi na pia mifano ya maswali ya kuuliza baada ya usomaji kumalizika. Aidha pana maswali ya kuwauliza wanafunzi baada ya kuwa wamesoma kitabu mara ya pili au zaidi.

**KIPINDI CHA KWANZA CHA USOMAJI**

**Kabla ya usomaji**

1. Je, jalada linakufanya upende kusoma hiki kitabu? Kwa nini? au kwa nini hapana? Unafikiri jalada linakuambia kitabu kinahusu nini? Kwa vipi?
2. Niambie kuhusu kile unachokiona katika ukurasa wa kwanza wa hadithi.

**Wakati wa kusoma**

Uliza maswali kuhusu jinsi hadithi ilivyoundwa na jinsi maneno na picha yanavyochangia katika muundo wa hadithi hii.

**Baada ya kusoma**

1. Umependa nini na hukupenda nini kuhusu hiki kitabu?
2. Je, kuna kitu kilichokushangaza kuhusiana na kitabu hiki?
3. Je, kuna ruwaza zozote ambazo umezigundua?
4. Picha gani unayoipenda zaidi? Unaweza kuniambia unaona nini katika picha hii?
5. Unafikiri jalada linafaa kuhusiana na kile kilichotokea katika hadithi hii?
6. Je, maneno au picha zinasisimua? Je maneno yanaeleza hadithi kwa njia mbalimbali? Je, maneno yangekuwa mazuri bila picha? Je, picha zingeendelea kuwa nzuri bila maneno?
7. Je, hadithi imesimuliwa kwa picha au vyote viwili? Je, hali hii ndivyo ilivyo kwa kitabu kizima?

**KIPINDI CHA PILI NA CHA TATU**

(Angalizo: Hivi ni lazima viwe vimepishana kwa wiki kadhaa )

**Kabla ya kusoma**

1. Umeshafikiri kuhusu kile kitabu tangu tulipokisoma kwa mara ya mwisho?
2. Ungependa kukisoma tena?
3. Nisimulie unachokumbuka zaidi kuhusiana na kile kitabu.

**Wakati wa kusoma**

Uliza tena maswali kuhusu muundo wa hadithi na jinsi maneno na picha vinavyochangia katika muundo huu.

**Baada ya Kusoma**

1. Umegundua kitu chochote wakati huu ambacho hukukigundua kabla?
2. Unajisikiaje kuhusiana na hadithi hii baada ya kuisoma tena?
3. Unapofikiria kitabu hiki sasa, ni kitu gani muhimu kuliko vyote kwako kuhusiana na kitabu?

Baada ya kuwa umekisoma kitabu hiki zaidi ya mara moja, je, ungependekeza wanafunzi wengine pia wakisome zaidi ya mara moja na mwalimu wao?

*Imechukuliwa kutoka: Swain, C. Gazeti Msingi la Kiingereza (The Primary English Magazine)*

## Nyenzo-rejea 3: Hadithi

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Andika hadithi ubaoni, lakini usiandike kichwa cha hadithi wala sentensi mbili za mwisho (‘Alitoa shuti – chini kuelekea kulia. Goli zuri!’) ubaoni mpaka sehemu ya mwisho kabisa ya somo lako.

[Kukimbilia utukufu na Mark Northcroft (umri miaka 12 )]

Alikimbia tena na tena. Miguu yake iliuma kama tindikali. Aliweza kusikia waliokuwa wanamfukuzia wakiwa wanamkaribia. Alihisi kuwa asingeweza kukaa nao sana na kwa muda mrefu lakini alijua lazima afanye vile. Hatua zilikuwa zinamkaribia. ‘Haraka! Haraka!’alilia. ‘Siwezi! Siwezi!’ alijibu. Alijisikia nguvu kutoka sehemu fulani ndani ya mwili wake. Sasa alijua kuwa atafanikiwa.

Ghafla mtu alitokea kusikojulikana. ‘Nipate sasa au nisipate kabisa,’ alifikiri.

[Alipiga shuti – chini kuelekea kulia. Goli zuri!]

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Tanbihi**

'Miguu yake iliuma kama tindikali' – Tashbiha hii au ulinganisho huu si rahisi kuueleza lakini unaweza kusema kuwa mwanaume au mvulana huyu alijisikia maumivu katika miguu yake kana kwamba kulikuwa na mchanganyiko wa kemikali iliyokuwa inachemka.

Maswali ya kuwauliza wanafunzi katika maandalizi ya uandishi wa mwanzo na mwisho mbadala wa hadithi hii

1. Unafikiri 'A' ni nani?
2. Unafikiri yuko wapi?
3. Unafikiri nini kitamtokea?
4. Nani 'mwanamume'?
5. Watu gani wengine wanaweza kuwa sehemu ya hadithi hii?
6. Kutakuwa kumetokea nini kabla ya sehemu hii ya hadithi?
7. Nini kinaweza kutokea baadaye?

## Nyenzo-rejea 4: Usomaji kimya endelevu

**Usuli/welewa wa somo wa mwalimu**

Kukuza Usomaji Kimya Endelevu darasani kwako ni muhimu katika kuwahamasisha wanafunzi wako wapende kusoma na kuboresha stadi zao za usomaji. Ili Usomaji Kimya Endelevu ufanikiwe kunahitajika kuwe na mpango makini kabla ya usomaji wenyewe. Utahitaji kukusanya pamoja Nyenzo-rejea kwa ajili ya kusomwa na darasa au kikundi chako. Vitu hivi vinaweza kuwa makala toka magazetini, vitabu, n.k. Unatakiwa uwe mbunifu katika kukusanya vitu hivi na pia kuvihifadhi ili visipotee au visiharibike.

Kama una Nyenzo-rejea kwa darasa zima, unaweza kufanya Usomaji Kimya Endelevu mara moja kwa wiki mwanzo au mwisho wa siku. Kama una idadi ndogo ya Nyenzo-rejea, unaweza kuendesha shughuli ya usomaji kwa kutumia kikundi kimoja kwa kila siku na pia kushirikiana na darasa lako kutengeneza vitabu zaidi vya darasa vya kusoma.

**Maswali ya kuuliza**

Hii ni mifano ya maswali ambayo yanaweza kuulizwa kuhusu aina na viwango mbalimbali vya vitabu vya hadithi, lakini unaweza pia kuwauliza wanafunzi wakupatie maoni mafupi.

1. Kumetokea nini katika sehemu ya kwanza (utangulizi, mwanzo) wa hadithi hii?
2. Kumetokea nini katika sehemu ya kati (wapi pana utata au migogoro katika hadithi hii)?
3. Kumetokea nini katika sehemu ya mwisho (suluhisho)?
4. Je, kuna tatizo linalohitaji kutatuliwa?
5. Nini lengo la mhusika mkuu au wahusika?
6. Kumetokea nini kwa wahusika katika sehemu mbalimbali za hadithi? Wamekumbwa na matatizo gani?
7. Je, umeshawahi kukutwa na jambo kama hilo?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

8. Kama jaribio lao la kwanza halikufanikiwa, je, mhusika mkuu alipata nafasi nyingine ya kujaribu kufikia lengo lake?
9. Mwishoni kimewatokea nini wahusika?
10. Unajisikiaje kuhusiana na hii hadithi? Je, imekufanya utafakari kuhusu maisha yako mwenyewe au ya mtu mwingine? Kama ndivyo, kwa vipi?

**Kutunza rekodi ya usomaji**

Wanafunzi wanapokuwa wanafanya Usomaji Kimya Endelevu ni muhimu kwao kutunza kumbukumbu ya vitabu ambavyo wameshavisoma na kutoa maoni ya kitu gani walikipenda au hawakukipenda kuhusiana na vitabu hivyo. Pia ni njia ya kujua aina ya vitu wanavyovisoma na aina ya vitu vinavyowasisimua. Utunzaji wa rekodi unakueleza wewe kuhusu wanafunzi wamesoma kwa kiasi gani, hasa ikiwa unawahimiza pia kusoma vitabu, magazeti, n.k ambavyo wanavisoma nyumbani au mahali penginepo. Kwa magazeti, unaweza kupendekeza kuwa wayaongeze kama wanayasoma mara kwa mara na waseme wameyasoma mara ngapi. Wanaweza kupendelea kuongeza makala kutoka kwenye magazeti fulani.

Kutunza kumbukumbu kusiwe kwa kuchosha kwani kutawafanya wanafunzi waache kusoma. Inatosha tu kuandika jina la kitabu na la mtunzi na labda mchapishaji kama unataka kukiweka kitabu hiki katika sehemu yake ya kukihifadhia (kama una bajeti). Wanafunzi wanaweza pia kusema kama walikipenda kitabu na kwa nini, na kama wangependekeza kisomwe na wengine.

Kumbukumbu inaweza kuwa ya darasa moja, ambapo kichwa cha kila kitabu cha maktaba kipo juu ya karatasi na kila wakati mtu anaposoma kitabu hiki anatia saini katika orodha hii na kuandika maoni mafupi. Njia nyingine ni kwa kila mwanafunzi kuwa na ukurasa mwishoni mwa daftari lake ambapo kunakuwa na orodha ya vitabu alivyosoma na kila mara anapomaliza kusoma kitabu au kusitisha kusoma kitabu anaandika maoni pembeni mwa jina la kitabu na jina la mtunzi. Itakuwa vizuri kama wanapotoa maoni waandike tarehe ili uweze kuona wanamaliza kusoma kitabu lini n.k.

Ukusanyaji na uoneshaji wa vifaa kwa ajili ya Usomaji Kimya Endelevu

Kama unahitaji kuanzisha maktaba yako mwenyewe ya darasa, hitaji la kwanza ni kukusanya vitabu na magazeti. Yapo mashirika ambayo yanaweza kuzisaidia shule kupata vitabu. Hapa kuna mawasiliano muhimu:

Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania
Katibu Mtendaji
CBP
S.L.P 78245
Dar Es Salaam, Tanzania simu: (255) 22-2760750
nukushi: (255) 222-761562
baruapepe: cbp@raha.com

Chama cha Kimataifa cha Usomaji
Makao Makuu
800 Barksdale Rd
S.L.P 8139
Newark, DE 19714-8139
Marekani
simu: +1 302-731-1600
Nukushi: +1 302-731-1057 baruapepe: pubinfo@reading.org

Huduma za Maktaba Tanzania
Mkurugenzi Mkuu
S.L.P Box 9283
Dar es Salaam
simu: (255) 22 2150048 9 baruapepe: tlsb@africaonline.co.tz

Kwa taarifa zaidi juu ya Usomaji Kimya Endelevu, wavuti hii inaweza kukusaidia:

www.trelease-on-reading.com

Wakati mwingine balozi za nchi za nje au mashirika yanayohusiana na balozi hizi, kama vile British Council, zinaweza kutoa mchango wa vitabu. Mashirika ya kutoa huduma kama vile Rotary Clubs pia hukusanya na kutoa mchango wa vitabu. Kama huwezi kuwasiliana na kampuni yoyote kwa ajili ya kuomba msaada, basi jaribu kuwaomba wenzako na rafiki zako wakupatie vitabu na magazeti ambayo watoto au wanafamilia wao wameshamaliza kazi nayo. Baadhi ya shule zinawaomba wazazi wawasaidie walimu kuendesha shughuli ya kuchangisha fedha na kisha wanazitumia fedha hizo ambazo zimechangwa kununulia vitabu. Nyenzo- rejea Muhimu: Kuwa mwalimu mbunifu katika hali zenye changamoto inatalii zaidi jambo hili.

Mara tu utakapokuwa na vitabu na magazeti ya kuwatosha wanafunzi wote darasani kwako kwa usomaji binafsi wa wanafunzi, unatakiwa utafakari namna ya kuvitunza vifaa hivi ambavyo ni vya thamani. Kama una shubaka, au unaweza kujitengenezea shubaka (au kutengenezewa na mtu mwingine), unaweza sasa kutandaza vitabu na magazeti hayo ili kuwavutia wanafunzi. Mashubaka yanaweza kupangwa pembeni au nyuma ya darasa lako. Ndani ya daftari la mazoezi andika vichwa vya habari vya vitabu na magazeti ili uendelee kuvifuatilia. Mwisho wa kipindi cha Usomaji Kimya Endelevu, kuwa makini katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wanarudisha vitabu kwenye shubaka.

Kama huna mashubaka, hifadhi vitabu na magazeti hayo kwenye maboksi. Unaweza kuwatumia baadhi ya wanafunzi kama watunzaji wa vitabu kwa kukusaidia kugawa vitabu kila kipindi cha usomaji kinapoanza na kuvihifadhi kwenye maboksi baada ya kipindi kumalizika.

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 3: Njia za Usomaji na upokeaji wa taarifa za matini

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kujiongezea stadi za uulizaji maswali ili kuwasaidia wanafunzi kutumia kwa njia inayofaa taarifa za matini

**Maneno muhimu:** taarifa za matini; ufahamu; muhtasari; maswali; tathmini

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Kujiongezea uwezo wa kutunga maswali na kazi ambazo zinahimiza usomaji wa matini kwa makini na majibu binafsi;
- Kugundua njia za kufundisha wanafunzi namna ya na kuandika juu ya taarifa zinazotolewa kwa muundo tofauti;
- Kuwasaidia wanafunzi kuendeleza stadi zao zinazohitajika kufupisha matini;
- Kutumia njia hizi kutathmini ujifunzaji.

## Utangulizi

Katika 'muda wa taarifa' sote tunahitaji kuweza kusoma na kushughulikia taarifa ziwasilishwazo katika miundo mbalimbali. Kusoma taarifa kutoka katika jedwali au mchoro kunahitaji stadi tofauti ukilinganisha na usomaji wa hadithi.

Ukiwa mwalimu, kazi yako ni kuwasaidia wanafunzi kuelewa wanachokisoma, kufanya muhtasari wa mawazo muhimu ya matini na kutoa maoni yao. Ingawa ni muhimu kwa wanafunzi kuweza kuandika majibu ya maswali kuhusu walichosoma, wengine watatoa kazi bora zaidi kama watapewa nafasi ya kuonesha walichoelewa kwa kutumia shughuli nyingine, k.m. kutengeneza mabango au chati.

Sehemu hii inapendekeza njia za kuwasaidia wanafunzi kuimarisha stadi za ufahamu na muhtasari.

## Somo la 1

Mazoezi ya ufahamu ni ya kawaida sana, lakini yanasaidiaje stadi za usomaji wa mwanafunzi?

**Uchunguzi kifani 1** inaonesha kuwa unahitaji kufikiri kwa makini hasa kama kweli maswali ya ufahamu katika usomaji wa vitabu yanasaidia kujua wanachoelewa wanafunzi kutokana na usomaji huo. Unahitaji kutunga maswali au shughuli ambazo zinahitaji wanafunzi kusoma taarifa za matini kwa uangalifu. **Shughuli 1** inakuonesha mifano ya kujaribu na kuitumia wakati unapotunga maswali yako na shughuli nyinginezo. **Nyenzo Rejea Muhimu: Kutumia maswali ili kusaidia kufikiri** inakupa mawazo zaidi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kufiria upya kuhusu 'ufahamu katika usomaji'

Katika warsha huko mjini Lusaka, Zambia, walimu wa Kiingereza kama lugha ya nyongeza walisoma matini ambayo haina maana na kujibu maswali kuhusu matini hiyo. Sentensi ya kwanza katika matini hii ilikuwa: **'Some glibbericks were ogging blops onto a mung'** na swali la ufahamu lilikuwa nani alikuwa **'ogging blops onto a mung?'** Kila mwalimu alijua jibu **'some glibbericks'** . Katika majadiliano yao, waligundua kuwa wangeweza kutoa jibu sahihi kwa sababu walijua kuwa katika Kiingereza **'some glibbericks'** ilikuwa ni kiima cha sentensi. Hawakuhitaji kujua nani au 'glibberick' kilikuwa ni kitu gani ili kutoa jawabu!

Baada ya majadiliano, walifanya kazi katika vikundi, ya kutunga maswali na kazi nyinginezo ambazo zingewaonesha kama wanafunzi wanaelewa au hawelewi matini iliyotumika katika kazi hizi. Walijifunza kuwa maswali yasiruhusu wanafunzi kunakili tu taarifa ya sentensi moja katika matini.

Walitayarisha kazi ambapo wanafunzi walijaza jedwali, walitengeneza bango au kutayarisha muhtasari wa kutumia katika mdahalo kama njia ya kuonesha walichojifunza kutoka katika matini waliosoma.

Walitafakari kuwa maswali waliyouliza na shughuli nyingine walizotayarisha zilimaanisha kuwa waliweza kutathmini welewa wa wanafunzi.

## Shughuli ya 1: Kufahamu na Kupokea taarifa za matini

Soma **Nyenzo rejea 1: Matini kuhusu takataka** . Toa nakala za makala na kazi au andika aya na kazi ubaoni.

Zifunike.

Kabla ya wanafunzi kusoma makala, uliza maswali ya utangulizi. Maswali yako yawasaidie wanafunzi kuoanisha wanayoyajua na taarifa mpya iliyomo katika matini (Angalia **Nyenzo rejea 2: Maswali ya utangulizi** ). Kama wanafunzi ni wenye umri mdogo au unahitaji kuwasomea matini, unaweza kuandika majibu yao ubaoni.

Baada ya hapo, funua makala na kazi ulizotayarisha, na kuwataka wanafunzi wasome makala hiyo kimya na kuandika majibu ya kazi hizo. Watakapokuwa wamemaliza, kusanya vitabu vyao na tathmini majibu yao

Rudisha vitabu na /au toa maoni yako kwa darasa zima kuhusu waliyofanya vizuri na jadili matatizo yoyote waliyokumbana nayo. Angalia majibu ya kazi hii yaliyopendekezwa katika **Nyenzo rejea 1** )

Katika somo linalofuata, watake wanafunzi wafanye kazi katika makundi madogo madogo kutengeneza bango linalokataza utupaji ovyo wa takataka na lioneshe darasani (Angalia **Nyenzo rejea 3: Mabango mazuri** ).

## Somo la 2

Fikiria taarifa mbalimbali za matini ulizokwisha soma. Taarifa hizi ama zikiwa katika kurasa za vitabu, au katika vipeperushi vya matangazo, au katika skirini za kompyuta, mara nyingi huambatanisha vielelezo,chati, grafu, michoro, picha au ramani. Kufanikiwa kama wasomaji, wewe pamoja na wanafunzi wako mnahitaji kuelewa jinsi maneno, tarakimu na sanamu zionekanazo (kama picha au michoro) zinavyofanya kazi pamoja kuwasilisha taarifa. Sasa waandishi wengi wa elimu wanasisitiza umuhimu wa vielelzo vya kufundishia kusoma na kuandika. Kujifunza jinsi ya kusoma na kuitika picha na michoro ni sehemu mojawapo ya kujua kusoma na kuandika. Kusoma na kuitika michoro, grafu na vielelezo ni njia nyingine. Chati ya pau na pai ni baadhi ya chati rahisi kuelewa na kutengeneza ili kufanya muhtasari wa taarifa.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutengeneza chati ya pai kuwasilisha namba ya tarehe za kuzaliwa za wanafunzi kwa kila mwezi

Mwalimu Maria Mutagwa anapenda kuwafanya wanafunzi wake wa Darasa la 6 kujisikia vizuri. Darasani kwake ana karatasi kubwa ikionesha mwezi na siku ya kuzaliwa kwa kila mwanafunzi. Kila siku ya kuzaliwa ya wanafunzi mmojawapo wanafunzi wenzake huimba wimbo wa “heri ya siku ya kuzaliwa.” Siku moja, mwanafunzi mmoja alitoa hoja kuwa katika baadhi ya miezi wanaimba wimbo huo mara nyingi kuliko miezi mingine. Maria aliamua kutumia hoja hiyo kufanya hesabu na kazi ya maonesho ya kihesabio katika chati za pai.

Kwanza, aliandika jina la mwezi ubaoni na baadaye aliwataka wanafunzi wamweleze ni wanafunzi wangapi walikuwa na siku yao ya kuzaliwa kwa kila mwezi. Aliandika namba mbele ya mwezi husika (k.m. Januari 5; Februari 3, na kadhalika).

Baadaye alichora mduara mkubwa ubaoni na kuwataka wanafunzi kufikiria kuwa hiyo ilikuwa chati ya pai na kwa kuwa walikuwa wanafunzi 60 darasani kutakuwa na sehemu 60 katika chati ya pai, moja kwa kila mwanafunzi.

Sehemu zitaunganishwa kutengeneza vijisehemu (vipande). Kutakuwa na vijisehemu 12, kwa sababu kuna miezi 12 kwa mwaka. Kila kijisehemu kitawakilisha idadi ya wanafunzi waliokuwa na siku ya kuzaliwa katika mwezi husika, lakini kila kijisehemu kitakuwa na ukubwa tofauti. Alianza na mwezi palipoangukia siku za kuzaliwa nyingi. –mwezi wa Septemba. Katika mwezi wa Septemba, wanafunzi 12 walikuwa na siku zao za kuzaliwa.

Wanafunzi walipata wazo haraka la kutengeneza vijisehemu 12 vya ukubwa tofauti ndani ya mduara ili kuwasilisha idadi ya siku za kuzaliwa za kila mwezi kama asilimia ya darasa. Walinakili chati ya pai katika daftari zao na kuchora kila kijisehemu kwa rangi tofauti.

Wanafunzi walizungumzia taarifa nyingine ambazo wangeweza kuziingiza katika chati ya pai na waliamua kutambua wanafunzi wangapi walicheza michezo tofauti, wangapi waliunga mkono kila timu katika michuano ya mashindano ya mpira Tanzania na wanafunzi wangapi wanazungumza lugha tofauti katika sehemu zao.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 2: Kufahamu na kutengeneza chati ya pai

Nakili chati ya pai ya **Nyenzo rejea 4: Chati ya pai ubaoni** .

Waulize wanafunzi kwa nini mchoro huu unaitwa chati ya pai.

Tunga maswali (sehemu b) kuhusu chati ya pai ubaoni na waulize wanafunzi kufanya kazi katika jozi na kuyajibu.

Jadili majibu darasani.

Tumia ubao wako kuwaonesha wanafunzi jinsi ya kubadili majibu haya katika aya kuhusu wikiendi ya Thomas. Watake wanafunzi wako wachore chati ya pai.Kwa kazi ya nyumbani watake wanafunzi kuchora chati ya pai kuonesha jinsi wanavyotumia muda wao wa wikiendi.

Baada ya kukagua kazi za nyumbani, watake wanafunzi wabadilishane chati zao na wenzao na kuandika aya kuhusu wenzao wanavyotumia muda wao wa wikiendi. Umejifunza nini kuhusu shughuli hizi? Utafanya kitendo gani wakati ujao kinachohusiana na shughuli hizi? (Angalia Nyenzo rejea 4 kwa mawazo zaidi).

## Somo la 3

Kujifunza kutafuta na kufanya muhtasari wa mawazo makuu kutoka katika sura za vitabu na vitini vingine kunakuwa muhimu kwa wanafunzi kwa jinsi wanavyopanda madarasa shuleni. Stadi hizi zinahitaji mazoezi kuzimudu.

Shughuli Muhimu na **Nyenzo rejea 5**: matini kuhusu mbuyu inatoa mifano ya njia ya kuwasaidia wanafunzi jinsi ya kufanya muhtasari wa taarifa za matini. Utahitaji kufanya shughuli hiyo mara nyingi. Kwa wanafunzi wakubwa, unaweza kuwaomba wenzako kukuonesha wanafunzi unaowafundisha wanahitaji kusoma nini katika masomo mengine kama vile masomo ya jamii au sayansi. Baadaye unaweza kutumia aya kutoka masomo ya fani ya jamii au vitabu vya sayansi kwa ajili ya kufanya kazi ya muhtasari katika somo la lugha kwa kufuata hatua zilizomo katika Shughuli Muhimu.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kufupisha mawazo muhimu kutoka katika sura za vitabu

Wanafunzi wa darasa la Mwalimu Emmanuel Chadwali walikuwa na wasiwasi kuhusu mitihani inayofuata. Walimwambia kuwa hawelewi walimu wao walimaanisha nini walipowaambia kupitia (kudurusu) sura za vitabu vyao. Emmanuel aliamua kutumia matini ya taarifa kutoka katika kitabu cha Kiingereza ili kuwapa wanafunzi wake baadhi ya mawazo kuhusu jinsi ya kutafuta na kuandika mawazo muhimu ya matini.

Aliwauliza wanafunzi wake kumwambia shabaha ya jedwali la yaliyomo, vichwa vya sura na sura ndogo katika vitabu vyao. Ilikuwa wazi kutokana na ukimya wao kwamba wanafunzi wengi walikuwa hawajawahi kufikiria jambo hilo. Wachache waliweza kusema kuwa majedwali haya humsaidia msomaji kupata mawazo kuhusu mada muhimu za kitabu. Emmanuel aliwaambia wanafunzi kuwa ili kusoma tena sura, wanapaswa kuandika vichwa vya habari katika ukurasa, wakiacha nafasi kati ya kichwa kimoja na kingine, wafunike daftari zao na kujaribu kuandika mawazo muhimu katika yale waliyosoma.

Baadaye, wanapaswa kucheki maelezo yao waliyoandika dhidi ya mawazo yaliyomo katika kitabu na kufanya masahihisho katika maandishi yao kwa kuongezea chochote muhimu walichosahau au wafute kile ambacho wameandika kwa makosa. Emmanuel alisema kuwa wanafunzi wengine hupendelea kuandika mawazo yao kwa njia ya michoro ya ramani ya mawazo ambapo kuna uhusiano wa mawazo muhimu. (Angalia **Nyenzo rejea 5** **na** **Nyenzo-rejea Muhimu: Kutumia ramani ya mawazo na**)

Mwisho, aliwakumbusha kuwauliza walimu wao kuelezea chochote ambacho hawakukielewa. Emmanuel aliwaelezea pia jinsi alivyoandika kumbukumbu kuhusu mambo ya wanafunzi wake aliyoyagundua na ujifunzaji wao ili kumsaidia kupanga masomo zaidi.

## Shughuli muhimu: Kuboresha stadi za kuandika muhtasari

Kabla ya somo , nakili matini kutoka **Nyenzo rejea 5**katika mbuyu au iandike ubaoni. Jaribu shughuli hizo kabla.

Kwa kuwaonesha wanafunzi kurasa za magazeti na majarida, waulize kwa nini matini yana vichwa vya habari na yanawaambia nini wasomaji wake.Watake wapendekeze kwa nini vitabu vyao vina vichwa vya habari na vichwa vidogo vya habari.

Watake wanafunzi wasome matini ya taarifa kuhusu mbuyu na kufanya kazi katika jozi kuamua ni aya zipi zinajadili mada ileile. Watake waandike kichwa cha habari kinachofupisha aya kwa kila mada. Watake baadhi ya wanafunzi wako kusoma kwa sauti vichwa vyao vya habari na kuviandika ubaoni.

Kubalianeni ni vichwa vipi bora vya habari kwa kila aya vinavyohusu mada ileile. Viache vichwa vya habari bora ubaoni ukiacha nafasi kwa kila kimoja. Watake wanafunzi washauri mawazo muhimu kutoka kwenye aya na kuyarekodi. Waonesha wanafunzi jinsi ya kuhusisha vichwa vya habari na mawazo muhimu katika ramani ya mawazo ili kuwasaidia kukumbuka kuhusu mbuyu.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea ya 1: Matini kuhusu takataka

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

**Takataka**

Takataka ni aina ya vitu vilivyoachwa au mabaki ya vitu visivyofaa ambavyo watu hawaviweki mahali pake, kama vile kwenye pipa la takataka. Watu ambao wanadondosha takataka kama vile ganda la tunda au kopo tupu kwenye udongo wana hatia ya kuchafua mazingira. Wakati mwingine tunawaita watu hawa "wadudu waharibifu".

**Takataka hazitokei tu**

Watu ndio wanaohusika na takataka. Takataka kama kipande cha karatasi inayofungia chokoleti, si takataka kama kitatupwa katika pipa la takataka. Kinakuwa takataka kama kitatupwa ovyo kwenye ardhi, anakiacha

kikielea kwenye ardhi ambapo amekuwa akikaa au anakitupa nje ya dirisha.

**Takataka zinaweza kuleta madhara kwa watu**

Glasi zilizovunjika na vipande vya mabati vyenye ncha kali ambavyo vimeachwa katika sehemu ambazo watu wanapita- na hasa watoto wadogo wanapochezea- vinaweza kuwakata. Sehemu hizi zilizokatwa zinaweza kuleta maambukizo ya hatari. Takataka za matunda na mboga kuna wakati huteleza na kama watu wakizikanyaga wanaweza kuanguka na kuvunja mguu au mkono. Takataka zinaweza kuleteleza ajali barabarani wakati madereva wanapotaka kuendesha magari yao au malori kuepuka vifaa vyenye ncha kali vinavyoweza kupasua matairi ya magari yao. Mifuko ya plastiki na vipande vya mbao hupeperuka mbele ya kioo cha mbele cha gari na huzuia madereva kuona vizuri.

**Takataka zinaweza kuwa hatari kwa wanyama na ndege**

Vipande vya glasi na makopo vinaweza kukata miguu au midomo ya wanyama wafugwao au wa porini wakati wakiwa machungani. Nyavu za nailoni za kuvulia zinazotupwa ardhini au kwenye maji zinaweza kusokota midomo au miguu ya ndege na zinaweza kusababisha vifo vyao kwa sababu hawawezi kutembea au kula. Wanyama wa baharini, kama vile sili na papa, wanaweza kunaswa katika nyavu chakavu za kuvulia. Kama hawakujinasua watakufa.

**Hatari za plastiki**

Takataka za plastiki zinaleta matatizo kwa samaki, ndege na watu. Katika mito na baharini, zinaweza kuleta madhara kwa samaki kwa sababu wanaweza kukanaswa na kushindwa kutoka. Takataka zilizoko ufukoni mwa bahari zimesababisha vifo vya shakwe wa baharini. Hata mifuko ya plastiki, ambayo huwekwa mboga na matunda, inaweza kuwa hatari kwa ndege. Ndege hawa huingia ndani yake na wanashindwa kupata njia ya kujitoa kwa kuwa plastiki ni ngumu. Vipande vya plastiki au mifuko ya plastiki inaweza kujipenyeza kwenye injini za boti na zinaweza kusababisha injini kutofanya kazi.

Kama tunataka kuweka nchi yetu katika hali ya usafi na inayopendeza na kuwalinda watu wetu na wanyama, lazima tuache kutupa takataka ovyo. Si vigumu kutupa kopo, chupa, mfuko wa plastiki au kipande cha karatasi kwenye pipa la takataka badala ya kuvitupa ardhini.

**Kazi za uandishi kuhusu Takataka**

Orodhesha aina saba za takataka zinazotajwa katika makala (kujibu swali hili kwa uhakika wanafunzi wanahitaji kutafuta taarifa katika aya mbalimbali, kwa hiyo wanapaswa kusoma kwa makini).

Fafanua maana ya takataka. (wanafunzi wanaweza kunakili jawabu kutoka katika aya ya kwanza ya matini bila kujua maana ya neno hilo lakini swali linalofuata linaweza kukusaidia kujua welewa wao kwa sababu unawataka watumie neno au maneno kutoka kwenye lugha wanazozifahamu - kwa wanafunzi lugha yao ya awali.)

Ni neno lipi (au maneno yapi) yanayotumika kwa neno takataka katika lugha nyinginezo unazozijua.

Orodhesha aina tatu za takataka ambazo zina madhara kwa ndege. (Ndege wametajwa mara nyingi katika aya, sio tu katika aya yenye kichwa cha habari kinachoelezea ndege. Wanafunzi wanahitaji kutafuta kila rejeo kuhusu ndege na hivyo kuhusisha tofauti hii na tofauti mbalimbali za takataka na matatizo yayosababishwa na takataka hizo.

Kwa maneno yako mwenyewe fafanua njia tatu ambazo watu wanaweza kudhurika nazo. (Wanafunzi watumie vichwa vidogo kuwaelekeza na wajaribu kuelezea maudhui ya aya katika maneno yao wenyewe badala ya kunakili kutoka katika aya. Hii itakusaidia kung'amua kama wameelewa walichosoma).

Unakubaliana na mwandishi kuwa si vigumu kutupa takataka katika pipa la takataka? Toa sababu za jibu lako. (Hili ni swali linalohitaji maoni ya wanafunzi binafsi kutafakari na kuelezea maoni yao).

Pendekeza kinachoweza kufanywa kuhusu mazao ya takataka kama vile vichupa, karatasi, plastiki, maganda ya matunda na mboga mboga (hili nalo ni swali linalohitaji majibu binafsi na linahimiza majadiliano darasani kuhusu mada za mzunguko wa mazingira).

Zingatia kuwa majibu ya swali la 1 mpaka la 5 yanahitaji wanafunzi wasome matini kwa uangalifu wakati swali la 6 hadi la 7 yanawahitaji kutumia maoni yao.

**Majibu ya kazi za kuandika**

Maganda ya matunda na mbogmboga, vichupa, makopo, plastiki, neti za kuvulia, makaratasi, vipande vya mbao.

Takataka ni vitu visivyohitajika ambavyo watu hawaviweki katika mahali pake panapohitajiwa (kama vile katika pipa la takataka).

Maneno yatokanayo na lugha zinazotumika darasani mwako.

Nyavu za nailoni za kuvulia, mifuko ya plastiki, vikapu vya kusuka na mifuko ya matunda.

Watu wanaweza kujikata kutokana na chupa zilizovunjika au makopo yenye ncha kali. Watu wanaweza kuteleza kutokana na takataka za matunda na mbogamboga na wanaweza kuvunja mikono au miguu. Watu wanaweza kupata ajali za barabarani wakati madereva wakitaka kukwepa takataka barabarani au ikiwa hawawezi kuona kwa sababu ya takataka zilizopeperushwa katika kioo cha mbele cha gari. Watu wanaosafiri baharini na boti wanaweza wasifike salama nchi kavu kama injini ya boti imeharibiwa na palastiki. (Njia nne zimeelezwa hapa.) Hili ni swali ambalo wanafunzi wahimizwe kutoa maoni mbalimbali. Kwa mfano, haiwezekani kuweka takataka katika pipa la takataka kama hakuna mapipa hayo katika uwanja wa shule au mitaani.

Kazi zinakupa wewe na wanafunzi nafasi ya kujadili njia mbalimbali za kutumia tena bidhaa ambazo zinakuwa takataka. Kwa mfano, maganda ya mbogamboga na matunda yanaweza kufanywa lundo la mbolea au kuwekwa moja kwa moja katika udongo shambani ili kurutubisha udongo. Plastiki zinaweza kusukwa katika mikeka au mazulia. Katika baadhi ya majiji na miji vipande vya chupa, kopo, na karatasi au vipande vya mbao vinaweza kuchukuliwa katika sehemu ambapo vinakusanywa na kutumika upya na watu wanaweza kulipwa kwa takataka wanazo kusanya na kuzipeleka katika mahali husika.

*Imetokana na Taitz, L. et al New Successful English, Learner's Book, Oxford University Press*

## Nyenzo-rejea ya 2: Maswali ya utangulizi

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Uliza maswali haya kabla ya kuanza kusoma ili kuwasaidia wanafunzi kuhusisha yale wanayoyajua na yale watakayosoma katika matini ya taarifa kuhusu takataka.

Je, kuna aina yoyote ya takataka katika eneo la shule au katika mazingira ya nyumbani?

Takataka hizo zilifikaje hapo?

Kama hakuna takataka, ni sababu ipi ya usafi wa mazingira hayo kuzunguka mazingira ya shule au nyumbani?

Ni neno gani lingine la takataka ambalo linatumika shuleni au mitaani? (kama wanafunzi hawajui, onesha 'takataka' ubaoni au katika nakala ya makala.)

Je, ni matatizo gani yanayoweza kusababishwa na takataka?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea 3: Mabango mazuri

**Usuli/taarifa ya msingi/ welewa wa mwalimu**

Sifa za bango zuri

Karatasi yote inatumiwa.

Maneno yameandikwa kwa herufi kubwa.


Mara nyingi maneno si sentensi zote.

Picha zinapaswa kuwa rahisi, wazi na zenye mvuto (nguvu).

Rangi za maneno na picha zivutie uangalifu.

Nafasi ya maneno na picha katika karatasi lazima zivutie uangalifu. (Hii inaitwa 'muundo' wa bango.)

Mfano wa bango/picha iliyotayarishwa na mtoto nchini Tanzania.




*Imechukuliwa kutoka: Rehydration Project, Website*

Ndama anywe maziwa ya ng'ombe.

Kichanga cha binadamu anywe maziwa ya (mama yake) binadamu.

Hatua za kufuata katika somo la kuchora na kuwasilisha mabango na ni kitu gani wanafunzi wanaweza kujifunza kutokana na shughuli hii.

Waambie wanafunzi kuwa watafanya kazi katika vikundi kuchora bango linaloelezea kutotupa takataka ovyo.

Anza na majadiliano ya darasa zima. Ni kitu gani kinafanya bango kuwa zuri? Ni taarifa zipi zitafaa katika bango ambazo zitawahimiza watu kuacha kutupa takataka ovyo?

Kipe kila kikundi karatasi kubwa au kadi na hakikisha kuwa wana penseli na peni.

Wakati vikundi vinafanya kazi, zungukazunguka darasani kusaidia ikiwa ni lazima na kuzingatia wanafunzi wanavyojifunza.

Wakati vimemaliza kazi, watake kila kikudi kuonesha kazi zao darasani na kuzungumzia kwa nini wametengeneza mabango yao katika hali hiyo.

Yabandike ukutani mabango hayo darasani au shuleni. Wanafunzi wanaweza kuonesha kuwa wanajifunza:

Jinsi ya kufanya kazi kwa kushirikiana katika vikundi vidogo;

Msamiati mpya;

Kuna aina gani za takataka (kwa kuelewa taarifa kutoka katika matini na kwa kutumia ujuzi wao);

Kunaweza kufanyika nini kuzuia kutupa takataka ovyo;

Jinsi ya kuzungumzia mabango yao.

Wanafunzi wameonesha ujifunzaji upi?

Umejuaje?


Ni sehemu zipi wanazohitaji marekebisho?

Utawasaidiaje?

## Nyenzo-rejea 4: Chati ya pai

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

a) Chati ya pai: Jinsi Thomas anavyotumia muda wake wakati wa mwisho wa juma (wikiendi)




taarifa muhimu kulala 30%

kutembelea marafiki 15%

kucheza mpira 15%

kusaidia kazi za nyumbani na shambani 5%

kuangalia televisheni 10% kufanya kazi za nyumbani 2%; kutengeneza gari 5% kumtembelea babu 10%;

kula 8%

b) Maswali kuhusu chati ya pai.

Chati ya pai inatwambia nini? (Jinsi Thomas anavyotumia muda wake wakati wa wikiendi)

Thomas anatumia muda wake mwingi zaidi akifanya nini? (Kulala)

Anatumia muda mchache zaidi akifanya nini? (kazi za nyumbani)

Anafanya nini kwa muda sawa kama aangaliavyo televisheni? (Kumtembelea babu).

Anafanya nini kwa muda awa kama asaidiavyo kazi za nyumbani na shambani? (Kutengeneza magari ya waya)

Wakati akiwa macho, ni mambo gani mawili ambayo Thomas hutumia muda mwingi kufanya? (Kuwatembelea marafiki na kucheza mpira)

Ukitengeneza chati ya pai ya kuonesha unavyotumia muda wako wakati wa wikiendi, Je, chati hiyo itafanana na ya Thomas au itakuwa tofauti? (majibu ya aina mbalimbali yatatokea)

c) Aya kuhusu wikiendi yaThomas

Thomas anapenda wikiendi. Anafurahia kukaa ndani ya kitanda cha joto kwa muda mwingi kuliko asubuhi siku za shule na kula chakula na familia. Anatumia muda wake mwingi akiwatembelea marafiki na kucheza mpira. Anaangalia televisheni na familia yake wakati wa jioni na wakati mwingine anakaa sana usiku. Jumamosi asubuhi yeye na dada zake huwasaidia wazazi kusafisha nyumba au kusaidia kazi za shambani.

Wanapomaliza, dada zake hupendelea kwenda madukani lakini yeye hupenda kuwatembelea marafiki zake au hutumia sehemu ya muda wake akitengeneza magari ya waya na malori ili kumuonesha babu yake anapomtembelea siku ya Jumapili. Kwa kawaida anahitaji kupata wakati siku ya Jumapili jioni kufanya kazi zake za nyumbani.

Baadhi ya taarifa katika aya hii haziwezi kupatikana kutoka katika chati.Waandishi wameongezea vipengele kutokana na ujuzi wao na data iliyotolewa. Unahitaji kugundua hili pamoja na wanafunzi wako. Waulize wanachoweza kusema kutokana na chati na ni vipengele gani vimeongezwa.

d) Mnaweza kujifunza nini wewe na wanafunzi wako kutokana na shughuli hizi.

Kusoma taarifa za chati ya pai.

Kulinganisha kipengele kimoja cha taarifa na kingine kutoka katika chati.

Kutengeneza chati ya pai ili kufupisha taarifa.

Kuelewa kuwa taarifa ileile inaweza kutolewa kwa namna mbalimbali.

Kutumia taarifa kutoka katika chati ya pai ili kuandika aya.

Kujifunza namna ya kueleza muda (k.m. kutumia maneno ‘mara nyingi’, ‘wakati mwingine’).

e) Mawazo kwa ajili ya shughuli nyinginezo

Ili kuimarisha ujifunzaji wa wanafunzi kuhusu chati za pai, wanaweza kutengeneza nyingine- labda kuhusu tarehe za kuzaliwa za wanafunzi au timu za michezo wanazoshabikia au lugha wanazozizungumza. Unaweza pia kuwaonesha njia nyingine za kuwasilisha taarifa kama vile kutumia grafu ya baa au jedwali kama una taarifa nazo. Marafiki zako wanaweza pia kukusaidia.

## Nyenzo rejea 5: Matini kuhusu mbuyu

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Kabla hujaanza Shughuli muhimu, unaweza kutumia Nyenzo rejea 1 kama mfano na kujadiliana na wanafunzi wako jinsi vichwa vidogo vya habari vinavyoweza kufanya muhtasari wa mawazo muhimu.



**Mbuyu**

Mbuyu sio mti wa kawaida. Baadhi ya watu hufikiria kuwa ni mbaya kwa kuwa ni mnene na muda mwingi huwa hauna majani. Unaonekana pia kutukua kwa utaratibu mzuri juu. Kwa hakika baadhi ya watu wanaishi katika sehemu ambazo kuna miti hii wanasema kuwa hukua kinyume matawi yake yakiwa ardhini na mizizi yake ikiwa juu.

Mbuyu unafanya vitu tofauti ukilinganisha na miti mingine. Miti mingi hushiriki mchavuko kwa kusaidiwa na nyuki na ndege ambao huchukua punje za chavua toka mti mmoja hadi mwingine ili miti irutubishwe na kutengeneza maua mengine, matunda au kokwa. Mibuyu husaidiwa na popo. Wakati wa mwanzo wa kiangazi mti huu hutoa maua makubwa yenye petali.

Maua huchanua usiku wakati popo wanapotokea. Popo hufyonza nekta na husafirisha chavua kutoka mti mmoja hadi mwingine katika mabawa yao na mwilini.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Mbuyu huishi kwa muda mrefu. Baadhi ya mibuyu mikubwa inaweza kuwa na umri wa miaka zaidi ya 3,000.

Mbuyu una matumizi mengi. Miaka iliyopita baadhi ya watu wa kabila la Khoi na San wa Afrika ya kusini walitumia mibuyu kujengea nyumba. Waliweka moto ndani ya mti wa mbuyu ili kulainisha sehemu za ndani ya mti, na kutengeneza tundu ambamo waliishi. Pamoja na kuwa na shimo kubwa ndani, mti huo uliendelea kukua.

Ganda la mti lina matumizi mengi. Linaweza kutumiwa kutengeneza zulia, karatasi na uzi. Unyuzi wa ganda unatengeneza kamba ngumu.

Sehemu nyingine za mti zina matumizi mengine. Mizizi ikisagwa, inatengeneza uji laini. Sehemu laini ya ndani ni kinywaji cha wanyama wenye kiu wakati wa majira ya ukame . Mbegu zikivundikwa majini kwa siku kadhaa, zinakuwa dawa za kutibu homa. Majani yakikaushwa na kusagwa, yanatengeneza kahawa nzuri lakini chungu. Majani yakichemshwa yanafanana kama kabeji na yanaweza kuliwa. Nchini Tanzania, wakati mwingine maganda yakisagwa yanatumika kama dawa ya kusugulia meno.

Kuna hadithi nyingi kuhusu mbuyu. Watu wa Venda Afrika ya kusini wanasema kuwa miti hii ilikuwa ni mahali pa maficho ya mizimu. Halafu mungu alikuja na kuchimbua miti hiyo toka ardhini na kuipanda upya kinyume, yaani mizizi juu na matawi chini. Kutokana na kitendo hicho, mizimu haikuweza kujificha katika miti hiyo.

Watu wengine husema kuwa ukifyonza mbegu hutashambuliwa na mamba, na ukinywa kinywaji kilichotengenezwa kutokana na maganda ya mbuyu utakua hadi kuwa mtu mkubwa na mwenye nguvu (cheo.) Mbuyu ni mti wa maajabu. Ni mmojawapo wa miujiza ya Afrika.

**Vichwa vidogo vya habari vilivyopendekezwa kwa ajili ya matini ya mbuyu**

Aya 1: Mbuyu hufananaje?

Aya 2: Jinsi poleni zinavyosafirishwa kati ya miti ya mbuyu?

Aya 3: Maisha ya mbuyu


Aya 4, 5, 6: Matumizi ya mbuyu

Aya 7, 8: Hadithi na imani kuhusu mibuyu

Zingatia: Hakuna taarifa katika aya ya mwisho. Aya hiyo inaonesha angalizo la mwandishi, akitoa maoni yake kuhusu mti huo.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Muhtasari wa ramani ya mawazo ya mbuyu**




*Imechukuliwa kutoka: Ellis, R. & Murray, S. Let's Use English, Learners' Book 5*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 4: Njia za kuwasilisha mtazamo wako

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuwasaidia wanafunzi wako wawe wawasilishi wa mawazo wanaojiamini na makini?

**Maneno muhimu:** hisia binafsi, mitazamo, mdahalo, barua, gazeti, uhusishaji

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Kuwasaidia wanafunzi katika kueleza mawazo yao katika mazungumzo na maandishi;
- Kuimarisha uwezo wako kuwasaidia wanafunzi kuelewa hali za watu wengine, hisia na maoni yao;
- Kutumia majadiliano kuchunguza masuala ya uhusishaji.

## Utangulizi

Sehemu hii inahusika na jinsi tunavyoeleza hisia na kuwasilisha mitazamo yetu. Ni muhimu kuwa walimu na wanafunzi kuweza kutenda hili kwa kujiamini, kwa mazungumzo na kwa maandishi, ili kushiriki katika kutoa maamuzi katika familia, shule na jamii pana. Ukiwa mwalimu, una wajibu mkubwa katika shauri hili. Unahitaji kuweza kutoa hoja kuhusu shauri lako shuleni katika masuala kama nyenzo na njia za kufanya kazi, na pia unahitaji kuwasaidia wanafunzi wako kadiri wanavyokuza stadi hizi.

Ni muhimu kuwa wanafunzi wajihisi wanashirikishwa darasani na katika jamii, licha ya hali zao za kiafya, hali zao za nyumbani au kutojiweza kwa aina yoyote.

## Somo la 1

Sehemu hii inatalii njia za kufanya kazi zitakazowasaidia wanafunzi kuelezea hisia zao na kugundua mawazo yanayohusu mambo mengi, ikiwa ni pamoja na yanayohusu maisha yao. Inazingatia jinsi ya kushughulikia migongano na mikanganyiko kwa njia iliyo bora zaidi.

Mara nyingi, unapoanza mada ambazo zinagusa masuala nyeti, inasaidia kuacha wanafunzi wagundue kwa siri mawazo yao kwanza. Kwanza, kuandika mawazo kuhusu suala kunaweza kusaidia kuchochea fikira. Hii ni mbinu ambayo inaweza kutumiwa kwa mada nyinginezo ili kugundua wanachojua wanafunzi kwanza.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Uandishi ili kueleza hisia na mawazo

Mwalimu Mariam Uledi wa Dar es Salaam, alijadiliana na wanafunzi wake wa darasa la 7 mambo ambayo yanawafanya wajihisi tofauti na/au kutengwa.

Baadaye, aliwataka waangalie picha ya mtoto aliyekaa peke yake wakati wenzake wakicheza ( **Nyenzo-rejea 1: Mtoto 'alitengwa'** ), na kuwataka kuandika kuhusu mtoto huyu.

Aliwauliza pia kama zamani walikwisha jihisi kama watu waliotengwa au wako tofauti na wengine au kama sasa wanajihisi hivyo. Aliwataka waandike kuhusu hisia hizo.

Halafu walicheza michezo ambayo iliwasaidia kupata ujuzi wa hali yamtu mlemavu (Angalia **Nyenzo-rejea 2: Michezo inayowezesha kusaidia kuelewa ulemavu wa viungo)** .

Baadaye, walizungumzia jinsi ulemavu huo unavyoweza kuwafanya watoto kujisikia tofauti na wakati mwingine kuwafanya watengwe na wenzao wa darasa. Walizungumzia juu ya watoto ambao wanaishi na virusi vya VVU/UKIMWI, au wale ambao wazazi wao wamekufa kutokana na ugonjwa wa UKIMWI. Mariamu aliwataka waandikie kuhusu ujuzi wao wakati wa michezo. Walijisikiaje kuwa na ulemavu?

Baada ya haya, kabla ya kuanza mada nyeti, mara nyingi Mariam huwataka wanafunzi wake kuandika au kuzungumza wawiliwawili au katika vikundi vidogo ili kutalii mawazo yao kwanza.

## Shughuli ya 1: Kuandika ili kuibua mawazo na hisia

Wakati wa kuanza mada nyeti na wanafunzi ni vizuri kwanza kutalii mawazo na hisia zao.

Chagua picha, shairi au hadithi ili kuamsha hamasa ya kufikiri kwao. (Angalia mfano mmoja kutoka katika **Nyenzo-rejea 1** ).

Waoneshe/wasome shairi au hadithi na uwatake wafikirie lina maana gani kwao.

Watake waandike au wazungumze na wenzao kuhusu mawazo yao na husisha na hisia zao pia.

Wakumbushe kuwa hakuna mtu yeyote atakayesahihisha au kuhukumu wanayoelezana. Ni kwa ajili yao kwa wakati huo kufikiri juu ya wanayofikiri na kuhisi.

Halafu, jadili pamoja na wanafunzi wanafikiri ni ujumbe upi unapatikana katika picha hizo.

## Somo la 2

Kujifunza namna ya kushiriki katika midahalo kunawasaidia wanafunzi (na walimu) kueleza maoni yao, kusikiliza maoni ya wenzao na kufikiri kwa umakinifu. Unapochagua mada za midahalo darasani kwako, hakikisha unachagua mada ambazo ni muhimu kwa wanafunzi wako ili waweze kueleza maoni yao.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Katika **Shughuli ya 2** utawaeleza wanafunzi wako sheria na kanuni za kufanya mdahalo na kuwasaidia wanapojitayarisha kufanya mdahalo huo. Katika **Uchunguzi-kifani 2,** mdahalo unahusu kushirikishwa darasani. Kwa watoto wadogo, unaweza kuendesha majadiliano rahisi au mdahalo kuhusu masuala kama kutopigana.

**Nyenzo-rejea 3: Muundo wa hotuba za midahalo** na **Nyenzo-rejea 4: Sheria na kanuni za kuendesha midahalo** utakupa mwongozo. Unaweza pia kuziona sheria na kanuni hizi kuwa za manufaa kama ni mwanachama wa chama cha kuendesha midahalo.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutayarisha na kuendesha midahalo

Baada ya mwalimu Mariam Uledi na wanafunzi wake kuandika juu ya 'kutengwa/kutoshirikishwa', walijadili hasa kuhusu watoto ambao hawakuwa shuleni kwa sababu kadhaa. Baadhi ya wanafunzi hawa walikuwa walemavu, wengine hawakuwa na wazazi na walikuwa ndio wanaolea/wanaosimamia familia na wengine hawakuja shuleni kwa kuwa walikuwa masikini kiasi cha kutoweza kununua sare ya shule.

Mariam alianzisha wazo la kufanya midahalo katika darasa, na kuwasilisha mada yenye kichwa kinachosema: ' Darasa hili linaamua kuwa "vijana wote walio nje ya shule", waliotengwa kwa sababu ya vizingiti vya kujifunza, lazima warudishwe shuleni.'

Aliwaweka wanafunzi 36 katika vikundi sita, na akawataka nusu ya vikundi kujadili mawazo yanayounga mkono mada ya mdahalo na nusu kujadili mawazo yanayopinga mada ya mdahalo.

Baadaye aliwapa mwongozo wa kutayarisha hotuba yao (Angalia **Nyenzo-rejea 3**). Kila kikundi kiliandika hotuba yake, ama ya kuunga mkono au ya kupinga mada ya mdahalo, na kumchagua msemaji kutoka katika wanachama wa darasa. Mwalimu Mariam aliziangalia hotuba zao wakati wa muda wa chakula, na akawashauri wazungumzaji jinsi ya kuziboresha. Wakazirekebisha zaidi nyumbani.

Mdahalo ulifanyika siku iliyofuata. Mariamu alifurahishwa na kiwango cha juu cha ushiriki wa wanachama wote wa darasa. Hoja ilipita, na wanafunzi walianza kuwasiliana na watoto ambao hawakuwa mashuleni, na kufanya kazi na walimu wao na mwalimu mkuu ili kuwarejesha shuleni. Mariam aligundua kuwa mdahalo umeleta nafasi nzuri kwa wanafunzi kuendeleza na kueleza hoja zao na kushughulikia suala muhimu la kijamii.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli ya 2: Kufanya mdahalo wa hoja; kueleza maoni

Wafafanulie wanafunzi kuhusu kushiriki katika mdahalo

Changiana mawazo kuhusu mada zinazowafurahisha na wasaidie kujieleza katika muundo wa hoja. Amua mada za mdahalo (Angalia **Nyenzo-rejea 3** ).

Fafanua sheria na taratibu za kufanya mdahalo, kwa kutumia taarifa iliyomo katika **Nyenzo-rejea 4.**

Andika sheria kuu na kanuni/taratibu ubaoni ili wanafunzi wazinakili kwa ajili ya marejeo katika siku za usoni.

Watake wanafunzi watayarishe hotuba za mdahalo katika vikundi na mchague msemaji mmoja kuwasilisha majadiliano yao.

Unaweza kuwasaidia kwa kuwaeleza taarifa ya utangulizi ili waitumie katika hotuba zao.

Hakikisha kama vikundi viko tayari kuanza mdahalo (labda mwishoni mwa wiki) na fuata sheria na kanuni/taratibu.

Watake wanafunzi wakueleze walichojifunza kutokana na tajiriba hii na itumie taarifa hiyo kupanga masomo ya siku za usoni na nafasi za kujadili mawazo.

Kwa watoto wadogo, unaweza kufanya mdahalo na mada zinazohusu shule, kama kwa mfano ni lazima wawe na kanuni za darasa. Unaweza kuwasaidia kujifunza namna ya kupeana nafasi ya kuzungumza na kusikiliza maoni ya wengine.

## Somo la 3

Ni muhimu kujifunza namna ya kueleza hoja kwa uwazi, ukithibitisha mawazo yako. Hii ni stadi inayofaa wakati wa kuandika insha za wanafunzi, lakini pia, unapokuwa mtu mzima, kama unaandika barua kuhusu mada ya mdahalo wa kijamii au wa kitaifa hasa barua ya kuchapishwa katika gazeti.

Barua ya gazetini inaweza kulinganishwa na sehemu ya kwanza ya mdahalo.

Mara nyingi mtu mwingine atajibu barua iliyochapishwa gazetini na atatoa hoja mbadala. Katika **Nyenzo-rejea 5: Mfano wa barua** kuna barua katika gazeti ambayo wanafunzi wanaandika kuhusu masuala muhimu ya kuwaingiza wanafunzi wote shuleni.

**Uchunguzi-kifani 3** na **Shughuli muhimu** inatoa mwongozo wa jinsi ya kufanya kazi na wanafunzi ili watoe hoja kwa njia ya barua.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kujifunza kuandika barua kwa mwalimu mkuu au katika gazeti

Miezi michache baada ya mwalimu Mariam Uledi kutoa wazo la kuwarudisha wanafunzi shuleni, kulikuwa na wanafunzi wageni wawili darasani kwake. Mmoja alikuwa hasikii, na mwingine alikuwa na mkono mmoja. Yeye na wanafunzi walikuwa wanaanza polepole kuwashirikisha darasani, kuzungumza nao, na kuwasaidia bila kuwafanya kujihisi kuwa wao ni 'tofauti' kabisa. Aliwashauri wanafunzi kuandika barua kwa mwalimu mkuu au gazetini kuhusu mada ya umuhimu wa kuwarudisha wanafunzi wote shuleni. Wangeweza kutuma barua yao kwa mwalimu mkuu au katika gazeti la **Nipashe** jijini Dar es Salaam, au katika gazeti la **Tanzania Daima** . Watapaswa kuandika kwa Kiswahili.

Wanafunzi walilipenda wazo hili na walijadiliana kuhusu watakayosema. Waliandika vidokezo vya barua.

Dhamira: Shule zijitahidi kuwarejesha shuleni 'watoto ambao hivi sasa hawasomi.

Sababu.

'Njia za kukabili maoni ya kupinga

Tajiriba yetu.

Kufaulu na changamoto.

Kurudia dhamira.

Mariam aliwaelekeza wanafunzi aina za virai vya kutumia, hasa namba 2 na 3, ambapo walikuwa wakiwasilisha mawazo. Walimuomba mwalimu aliyekuwa na kompyuta kuwachapia kazi yao, na kutuma nakala magazetini (Angalia barua katika Nyenzo-rejea 5 ).

## Shughuli muhimu: Barua kwa mwalimu mkuu au gazetini ili kutoa hoja

Chagua mada ambayo imekwisha jadiliwa na wanafunzi katika mijadala yao na toa hoja ya kutoa mawazo yao katika barua kwa mwalimu mkuu au, kama kuna gazeti la mahali hapo, itume katika gazeti.

Uwatake wabunge bongo, katika vikundi, mambo wanayotaka kuyaandika. Baadaye andika muundo wa barua ubaoni ukitumia vidokezo vilivyomo katika **Uchunguzi-kifani namba 3** (ingawa dhamira yako inaweza kuwa tofauti).

Wanafunzi wanaweza kuandika barua hii katika lugha nyingineyo (k.m. Kiingereza) hivyo wasaidie kuwapa virai vya kutumia katika utangulizi na katika hoja zao (Tazama Nyenzo-rejea 6: Virai vinavyotumika katika 'majadiliano' )

Vitake vikundi kutathmini barua zao na barua za watu wengine, na amua ipi ni bora ya kutuma kwa mwalimu mkuu au katika magazeti (Tazama Nyenzo-rejea 6 kwa maelekezo). Utahitaji kufanya uhariri kabla hujatuma barua, lakini jitahidi kubakiza maneno ya wanafunzi.

Fikiria wanafunzi wamejifunza nini katika kubadili majadiliano ya mdahalo hadi kwenye barua. Kwa watoto wadogo au wale wasiojiamini na wasiokuwa na uwezo wa kuandika, unaweza kulifanya kama zoezi la darasani ukiandika mawazo yao. Tumia shughuli hii kuendeleza msamiati wao katika lugha husika.

# Nyenzo-rejea ya 1: Mtoto 'aliyetengwa'

**Nyenzo ya Mwalimu kwa ajili ya kupanga/kurekebisha na kutumia na wanafunzi**



*Vyanzo vya asili: Umthamo 6, Chuo Kikuu cha Fort Hare, Mradi wa Elimu ya Masafa Marefu*

# Nyenzo-rejea ya 2: Michezo inayohimiza uelewa wa ulemavu wa viungo

**Nyenzo-rejea ya Mwalimu ya kutumia na wanafunzi kwa ajili ya kupanga/ kurekebisha**

Unaweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa baadhi ya matatizo ambayo wanafunzi wenye ulemavu wanayapata katika kucheza michezo kama inayoelezwa hapa chini:

1. Leta shuleni baadhi ya soksi ndefu za zamani au vipande vya kamba au sufu. Wape vifaa hivi wanafunzi na watake kuifunga mikono yao wanayoitumia kuandika nyuma ya migongo yao. Mpe kila mwanafunzi kipande cha karatasi. Waeleze kuwa mchezo huu unahusu kutaka kujua nani anaweza kuandika kwa mwandiko mzuri sentensi ambazo uko karibu kuzitaja kwa haraka. Zisome sentensi hizo na sasa angalia kutatokea nini! Baada ya kumchagua mshindi, jadiliana na wanafunzi wako walivyojisikia wakati wakicheza mchezo huu na hali ikoje kwa wanafunzi wenye ulemavu au wanaopungukiwa mkono, kama hawawezi kuandika, watake kuchora mti.

2. Leta shuleni baadhi ya vipande vya nguo au skafu (au waambie wanafunzi kuleta vifaa hivyo) ili nusu ya wanafunzi hao waweze kufunika macho na vipande hivyo. Lichukue darasa nje. Watake wanafunzi kufanya kazi wawiliwawili. Yule ambaye amefungwa macho yake anatakiwa kutembea akipita katika vizingiti mbalimbali ulivyoweka, huku akiongozwa na mwenzake. Katika zoezi hili unaweza kutumia madawati na viti.
3. Zingatia muda kwa kila kikundi. Kama darasa lako si kubwa sana watake wanafunzi wako wabadilishane majukumu hayo na zingatia muda tena kwa kila kikundi. Mshindi ni kikundi cha wawiliwawili waliomaliza majukumu yote kwa muda mfupi zaidi, bila kujikwaa katika kizingiti chochote. Baada ya hapo, waulize wanafunzi walijisikiaje kwa kufunikwa macho na kumtegemea mwenzao.
4. Leta shuleni manyoya ya pamba ya kutosha kwa kila mwanafunzi ili waweze kuweka manyoya masikioni mwao ili kuwazuia kusikia vizuri. Halafu watake wanafunzi kukusikiliza wakati ukiwapa wanafunzi taarifa ya kuandika. Mshindi ni mwanafunzi wa kwanza kumaliza kuandika taarifa bila makosa. Baadaye waulize wanafunzi walijisikiaje walipokuwa hawasikii vizuri na wangefanya nini kumsaidia mwanafunzi mwenye matatizo ya kusikia.
5. Kama shule yako inaweza, nunua pipi nyingi. Mpe za kutosha kila mwanafunzi ili midomo yao iwe imejaa pipi. Waambie wasimung’unye wala kumeza pipi yoyote bali kumwambia mwenza taarifa uliyoandika ubaoni. Hili ni gumu kulifanya na watagundua inakuwaje unapokuwa na matatizo ya kuzungumza ambayo yanamzuia mtu kusema vizuri. Mwishoni, wanakula pipi hizo!

## Nyenzo-rejea ya 3: Muundo wa hotuba za mdahalo

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

**Maelezo ya hoja**

Bungeni, au katika kamati muhimu, wakati wajumbe wanatoa maamuzi, mmoja anaweza kutoa hoja ya kujadiliwa. Hoja ni tamko kuhusu kitu kinachopaswa kufanywa au kujadiliwa. Mdahalo unatalii sehemu zote za mjadala. Kwa mfano, kama mbunge akisimama na kusema: ‘Natoa hoja kuwa adhabu ya viboko ifutwe,’ wazo hili linajadiliwa na uamuzi unafikiwa, ambao unatoa suluhisho linalotakiwa kutekelezwa au kutotekelezwa.

Taarifa zifuatazo ni mifano ya masuala unayoweza kutumia shuleni. Unaweza kurekebisha hizi kwa kutegemea ukubwa wa darasa lako na umri wa wanafunzi wako.

Wazazi wasitumie adhabu ya viboko kuwafundisha nidhamu watoto. Tunayojifunza nyumbani ni muhimu kuliko tunayojifunza shuleni.

**a) Wanaounga mkono mada ya mdahalo**

Eleza mada: Nakubaliana na hoja kuwa vijana wote walio nje ya shule, wanatengwa kwa sababu ya vizingiti vya kujifunza, warudishwe shuleni.

Fafanua istilahi. Katika hali hii utahitaji kueleza una maana gani unaposema vijana walio ‘nje ya shule’, na vizingiti vya kujifunza. (Hili linapaswa kufanywa na mzungumzaji wa kwanza)

Toa sababu za kuunga mkono mada: k.m. sababu yangu ya kwanza katika kuunga mkono mada hii ni........

*Sababu ya pili, …*

*Sababu ya tatu, …*

Fanya hitimisho ya sababu zako za kuunga mkono mada: *Kwa ufupi au kwa kuhitimisha* ....

Eleza tena mada ya mdahalo: Kwa hiyo narudia tena au kwa hiyo nawasihi nyote kuunga mkono mada ambayo inasema kuwa.......

**b) Wanaopinga mada ya mdahalo**

Eleza msimamo wako kuhusu mada: Napinga mada inayosema kuwa........AU Nawaunga mkono wanaopinga mada kwamba........

Fafanua istilahi. Katika hali hii utahitaji kueleza una maana gani unaposema vijana walio 'nje ya shule', na vizingiti vya kujifunza. (Hili linapaswa kufanywa na mzungumzaji wa kwanza). Wote wanaohusika wanahitaji kukubali ufafanuzi wa istilahi.

Toa sababu zako za kupinga mada: k.m. sababu ya kwanza ya kupinga mada hii ni...

*Sababu ya pili,...*

*Sababu ya tatu, …*

Fanya hitimisho la sababu zako za kupinga mada: *Kwa ufupi au kwa kuhitimisha...*

Eleza tena msimamo wako: *Ninarudia tena AU ninawasihi nyote kutounga mkono mada inayodai kuwa .........*

## Nyenzo-rejea ya 4: Sheria na taratibu za kuendesha mdahalo

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

*Mdahalo ni mashindano, au, labda, ni kama mchezo ambapo wazungumzaji wawili au zaidi hutoa hoja zao kwa nia ya kushawishiana...*

**Kwa nini tunafanya midahalo?**

Kwa kujitayarisha na kushiriki katika midahalo wanafunzi wanajifunza kutumia taarifa kuunga mkono hoja zao. Wanajifunza namna ya kuwasilisha mawazo yao kwa uwazi na kwa ushawishi mkubwa.

Kwa kushiriki katika midahalo, wanajifunza kuelewa mawazo ambayo ni tofauti na yao kwa sababu, wakati wa kufanya mdahalo, wanaweza kujadiliana kwa kutoa hoja kwa jambo ambalo hawakubaliani nalo kikamilifu, na wanapaswa kuelewa mawazo ya wenzao wa timu ya wasiokubali hoja zao.

**Matayarisho**

Wafanya midahalo wazuri wanajitayarisha vizuri. Mdahalo unaofanya darasani unaweza usiwe rasmi, lakini unaweza kuwajenga wanafunzi katika hali inayowafanya wanafunzi wako wafanye mdahalo rasmi katika mashindano.

Kabla ya kuandaa hotuba, wafanya midahalo wanakusanya taarifa nyingi kwa kadri iwezekanavyo, kutoka katika maktaba, magazetini, na kwa kujadiliana na watu.

Wanafikiria hoja zote zinazounga mkono mada yao, na zile zinazopinga hoja yao. Kwa maana nyingine ni kuwa, wanaelewa hoja za wapinzani wao pamoja na hoja zao. Wanajitayarisha kwa maswali yoyote wanayoweza kuulizwa na wapinzani wao, na changamoto zozote zinazoweza kutolewa.

Wafanya midahalo wazuri wanatayarisha hoja zao katika muundo mzuri wa ushawishi. Wanawasikiliza watu wengine wanaofanya mdahalo, ili wajifunze ufundi na stadi za kufanya mdahalo. Wanajiunga na vyama vya kufanya midahalo, na kufanya midahalo mara kwa mara.

**Mchakato**

Kuna timu mbili, kila timu ina wazungumzaji wawili au watatu. Timu moja (chanya) inaafiki hoja, na timu nyingine (hasi) inapinga hoja.

Kuna mwenyekiti, ambaye anaendesha utaratibu.

Hotuba na muda wa hotuba hizo unagawanywa sawasawa kwa timu zote mbili.

Kila mzungumzaji anatoa hotuba upande wake umeandaa kuunga mkono hoja zao.Pande zinazungumza kwa zamu, wakianza na anayependekeza hoja (chanya, hasi, chanya, hasi). Kila mzungumzaji ana muda maalum wa kuzungumza (k.m. dakika tatu au tano)

Baadaye mdahalo unaweza kufunguliwa kwa washiriki wengine, kwa wasemaji kusimama na kutoa hoja zao za kuunga mkono au kupinga mada ya mdahalo. Kila mzungumzaji kutoka upande wa wasikilizaji anapewa muda maalum wa kuzungumza ( k.m. dakika moja au dakika tatu).

Kila timu inaweza pia kuzungumza kwa kujibu hoja za wapinzani wao, baada ya kila timu kupewa muda kidogo wa mashauriano. Hii ina maana kuwa wana nafasi ya kupinga hoja dhidi ya hoja zilizotolewa na wapinzani wao. Kila timu inaweza kupewa nafasi ya kupinga hoja dhidi ya hoja zilizotolewa na wenzao mara moja au zaidi. Nafasi ya kwanza ya kupinga hoja wanapewa wale wanaopinga mjadala na nafasi ya mwisho inatolewa kwa wanaunga mkono mjadala.

**Kanuni muhimu**

Timu inayounga mkono mjadala haitakiwa kubadili hoja zao. Aidha ile inayopinga mjadala nayo pia hairuhusiwi kubadili hoja zao. Wanapaswa kupinga kabisa mjadala licha ya maoni yao binafsi).

Ikiwa mzungumzaji anatoa tamko, wanatakiwa kutoa ushahidi au sababu za kuunga mkono tamko hilo.

Taarifa zinazotolewa katika mdahalo lazima ziwe sahihi.

Wazungumzaji hawaruhusiwi kuleta hoja mpya wakati wa kujibu/kupinga hoja za wenzao.

**Hoja ya utaratibu na hoja ya taarifa**

Yeyote anayehusika na mdahalo anaweza kuingilia kati wakati msemaji akizungumza kwa kunyoosha mikono na kusema kuwa 'anataka kutoa hoja'. (Hii ni 'hoja ya utaratibu'). Hii ina maana kuwa anataka kueleza kuwa moja ya kanuni za mdahalo imevunjwa (k.m. mzungumzaji amezidisha muda wake wa maongezi, au hana ushahidi wa kuthibitisha hoja zake).

Wana-mdahalo wanaweza pia kunyoosha mikono yao wakitaka kutoa 'hoja ya taarifa' (swali au taarifa za ziada wanazoweza kutoa). Msemaji anaweza kuamua kumruhusu mwanachama kuzungumza, lakini halazimiki.

**Uamuzi**

Timu inayoshinda katika mdahalo inaamuliwa na jaji au majaji kwa kutegemea ubora wa mjadala.

Aidha inaweza pia kuamuliwa kwa kupigiwa kura.

Vyanzo vya asili*: Trivium Pursuit, Website.*

## Nyenzo-rejea ya 5: Mfano wa barua- iliyoandikwa na darasa la mwalimu Mariam

**Mfano wa kazi za wanafunzi**

Barua hii ni kwa ajili ya kutumwa katika gazeti, lakini unaweza kuandika barua yako kwa mwalimu mkuu kuhusu jambo jingine ukitaka.

Mhariri

**Nipashe**

Dar es Salaam

Ndugu

**Yah.: Shule ziwalete wanafunzi wanaokaa majumbani**

Katika Tanzania, elimu ya msingi ni bure. Ni kwa ajili ya watoto wote. Lakini bado kuna watoto ambao wamekaa majumbani, bila kusoma. Baadhi wana ulemavu, wengine wana wazazi wao wenye virusi vya UKIMWI, na wazazi wengine ni masikini mno kiasi cha kutoweza kuwanunulia watoto wao sare za shule.

Shule lazima ziwalete watoto hawa mashuleni, ili wapate elimu na wenzao. Kwa nini tunasema hivyo?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kwanza, ni haki yao ya kidemokrasia kuelimishwa. Waziri wa elimu anasema kuwa watoto wote lazima wajumuishwe darasani.

Pili na muhimu zaidi, wahitaji kuwa na marafiki na kuwa sehemu ya maisha.

Baadhi wanasema kuwa walimu hawajui kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu. Wengine wanasema kuwa wazazi hawataki watoto wao kuwa na marafiki 'walemavu' Lakini hatutaki jumuiya yetu iwe ile ya kubagua. Kila mmoja lazima ashughulikiwe kwa namna ileile.

Watoto wanaweza kuwasaidia wenye ulemavu, na kulifanya kuwa jambo jepesi kwa mwalimu.

Darasa la saba katika shule ya msingi Bunge jijini Dar es Salaam iliwakuta watoto wawili wakiwa peke yao nyumbani. Tuliwahimiza kuja shuleni. Kibena alikuwa na mkono mmoja. Tunamsaidia kujifunza kuandika na kucheza michezo. Ni hodari na anajifunza kwa haraka.

Masanja ni mlemavu asiyesikia, lakini akikuangalia midomo yako, anaweza kusikia. Anajitahidi. Pia amekuwa hodari wa kusoma. Tunaweza kumuandikia ujumbe. Tunajifunza mambo mengi kutoka kwa watoto hawa, na marafiki zetu.

Bado ni vigumu kwao, na mwalimu anawapa msaada wa ziada baada ya shule. Kamati ya shule inawasaidia pia kwa kuwanunulia sare za shule. Bado hawana sare za shule.

Tunafurahi kuwa wamekuja darasani mwetu, na tunataka kuziambia shule nyingine kufanya kama tulivyofanya sisi.

Wako

Darasa la 7, Shule ya msingi Bunge

## Nyenzo-rejea ya 6: Vifungu vya utoaji hoja

**Usuli/maarifa ya somo kwa ajili ya uelewa wa mwalimu**

**Vifungu vya mabishano**

Tunasisitiza kuwa ... …

Sababu zetu kwa kusema haya ni: Kwanza, ............Pili,.......Mwisho na muhimu zaidi, ................ …

Katika (jina la gazeti), la (tarehe), (jina la mtu) ameandika kuwa .....AU (jina la mwandishi/mtunzi), katika kitabu chake (jina la kitabu), anasema ... hii inaonesha kuwa.....AU hii inathibitisha kuwa .....

Wengine wanasema kwamba ...... Lakini sisi tunaamini kuwa.......

Uzoefu wetu umeonesha kuwa.........

**Maswali ya tathmini**

Je, barua inaanza kwa kueleza waziwazi hoja, au majadiliano? Inawasilisha hoja za kuunga mkono kauli hii?

Inajumuisha baadhi ya taarifa ambazo zinahusisha hali ya mazingira ya mahali panapohusika au matukio na kuyaeleza kibinadamu?

Inaeleza hoja tena, kwa uhakika zaidi, katika aya ya mwisho?

Je, ina muundo mzuri, imegawanywa katika aya, kila aya ikiwa na wazo kuu?

Je, ni sahihi, bila kuwa na makosa ya sarufi, tahajia au uakifishi?

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 5: Njia za kuwa msomaji na mwandishi makinifu

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuendeleza stadi za umakinifu wa kufikiri wa mwanafunzi wakati wa usomaji na uandishi

**Maneno muhimu:** usomaji makinifu; uandishi makinifu; maoni/mitazamo; uulizaji (maswali); tathmini

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Kutumia maswali kuwasaidia wanafunzi wako kuwa wasomaji makinifu wa matini mbalimbali;
- Kuwasaidia wanafunzi wako kubuni na kuandika hadithi, matini na barua za taarifa ambazo zinatokana na matini walizosoma kwa umakinifu na hivyo kukuza stadi za kufikiri;
- Kutumia njia mbalimbali za kutathmini ujifunzaji.

## Utangulizi

Waandishi wote - wawe wa hotuba za kisiasa, matangazo ya biashara, makala za magazeti, vitabu vya shule au vyuo (vikuu), hadithi za watoto, au aina nyingine yoyote ya matini - huandika kwa kuzingatia mtazamo fulani na kwa nia fulani. Ni muhimu kuweza kubainisha mtazamo wa mwandishi na kuamua kama unakubaliana nao au hukubaliani nao.

Kufikiria uzoevu wako na imani zako na uliyojifunza katika masomo yako kunaweza kukusaidia kuuliza maswali makinifu kwa kila kitu unachosoma. Itakusaidia kama mwalimu kukumbuka kuwa wanafunzi wako wanaweza kuwa na mawazo ambayo ni halali kama yako. Ukiwafundisha wanafunzi wako kuuliza maswali kuhusu wanachosoma na kufikiria misimamo mbalimbali, utakuwa unawasaidia kuwa raia wanaofahamu kwa makini mambo mengi.

Unaweza kuanza jambo hili hata kama wanafunzi ni wadogo. Ukiwa unawasomea hadithi, wahimize wajadiliane yapi wanayakubali na yapi hawayakubali.

Shughuli tatu katika sehemu hii ni mifano ya njia za kuwasaidia wanafunzi wako kuwa wasomaji na waandishi makini wa matini.

## Somo la 1

Wakati wewe na wanafunzi wako mnasoma hadithi, unaweza kuwasaidia kutambua nani amehusishwa katika hadithi na amehusishwaje, na nani hakuhusishwa.

Unaweza kuwasaidia kuona jinsi mandhari ya hadithi (shule, kijiji, mji, n.k.) yanavyoelezwa. Unaweza pia kuwasaidia wanafunzi kwelewa mtazamo au msimamo wa mwandishi, kufikiria kama kunaweza pia kukawa na maoni mengine na, kama yapo, ni yapi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Unapofanya hivyo na wanafunzi, unawasaidia kuendeleza stadi za kufikiri na stadi za kuuliza maswali makinifu. Utajifunza pia wanafunzi wanapendelea nini na misimamo yao ni ipi. Unaweza kutumia njia hii kutimiza zaidi matakwa yao.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kusimulia hadithi kutokana na misimamo tofauti

Mwalimu Pinkie Motau wa Soweto, Afrika ya Kusini ana makasha matatu ya vitabu vya hadithi darasani mwake. Wakati mwingine anasoma vitabu hivi kwa darasa lake la 4 na wakati mwingine wanafunzi wanasoma wenyewe. Hadithi zinahusu watoto na familia, zinahusu wanyama na zinahusu viumbe vya kufikirika kama vile mazimwi.

Siku moja alipokuwa akisoma hadithi kuhusu mamba, Sizwe alisema alijisikia vibaya kuhusu mamba kwa kuwa kila wakati mamba alionekana 'mbaya'. Wengine walisema kuwa hii ilikuwa sahihi kwa kuwa mamba ni mnyama hatari, lakini wengine walisema hii haikuwa halali kwa sababu mamba wanapaswa kujilinda kama wanyama wengine wanavyofanya. Hali hii ilimpa wazo mwalimu Motau. Aliwataka darasa kutoa maoni ya jinsi hadithi ingesimuliwa kutokana na msimamo wa mamba mwenyewe. Wanafunzi walikanganyikiwa, kwa hiyo akasema, 'Jifikirie kuwa wewe ni mamba katika hadithi hii. Unataka kuwaambia nini wanyama wengine kuhusu hali yako?' Swali hili liliwasaidia wanafunzi kutoa maoni. Baada ya majadiliano darasani, mwalimu Motau aliwataka kufanya kazi katika vikundi vya watu watanowatano, kuchora na kuandika hadithi ambayo itaonesha kuwa mamba ni mnyama 'mzuri'.

Kwa kubadilishana mawazo, waliandika hadithi na kuchora picha na vielelezo kuhusu hadithi hizo zenye ubunifu wa hali ya juu.

Wakati mwalimu Motau alipokuwa akisoma hadithi hizo, alifikiria maneno na michoro 'vilimwambia' nini kuhusu uwezo wa wanafunzi wa kubuni hadithi kutumia msimamo wa mamba mwenyewe. Siku iliyofuata, alisoma hadithi za kila kikundi kwa sauti na kuonesha picha na vielelezo. Baada ya kusoma kila hadithi, aliliambia darasa zima kikundi kimefanikiwa katika mambo yapi, na pia aliwataka wanafunzi kutoa maoni yao kuhusu maandishi na picha za kila kikundi.

Mwishowe, hadithi hizo zilitengenezwa kitabu kwa ajili ya maktaba ya darasa.

## Shughuli ya 1: Kuwa msomaji makinifu wa hadithi

Tafuta hadithi ambapo wahusika, mandhari na matukio vimeandikwa na kuchorwa kutokana na msimamo mmoja (k.m. wanyama wazuri, wazazi wa mwanafunzi mtukutu).

Isome hadithi hii kwa wanafunzi darasani, ukihakikisha kuwa umewaonesha michoro.

Waulize maswali yanayowachochea kufikiri kimakinifu kuhusu hadithi ilivyoandikwa na vielelezo vilivyochorwa. (Angalia **Nyenzo-rejea 1: Uulizaji wa maswali** kwa mifano ya maswali ambayo ungetumia.)

Baadaye, watake wanafunzi kufanya kazi katika vikundi vya wawiliwawili kwa kuandika barua kwa mhariri, wakifafanua wanachotaka/wasichotaka kuhusu jinsi barua waliyosoma ilivyoandikwa na vielelezo vilivyochorwa. Andika barua ubaoni na jadili mawazo na wanafunzi kabla ya wanafunzi katika vikundi vyao kuanza kuandika barua (angalia **Nyenzo-rejea 2: Vidokezo vya barua kwa mwandishi** ) au kwa watoto wadogo iandike rasimu hiyo pamoja.

Wanafunzi wamefanikisha nini katika masomo haya ya usomaji na uandishi makinifu? Umejuaje? Una ushahidi gani?

Wamefanya kitu chochote kilichokushangaza, kilichokupendeza au kilichokuchukiza? Kuna kitu ambacho ungefanya tofauti kama ungekuwa unafundisha masomo haya tena?

## Somo la 2

Hadithi zote husimuliwa kwa kuzingatia msimamo fulani. Maoni yetu kama waandishi na wasomaji yanaweza kuathiriwa na hali mbalimbali; maoni haya hutegemea kama ni sisi vijana au wazee, wanaume ama wanawake, ni wanachama wa chama fulani cha siasa, ni waumini wa dini Fulani, tunafurahia shughuli fulani, tuna afya njema au afya mbovu, tunafanya kazi au hatufanyi kazi, n.k. Ni muhimu wanafunzi wakajifunza kuwa hadithi zinaweza kuhadithiwa kwa njia mbalimbali kwa kuhusishwa na msimamo fulani au kutohusishwa nao. Ni kweli pia kuwa katika maisha halisi kuwa kuna njia zaidi ya moja ya kulitazama suala fulani na njia mbalimbali za kutatua tatizo.

Unaweza kuwasaidia wanafunzi wakajifunza hili kwa kuwapa nafasi ya kusimulia hadithi ileile au hadithi inayofanana kutokana na mitizamo tofautitofauti au kwa kubadilisha hadithi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kumbadilisha ‘mhusika wa nje’ kuwa mhusika mkuu katika hadithi.

Mwanafunzi mmojawapo aitwaye James katika darasa la 6 la Mwalimu Fortunate Mabuso, ameumia sana kutokana na ajali ya gari na angeweza kutembea kwa magongo. Siku moja, alimwambia mwalimu Mabuso kuwa alijisikia vibaya kwa kuwa hadithi zote kuhusu wavulana zilieleza namna walivyofurahia shughuli ambazo hawezi kuzifanya. Mwalimu Mabuso alighadhabika kwa kuwa hakuwahi kulifikiria jambo hili. Alimuuliza alikuwa akifanya nini wakati akiwa nyumbani na akagundua kuwa alikuwa mwanamuziki hodari ambaye alijua kupiga ngoma na filimbi ya chuma. Alimuuliza anaweza kucheza kwa kutumia filimbi hiyo darasani. Kwanza alikuwa na aibu kuhusu jambo hili lakini mwisho akakubali kuwa anaweza.

Katika somo lake lilifuata la Kiingereza, Mwalimu Mabuso aliwaambia kuwa anataka kuwapa mawazo ya kuandika hadithi. Alimwomba James kuwachezea ngoma. Wanafunzi walishangaa na kufurahia uhodari wa James.

Mwalimu Mabuso aliwataka wafikirie hadithi ambapo James, mwanamuziki, alikuwa mhusika mkuu. Darasa zima lilibadilishana mawazo halafu wakafanya kazi wawiliwawili na kuanza kuandika hadithi na/au kuchora

Wakati wa somo, baadhi ya wanafunzi walikwenda kwa James na mwenzake kuomba ushauri wa mambo zaidi ya kuandika hadithi yao. Katika somo lililofuata, wanafunzi katika vikundi vya wawiliwawili, waliendelea na majadiliano yao na kuandika na kuchora hadithi zao binafsi.

Wakati mwalimu Mabuso alipokuwa akisoma hadithi, aligundua kuwa kulikuwa na wanafunzi wengine darasani ambao labda nao walijisikia ‘kutengwa’ katika hadithi katika vitabu vya kiada na vitabu vya hadithi vya darasa. Alianza kupanga njia za kuwashirikisha wanafunzi hawa pia.

## Shughuli ya 2: Kuandika hadithi kwa kuzingatia mitazamo tofauti

Tumia hadithi ileile kwa shughuli ya 1 au nyingine uliyochagua.

Isome na wanafunzi na jadili jinsi ambavyo ingesimuliwa tofauti. Kwa mfano, wahusika wapya wangeongezwa au wahusika waliopo wangeshiriki kwa uhusika tofauti. Katika ya familia, baba angebaki nyumbani na kupika wakati ambapo mama angekuwa akifanya kazi katika gereji. Familia ingekuwa na mtoto au mtu mzima ambaye ana ulemavu au upungufu wa akili. Watake wanafunzi wafanye kazi katika vikundi vidogo kuandika na/au kuchora kwa namna mbalimbali za hadithi mliyosoma. Zungukia darasa, ukizingatia mambo yapi yanawafurahisha wanafunzi. Kama kuna kikundi chenye matatizo, kisaidie.

Vikundi vikisha maliza, mtake mwanafunzi mmoja kutoka katika kila kikundi kusoma hadithi hiyo mpya darasani na kuonesha picha. Kusanya hadithi hizo kwa ajili ya kuzitathmini. Unaweza kuzichapisha hadithi hizo katika kitabu kwa ajili ya maktaba ya darasa au ziweke kwenye maonesho darasani. Hadithi zinakuonesha nini kuhusu mawazo ya wanafunzi na hatua yao ya maendeleo ya kuandika.

## Somo la 3

Matangazo katika mabango, redio, televisheni na skrini ya kompyuta, magazeti na majarida, katika maduka au katika barua za posta, hujaribu kutufanya tutende kwa njia fulani - hasa kutumia pesa. Ni muhimu kwako na kwa wanafunzi kwelewa jinsi matangazo yanavyojaribu kufanya hili ili wewe na wanafunzi wako muyasome kwa umakinifu na pia mtambue namna ya ujanja unaotumika katika matangazo hayo.

Mwitiko wa wanafunzi katika **Shughuli Muhimu** zitakuonesha kama wameanza kwelewa au hawajaanza kwelewa jinsi ya kusoma matangazo kwa umakinifu.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kujifunza kusoma matangazo kwa umakinifu

Wakati mwalimu Stella Mapuga aliposhiriki katika programu ya maendeleo ya walimu, alivutiwa na shughuli za kusoma kwa umakinifu. Yeye na wenzake walilinganisha matangazo ya bidhaa ileile katika magazeti kwa ajili ya wasomaji tofauti (vijana au wazee, au watu waliotoka katika 'jamii' au makundi ya vipato tofauti). Waligundua kuwa picha na maneno yaliyotumika katika kutangaza bidhaa yalikuwa tofauti katika magazeti tofauti na kwamba baadhi ya bidhaa yalitangazwa katika gazeti moja tu kati ya magazeti hayo. Walimu waliangalia lugha iliyotumiwa na watangazaji. Waliangalia pia picha au michoro katika matangazo hayo. Rafiki yake na mwalimu Stella alilalamika kuwa wanawake waliotumiwa walikuwa vijana na wenye umbo la kuvutia! Mwishowe, walijadili jinsi matangazo yalivyochanganya maneno na picha katika ukurasa na walimu waliona nini kwanza walipoangalia matangazo.

Mhadhiri wao alipowauliza walichojifunza, walimu walisema wamejifunza kuangalia matangazo kwa umakinifu zaidi siku za usoni. Walijifunza kuwa wasanifu wa matangazo huteua maneno na picha ili kuwahimiza wasomaji kununua bidhaa. Wasanifu hawa huteua maneno na picha zenye ukubwa tofauti na huziweka katika ukurasa katika njia ambayo inawahimiza wasomaji kuona zaidi baadhi ya maneno au picha.

Baadhi ya walimu walisema kuwa wana hamu ya kuwaonesha wanafunzi wao jinsi matangazo yanavyojaribu kushawishi wasomaji kuchukua hatua-hasa hatua ya kununua - na kuwahamasisha kuwa wateuzi.

## Shughuli muhimu: Kusoma matangazo kwa umakinifu

Tayarisha shughuli hii na iwasilishe kwa wanafunzi kwa kufuata hatua kama zilivyo kwenye **Nyenzo-rejea 3: Usomaji wa matangazo kwa umakinifu.** Unahitaji kukusanya maandishi ya matangazo mbalimbali au andika baadhi uliyokwishaona katika maduka ya mitaani au sokoni.

Wape matangazo hayo vikundi na watake wajadili maswali yafuatayo:

Ni bidhaa gani inayotangazwa?

Ni nani mlengwa wa kununua bidhaa au huduma hiyo?

Watangazaji wanajaribuje 'kuuza' bidhaa au huduma? Rejelea mawazo yaliyo katika orodha ya ubaoni

Nani haihussishwi katika tangazo hili?

Ungetaka kuwauliza maswali gani watangazaji?

Baada ya dakika kama 15, viulize baadhi ya vikundi kutoa majibu yao.

Kwa kazi za nyumbani, watake wanafunzi kutafuta tangazo, waliweke katika daftari zao na waandike majibu ya maswali (1-5) yanayohusu tangazo hilo.

Baada ya kusahihisha kazi zao za nyumbani, panga na fundisha somo jingine ambapo wanafunzi watapanga na kutengeneza matangazo yao wenyewe. Angalia **Nyenzo-rejea 4: Utengenezaji wa matangazo** kwa mapendekezo ya jinsi ya kutathmini na kupanga shughuli hiyo.

# Nyenzo-rejea ya 1: Uulizaji wa maswali – kuwahimiza wanafunzi kufikiri kwa umakinifu kuhusu hadithi

**Nyenzo ya Mwalimu kwa ajili ya kupanga/kurekebisha na kutumia na wanafunzi**

**Mfano A: Hadithi kuhusu familia**

Unaweza kuuliza maswali kama:

- Ni wanafamilia wapi waliomo katika hadithi?
- Wapi wanaonekana muhimu? Unawatambuaje?
- Je, familia yako inafanana na hii? Kama hivyo ndivyo, kwa njia zipi? Kama sivyo, inatofautianaje?
- Wanafamilia wanafanya nini? Je, watu katika familia yenu wanaweza kuwa na mwenendo kama huo?
- Unafikiri mwandishi anataka watu waamini nini kuhusu familia?

**Mfano B: Hadithi iliyotayarishwa shuleni**

Unaweza kuuliza maswali kama:

- Shule katika hadithi inafanana na shule yetu?
- Ni kwa njia zipi majengo yanafanana? Ni kwa njia majengo ni tofauti?
- Ni kwa njia zipi watu - mwalimu mkuu, walimu, wanafunzi - wanafanana na wale wa shuleni kwetu? Ni kwa njia zipi wanatofautiana?
- Je, watu katika hadithi wana mwenendo au wana matendo kama watu wa shuleni kwetu au wana mwenendo au wanatenda tofauti? Toa mifano kuthibitisha jibu lako.
- Unafikiri mwandishi katika hadithi anawataka wasomaji kuamini nini kuhusu shule?

Angalizo: Unaweza kuuliza maswali kama haya kuhusu kijiji, mji, jiji ambapo hadithi kama hii inatolewa. Lengo ni kuwafanya wanafunzi kulinganisha kati ya yale wanayoyajua na wanayosoma juu yake.

# Nyenzo-rejea ya 2: Vidokezo vya barua ya mwandishi

**Nyenzo-rejea ya Mwalimu ya kutumia na wanafunzi kwa ajili ya kupanga/ kurekebisha**

Mwandishi anaweza kuwa mwanafunzi darasani kwako. Kama mna vitabu mnavyochangia na darasa jingine, mwandishi anaweza kuwa darasa hilo au mwanafunzi katika darasa hilo.

Bwana ………

Tumesoma ……… (kichwa cha habari cha hadithi) darasani kwetu. Tulifikiri kuwa ungependa kujua maoni yetu kuhusu hadithi hii.

Kwanza, tunapenda……… (sentensi moja au mbili hapa). Tunapenda hii kwa sababu……… (wanafunzi waandike sababu zao).

Tunapenda pia……… (sentensi moja au mbili hapa). Tulifurahia hadithi hii kwa sababu……… (wanafunzi wanaandika sababu zao).

Lakini , hatukupenda ……… (sentensi moja au mbili hapa). Hatukupenda hili kwa sababu (wanafunzi waandika sababu yao).

Tunatarajia kuwa utakapoandika hadithi nyingine ………….(wanafunzi wanatoa mapendekezo yao).

Wako

(jina la darasa)

## Nyenzo-rejea ya 3: Usomaji makinifu wa matangazo

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

Orodha iliyopo hapa chini imetayarishwa kwa ajili ya usomaji wa matangazo kwa umakinifu zaidi lakini inaweza kurekebishwa kutumiwa katika usomaji wa matini nyinginezo kama mashairi, picha au barua kutoka kwa watu wanaohusika na masuala ya shule k.m. ofisa ya elimu wilayani.

Misingi na maswali unayouliza yanaweza kubadilishwa kwa sababu hii ili kukidhi zaidi haja ya muktadha lakini bado itawasaidia wanafunzi kusoma kwa ajili ya kupata maana ya ndani zaidi.

- Kusanya au andika matangazo ya kutosha toka gazetini, matangazo ya maduka, masoko ya mitaani n.k. kwa kila kikundi cha wanafunzi wanne darasani ili kila kikundi kiwe na mfano mmoja wa kufanyia kazi.
- Kabla ya kuvipa vikundi matangazo haya, watake wanafunzi wazungumze na wenzao kuhusu maana ya kutangaza vitu fulani na jinsi wanavyoweza kutangaza shule yao kwa wazazi ambao wangependa kuandikisha watoto wao katika shule hiyo.
- Watake wanafunzi waliambie darasa zima walichojadili. Halafu watake wanafunzi kupendekeza watangazaji wanachofanya ili kufanya bidhaa zao kuwavutia wanunuzi.
- Andika mapendekezo yao ubaoni.

Hapa kuna mifano ya wanayofanya watangazaji:


- Tumia picha au michoro inayovutia.
- Tumia rangi inavyotakiwa .
- Andika maneno na kuweka picha au michoro katika sehemu ya ukurasa panapovutia nadhari.
- Jaribu kuwavutia wasomaji ambao wanathamini moja au zaidi ya haya:
    - Uwezekano wa kununuliwa – bidhaa hii si aghali au ni bei nzuri.
    - Upatikanaji kwa urahisi – bidhaa hii inaondoa usumbufu.
    - Uzuri/uimara – bidhaa hii inakupendeza na inadumu.
    - Utajiri – bidhaa hii itakufanya uwe tajiri.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net


- Afya – bidhaa hii itakufanya uwe mwenye afya.
- Furaha – bidhaa hii hukufanya ujisikie mwenye furaha.
- Ubora – bidhaa hii ni bora kuliko zote za aina yake.
- Usalama – bidhaa hii inakufanya uwe salama.
- Umashuhuri – bidhaa hii itakufanya upendwe na watu.
- Ladha – bidhaa hii ina ladha nzuri.

*Imerekebishwa kutika: Focus on English, Grade 10*

**Mifano ya matangazo ya biashara kutoka Tanzania.**




*Chanzo chake cha asili: PIETERFOURIE, Website.*




*Chanzo chake cha asili: [Leeryanmiller](), Website.*



*Chanzo chake cha asili: BBC World, Website.*

## Nyenzo-rejea ya 4: Kutengeneza matangazo

**Nyenzo-rejea ya Mwalimu kwa ajili ya kupanga/kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

**Tathmini ya mwitiko wa wanafunzi katika kujibu maswali yanayohusu matangazo.**

Tumia maswali haya kutathmini kazi za wanafunzi:

1. Kuna ushahidi kuwa wanafunzi wameelewa kazi waliyotarajiwa kuifanya? Kwa mfano, mwanafunzi amechagua/hakuchagua tangazo; mwanafunzi amejaribu/hakujaribu kujibu swali?
2. Ni maswali yapi ambayo mwanafunzi amejibu kwa mafanikio zaidi? Kuna ushahidi upi unaoonesha kuwa majibu ni ya mafanikio?
3. Ni maswali yapi ambayo mwanafunzi hakujibu vizuri au kwa usahihi? Ni kitu kipi kinakosekana katika majibu yake au ni makosa yapi yaliyomo katika majibu yake?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Masomo ya ufuatiliaji**

4. Warudishie wanafunzi kazi zao na toa maoni ya jumla kuhusu kazi walizozifanya vizuri na ni mahali papi ambapo wangepaboresha zaidi.
5. Watake wanafunzi wafanye kazi katika vikundi vilevile kama walivyofanya katika somo la kujibu maswali kuhusu matangazo.
6. Kipe kila kikundi karatasi kubwa na, kama inawezekana, kalamu za kuchorea au rangi pamoja na brashi.
7. Watake wafikirie bidhaa mpya (k.m. aina ya chakula, gari, kifaa cha nyumbani, nguo) na wapange jinsi ambavyo wangechora au wangeandika tangazo. Wanatakiwa kufikiria juu ya maswali waliyojibu katika somo lililopita.
8. Watake wachore na kutengeneza tangazo la bidhaa hii mpya.

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

TESSA

Teacher Education in Sub-Saharan Africa

www.tessafrica.net

Rasilimali za Msingi

# Kujua kusoma na kuandika

## **Namba ya moduli 2** Kutumia Sauti za Kijumuia Darasani Kwako

**Sehemu ya 1** Kuchunguza hadithi

**Sehemu ya 2** Njia za kukusanya na kutenda hadithi

**Sehemu ya 3** Kutumia michezo ya jadi katika kujifunza

**Sehemu ya 4** Utumizi wa hadithi na ushairi

**Sehemu ya 5** Kubadilisha hadithi simulizi, mashairi na michezo kuwa vitabu

**KISWAHILI**

*TESSA (Teacher Education in Sub-Saharan Africa) inalenga kuboresha utekelezaji darasani wa walimu wa msingi na walimu wa sayansi wa sekondari barani Afrika kupitia matoleo ya Rasilimali Huria za Elimu (OERs) ili kuunga mkono walimu kuunda njia zinazowalenga wanafunzi na kuwashirikisha. OER ya TESSA huwapa walimu kitabu cha kurejea pamoja na vitabu vya shule. Zinatoa shughuli kwa walimu kujaribu madarasani pamoja na wanafunzi wao, pamoja na masomo ya utafiti inayoonyesha jinsi walimu wengine wamefunza mada hiyo, na rasilimali husishi za kuwaunga mkono walimu katika kukuza mipango ya masomo yao na ufahamu wa somo.*

OER ya TESSA imeandikwa kwa ushirikiano wa waandishi wafrika pamoja na wa kimataifa *ili kushughulikia mtalaa na muktadha. Zinapatikana kwa matumizi ya mtandaoni na chapa (*http://www.tessafrica.net*). OER Msingi zinapatikana katika matoleona lugha kadhaa (Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili). Mara ya kwanza, OER ilitolewa kwa Kiingereza na kupatikana Afrika nzima. OER hizi zimebadilishwa na washirika wa TESSA ili kufaa Ghana, Nijeria, Zambia, Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania na Afrika Kusini, na kutafsiriwa na washirika nchini Sudani (Kiarabu), togo (Kifaransa) na Tanzania (Kiswahili) OER ya Sayansi ya Sekondari zinapatikana kwa Kiingereza na zimebadilishwa ili kufaa Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania. Tunakaribisha maoni kutoka kwa wale wanaosoma na kutumia rasilimali hizi. Leseni ya uundaji wa ubunifu huwawezesha watumiaji kuchukua na kujanibisha OER zaidi ili kutimiza mahitaji na muktadha wa kindani.*

*TESSA inaongozwa na Open University, Uingereza, na inafadhiliwa kwa sasa na ruzuku za ufadhili kutoka kwa Wakfu wa Allan and Nesta Ferguson, Wakfu wa William and Flora Hewlett na Open University Alumni. Orodha kamili ya wafadhili inapatikana kwenye tovuti ya TESSA (*http://www.tessafrica.net*).*

*Pamoja na rasilimali kuu za mafundisho za kuunga mkono mafunzo katika masomo maalum, ni chaguo za rasilimali za ziada ikiwa ni pamoja na sauti, rasilimali kuu ambazo zinafafanua utendakazi, vitabu na zana maalum.*

**TESSA Programme**
**The Open University**
**Walton Hall**
**Milton Keynes, MK7 6AA**
**United Kingdom**

**tessa@open.ac.uk**

Copyright © 2017 The Open University
Except for third party materials and otherwise stated, this content is made available under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 licence: http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/. Every effort has been made to contact copyright holders. We will be pleased to include any necessary acknowledgement at the first opportunity.

***TESSA_SwPA_LIT_M2 August 2017***

*This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 License*

# Contents


Sehemu ya 1: Kuchunguza hadithi 5
- Utangulizi 5
- Somo la 1 5
- Somo la 2 7
- Somo la 3 8
- Nyenzo-rejea ya 1: Ngano za kimapokeo 9
- Nyenzo-rejea ya 2: Kwa nini watu husimulia hadithi 11
- Nyenzo-rejea ya 3: Maswali kuhusu hadithi 12
- Nyenzo-rejea ya 4: Namna Bibi Mwenda alivyopata hadithi yake 13
- Nyenzo-rejea 5: Mto uliofagilia mbali waongo 13
- Nyenzo-rejea 6: Kukadiria hadithi yako 14

Sehemu ya 2: Njia za kukusanya na kutenda hadithi 15
- Utangulizi 15
- Somo la 1 15
- Somo la 2 17
- Somo la 3 18
- Nyenzo-rejeaya1: Mfano wa barua ya mwaliko 20
- Nyenzo-rejea ya 2: Tathmini uigizaji wa hadithi za vikundi 20

Sehemu ya 3: Kutumia michezo ya jadi katika kujifunza 22
- Utangulizi 22
- Somo la 1 22
- Somo la 2 24
- Somo la 3 25
- Nyenzo-rejea ya 1: Duara la tenda - tafakari 26
- Nyenzo-rejea ya 2: Tathmini uigizaji wa hadithi za vikundi 27
- Nyenzo rejea 3: Utafiti juu ya michezo ya jadi katika mtalaa 28
- Nyenzo rejea 4: Michezo ya maneno 30
- Nyenzo Rejea 5: Wimbo wa kurukaruka maneno 35


Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Sehemu ya 4: Utumizi wa hadithi na ushairi 36
Utangulizi 36
Somo la 1 36
Somo la 2 38
Somo la 3 39
Nyenzo-rejea ya 1: Kuandaa masomo juu ya mashairi ya majina au ya kusifu 41
Nyenzo-rejea ya 2: Mashairi na hadithi za majina 42
Nyenzo-rejea 3: Mashairi na hadithi za kusifu 44
Nyenzo-rejea 4: Kuandaa masomo juu ya hadithi za maisha 46
Sehemu ya 5: Kubadilisha hadithi simulizi, mashairi na michezo kuwa vitabu 48
Utangulizi 48
Somo la 1 48
Somo la 2 50
Somo la 3 51
Nyenzo-rejea 1: Jinsi hadithi zinavyoandikwa kuwa vitabu 53
Nyenzo-rejea 2: Orodha ya kuhakiki kwa ajili ya wanafunzi - ili kutumika wakati wanapohariri kazi zao kwa ajili ya kitabu 56
Nyenzo-rejea 3: Kubadilisha hadithi za wanafunzi kuwa ‘kitabu kikubwa’ 57
Nyenzo-rejea 4: Sifa za usanifishaji wa gamba la kitabu 59


Creative Commons Attribution-Share Alike - www,tessafrica.net

# Sehemu ya 1: Kuchunguza hadithi

**Swali Lengwa muhimu:** Je, unawezaje kutumia uchunguzi kuendeleza mawazo juu ya hadithi?

**Maneno muhimu:** utafiti; hadithi; lengo; maswali; kuchunguza; jumuia

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- kutumia njia za utafiti na uchunguzi katika kuendeleza mazoezi ya darasani mwako;
- kuchunguza welewa wa wanafunzi juu ya hadithi;
- kuchunguza njia za kutunga hadithi mpya.

## Utangulizi

Usimuliaji wa hadithi ni sehemu muhimu ya maisha na utamaduni wa jamii nyingi. Moduli hii inachunguza jinsi ya kuimarisha uhusiano baina ya shule na jamii kwa kutumia jamii na hadithi zake kama rasilimali ya kujifunza.

Sehemu hii inakufahamisha juu ya umuhimu wa utafiti katika kufundisha na kujifunza. Kwa kuandaa shughuli za utafiti, utaweza kupata majibu kwa maswali yako, kujaribu mawazo mapya na kisha kuyatumia katika kuunda kazi mpya halisi.

## Somo la 1

Sote husimulia hadithi, kuhusu maisha yetu ya kila siku au yaliyopita.We all tell stories, about our daily lives or about the past. Kuna desturi nyingi katika usimuliaji hadithi na mafundisho mengi kutoka kwenye hadithi. **Shughuli 1** talii kutafiti ni nini, unafanywaje, na matokeo yanaweza kuchanganuliwa. As you work alongside the class on the task, utajifunza ni nini wanafunzi wako wanakiweza.

Tunashauri usome **Nyenzo-rejea muhimu: Kuchunguza darasani** kabla ya kuanza. Kama ungependa kusoma tafiti za watu wengine, **Nyenzo-rejea 1: Ngano za kimapokeo** pia ni nzuri, inatoa taarifa juu ya warsha iliyofanyika Qunu mashariki ya rasi ya Afrika-kusini, ambapo wazazi, walimu na wanafunzi walijadili maswali unayotafiti.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kutafiti ni kwa nini watu husimulia hadithi

Bibi Rashe na wanafunzi wake wa darasa la 3 katika shule ya Nqamakwe, mashariki mwa rasi ya Afrika kusini husimulia hadithi kila siku.

Siku moja aliandika swali ubaoni 'Kwa nini watu husimulia hadithi?' na kuorodhesha majibu ya wanafunzi:

Kufurahisha

Kuogopesha watu

Kunifundisha nisifanye jambo fulani.

Alimuomba kila mwanafunzi aende nyumbani na kumuuliza mtu mzima swali hilo hilo na kuleta majibu. Alihakikisha kwamba amewakumbusha wanafunzi kuwa wanatakiwa kuwakabili watu kwa unyenyekevu pindi wanapouliza maswali. Pia aliwakumbusha kuelezea vipi taarifa zingetumika.

Siku iliyofuata aliongezea majibu yao kwenye orodha. Pale ambapo watu zaidi ya mmoja walitoa jibu sawa aliongeza alama (√) (angalia **Nyenzo-rejea 2: Kwa nini watu husimulia hadithi** ).

Aliwaomba wanafunzi kuongeza tiki kwa kila sababu. Walijadili maswali yafuatayo:

Sababu zipi ni maarufu sana? Umejuaje? Unakubaliana na mawazo ya wakubwa? Kwa nini ndio/hapana? Baada ya majadiliano, Bibi Rashe aliwaomba wanafunzi wake waandike wamepata nini kutokana na utafiti wao.Siku iliyofuata, aliwaomba wanafunzi wachahe wenye mawazo tofauti kusoma ripoti zao. Alikuwa akishangazwa na kufurahishwa na mawazo tofauti ambayo wanafunzi walikuja nayo.

## Shughuli ya 1: Kuchunguza usimuliaji hadithi

Waeleze wanafunzi kuhusu utafiti, tumia **Nyenzo-rejea muhimu: Kuchunguza darasani**ikusaidie kupanga unachotaka kusema. Waeleze kuwa watakusaidia katika kuchunguza usimuliaji wa hadithi (angali **Nyenzo-rejea muhimu: Kuelezea na kuonesha darasani)**

Andika maswali ubaoni kutoka katika **Nyenzo-rejea 3: Maswali kuhusu hadithi** .

Eleza kuwa kila mwanafunzi ataenda kuuliza maswali haya kwa mtu mzima mmoja miongoni mwa jamii. Wakumbushe pia kuwakabili watu wazima kwa heshima na kurekodi majibu watakayopewa.

Siku kadhaa baadaye, wagawe wanafunzi katika makundi ya watu sita mpaka nane na waache waorodheshe (kwa kila swali) majibu waliyoyapata; ongeza alama ya tiki kwa jibu lililotolewa na mtu zaidi ya mmoja.

Sasa kila kundi liripoti, na wewe kumalizia seti ya data (taarifa zilizokusanywa na darasa) ubaoni.

Jadili mawzo yaliozoeleka sana. Je, wanafunzi wanakubaliana nayo?

Wasaidie wanafunzi kuandika ripoti rahisi kuhusiana na walichokipata (angalia **Nyenzo-rejea 2** kwa mpango wa ripoti ya utafiti).

## Somo la 2

Unapokuwa na matokeo ya utafiti, yanatakiwa yatafsiriwe ili uweze kutumia taarifa. Katika mfano wetu, hii ina maana kuwasaidia wanafunzi wako kutumia taarifa iliyopatikana kuelewa hadithi zaidi. **Shughuli 2** inakusaidia kutalii maana katika hadithi kama ufuatiliaji baada ya uchunguzi.

**Uchunguzi-kifani 2** inatambulisha wazo muhimu la kuwasaidia wanafunzi kutunga maswali yao wenyewe na kujaribu kuyatafutia majibu. Kuweza kuuliza maswali yao wenyewe katika makundi madogo huwajengea fikra huru na hukuza uwezo wa wanafunzi wa kufikiri kiubunifu na kwa makini.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kumalizia hadithi

Bibi Mwenda kutoka Dodoma alifanya utafiti makini katika vipengele vya hadithi nzuri ambayo haifahamiki sana (angalia **Nyenzo-rejea 4: Namna Bibi Mwenda alivyopata hadithi yake** ).

Siku moja aliwakusanya wanafunzi wake wa darasa la 2 kumzunguka, na aliwasimulia sehemu ya kwanza ya hadithi (aya tatu za mwanzo za **Nyenzo-rejea 5: Mto ambao ulifagilia mbali waongo** ). Baadaye, aliwaomba kila mmoja afikirie swali juu ya kingetokea nini katika sehemu iliyobaki ya hadithi. Baada ya dakika mbili walimpa maswali yao, na aliyaandika ubaoni.

Aliomba darasa kufikiria majibu ya maswali, kuchukua swali baada ya swali. Wanafunzi walitoa sababu za majibu yao.

Baada ya kuyapitia maswali na majibu yote, aliwaomba kumsaidia kuandika mwisho wa hadithi. Wallipendekeza nini kingeweza kutokea baadaye na aliyaandika maoni yao ubaoni. Hakukurupua mchakato, au kulazimisha mawazo yake kwa wanafunzi.

Pale hadithi ilipokuwa imekamilika, waliisoma kwa pamoja.

Wanafunzi walipenda kushughulika pamoja kwenye hadithi. Siku iliyofuata, katika watu wawili wawili, walichora picha za sehemu mbalimbali za hadithi. Hizi ziliwekwa pamoja katika kitabu.

Mwisho, Bibi Mwenda aliwasomea hadithi yenyewe. Wanafunzi walifurahishwa na mwisho wa hadithi zao ikilinganishwa na mwisho wa hadithi halisi na walizungumza mengi juu ya matatizo ya kusema uongo.

## Shughuli ya 2: Kujadili kwa nini hadithi maalumu husimuliwa

Chagua hadithi nzuri kutokana na unazozijua. Hakikisha una masimulizi kamili ya hadithi.

Andaa nakala moja kwa kila kikundi katika darasa lako, au uandike hadithi ubaoni, mahali ambapo wanaweza kuiona wote.

Pia andika sababu za kusimulia hadithi zilizotokana na utafiti wa darasa.

Wambie wanafunzi wako kujadili katika makundi kwanini wanafikiri watu wangewasimulia hii hadithi (k.v lengo lake).

Kadri makundi yatoavyo ripoti, waambie waeleze sababu zao. Kasha, jadili wahusika wa hadithi na tabia zao.

Waulize wanafunzi ni jinsi gain wangeweza kutumia hadithi hii katika maisha yao wenyewe.

Waambie, katika makundi, kujadili lengo la hadithi nyingine, labda moja kutoka nyumbani na kasha kuandika aya juu ya lengo la hadithi.

Je, wote walielewa malengo ya hadithi zao? Umelijuaje hili?

Hii shughuli haihitaji kumalizwa kwa muda wa somo wa dakika 30. inaweza ikaendelea katika vipindi vya somo jingine kama wanafunzi wako wana mambo mengi ya kujadili.

## Somo la 3

Utafiti unaonesha kuwa watu hujifunza vizuri pale ambapo kile kilichokuwa kikifundishwa ni muhimu kwao. Ukiwa kama mwalimu daima unatakiwa kuhakikisha kuwa wanafunzi wako wanapata maarifa ambayo yatawasaidia kuuelewa ulimwengu wao.

Wewe na darasa lako mmetafiti ni kwa nini watu husimulia hadithi na mmeangalia maana ya hadithi maalum. Sasa tunaangalia ni jinsi gain unaweza kuwasaidia wanafunzi wako kutumia usimuliaji wa hadithi katika hali ya maisha halisi na kwenye matatizo.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kuandika hadithi

Bibi Kaniki alitaka kuwasidia wanafunzi wake wa darasa la 6 pale Arusha kuandika hadithi zao wenyewe katika vikundi vya watu wawili wawili. Aliandika orodha ya sifa yamkini za hadithi (angalia chini) ubaoni na alizijadili na wanafunzi wake jinsi sifa hizo zinaweza kuabiri aina ya hadithi inaandikwa.

Wanyama wanawakilisha binadamu

Matukio ya ajabu, viumbe visivyo vya kawaida

Mtu kupata matatizo na kutafuta njia ya kuyatatua

Mwema na muovu

Maelezo ya jinsi vitu vilivyo

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Pia aliwapa orodha ya matukio, mazuri na mabaya, yaliyotokea mjini hivi karibuni na alipendekeza watumie moja ya matukio haya kama muktadha wa hadithi zao. Baadaye , aliwaambia wachague ikiwa wahusika wa hadithi zao wangekuwa ni watu au wanyama. Mwisho, aliwauliza dhamira wangechagua, kama vile vita kati ya wema na uovu. Walipokuwa wamshaamua dhamira, aliwapa moyo kila kikundi cha watu wali kuanza kuandika.

Baada ya wiki moja au mbili, Bibi Kaniki aliliambia kila kikundi kuchangia (mawazo) ya hadithi na darasa zima, halafu walijadili lengo la hadithi lilikuwa lipi. Aliridhishwa na aina anuai za hadithi.

## Shughuli muhimu: Kutunga hadithi mpya (halisi)

Waambie wanafunzi wafikirie matatizo katika familia zao, shule na jamii ambayo hutokana na jinsi wanavyotendeana. Matatizo yangeweza kuanzia yale ya kila siku, kama uvivu hadi mambo mazito, kama vile virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Ungeweza kuwachochea kwa kueleza hali za kawaida zinazohusisha baadhi ya aina za tabia, lakini kuwa makini na hali binafsi za wanafunzi katika darasa lako. Ungeweza kutumia magazeti kusaidia kupata mawazo ya hadithi.

Kila kundi lichague tatizo moja na kulitungia hadithi ambayo inaonesha athari za aina hii ya tabia na kutoa busara juu ya tabia hiyo.

Jadili baadhi ya sifa za hadithi kabla hawajaandika hadthi zao au panga jinsi gain wataisimulia (angalia **Uchunguzi-kifani 3** ).

Waambie kila kundi kusimulia hadithi zao darasani. Jadili lengo la kila hadithi, yaorodheshe, na yalinganishe na matokeo ya utafiti wao kutoka **Shughuli 1**.

Waache wanavikundi wajiamulie kama hadithi yao ilifanikiwa na kwa nini (Angalia maswali katika **Nyenzo-rejea 6: Kuikadiria hadithi yako** .)

Kwa kiasi gani walifanikiwa kujikadiria?

Je, unakubaliana na makadirio yao?

Kama una wanafunzi wadogo, ungeweza kufanya zoezi hili kama shughuli ya darasa zima ambapo unaandika mawzo yao ubaoni au kwenye karatasi.

## Nyenzo-rejea ya 1: Ngano za kimapokeo

### Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu

**Usuli**

Warsha iliendeshwa kama sehemu ya kazi za kitengo cha maendeleo na kisomo vijijini cha mfuko wa Nelson Mandela na shule tano kutoka eneo la Qunu mashariki mwa rasi zilishiriki. Kutoka kila shule kulikuwa na walimu wawili na mwanafunzi mmoja na mzazi mmoja na mjumbe mmoja wa kamati ya shule.

Lengo la warsha lilikuwa ni kuakisi pamoja juu ya thamani ya ngano za kimapokeo katika elimu ya watoto na jamii, na kupanga njia za kutumia hadithi hizi ndani na nje ya shule.

Kifuatacho ni ripoti ya majadala uliokuwa ukiendeshwa katika makundi katika siku ya kwanza ya warsha. Washiriki walitoa mawazo yao.

Je, unakubaliana na mwazo na maoni yao?

**Ngano ni nini?**

Ngano ni hadithi fupi zenye lengo maalum, zina baadhi ya mafundisho, ucheshi, maonyo. Husifu, hukosoa na hurekebisha. Hunoa ubongo kuufanya ufikiri kwa makini na hujenga ufikiriaji wa kina. Baadhi ni matukio halisi ambayo baadaye hubadilishwa kuwa ngano; baadhi zimekuwa zikitungwa maalum kwa dhamira ya kuchoma au kuumiza ili kuachana na matukio yaliopita na kufundisha staha.

**Ni watu gain husimulia au husimuliwa ngano?**

Kwa kauli moja walisema ni watu wazima- bibi na babu, pia watoto wenyewe kwa wenyewe, kipindi cha mafunzo ya jando na unyago. Pia walimu, watangazaji wa redio na luninga husimulia hadithi.

**Waliwasimulia/huwasimulia nani?**

Zilisimuliwa kwa watoto, vijana na watu wazima.

**Lini na wapi ngano zinasimuliwa/zilisimuliwa?**

Chumba cha kupumzikia mara nyingi hutumika, wakati mwingine chumba cha kulala na mara nyingine hadithi zilisimuliwa wakati wakiota jua karibu na maboma ya ng'ombe. Seheme nyingine zilikuwa kingo za mito, malishoni, viwanja vya nyumba na kwenye kumbi za jando na unyago.

**Kwa nini walisimuliwa/ wanasimuliwa hadithi?**

Zilikuwa kwa ajili ya kufurahisha, kunoa ubongo, kama kikumbushi, kama katazo au onyo, kuchochea uzalendo kupitia tabia fulani, kutupa msamiati na vitatanishi vyake (kama tamathali za usemi, nahau, methali na maneno mapya ambayo huingia kwenye kamusi).

**Wanasimuliwaje/ walisimuliwaje hadithi? (mtindo wa usimulizi)**

Kulikuwa na mashindano katika usimuliaji wa hadithi. Ilikuwa sanaa, iliyohusisha muziki, ucheshi na kubadili sauti. Ngano za kimapokeo zina mwanzo na mwisho wa pekee.

**Hadithi mpya husimuliwa kama zinavyosimuliwa hadithi za zamani? Kwa sababu zipi hadithi mpya hutungwa ?**

Ngano za zamani na mpya zimekuwa zikitumika, na hufanya kazi moja.

Kwa kawida, hadithi mpya hujumuisha maeneo yote mpya za maisha.

**Je, una masimulizi ya ngano yalioandikwa? Yataje.**

Kuna ngano za zamani chache zilizo katika maandishi ( Baadhi zimetajwa)

Kilichokuwa kimeonekana ni kwamba ngano chache sana zilikumbukwa na kundi na haikuwa kazi rahisi kufanya hivyo.Mtu mmoja pekee alikumbuka tatu, baadhi hawakuweza kukumbuka yoyote. Kutokana na washiriki 23, ngano 19 tu zilitolewa. Hii inamaanisha nini?

**Wapi na kwa namna gain ngano zilizoandikwa hutumika?**

Ngano husomwa kutoka vitabuni mara kwa mara. Ndicho kinachotokea nyumbani ambapo ngano zile zile hurudiwa kusimuliwa kwa kujifurahisha. Shuleni husomewa watoto. Zina mchango kwa msamiati wa watoto. Ni chache. Kuna baadhi katika maktaba na wakati mwingine huigizwa jukwaani.

**Lugha inayotumika**

Lugha iliyozoeleka ni lahaja, lugha za kitoto pia hutumika, vile vile maneno yalioundwa kuonesha staha

*Dondoo limendondolewa kutoka ripoti ya warsha juu ya ngano za kimapokeo iliyofanyika Qunu, Rasi ya Mashiriki.*

## Nyenzo-rejea ya 2: Kwa nini watu husimulia hadithi

**Mfano wa kazi za wanafunzi**

**Ubao wa Bibi Rashe**

**Ni kwa nini watu husimulia hadithi?**

**kufurahisha** √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ **35**

**kuogopesha watu** √√√√√ √√ **7**

**kunifundisha kutofanya jambo fulani** √√√√√ √√√√√ **10**

**kufundisha busara juu ya maisha** √√√√√ √√√√√ √√√√ **14**

**kuonesha tabia sahihi,** √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√√√√ √√ **32**

**kukuza lugha yetu,** √√√√√ √√ **7**

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**mpango wa ripoti ya utafiti**

Swali la utafiti

Tulifanya nini

Tunachambuaje data

Tulipata nini

**Ripoti juu utafiti wa hadithi**

Wanafunzi wa darasa la 3 waliwauliza watu wazima: 'Kwa nini watu husimulia hadithi?'

Watu wazima wapatao 35 walilijibu swali hilo.

Wanafunzi waliandaa orodha ya majibu, na walihesabu watu wangapi walijibu kila swali.

**Kifani cha ripoti**

Watu 34 walidhani kuwa hadithi husimuliwa kwa ajili ya kuwafurahisha wasikilizaji.

Watu 32 walidhani kuwa hadithi husimuliwa ili kuonesha tabia nzuri/sahihi.

Watu 14 walidhani kuwa hadithi husimuliwa ili kufundisha busara katika maisha.

Watu 10 walidhani kuwa hadithi husimuliwa ili kufundisha watu kutofanya jambo fulani.

Watu 7 wao walidhani hadithi husimuliwa ili kukuza lugha.

Watu 7 walidhani kuwa hadithim husimuliwa ili kuogofya watu.

## Nyenzo-rejea ya 3: Maswali kuhusu hadithi

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

1. Ni watu gani ambao kwa kawaida husimulia hadithi?
2. Wanawasimulia nani?
3. Wapi na lini hadithi husimuliwa?
4. Kwa nini watu husimulia hadithi?
5. Husimuliaje hadithi? (mtindo wa usimulizi)
6. Je, hadithi mpya pia husimuliwa kama zinavyosimuliwa za zamani ?
   Ni sababu zipi zinazopelekea kutungwa kwa hadithi mpya?

Nyenzo-rejea hii ni nzuri kwa matumizi ya wanafunzi wakubwa. Kwa wanafunzi wadogo ungeweza kuwa na hiyari ya kuchagua swali moja au mawili kati ya haya kwa ajili wanafunzi wako kuchunguza.

# Nyenzo-rejea ya 4: Namna Bibi Mwenda alivyopata hadithi yake

### Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu

Patricia Mwenda alijaribu kutafakari juu ya hadithi ambayo haikutambulika sana. Aliikumbuka nahau iliyorandana na hadithi yake. Nahau yenyewe ilisema: 'Hakuna mbweha aliye mkubwa kuliko mwingine, mbweha wote wana umbo sawa.' Alikumbuka kuwa hadithi ilikuwa juu ya Bwana na mtumishi wake waliokuwa wakisafiri juu ya farasi, na yule mtumishi alimsimulia Bwana wake juu ya hadithi ya mbweha aliyekuwa na umbo la ndama au maksai. Bibi Mwenda alikumbuka pia kulikuwa na mito ipitayo, na mmoja wapo uliitwa 'mto unao somba waongo wote'.

Alipokuwa hana uhakika na nini haswa kilijiri, alimuuliza wifi yake aitwaye Amina juu ya hadithi. Amina alimwambia kuwa, mtumishi yule alikuwa muongo sana. Hapo zamani alijaribu pia kusimulia hadithi ya kunguni kumfananisha na kitu kikubwa sana, hadithi ambayo haiwezi kuwa kweli. Bado walikuwa na tondoti chache, hivyo walikwenda kwa Bwana Majengo ambaye aliyewahi kuwa mwalimu wa Kiswahili, kwa sasa ni mkaguzi wa shule. Hakuweza kukumbuka hadithi, lakini alikumbuka kuwa tafsiri yake ipo kwa msomaji maalum.

Siku moja, Patricia alikuwa akiongea na Bi. Kolisa Ngodwana, mwalimu wa hisabati, aligundua kuwa alifamu ujumbe uliopo kwenye hadithi. Alisema kwamba yule Bwana alitumia mbinu fulani kumsimamisha yule mtumishi kudanganya. Hakutaka kumshutumu moja kwa moja kwa uongo. Bi. Ngodwana alisema kuwa mbinu zile zilifanikiwa, kwani mtumishi alitubu na kuzungumza kabla ya kufika mtoni. Lakini Bw. Ngodwana pia hakuweza kukumbuka tondoti za hadithi yote.

Kisha Patricia alikwenda kwa Bw. Mr Hintsa Siwisa, mwanasheria. Alijua nahau na ujumbe wa hadithi. Alifikiri ilitokana na jamii kuchoshwa na uongo wa mtu yule. Waliamua kumuweka kwenye jaribio la nguvu na kumpa somo. Masimulizi ya hadithi ya Bw. Siwisa ipo kwenye **Nyenzo- rejea 5: Mto uliofyagilia mbali wa waongo**.

*Imenakiliwa kutoka: Umthamo 2, University of Fort Hare Distance Education Project*

# Nyenzo-rejea 5: Mto uliofagilia mbali waongo

### Nyenzo ya mwalimu kwa ajili ya mpango au utohozi utakaotumiwa na wanafunzi

Bwana mmoja alikuwa safarini na mtumishi wake. Ilikuwa ni safari ndefu juu ya farasi. Kadri walivyokuwa wakisafiri, yule Bwana aliona mbweha akikatiza kwenye njia.Yule Bwana alisema: 'Mbweha yule ni mkubwa sana.' Yule mtumishi akajibu, 'Oh, Bwana huyu si chochote ukilinganisha na niliyemuona jana.' 'Ndivyo hivyo?' alidakia yule Bwana. 'Oh! Ndiyo, Alikuwa mkubwa sana sana. Kwa hakika alikuwa mkubwa kama maksai!' 'Mkubwa kama maksai?' Bwana aliuliza. 'Ndiyo mkubwa kama maksai,' alijibu mtumishi. Bwana akasema tena, 'Umesema "ni mkubwa kama maksai"?' 'Ndiyo haswa, mkubwa kama maksai,' alisema mtumishi. Yule Bwana hakusema neno waliendelea na safari yao, bila kusemezana takribani kwa muda wa saa moja.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Mtumishi alibaini kuwa Bwana wake hakuwa na raha na hukujua ni nini kilimsumbua. Kwa hiyo alimuuliza alikuwa na jambo gani. Yule bwana alimwambia kwamba wangevuka mito minne kabla ya kufika mwisho wa safari yao. Mto wa mwisho ni mkubwa na hatari zaidi kuliko yote. Mto huu ulikuwa na mzio na waongo na hakuna mwongo angeweza kuepuka hasira yake. Iliwazoa waongo huku na huko hadi kwenye kina kirefu cha bahari ya bluu. Haikuwahi kumkosa mwongo hata kama wakimuomba 'Ifa' awaletee bahati (watu humuomba Ifa awaletee bahati, na kuwapa nguvu ya kuwashinda pepo waovu).

Mtumishi aliposika hivi, alitishika sana kwa sababu alijua uwezo aliokuwa nao Ifa. Kama mto huu usingeshindwa na Ifa, basi alijua wazi kuwa ni lazima utakuwa ni mto wenye nguvu SANA. Kwa kadri walivyokuwa wakiendelea na safari ndivyo alivyoendelea kukosa utulivu. Bwana wake naye aliendelea kukasirika sana. Na jinsi anavyoendelea kukasirika ndivyo mtumishi wake alivyoendelea kushikwa na hofu na hofu kubwa.

Wakati walipokwa wanaukaribia mto mmoja baada mwingine, ndivyo umbo la mbweha nalo lilivyokuwa likipungua. Walipoukaribia mto wa kwanza, mtumishi alisema, 'Bwana wangu, mbweha si mkubwa kabisa kama maksai, ni mdogo kidogo kuliko maksai.' Bwana hakusema kitu chochote.

Walipoufikia mto wa pili, mtumishi alisema , 'Mbweha hata hakaribiani kwa umbo na maksai. Ni mkubwa kama ndama.' Lakini yule Bwana, akaendelea kukaa kimya. Walipovuka mto wa pili yule Bwana alieleza jinsi anavyojisikia kuhusiana na ule mto hatari wa mwisho na hakusema kitu tena.

Walivyoukaribia mto wa tatu, mtumishi alimwambia Bwana wake, 'Mbweha sio mkubwa kama ndama. Ni mkubwa kama mbuzi.'

Kabla tu hawajakaribia mto wa mwisho, mbweha alikuwa na umbo sawa na mbweha wengine, ambao hupatikana kila sehemu.

*Imenakiliwa kutoka: Umthamo 2, University of Fort Hare Distance Education Project*

## Nyenzo-rejea 6: Kukadiria hadithi yako

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

**Maswali**

1. Darasa lilifurahia hadithi yako?
2. Umejuaje ?
3. Darasa limejifunza kitu kutokana na hadithi yako?
4. Hadithi yako inatoa ujumbe wake vizuri?
5. Umejuaje?

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 2: Njia za kukusanya na kutenda hadithi

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kutumia utendaji katika kukuza stadi za lugha za wanafunzi wako?

**Maneno muhimu:** hadithi; kusanya; kuigiza; kujiamini; uhodari; heshima; urithi wa utamaduni

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Kufanya kazi na jumuia yako katika kukuza /kujenga stadi za lugha na heshima katika urithi wa utamaduni;
- Kupanga na kusimamia nafasi za utendaji mbele ya hadhira.

## Utangulizi

Matumizi ya mazoezi mbalimbali ya mdomo yanaweza kukuza kujiamini kwa wanafunzi katika kuzungumza na kusikiliza na kuwajengea heshima katika lugha zao za nyumbani. Jambo hili litakuwa na athari chanya katika kujistahi. Wanafunzi wanaojiamini na kujitambua wataweza kujifunza kwa wepesi zaidi.

Uigizaji katika sehemu hii unatoa nafasi kwa wanafunzi wako katika kukusanya, kukariri na kusimulia hadithi mbele ya hadhira. Inapendekezwa kwamba, ufanye kazi na wanajumuia wenye umri mkubwa kwa kuomba msaada wao katika kusimulia hadithi na kubadilishana ujuzi katika kusimulia hadithi. Shughuli hizi zitajenga umahiri katika lugha za nyumbani, ambapo baadaye unaweza ukajenga stadi za kujifunza lugha nyingine.

## Somo la 1

Ujuzi wa hadithi kwa wanajumuia ni nyenzo muhimu katika mazoezi ya kusikiliza na kuzungumza nje na ndani ya darasa. Ni muhimu wanafunzi wajifunze kuheshimu na kupenda busara na urithi wa lugha zao za nyumbani na tamaduni zao. Kwa kuimarisha stadi zao za kuzungumza na kusikiliza lugha za nyumbani kwa njia inayofurahisha, wanafunzi watakua katika hali ya kujiamini pia.

Kwa kuwa sanaa ya kusimulia hadithi haipewi thamani katika baadhi ya jumuia, watu wanaweza kuwa wamesahau baadhi ya tondoti na thamani za hadithi. Njia ya kujenga Nyenzo-rejea lugha kwa wanafunzi wako ni kuweka wazi matoleo ya zamani na halisi ya hadithi. Unaweza kufanikisha jambo hili kwa kuzungumza na watu wengine katika jumuia.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Matumizi ya lugha nyingi za wanafunzi wako darasani

Bwana Kimaryo hufundisha darasa la 4 katika shule ya msingi Makanya iliyopo nchini Tanzania. Shule ipo karibu na shamba la mkonge, ambapo wafanyakazi huzungumza lugha nyingi mbalimbali. Katika darasa lake lenye wanafunzi 70, wanafunzi 10 wanazungumza Kichaga, wanafunzi 6 wanazungumza Kirundi, wanafunzi 3wanazungumza Kinamwanga na waliobakia wanazungumza Kipare. Kwa kawaida yeye huzungumza Kiswahili anapowafundisha

Bwana Kimaryo aliwataka wanafunzi wake kukusanya hadithi toka majumbani mwao na kuwajengea hali ya kujiamini katika kuzungumza kwa kusimulia hadithi kwa kutumia lugha zao za nyumbani. Alianza somo lake kwa kuwaonesha wanafunzi picha ya mtu wa makamo na baadhi ya wanafamilia waliokuwa wamekaa pembezoni mwa moto. Kisha akawataka wanafunzi wawili wawili kujadili watu hawa wanafanya nini. Vikundi viliwasilisha majibu yao darasani. Kisha akawauliza wanafunzi kama na wao hukaa pembezoni mwa moto na kusikiliza hadithi, wengi waowalisema hawafanyi hivyo. Aliwataka wanafunzi waende nyumbani na kumuomba mtu mmoja wa makamo awasimulie hadithi.

Katika somo lililofuata, aliwaganya wanafunzi katika vikundi. Aliunda vikundi viwili vya wazungumzaji wa Kichaga, kikundi kimoja cha wazungumzaji wa Kirundi, na kikundi kimoja cha wazungumzaji wa Kinamwanga. Aliwagawanya wazungumzaji wa Kipare katika vikundi kumi. Akamtaka kila mwanafunzi asimulie hadithi yake kwa wanakikundi wenzake kwa kutumia lugha ya nyumbani.

Bwana Kimaryo alizunguka katika vikundi na kusikiliza namna wanafunzi walivyokuwa wakisimulia hadithi. Alifurahia sana namna walivyokuwa wakisimulia hadithi, hususani namna walivyokuwa wakitumia sauti zao kuongeza mvuto.

## Shughuli ya 1: Kusimuliana hadithi kwa kutumia lugha za nyumbani

Katika **sehemu ya 1**,wanafunzi wako wameshabaini mbinu muafaka ya kusimulia hadithi toka kwa wazee wao. Huu sasa ni wakati muafaka kwa wao kukusanya hadithi toka kwao.

Zungumza na wanafunzi wako kuhusiana na uzoefu wao katika kusikiliza hadithi na kubaini ni aina gani ya hadithi wanazozifurahia. Waulize kama wanasikiliza hadithi nyumbani na akina nani husimulia hadithi katika jumuia zao.

Waagize wamtafute mtu mmoja toka katika jumuia zao za nyumbani ili awasimulie hadithi. Watatakiwa kuwa na kumbukumbu za hadithi hizi, kwa sababu watahitajika kuwasimulia wenzao darasani. Njia nzuri ya kujifunza hadithi ni kwa wao kuwasimulia watu mbalimbali nyumbani. Kadiri watakavyokuwa wanafanya hivi, watatakiwa kuzingatia kuwa wana taarifa zote muhimu za hadithi.

Katika somo lijalo, waweke pamoja wanafunzi wenye lugha za nyumbani zinazofana (tazama Nyenzo-rejea muhimu: Tumia kazi ya kikundi katika darasa lako). Waagize wasimuliane hadithi walizokusanya kwa kutumia lugha zao za asili.

Je wanafunzi wako wamepokea vipi shughuli hii?

Je unaweza vipi kujenga utashi katika hadithi hizi?

## Somo la 2

Kuwaalika wanajumuia darasani kutasaidia katika kuwahamasisha wanafunzi na kuwajengea ustadi katika kusimulia hadithi kwa kutumia lugha zao za asili. Unaweza pia ukawataka wageni wako kutumia ujuzi wao wa hadithi ili kuhakikisha kwamba hadithi zinazosimuliwa na wanafunzi ni za kweli na zenye kujitosheleza kadiri iwezekanavyo. Hii itamaanisha kwamba hadithi zitakuwa nyenzo za msingi ya kujifunzia.

Kama una darasa kubwa, aina hii ya uungwaji mkono na jumuia inasaidia sa Kuomba kuungwa mkono na mkuu wako wa shule na walimu wenzio kutalifanya jambo hili kuwa katika msingi unaoeleweka.

## Uchunguzi kifani ya 2: *Kuwaalika wanajumuia katika siku wanajumuiya*

Walimu wanne wa shule ya msingi ya Mtakatifu Maria iliyopo Dar es Salaam wameandikishwa katika programu ya kuwaendeleza walimu. Moja ya moduli katika programu hii, inawataka kuchunguza ni kwa namna gani Nyenzo-rejea zinazowazunguka zinaweza kutumika darasani. Walifanya kazi ya kukusanya maboksi, chupa, mimea na nyenzo nyingine na kuzitumia katika mazoezi ya sayansi, hesabu na lugha.Hata hivyo, moduli ziliwakumbusha kuwa watu ni nzenzo muhimu kwa ajili ya kujifunzia.

Ilipendekezwa kuwa wapange siku ya kuwakutanisha pamoja wanafunzi na wanajumuia wanye umri mkubwa kwa lengo la kubadilishana maarifa na ujuzi.

Siku ambayo walimu hawa wanne waliipanga, ilikuwa na mafanikio makubwa. Bibi Rwakatare, mwenyekiti anayeongoza bodi ya shule, alielezea historia ya shule. Baadhi ya wanajumuia walioshiriki walionesha kwa vitendo stadi mbalimbali kama vile,ususi wa vikapu,ukaushaji wa tumbaku, na kutengeneza shanga,.wanawake walisifika kwa kutoa maelezo kuhusu mapishi ya vyakula vya asili. Wazee mbalimbali, wanaume kwa wanawake walisimulia ngano.

Kisha ikafuata zamu ya wanafunzi kuonesha kwa vitendo mambo waliyojifunza shuleni. Siku ilimalizika kwa kuimbwa nyimbo na dansi toka katika vikundi mbalimbali.

Kutokana na shughuli za siku hii, wanajumuia mbalimbali wakawa wanatembelea shule mara kwa mara. Walitoa ujuzi wao katika stadi mbalimbali na pia walisimulia hadithi ambazo baadaye zilitumiwa darasani.

## Shughuli ya 2: Mafunzo toka wanajumuia 'mahiri'

Utatakiwa kupangilia vema shughuli hii mapema na kutenga muda wote wa asubuhi au mchana kwa ajili ya shughuli hii.

Wapange wanafunzi wako katika vikundi kulingana na lugha zao za nyumbani. Waagize kila kikundi kualika mtu mmoja toka katika jumuia zao kuja darasani ili kuwasaidia wanafunzi katika ustadi wao wa kusimulia hadithi. Wape kila kikundi barua ya mwaliko waendenayo nyumbani. (tazama **Nyenzo-rejea 1: Mfano wa barua ya mwaliko** ).

Waagize wanajumuia wajiunge na kikundi na kusikiliza wanafunzi wakiwa wanasimulia hadithi siku hiyo. Waombe wageni waalikwa wawape wanafunzi muongozo na ushauri juu ya namna ya kuboresha hadithi na masimulizi yao.

Kipindi cha mafunzo kikimalizika, vikundi vinaweza kukaa pamoja na kusikiliza hadithi kutoka kwa wageni waliowaalika. Nyimbo, mashairi na vitendawili vinaweza vikatolewa siku hiyo.

Je, ushirikishwaji wa wanajumuia umeongeza nini katika ujifunzaji darasani mwako?

Je umefurahia namna ulivyopangilia shughuli zako?

Je utafanya nini cha tofauti wakati ujao?

## Somo la 3

Ni muhimu kila mwanafunzi awe na uwezo wa kuwasiliana vema na kuwa kuwa anapewa nafasi ya kuwa mbunifu.Uwasilishaji wa hadithi katika vikundi unatoa nafasi hata kwa wanafunzi wakimya kuzungumza, kuimba, kutenda,kucheza n.k bila ya shinikizo. Kila mwanafunzi katika uigizaji wa hadithi anaweza kupata nafasi ya kuwa muhusika katika hadithi, msimuliaji ama kuwa sehemu ya kiitio. Wanafunzi wenye vipaji maalum wanaweza wakaandaa 'vifaa' na 'mavazi' wakiwa na vitu kama vipande vya nguo ama karatasi ama matawi ya mti.

Katika madarasa ambapo wanafunzi wote hawazungumzi lugha moja ya nyumbani, kufanya kazi na wazungumzaji wa lugha inayofanana kwa lengo la kuandaa uigizaji katika lugha hii kunaweza kuwa na matokeo bora.

Sehemu inayofuata inakupa njia ya kukuza kujiamini na stadi kwa wanafunzi katika lugha zao za nyumbani. Njia hizi pia zinaweza zikatumika katika kuimarisha stadi katika lugha ya mawasiliano ama lugha ya ziada.

## Uchunguzi kifani ya 3: Siku ya kuigiza hadithi katika darasa kubwa

Bibi Rebecca Kassam hufundisha darasa la tano lenye wanafunzi 100, katika kijiji kilichopo karibu na Tanga Kaskazini mwa Tanzania. Aliamua kuwa na siku ya kuigiza hadithi mwisho wa muhula. Aliwapanga wanafunzi wake katika vikundi vya watu watanowatano na kisha kuwahimiza sio tu wasimulie hadithi bali pia waigize, hivyo, waigizaji na hadhira kwa pamoja wataweza kufurahia. Aliwaeleza wanafunzi kwamba kama watataka kuigiza katika lugha ambayo si kila mtu anaifahamu, hawana budi kuamua kuisaidia hadhira kuelewa maana inayokusudiwa kwa kutumia vitendo, ishara na vitu mbalimbali.

Bibi Kassam huwapa wanafunzi wake muda wa kuandaa na kukariri hadithi zao. Wanapokuwa wanafanya kazi hii husimamia maendeleo yao na wakati mwingine huweza kufupisha ama kurefusha muda wa maandalizi. Alibaini kuwa wanafunzi wanapendelea kuandaa na kuigizia kazi zao nje.

Kwa wanafunzi 80, itachukua muda mrefu kama makundi yote yataigiza darasani. Katika siku ya kuigiza hadithi, Bibi Kassan huwaagiza wanafunzi waunde maduara manne ambapo kila duara linakuwa na makundi manne. Huyapa namba makundi katika kila duara kuanzia 1-4. Kikundi cha 1 huigiza katikati ya duara kwa ajili ya kikundi cha 2,3 na 4, kisha kikundi cha 2 huigiza kwa ajili ya kikundi cha 1,3,na 4 na kuendelea hadi makundi yote yamalize mzunguko

Baada ya uigizaji, Bibi Kassam, hukitaka kila kikundi kujadili juu ya kile walichojifunza. Hufikiri juu ya kile ambacho mwanafunzi mkimya darasani mwake alichoonesha kuhusu uelewa wake wa siku ile na namna anavyoweza kutumia taarifa hizi kuandaa hatua nyingine ya kujifunzia.

**Nyenzo-rejea muhimu: Kufanyakazi na madarasa makubwa na/au madarasa ya viwango mbalimbali** inatoa mawazo ya ziada kwa ajili ya kufundishia madarasa makubwa.

## Shughuli muhimu: Kuigiza hadithi kwa ajili ya hadhira

Waagize wanafunzi kujigawa katika vikundi vya watu sita sita. Waagize wanafunzi:

Kukumbuka kuhusu hadithi walizosimulia na kusikiliza

Kuamua ni hadithi ipi wanadhani itakuwa bora kuigizwa kwa ajili ya darasa ambapo kila mmoja ataweza kuelewa na kuifurahia. Kikundi zaidi ya kimoja kinaweza kuchagua hadithi ileile.

Wateue wahusika wote na kuamua kila nafasi itachukuliwa na nani. Watahitaji pia kuwa na msimuliaji.

Toa maamuzi juu ya lugha (z)itakayotumika, athari za sauti, matumizi ya ishara,mavazi, na vitu vitakavyosaidia kuipa hadithi uhai na nani ataleta Nyenzo-rejea zipi.

Wape muda wa kukariri na kuweka muda maalum kwa ajili ya uigizaji. Simamia kila kikundi na kuwasaidia kadiri inavyowezekana kwa kutoa mawazo na mapendekezo juu ya njia ya kufanya kazia.

Itake hadhira kutoa kuleta mwitikio kwa kila kikundi. ( **Tazama Nyenzo-rejea 2: Tathmini uigizaji wa hadithi katika vikundi** ).

Kama utaweza, rekodi hadithi zitakazoigizwa.Vinginevyo chukua dondoo kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Hadithi zinaweza kuigizwa mbele ya wazazi na viongozi wa jumuia katika eneo lako kwa lengo la kukusanya michango kwa ajili ya kununulia nyenzo za darasa lako.

## Nyenzo-rejeaya1: Mfano wa barua ya mwaliko

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kutohoa na kutumia na wanafunzi.**

Mpendwa …………………

Darasa letu la …… linajifunza kuhusu hadithi za asili na stadi za kusimulia hadithi. Tumesikia kuhusu ubingwa wako na tunapenda kukukaribisha kuja na kutusaidia kujifunza ni namna gani tunaweza kukuza stadi zetu za kusimulia na kujifunza hadithi pia.

Tungependa uje …………………………………. Tafadhali tujulishe kama muda huu ni mwafaka kwako. ………………………………… kutoka katika darasa letu atakusubiri geti la shule saa 4.00 asubuhi.

Tunashukuru sana

Darasa la 5

*Shule ya Msingi ya Mtakatifu Maria*

## Nyenzo-rejea ya 2: Tathmini uigizaji wa hadithi za vikundi

**Matumizi ya mwanafunzi**

| **Sifa ya uigizaji** | **Vizuri sana** | **Vizuri** | **Wastani** | **Dhaifu** |
|---|---|---|---|---|
| Hadithi ya kufurahisha na rahisi kufuatilia. | | | | |
| Matumizi ya sauti mbalimbali | | | | |
| Matumizi ya athari za sauti | | | | |
| Matumizi ya miondoko | | | | |
| Matumizi ya mavazi na/au vifaa | | | | |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net



*Watu wa Afrika Mashariki wakiigiza hadithi*

*Vyanzo vya asili: Two Help; Website.*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 3: Kutumia michezo ya jadi katika kujifunza

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kutumia michezo ya jadi ili kusaidia ujifunzaji wa lugha?

**Maneno muhimu:** kutafakari; utafiti; michezo ya jadi; mapokeo; mashairi; nyimbo; kuchunguza

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia michezo ya jadi na ya mahali husika katika kusaidia shughuli za ujifunzaji;
- umewahamasisha wanafunzi na kuongeza ujasiri wao wa kutumia lugha kwa njia ya michezo, nyimbo na mashairi;
- umepanua stadi zako mwenyewe katika kutafakari wajibu na uwezo wako kwa kuchunguza thamani ya michezo katika ujifunzaji.

## Utangulizi

Baadhi ya walimu ambao wamefundisha kwa miaka 20 ni kama tu wanakuwa na uzoevu wa mwaka mmoja tu, ambao unarudiarudia. Hii ni kwa sababu hawajifunzi tena kwa bidii au hawajiendelezi ili waweze kuwa walimu bora zaidi.

Walimu wazuri ni wale ambao wanapanga kile wanachotaka kukifanya, na mara wanapokifanya, wanarekodi kilichotokea, na kujiuliza wenyewe mafanikio ni yapi na ni wapi panahitaji kuboreshwa. Wanatafakari endapo wanafunzi wamejifunza chochote, na kama wamejifunza, wamejifunza nini? Kwa msingi huu wa 'tafakari', wanapanga tena kwa ajili ya shughuli inayofuata. **Nyenzo rejea 1: duara la tenda-tafakari** huonesha mchakato huu katika muundo wa kielelezo.

## Somo la 1

Watoto hawajifunzi tu wakiwa darasani, wanajifunza pia wakiwa wanacheza. Wanajifunza kutoka kwa wengine, kwa kuangalia kile wanachokifanya wengine. Hujifunza kwa kuzungumza, kuimba, kwa kukariri na kwa kushirikishana katika mazungumzo. Unaweza kutumia mchezo ili kufanya ujifunzaji katika darasa lako uwe wa mafanikio na kuziba uwazi kati ya kinachotokea darasani na nje ya darasa.

Katika **Shughuli 1**, wanafunzi wako wanakuwa kama watafiti, na wanakwenda kwenye uwanja wa michezo (au mahali pengine) ili kurekodi kile wanachofikiri kuwa wataweza kujifunza pale. Wanaporudi darasani wanazungumzia kile ambacho wamekigundua: Unaweza kusikiliza mazungumzo yao ili kuona kile ambacho unafikiri wanafunzi wako wamejifunza uwanjani hapo.

## Uchunguzi kifani ya 1: Mwanafunzi wa miaka sita ajifunza na kufundishaKiswahili

Maria ambaye ana umri wa miaka sita anasoma katika shule ambayo

Kiswahili ni lugha inayotumika darasani, ingawa si lugha yake ya kuzaliwa.

Kila siku kwa muda wa wiki nzima, Maria aliweza kuonekana wakati wa mapumziko akiwaangalia watoto wengine wakiruka kamba. Hakujiunga, lakini alisimama karibu ili kuweza kuona na 'kusikiliza' wimbo ambao wanafunzi walikuwa wakiuimba. Siku ya kwanza ya wiki ya pili, Maria alikuwa kwenye ile sehemu yake ya kawaida hatua chache kutoka eneo la kuchezea, lakini sasa aliweza kusikika 'akitoa sauti' za maneno ya kwenye wimbo.

'Ruu-ka, ruuu-kia ndani na seeema

Moja-aa mbili-iii, tatuuu,

Ruuu-kia na-a mimi.'

Alirudia maneno haya tena na tena, akijitahidi kuyasema kwa sauti kubwa, kwa wororo na kwa kutumia mkazo tofauti tofauti kwenye sehemu za neno. Alirudia wimbo huu mara kadhaa na kisha kuwasikiliza tena wanafunzi wengine. Alitabasamu, na kuimba tena ule wimbo.Mwishoni alitafuta kamba na kwenda kwa rafiki yake, Migueli. Aliimba ule wimbo, mstari kwa mstari, akimfundisha rafikiye huu wimbo. Alitafsiri yale maneno ya Kiswahili ili rafiki yake aweze kuelewa alichokuwa akijifunza. Kwa muda mfupi Migueli aliweza kuimba wimbo ule pamoja na Maria.

## Shughuli ya 1: Kuchunguza ujifunzaji wa asili

Kabla ya kuanza shughuli hii, soma **Nyenzo Rejea 2: Utafiti juu michezo ya jadi katika mtalaa** . Nyenzo rejea hii inaeleza kazi moja ya utafiti na micezo miwili ambayo walimu waliibuni kama matokeo ya utafiti huo. Kusoma pia **Nyenzo Rejea Muhimu: Kufanya utafiti darasani** kutasaidia sana. Zungumza na wanafunzi wako kuhusu ujifunzaji. Je, wanajua kwamba daima hujifunzia: nyumbani, shuleni, wakati wanapocheza?

Liambie darasa lifanye uchunguzi katika ujifunzaji wa 'asili'. Swali lao ni: Ujifunzaji gani unaotokea wakati watoto wanapocheza? Wanafunzi lazima waandike na kuchora kuhusu ujifunzaji wanaouona kwenye uwanja wa michezo na baada ya kutoka shule, wakati wanafunzi wengine wanapocheza, na wanapocheza wao wenyewe.

Wwaambie wanafunzi darasani washirikishane matokeo yao, kwenye vikundi. Kiambie kila kikundi kioneshe jinsi ya kucheza mchezo mmoja. Rekodi nyimbo au mikarara/viitikio wanavyoimba wakati wa mchezo, kwenye tepu, au kwa kuandika.

Waambie wanafunzi kwenye kila kikundi wajadili kile ambacho wanaweza kujifunza kutokana na michezo hii. Andika mawazo yao.

Umejifunza nini kutokana na shughuli hii inayohusu namna michezo inavyoweza kusaidia katika ujifunzaji?

## Somo la 2

Aina zote za michezo zinaweza kutumika kwa kujifunzia na unahitaji kufikiri kiubunifu jinsi ya kuitumia michezo darasani (angalia **Shughuli 2**). Inasaidia kama unaweza kushirikiana na wenzako pamoja na rafiki zako, na pia kushirikiana na wanafunzi wako, katika kubuni mawazo mapya ambayo yanaweza kufanya ujifunzaji darasani kwako uwe wa kufurahisha na wenye mafanikio.

Katika sehemu hii, wewe na darasa lako panueni utafiti wenu kwa kuwauliza wanajumuiya kuhusu michezo waliyokuwa wanaicheza walipokuwa wadogo.

## Uchunguzi kifani ya 2: Michezo na mikarara/viitikio katika kadi za kusoma

Kuna ongezeko la kupenda lugha nyingi za nyongeza katika mitalaa kote Afrika. Hii ina maana kuna ujifunzaji wa awali unaotumia lugha mama, na lugha nyingine za nyongeza (bila kuchukua nafasi ya ile lugha mama). Mtalaa unalenga kuingiza lugha zote ambazo watoto wanazijua wakati wa masomo yao.

Bwana Maleke mkoani Lindi hutumia shughuli ifuatayo, ambayo hujumuisha lugha nyingi za nyongeza, pamoja na wanafunzi wake wa darasa la 5. Humpatia kila mwanafunzi kipande cha kadi. Wanafunzi huchora picha katika upande mmoja wa kadi. Kwa upande mwingine, huandika nyimbo, michezo, mikarara/viitikio au mashairi, ambayo wanayapata nyumbani.

Kila siku, wana kipindi cha kusoma ambapo wanafunzi wanasoma (au wanaimba!) kile kilichoandikwa kwenye zile kadi. Wakati mwingine, msomaji bora husoma kadi na msomaji anayesoma polepole zaidi. Wakati mwingine, mzungumzaji wa lugha moja, humsaidia mwanafunzi mwingine kusoma lugha yake na kuingiza sauti. Wakati mwingine, wanaigiza hayo mashairi au wanacheza michezo hiyo. Bwana Maleke amegundua jinsi darasa lake linavyokuwa na furaha na jinsi wanafunzi wanavyoshirikiana vizuri katika mazungumzo na wanavyochanganyika vizuri zaidi tangu waanze kufanya hivi.

## Shughuli ya 2: Michezo na nyimbo kutoka kwa wanajumuiya ambao ni watu wazima

Waambie wanafunzi wako wamwombe mtu mzima (mzazi, babu/bibi, jirani n.k.) awafundishe mchezo, wimbo au mkarara ambao walikuwa wakiufurahia wakati wa utotoni. Wanatakiwa wajue kanuni za maneno na nyenzo zozote ambazo zinahitajika.

Siku inayofuata, orodhesha michezo na nyimbo ambazo wanafunzi wamezileta toka nyumbani.

Waweke pamoja wanafunzi wanaojifunza mchezo au wimbo wa aina moja. Waambie wajiandae kufundisha darasa mchezo au wimbo huo.

Waambie waandike huo wimbo au huo mkarara au wacheze mchezo wa kwenye kadi.

Darasa litakapomaliza kujifunza mchezo au wimbo huo, jadilianeni kitu ambacho wanaweza kujifunza kutokana na mchezo au wimbo huo. Andika tini kama ulivyofanya hapo awali.

Kwa masomo yatakayofuata, wahamasishe wanafunzi wasome magazeti ili kutafuta nyimbo, michezo, vitendawili na mizaha kama msingi wa kuandika vitu vyo wenyewe.

## Somo la 3

'Kuakisi' ni kutafakari juu ya kile kilichotokea na kuona jinsi ya kufanya vizuri zaidi wakati mwingine. Baada ya kuwa umejaribu shughuli mpya, inasaidia sana kuakisi/kutafakari juu ya mafanikio na kitu gani kinahitaji maboresho. Fanya mchakato wa 'Panga-Tenda-Rekodi-Tafakari' kuwa sehemu ya mazoea yako ya kila siku (angalia **Nyenzo Rejea 1** ).

Sasa una mkusanyiko mzuri wa michezo, unaweza kuitumia michezo hii kama msingi wa shughuli za ujifunzaji, na kama msingi wa kuakisi/kutafakari na uboreshaji. (kazi hii pia inaweza kufanywa kwa kutumia hadithi.)

**Nyenzo Rejea 3: Michezo ya maneno** ina michezo kadhaa ambayo unaweza kuijaribu pamoja na wanafunzi wako.

## Uchunguzi kifani ya 3: Vitenzi vya Kiswahili katika wimbo wa kurukaruka maneno

Bi Alison aliimba wimbo wa kurukaruka maneno wakati alipokuwa mtoto pale Mazimbu, Morogoro. Aliamua kuutumia wimbo huo kufundishia wanafunzi wake wa darasa la 2 maneno kadhaa na virai vya wakati uliopo vya Kiswahili.

Kwanza wanafunzi waliuimba kwa Kiswahili na kisha aliwasaidia kuuimba kwa Kiingereza.

Alimpatia kila mwanafunzi kipande cha karatasi chenye kitenzi (m.f. la, nywa, cheka, kohoa, ruka, kimbia, rukaruka) kilichoandikwa kwenye karatasi hiyo. Alihakikisha kuwa kila mtoto anafahamu maana ya neno hilo na jinsi ya kufanya vitendo vinavohusiana na neno hilo.

Alimwambia kila mwanafunzi mmoja mmoja afanye vitendo bila maneno, na darasa liliimba ubeti mpya: 'Antoni, msichana huyu anafanya nini? Antoni, msichana anacheka,' n.k.

Baada ya somo, alitafakari kuhusu:

Kile kilichokwenda vema;

Kile ambacho hakikwenda vema sana;

Kile kilichomshangaza;

Kile ambacho angekibadili kama angerudia lile somo.

Bi Alison alishangazwa na jinsi wanafunzi walivyoutumia muda katika kujifunza toleo la Kiswahili lakini pia jinsi wanafunzi waliufurahia muda. Aliona kuwa alihitaji kutumia muda zaidi katika shughuli hii, na pia kufundisha maneno machache zaidi.

Wiki iliyofuata, alitumia toleo la aina nyingine la Kiswahili lililokuwa na wimbo wa kurukaruka maneno kwa jinsi ile ile, ya kutunga beti zenye aina mbalimbali za vyakula.

(Angalia **Nyenzo Rejea 4: Wimbo wa kurukaruka maneno** kutoka katika wimbo wa kurukaruka maneno wa Igbo.)

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli muhimu: Kujifunza kutokana na mkarara, wimbo au mchezo

Je, kuna mkarara kwenye makusanyo ya darasa lako ambao lugha yake inaweza kubadilishwa na kuwa kama lugha ya nyongeza na kuweza kutumiwa katika kuhamasisha ujifunzaji wa lugha?

Bainisha sentensi katika mkarara ambayo neno (au maneno) yangeweza kubadilishana nafasi kwa zamu. Kwa mfano, 'Anacheka' lingeweza kubadilishana nafasi na (Anaruka, anarukaruka, anakimbia' n.k.). Kila mwanafunzi, au kikundi, kinaweza baadaye kuimba ubeti mpya, wenye neno jipya katika sentensi ya mwanzo.

Ingeweza hata kufurahisha zaidi kama maneno au sentensi yataweza kuambatana na vitendo.

Panga jinsi utakavyopanga darasa lako kwa ajili ya kuimba/ kukariri na kuigiza (zoezi hili ni mbadala'. (Huu ni mfululizo wa sentensi, ambazo zinafanana isipokuwa kwa neno au kishazi kimoja. Sentensi hizi zinatumika kufanya mazoezi ya mitindo ya lugha.)

Kama hutafanikiwa, utatakiwa kujaribu wimbo mwingine, au njia nyingine ya kuendesha shughuli hii.

## Nyenzo-rejea ya 1: Duara la tenda - tafakari

**Nyenzo-rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kutohoa na kutumia na wanafunzi.**

**Mpendwa …………………**

Darasa letu la …… linajifunza kuhusu hadithi za asili na stadi za kusimulia hadithi. Tumesikia kuhusu ubingwa wako na tunapenda kukukaribisha kuja na kutusaidia kujifunza ni namna gani tunaweza kukuza stadi zetu za kusimulia na kujifunza hadithi pia.

Tungependa uje …………………………………. Tafadhali tujulishe kama muda huu ni mwafaka kwako. ………………………………… kutoka katika darasa letu atakusubiri geti la shule saa 4.00 asubuhi.

Tunashukuru sana


Darasa la 5

*Shule ya Msingi ya Mtakatifu Maria*

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea ya 2: Tathmini uigizaji wa hadithi za vikundi

**Usuli/welewa wa somo wa mwalimu**




Kielelezo kinaonesha hatua zifuatazo katika mduara wa tenda- Akisi/Tafakari:

**Panga** shughuli.

**Tenda** kwa kuweka mpango katika vitendo, na chunguza unavyoendelea.

**Rekodi** kile unachokiona.

**Akisi/Tafakari** juu ya kilichotokea.

Pitia tena **mpango** wako, au andaa **mpango mpya**.

Weka mpango uliopitiwa tena au mpango mpya katika **vitendo**, na angalia tena.

**Rekodi** na **tafakari** tena.

Na kadhalika, na kadhalika …

Kila kitu unachokifanya kama mwalimu kinaweza kuwa sehemu ya mduara wa

Tenda -Tafakari.

(Angalia pia Nyenzo Rejea Muhimu: Kufanya utafiti darasani)

# Nyenzo rejea 3: Utafiti juu ya michezo ya jadi katika mtalaa

**Usuli/welewa wa somo wa mwalimu**

Nonhlanhla Shange alifanya utafiti katika Shahada yake ya Uzamili katika Kitengo cha Usomeshaji wa Vijijini cha Nelson Mandela katika Chuo Kikuu cha Fort Hare nchini Afrika Kusini. Alitafiti kuhusu utumizi wa michezo ya jadi darasani, utafiti ambao aliufanya katika shule nne za vijijini.


Wanafunzi na walimu wao walifanya utafiti wa vitendo katika michezo ya jadi.

Walimu walisikiliza kwa makini na waliandika tini za michezo ambayo wanafunzi waliileta darasani. Walijaribu kutayarisha masomo yanayohusu michezo hii. Wanatunza juzuu, ambamo huwekwa kumbukumbu za masomo haya, na kujaribu kufanya maboresho kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

Maelezo ya michezo miwili ambayo ilichezwa kama sehemu ya utafiti huu ni haya yafuatayo hapa chini.

**1. Mchezo wa duara**

Matayarisho ya mchezo huu yanajumuisha uchoraji wa kielelezo kama hiki hapa chini ambacho huchorwa ardhini.



**Mchezo unachezwaje?**

Mchezo huu unachezwa kwa vikundi vidogo vya wanafunzi watano watano au sita sita. Mwanafunzi mmoja anarukia ndani ya nafasi za duara, akigeuka upande hadi upande, wakati wanafunzi wengine wakiimba wimbo mfupi au shairi fupi, kwanza kwa lugha ya asili, na kisha kwa Kiswahili.


Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Shughuli gani za ujifunzaji zilizohusiana na mchezo huu?**

Mchezo ulibuniwa ili kuonesha ni jinsi gani kurudia rudia kwa kutumia lugha ya wanafunzi wenyewe na lugha ya Kiswahili kunavyoweza kusaidia katika kujifunza. Kwa kutumia wimbo mfupi au shairi, mchezo huu pia uliweza kutumika katika kuwafundisha wanafunzi kuhesabu.

**2. Mcezo wa mawe**

Matayarisho kwa ajili ya mchezo hujumuisha uchoraji wa duara chini ardhini na kuweka idadi fulanii ya mawe kwenye duara hilo. (duara lisizidi kipenyo cha mita moja.)



**Mchezo unachezwaje?**

Wanafunzi wanagawanywa katika vikundi vya watano watano au sita sita. Kila kikundi kinakuwa na duara lake lililochorwa ardhini na kuwekwa mawe ndani yake.

Mchezaji anarusha jiwe moja juu; kabla halijatua ardhini, lazima wajaribu kuokota mawe mengine ndani ya duara.

Kila mwanafunzi katika kikundi lazima ajipe namba mwenyewe (chini ya 10). Namba hii ni idadi ya mawe ambayo mchezaji atajaribu kucheza na kuokota.

Mchezaji mmoja anaingia kwanza. Kama mchezaji huyu ataokota idadi ya mawe inayotakiwa kutoka kwenye duara, wanasema orodha ya kuzidisha ya namba hii (kwa mfano, orodha ya 3 ya kuzidisha, wanakomea kwenye 30 – hii inaweza kuwa ni ya chini kwa wanafunzi wadogo zaidi).

Kama mchezaji atashindwa kuokota idadi inayotakiwa ya mawe kutoka kwenye duara, watapaswa kuzidisha idadi ya mawe waliyookota kwa idadi ya mawe ambayo walipaswa kuokota, na kupata jibu sahihi. Kwa mfano, kama walitakiwa kuokota mawe hadi 5, lakini wakaokota mawe 3 tu, watatoa jibu sahihi la 5 x 3.

Wachezaji wengine watapima/watajaji endapo wametoa jibu sahihi au jibu ambalo si sahihi.

**Shughuli gani za ujifunzaji ambazo zinahusishwa na mchezo huu?**

*Mchezo huu ulitumiwa ili kuwafanyia wanafunzi mazoezi ya ’ stadi’ za kuzidisha.*

*Chanzo cha Asilia: Shange, N., Kitengo cha Mfuko wa Nelson Mandela wa Usomeshaji na Maendeleo ya Vijijini [ utafiti haujachapishwa ] Nelson Mandela Foundation’s Unit for Rural Schooling and Development [unpublished research]*

## Nyenzo rejea 4: Michezo ya maneno

**Nyenzo rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

Michezo hii inaweza kuchezwa kwa kutumia lugha yoyote na kwa umri wowote, ilimradi tu wanafunzi wanajua vizuri stadi za kusoma na kuandika.

**Mchezo 1: Bingo**

Wasomee wanafunzi hadithi wanayoipenda na waambie wachague maneno mawili wanayoyataka.

Mwulize kila mwanafunzi maneno yao na andika maneno muhimu ubaoni ambapo kila mmoja ataweza kuona.

Ligawe darasa katika vikundi vya wanafunzi sita sita na kiambie kila kikundi kichague maneno 12 kwa ajili ya kikundi chao. Haya yanaweza kutofautiana kwa kila kikundi.

Kila mwanafunzi atengeneze karatasi ya bingo kwa kuchora mraba mkubwa uliogawanyika katika miraba midogo tisa (angalia mfano hapa chini).

Mwambie kila mwanafunzi achague maneno yoyote tisa kutoka kwenye orodha yao ya maneno 12 na kuyanakili katika karatasi yao ya bingo, neno moja kwa kila mraba. Makaratasi ya wanafunzi yatakuwa tofauti, kwa sababu wataweza tu kuchagua maneno tisa kati ya maneno 12.

Mwanafunzi mmoja atakuwa na karatasi kuu yenye maneno 12. Watatoa maneno bila mpangilio maalum. Neno linavyotajwa kila mwanafunzi ambaye atakuwa na neno hilo katika karatasi ya bingo atatakiwa kulikata. Wa kwanza kukata maneno yake yote atapiga kelele ‘Bingo’ na atakuwa ameshinda.

Kiache kila kikundi kicheze tena na kila mwanafunzi apate zamu ya kutaja maneno.

Kama unataka kutumia karatasi ya bingo zaidi ya mara moja, waambie wanafunzi wazibe maneno hayo kwa mawe au vihesabio wakati wa kutaja maneno.

Je, wanafunzi walijifunza maneno mapya? Unajuaje?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Orodha ya Sampuli ya maneno kwa ajili ya Bingo:**

Ndizi

Maharage

Kabeji

Mihogo

Nazi

Punje za mahindi

Maembe

Mahindi

Machungwa

Mapapai

Mapeasi

Spinachi

Viazi vitamu

**Mifano miwili ya kadi za bingo:**

| | | |
|---|---|---|
| Spinachi | Mapapai | Maharage |
| Mhogo | Ndizi | Nazi |
| Mahindi | Maembe | *Kabeji* |

| | | |
|---|---|---|
| Ndizi | Machungwa | Viazi vitamu |
| Spinachi | Maharage | Punje za mahindi |
| Nazi | Mhogo | Mahindi |

**Mchezo 2: Maneno yanayohusu supu**

Tengeneza orodha ya maneno tisa, mf. sehemu za mwili, vyumba vya nyumba, au mboga za majani. Weka orodha hii ubaoni (pembeni mwa picha toa maelekezo ya maneno kama unaweza).

Mpatie kila mwanafunzi kipande cha karatasi cha mraba, herufi moja kwa kila mraba. Waambie waingize maneno muhimu katika karatasi hiyo kwenye miraba hiyo, herufi moja kila mraba mmoja. Waambie kuwa maneno yanaweza kutoka kushoto kwenda kulia, au juu mpaka chini. Waambie wanafunzi wajaze miraba ya ziada kwa herufi zozote zile za alfabeti. (Angalia mfano hapa chini).

Kila mwanafunzi akishafanya hivi, kusanya makaratasi yote na yachanganye. Sasa wagawie wanafunzi makaratasi hayo bila mpangilio maalum, na waambie wanafunzi wazungushie maneno yote wanayoweza kuyapata. Kila mwanafunzi anajua lazima maneno yawe tisa. Wa kwanza kumaliza ndiye mshindi.

Wanafunzi wanaweza baadaye kuchagua somo lao wenyewe au eneo lao wenyewe na maneno yanayohusu supu kutoka kwenye orodha hii na kumpatia rafiki acheze.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Mfano wa maneno yanayohusu supu**

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | I | M | B | A | B | D | E |
| T | N | Y | A | N | I | Y | C |
| S | U | N | G | U | R | A | Y |
| V | A | D | C | H | U | I | R |
| I | F | A | R | A | S | I | W |
| S | N | Y | O | K | A | U | M |
| D | O | P | M | B | U | Z | I |
| R | N | G | A | M | I | A | C |

**Maneno ya kutafuta kwenye maneno ya supu**

| | |
|---|---|
| **Mbuzi** | **Ngamia** |
| **Simba** | **Twiga** |
| **Nyoka** | **Nyani** |
| **Chui** | **Farasi** |

Unaweza kufanya shughuli hii iwe ya kusisimua zaidi kwa kuwauliza ‘Neno gani ambalo LINALOHUSIKA katika supu?’ Unaweza kutumia mchezo huu kwa maneno mengi mbalimbali na kwa masomo mbalimbali.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kiolezo wazi kwa ajili ya maneno ya supu ni hiki hapa chini. Unaweza kuongeza miraba zaidi au kuifanya iwe midogo zaidi ili kufanya mchezo uwe mgumu zaidi au mrahisi zaidi kutegemeana na umri na uwezo wa wanafunzi wako.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| | | | | | | | |

# Nyenzo Rejea 5: Wimbo wa kurukaruka maneno

**Nyenzo rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

**Wimbo wa Kiigbo wa kurukaruka maneno**
Ikuku buru gi
Zamiriza
Buru gi buru nwa nnegi
Zamiriza
Nwa nnegi idobere na ukwu osisi kporonku
Chọ ya ịhuyi ya (2x)
**Tafsiri ya Kiswahili**

**Acha upepo ukupeperushe**
Zamiriza
Ukupeperushe wewe na mdogo wako wa kike
Zamiriza
Yule mdogo wako wa kike yupo chini ya mti wenye matawi yote yenye kivuli
Unamtafuta mdogo wako huyo, huwezi kumpata (x2)

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 4: Utumizi wa hadithi na ushairi

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kutumia ushairi na hadithi kuhamasisha wanafunzi ili waandike?

**Maneno muhimu:** jina; sifa; mashairi; hadithi; wasifu, uandishi

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umetumia mashairi au hadithi za majina au za kusifu ili kuchochea mawazo ya wanafunzi ya uandishi;
- umetumia Nyenzo-rejea kama vile makala za kwenye magazeti ili kuchochea mawazo ya uandishi wa hadithi za maisha (wasifu);
- umetalii 'uandishi wa rasimu ' na 'uandishi wa kisanaa' wakati wa kuandika.

## Utangulizi

Afrika nzima, tuna utajiri wa fasihi simulizi na fasihi andishi kuhusu watu ambao bado ni muhimu au hapo zamani walikuwa muhimu kwa familia zao, jumuiya zao na nchi zao. Watu hawa hushangiliwa kupitia nyimbo na mashairi ya kuwasifu na hadithi zinazohusu maisha yao (wasifu). Kwa kutumia utajiri huu wa historia ya kitamaduni katika ufundishaji wako kunaweza kukusaidia ili kujua vitu vya kusoma kwa ajili ya lugha itakayotumika darasani na kuamsha mvuto wa wanafunzi katika uandishi.

## Somo la 1

Kama wanafunzi wanasikiliza na kusoma mashairi na hadithi wanazozifurahia, ni rahisi sana wakapenda kuendeleza stadi zao za usomaji na uandishi kwa kutumia lugha zao za asili au lugha wanayoitumia darasani.

Ili kuwa waandishi wenye mafanikio, wanafunzi wanahitaji 'zana' mbalimbali. Kwanza, wanahitaji mada ya kuandikia. Katika **Shughuli ya 1**, utatumia mifano ya mashairi ya majina au ya kusifu au hadithi ili kuwapatia wanafunzi mawazo. Kisha utawaongoza katika kuandika rasimu ya kwanza ya shairi la majina au la kusifu au hadithi. Hii ina maana kwamba itabidi kuandika matoleo kadhaa ya rasimu, ambayo yatazidi kuboreshwa, mpaka watakaporidhika kuwa shairi au hadithi zao ni nzuri na wanaweza kutoa toleo la mwisho.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kusoma na kuandika mashairi ya majina na hadithi katika warsha ya mwalimu

Katika warsha ya siku nne mjini Johannesburg nchini Afrika Kusini, baadhi ya walimu wa Kiingereza/Kiswahili walisoma mashairi na hadithi kuhusu majina. Katika warsha hii, waandishi walieleza jinsi walivyopata hayo majina yao, kitu walichokipenda au ambacho hawakukipenda kuhusiana na majina yao na maneno ambayo yalihusiana na majina hayo. Kwa kweli walimu walifurahia kile walichokisoma na kuomba iwapo wangeweza kupatiwa nafasi ya kuweza kuandika mashairi au hadithi zinazohusu majina yao wenyewe wakati wa warsha.

Siku ya pili, kila mwalimu alimsomea mwenzake rasimu yake ya kwanza. Walipeana majibu ya kile walichokipenda na kile ambacho walifikiri kinafaa kiboreshwe, kwa mfano kwa kuongeza maelezo na kuchagua msamiati tofauti au alama za uakifishi.

Siku ya nne, wakiwa wameshafanyia kazi rasimu zao siku moja kabla, kila mmoja alikisomea kikundi kizima shairi au hadithi ambayo ilikuwa imekamilika. Kulikuwa na kicheko, kulikuwa na machozi na kulikuwa na makofi mengi.

Walipoambiwa waakisi uzoefu wao, walisema:

- hakuna mtu aliyekuwa 'amekwama' kuhusiana na kitu/mada ya kuandikia;
- wakati wengi wao waliandika kwa Kiingereza, walifurahia mara kadhaa kutumia maneno au virai vya Lugha ya Kiafrika ili kueleza wazo fulani;
- walinufaika na matokeo ya rasimu zao za kwanza; walijisifu sana kutokana na toleo la mwisho; walifurahia kusikiliza hadithi/mashairi ya wengine;
- mengi ya mashairi yalikuwa yanafanana na yale mashairi na zile nyimbo za jadi za kusifu.

Walimu waliamua kuwasomea wanafunzi mashairi na hadithi zao pamoja na mashairi na hadithi nyinginezo za majina katika kuwasaidia ili waweze kuandika kuhusu majina yao.

## Shughuli ya 1: Kuandika rasimu ya mashairi au hadithi za majina

Ili kupata mawazo jinsi ya kuandaa shughuli hii, tumia **Nyenzo-rejea 1:** Kuandaa masomo juu ya mashairi ya majina au ya kusifu na **Nyenzo-rejea 2:** Mashairi na hadithi za majina au **Nyenzo-rejea 3:** Mashairi na hadithi za kusifu. Chagua ama mashairi/hadithi za majina au mashairi/hadithi za kusifu.

Waambie wanafunzi wapendekeze shairi/hadithi ya majina au shairi/hadithi ya kusifu itahusu nini.

Waambie wasikilize wakati wewe ukiwa unasoma shairi (ma)/hadithi uliyoandaa kwa sauti.

Waulize maswali kuhusu kile ulichowasomea.

Waambie wanafunzi wajadiliane na wenzao ama kuhusu kile wanachokijua kuhusu jina hili ulilowasomea, au kile wanachokijua kuhusu mtu, mnyama au kitu wanachotaka kukisifia.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Baadaye, waambie baadhi ya wanafunzi watoe ripoti ya mjadala wao darasani.

Waambie wanafunzi waandike rasimu ya kwanza ya shairi au hadithi kuhusu wao wenyewe au wanafamilia au kumsifu mtu, mnyama au kitu watakachokichagua.

Kusanya rasimu ili kutayarisha Shughuli Muhimu.

Je, kuandika mashairi/ hadithi za majina au za kusifu kunawapa wanafunzi mawazo ya kuandika?

Uliridhika na jinsi ulivyoendesha somo? Utafanya marekebisha gani wakati ujao?

Ukiwa na watoto wadogo zaidi, unaweza kuandika mashairi ya majina kwa pamoja, mkishirikishana mawazo na kutumia maneno yaliyozoeleka katika lugha inayotumika

darasani.

## Somo la 2

Baadhi ya hadithi za kwanza wanazozisikia watoto ni zile ambazo zinahusu uzoefu wa maisha ya familia au wanajumuiya. Hadithi za maisha ya watu mashuhuri (wasifu wao) mara nyingi huchapishwa katika magazeti na hata katika muundo wa vichekesho, hivyo, kama wanazisikia au wanazisoma, wanafunzi wengi watakuwa wana fununu juu ya hadithi kuhusu maisha. Huu ni mwanzo mzuri ili kuamsha hamasa ya kusoma na kuandika.

Darasani, wanafunzi wanahitaji msaada kutoka kwa mwalimu wao na kutoka kwa wenzao wakati wanapojifunza kuzungumza, kusoma na kuandika –hasa kama lugha hii ni ya nyongeza. **Uchunguzi Kifani 2** na **Shughuli 2** zinaonesha jinsi unavyoweza kuwapatia wanafunzi fursa ya kusoma, kuzungumza, kufanya kazi pamoja katika vikundi vidogo na kuandika rasimu za kwanza za hadithi za maisha ya watu wanaowapenda.

Wanafunzi wanahitaji mifano ili kuwaendeleza kama waandishi. Makala wanazozisoma zinaweza kuwasaidia katika kupangilia uandishi wao na kuwasaidia katika miundo ya sentensi na msamiati. Wanafunzi wadogo watakuhitaji wewe ili ufanye nao kazi, uwaongoze katika uandishi wao na polepole wapanue msamiati wao.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kutumia mambo yanayowavutia wanafunzi ili kuendeleza stadi za usomaji na uandishi

Bw. Simoni Raphaeli aligundua kuwa, katika uwanja wa mpira, baadhi ya wavulana wa darasa la 6 –ambao hawakuonesha kuvutiwa na usomaji na uandishi wakati wa masomo ya Kiingereza – mara kwa mara walikaa pamoja ili kusoma gazeti la soka, *Mwanaspoti*. Walimwambia Bw. Simon kuwa wanafurahia kutafuta taarifa zinazohusu maisha ya wachezaji wanaowapenda.

Hali hii ilimpa Simoni wazo. Aliwauliza wanafunzi wa darasa lake kama wameshawahi kusoma magazeti na, kama wameshawahi kuyasoma, walifurahia kusoma kitu gani. Wengi walisema kuwa walijaribu kusoma hadithi kuhusu watu ambao waliwavutia, hata kama hawakuweza kuelewa maneno yote. Simon aliandaa mkusanyiko wa magazeti kwa ajili ya darasa. Kisha aliwauliza wanafunzi kuhusu mambo waliovutiwa nayo na kuwafanya wasome magazeti hayo. Nyota wa michezo ndio waliopendwa zaidi (hasa wachezaji wa soka, pia mpira wa kikapu, mbio na ndondi), wanamuziki, nyota wa filamu na TV, wakifuatiwa na wanamitindo, wanasiasa, viongozi wa jumuiya na wafanyabiashara maarufu.

Simoni aliwapanga wanafunzi kufuatana na yale mambo yaliyowavutia. Kulikuwa na vikundi kadhaa vya nyota wa michezo na wanamuziki! Alikipatia kila kikundi magazeti na kuviambia vikundi vitafute makala/picha kuhusu mtu mmoja aliyewavutia wanakikundi. Kisha, kama kikundi, walisaidiana kuandika sentensi fupi moja au mbili kuhusu maisha ya mtu huyo. Walitumia maneno yao wenyewe na pia msamiati kutoka kwenye makala. Waliandika kichwa cha habari chao wenyewe.

Simoni aliridhika kuona kuwa wanafunzi wengi walishiriki katika usomaji na, wengine wakiandika sana kuliko wengine, wote walishiriki. Kila kikundi kilifurahia kusoma na kukisomea kikundi kingine wasifu wa kikundi.

## Shughuli ya 2: Usomaji na uandishi wa hadithi za maisha

Ili kuandaa shughuli hii tumia Nyenzo-rejea 4: Kuandaa msomo ya hadithi za maisha.

Waambie wanafunzi wasome kwa pamoja hadithi uliyoinakili ubaoni au kwenye karatasi. Au wasomee hadithi hiyo na eleza inahusu nini.

Jadilini sifa za hadithi za maisha (wasifu). Waulize wanafunzi wakuambie ni kategoria gani za watu (m.f. wachezaji wa taifa wa mpira wa miguu, wanamuziki wa jadi) ambao wanawapenda, na kwa nini.

Kipatie kila kikundi chenye mwelekeo wa aina moja magazeti mbalimbali ambayo yana makala kuhusu kategoria ambayo wanakikundi wanaipenda/wanaifurahia.

Waambie watafute makala kuhusu mtu kutoka katika kwenye kategoria waliyoichagua na watumie taarifa ili kuandika mambo mawili yanayomhusu mtu huyu (angalia Nyenzo-rejea 4 kwa mwongozo katika kuwasaidia wanafunzi wako kuweza kufanya kazi hii).

Kusanya rasimu hizi ili kuzitumia katika Shughuli Muhimu.

Kama darasa lako ni kubwa sana, ungeweza kufanya shughuli hii kwa kuhusisha nusu ya darasa au vikundi vidogo kwa zamu. Ungeweza pia kuwaweka wanafunzi katika vikundi kulingana na uwezo wao –ukichanganya wenye uwezo zaidi na wale wenye uwezo mdogo ili wasaidiane. Ukiwa na wanafunzi wadogo, unaweza kufanya kazi hii kama zoezi la darasa zima ambapo unawasaidia kunukuu mawazo yao na kushirikishana maneno yao.

## Somo la 3

Tunapoandika kitu, ni muhimu tuweke wazi kile tunachotaka kukisema. Tunatakiwa tupange. Baadaye, tunaanza kuandika na kusoma kile tulichokwisha andika. Tunaweza kuamua kubadili mpangilio wa baadhi ya maneno, kuongeza, kupunguza baadhi ya maneno na kuongeza au kubadili baadhi ya taarifa. Mwishoni, tunakagua uandisha ambao si sahihi, alama za kiuakifishi/uandishi au sarufi. Kazi ya mwisho inaweza kuwa tofauti kabisa na ile rasimu yetu ya mwanzo. Tunakuwa tumefanya uandishi wetu uwe wa kisanaa.

Katika darasa, kazi moja ingeweza kukamilika (yaani iwe imeandikwa kisanaa) kabla ya kuanza kazi nyingine. Uchunguzi Kifani 3 na Shughuli Muhimu hukuonesha jinsi ya kuandaa masomo ambapo wanafunzi wanatakiwa wafanye uandishi wao uwe wa kisanaa.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kushirikiana na mwenzako ili kuwasaidia wanafunzi katika uandishi

Bibi Dorcas Mabula na Bibi Beatrice Mntambo wanafundisha wanafunzi wa darasa la 6 katika Wilaya ya Kinondoni somo la Kiingereza. Huwapatia wanafunzi maoni ya kina kuhusiana na uandishi wao, hivyo wakati mwingine walimu hawa hubaki shuleni baada ya saa za shule na kushirikiana katika kusahihisha.

Siku moja mchana, kabla ya kuanza kusahihisha wakiwa wanakunywa Maltina, wote wawili walielezana kuwa walikuwa wanajisikia kuchanganyikiwa kutokana na baadhi ya wanafunzi kupuuzia maoni na masahihisho katika madaftari yao. Marafiki hawa waliona kuwa hali hii ilikuwa inatisha, kwa sababu waligundua kuwa maoni waliyowapatia katika rasimu ya kwanza katika kazi zilizotangulia yaliwasaidia kuboresha matoleo yao ya mwisho ya kazi kwa ajili ya kuendeleza kozi zao za kitaalamu. Baadaye Dorcas aligundua kitu muhimu! Wanafunzi wake hawakupata nafasi ya kufanya kazi nyingi zinazohusiana na kazi hii ya uandishi. Badala yake, kulikuwa na mada mpya katika kila somo la uandishi.

Alipomwambia Beatrice jambo hili, rafiki yake alikubali kuwa jambo hili pia lilitokea katika darasa lake. Hivyo ndivyo walivyofundishwa walivyokuwa shuleni!

Waliamua kujaribu mkabala mpya. Wakaamua kutumia masomo kadhaa kuandika rasimu na kuandika kisanaa andiko hilohilo. Wakawapatia wanafunzi mawazo ya kuwaongoza katika uandishi wao na katika marudio ya andiko hilo. Mwanzoni, wanafunzi hawakupenda kurudia kuandika andiko hilohilo, lakini walipoona jinsi kazi zao zilivyokuwa bora, walianza kulipenda zoezi hili.

## Shughuli muhimu: Kutoka kwenye uandishi wa rasimu wa mashairi/hadithi mpaka uandishi wa kisanaa

Kabla ya somo, soma rasimu za kwanza za wanafunzi na amua juu ya maswali ya jumla ya kuwauliza ili kuboresha kazi zao (angalia **Nyenzo-rejea 5: Maswali kwa ajili ya wanafunzi** ). Yaandike maswali haya ubaoni.

Warudishie wanafunzi rasimu zao, zikiwa na maoni ya jumla juu ya kile unachotaka kuhusu uandishi wa wanafunzi. Eleza kuwa sasa uandishi wao utakuwa wa kisanaa.

Waambie wasome tena rasimu zao za kwanza na watumie maswali yaliyoko ubaoni katika kuandika na kuboresha rasimu za pili.

Waambie wabadilishane na wenzao rasimu zao za pili na wapeane mapendekezo kwa ajili ya maboresho.

Waambie watumie mapendekezo haya kuandika toleo la mwisho. Zungukia darasa na toa msaada inapobidi. Wahimize watumie michoro katika uandishi wao.

Kama hakuna muda ili kumalizia shughuli hii katika muda wa kipindi darasani, waambie wanafunzi wamalizie shughuli hii nyumbani na watoe ripoti siku inayofuata.

Waulize jinsi mchakato huu wa kuandika rasimu ulivyowasaidia. Kulikuwa na maboresho yoyote katika uandishi wa wanafunzi kama matokeo ya mchakato wa wanafunzi wa uandishi wa rasimu na uandishi wa kisanaa? Unaweza kujenga mambo haya?

Ukiwa na wanafunzi wadogo au ambao hawajui sana lugha inayotumiwa darasani, ungeweza kufanya nao kazi ya kuandika rasimu na kuandika tena rasimu ya kazi rahisi kwa vipindi viwili – ukiwapatia muda katika somo ambao wataweza kutafakari kile ambacho walitaka hasa kukisema.

## Nyenzo-rejea ya 1: Kuandaa masomo juu ya mashairi ya majina au ya kusifu

**Usuli/welewa wa somo wa mwalimu**

Amua kama unataka kuchagua mashairi/hadithi za majina au za kusifu ili kuzifanyia kazi na wanafunzi wako.

1. Chagua mfano mmoja au zaidi kutoka Nyenzo-rejea 2 au 3 AU kutoka katika Nyenzo-rejea nyingine ulizonazo AU andika shairi au hadithi yako mwenyewe.
2. Andika shairi (ma)/ hadithi hiyo au hadithi hizo kwenye karatasi kubwa au ubaoni ili unapozitumia darasani wanafunzi waweze kusoma chapa kubwa pamoja na wewe na baadaye waweze kurejelea mashairi na hadithi hizo wanapoandika mashairi au hadithi zao wenyewe. Kama huna karatasi kubwa, andika kwenye ubao wako.

Andaa maswali ya kuwauliza wanafunzi kuhusu shairi (ma)/hadithi. Kwa hakika, aina ya swali itategemea kile ulichokichagua.

Kwa mfano, kama utachagua shairi la Thabo, ungeweza kuanza na:

‘Unagundua nini kuhusu jinsi shairi hili lilivyoandikwa?’ (Jibu: Kila mstari umeanza kwa herufi moja ya jina la Thabo).

Ukichagua hadithi ya kusifu ya Hugh Lewin kuhusu mama yake Jafta, ungeweza kuuliza: ‘Ungependa kuwa na mama kama mama yake Jafta? Nipatie sababu ya jibu lako.’

Ukishamaliza maandalizi haya, uko tayari kufundisha masomo kuhusu mashairi na hadithi za majina na za kusifu. Wanafunzi wanapoanza kuandika, zungukia darasa ili kumsaidia yeyote ambaye atapata shida katika kuanza. Wengine watahitaji msaada wa mawazo, wengine shida ya msamiati.

Nyenzo-rejea 2 na 3 zote ni mashairi, nyimbo na hadithi za kusifu lakini lugha ni ngumu kwa baadhi yazo kuliko nyingine.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Nyenzo-rejea ya 2: Mashairi na hadithi za majina

**Nyenzo rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

**Shairi la majina lililoandikwa na mwalimu nchini Tanzania:**

***Hanna – Jina langu la Sifa*** **lililoandikwa na Hanna Simpassa**

Fahari ya moyo wangu –
Nani alileta jina hili?
Nililipataje?
Hakuna hata mmoja katika familia aliyeliota – ila mimi!
Jina langu la Kikristo.

Wazazi wangu hawakulichagua – Nililiunda,
Zamani kabla sijawa Muislamu.
Hasina – jina linalomaanisha uzuri.
Hasina – jina langu maalumu.

Roho ziliniambia katika ndoto
Umebadilishwa dini kuwa Mkristo
Hanna ni jina lako.
Hanna – jina linalomaanisha ‘Neema, huruma na sala’.

Yeye ni wa thamani kama almasi,
Hujua thamani ya kujitoa,
Kamwe hakati tamaa,
Anapata marafiki kwa urahisi,
Furaha ni nguvu yake,
Kicheko chake ni dawa nzuri;
Mtu ambaye asili yake ni maarifa thabiti.
Yeye ni mtoto wa ulimwengu.

Hivyo nilibadilishwa dini

Hasina kuwa Hanna

Na ninajivunia jina langu

**Shairi la jina lililoandikwa na mwalimu nchini Afrika Kusini**

**Mawazo kuhusu herufi za jina langu na Thabo X**

T inasimama badala ya thabiti – Mimi ni mtu imara

H kwa ajili ya hafukasti – baba na mama yangu wana asili tofauti

A ni aminifu…

Bora

Ona nilivyo–ni mimi hasa!

**Hadithi ya jina iliyoandikwa na mwalimu nchini Tanzania:**

***Hadithi ya kupewa jina niliyohadithiwa na*** **Nyalupala Mtavangu**

Zamani, katikati ya kiangazi, babu yangu, wakati huo alikuwa anaitwa Nyalukolo, alikwenda mtoni ili kukamilisha sherehe za matambiko. Pale mtoni alitokea simba mkubwa ambaye alikwenda kunywa maji. Mnyama huyu alimshambulia, na Nyalukolo alipambana naye. Aliwaua wanyama wengi wa mwituni na haraka alikimbilia nyumbani kumwambia baba yake kuhusu kitendo hiki cha ushujaa cha kushangaza.

Baba yake, Mungai, alituma ujumbe kijiji kizima na watu walikimbilia mtoni. Ilikuwa kweli – simba aliyekufa alikuwa amelala pale chini!

Tangu siku ile, Nyalukolo alipata heshima kutoka kwa kila mtu ambaye alijua alichokifanya. Wanaume na wanawake, vijana na wazee, walimheshimu. Katika sehemu nyingine walimtania kichinichini 'Nyalupala'. Jina hilo la minong'ono lilimfikia baba yake, Mungai, ambaye aliamua kuita watu wa kabila lile pamoja kwa ajili ya sherehe ya kubadili jina. Nyalukolo aliitwa Nyalupala rasmi, kwa maana ya 'simba' katika lugha ya Kihehe.

Wakati nilipozaliwa, katikati ya karne ya 20, nilipewa jina la babu yangu. Ni jina ninalolihusisha na ushujaa na ushupavu wa mzimu wangu na ninajivunia jina hili.

# Nyenzo-rejea 3: Mashairi na hadithi za kusifu

**Nyenzo rejea ya mwalimu kwa ajili ya kupanga au kurekebisha ili kutumia na wanafunzi**

**Shairi la Kiyoruba la kusifia chatu**

Baadhi ya ushairi wa kusifu husifia wanyama au vitu kuliko watu. Hapa pana shairi kutoka kwa Wayoruba wa Naijeria. Maelezo kwa baadhi ya lugha iliyotumika yametolewa baada ya shairi hili.

**Chatu**

Mwana wa mfalme mwenye mikogo [Mstari 1]

Mkubwa miongoni mwa nyoka.

Wanasema chatu hana nyumba.

Nilisikia maneno haya zamani

Na nilicheka nikacheka na kucheka.

Kwani ni nani anamiliki ardhi chini ya nyasi za mlimao? [Mstari 6]

Nani anamiliki ardhi chini ya nyasi za tembo?

Nani anamiliki kinamasi – baba wa mito?

Nani anamiliki dimbwi lililosimama – baba wa maji?

Kwa sababu hawatembei kwa kuongozana [Mstari 10]

Watu wanasema kuwa nyoka hutembea tu pekee pekee.

Lakini hebu fikiria

Chukulia kipiribao atembee mbele ya wote

Hongo afuatie

Na chatu atambae akinguruma nyuma yao [Mstari 15]

Nani atakuwa jasiri

Kuwasubiri?

Tini

1. Kutembea kwa mikogo ni kutembea kwa kujivuna – ukidhani kuwa wewe ni bora kuliko wote, kujidai. Katika mstari 1, shairi linamweleza chatu kama mtoto wa mfalme mwenye mikogo.
2. Maswali yaliyopo kwenye mstari wa 6 hadi wa 9 inaonesha kuwa chatu ana nyumba nyingi – sehemu zote mbili; katika ardhi na kwenye maji.
3. Katika ubeti wa pili, shairi linaonesha kuwa wanyama na watu wengine wangeogopa sana kutembea karibu na nyoka – ndio maana nyoka 'hutembea' pwekepweke.

**Hadithi ya kumsifu mama**

Mama na Hugh Lewin

Ningependa wewe, alisema Jafta, ukutane na mama yangu. Hakuna yeyote kati ya watu ninaowafahamu ambaye ni kama mama yangu. Mama yangu ni kama ardhi – amejaa mambo mazuri, mwenye joto na nguvu, na wa rangi ya kahawia. Mama yangu ni kama jua linalochomoza alfajiri, likiangaza sehemu zenye giza na kutuamsha likitubembeleza taratibu.

Huchochea moto ili uwake na baada ya muda kila mahali panajaa harufu ya chakula, ambayo hulifanya tumbo langu lingurume na kunifanya nitake kuamka.

Jinsi jua linavyoaanza siku yake na maua yakichanua na kurusha maua hayo angani ninamkumbuka mama yangu. Kama lilivyo anga, daima yeye yuko pale. Daima unaweza kumwangalia na kumwona.

Mchana jua linapokuwa kali, hutupatia kivuli na kutuburudisha, kama mti ulioko kwenye mto. Au wakati hali ya hewa inapokuwa na joto sana na vurugu, anatupoza kama mvua ifanyavyo inapoondoa vumbi kwa njia ya mawimbi, na kunyeshea nyasi na kuzifanya tena za kijani.

Halalamiki mara kwa mara, hata katika saa mbaya. Lakini kuwa makini! Akikukamata unafanya mchezo wa kudang'anya, au kuwachokoza wadogo zako wa kike, anaweza kutoa sauti kama ya radi ya mchana na macho yake yakatoa mwanga kwenye mawingu meusi.

Mama yangu hakasiriki mara kwa mara, alisema Jafta, ila ni vema zaidi anapoimba. Anatuimbia anapopika mlo wa jioni. Kama umeshawahi kusikia hopoe akiita kwenye mahindi, basi utakuwa umeshasikia mama yangu akiimba.

Baada ya mlo wa jioni, unafuata muda wa hadithi. Kwa kiasi fulani, alisema Jafta, takriban ninampenda mama wakati huo kuliko wakati wowote – baada ya kula chakula, na pilikapilika za hapo, pindi jua linapokuchwa na kila kitu ni kitulivu na kimepoa. Hapo mama hutukumbatia na kuondoa masikitiko yetu. Tunazungumzia ya leo, ya kesho, na hasa ya kesho.

Kisha blanketi la usiku linapofunika dunia, na mwezi ukiwa juu yake, mama yangu hutufunika kwa uangalifu na kutubusu na kututakia usiku mwema; hutulaza.

*Vyanzo vya asili:*

***Chatu** imechukuliwa kutoka English Matters, Grade 7 Anthology, iliyokusanywa na Lloyd, G. & Montgomery, K.*

*Mama na Hugh Lewin imechukuliwa kutoka New Successful English, Reading Book, Grade 6*

# Nyenzo-rejea 4: Kuandaa masomo juu ya hadithi za maisha

**Usuli/welewa wa somo wa mwalimu**

1. Kusanya Nyenzo-rejea utakazozihitaji. Kazi hii inaweza kuchukua muda, lakini magazeti na vichekesho unavyokusanya vinaweza kutumika kwa masomo ya lugha nyingi mbalimbali pamoja na zile za usomaji na uandishi wa hadithi za maisha. Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuleta magazeti kutoka nyumbani, hivyo waambie waziombe familia zao ruhusa ya kuchukua magazeti hayo. Waombe wenzako na rafiki zako wakukusanyie magazeti ambayo wameshamaliza kuyasoma. Katika baadhi ya nchi, wachapishaji wa magazeti huweza kutoa msaada wa nakala za magazeti kwa shule yako. Baadhi ya AZAKI pia zina machapisho mazuri sana. Kwa mfano, makala kuhusu maisha ya Julius Nyerere yanapatikana kutoka magazeti mbalimbali ya Kitanzania na nchini Afrika Kusini ucheshi kuhusu maisha ya Nelson Mandela unapatikana katika Mfuko wa Nelson Mandela.
2. Kabla ya kuanza masomo haya lazima uwe na vitu vya kutosha vya kusoma kuhusu aina mbalimbali za watu maarufu kwa ajili ya kufanyiwa kazi na kila kikundi cha wanafunzi.
3. Nakili katika karatasi kubwa au ubaoni, hadithi ya maisha ya Freddy Macha (wasifu ufuatao hapa chini) AU hadithi nyingine utakayoichagua ambayo imeandikwa kwa kutumia lugha rahisi.
4. Tengeneza orodha ya vipengele vinavyofanana vya hadithi hizi za maisha ili kuvijadili pamoja na wanafunzi wako. Hivi hujumuisha:
   I. kwa kawaida usimulizi wa hadithi huzingatia mfuatano wa wakati toka miaka ya awali mpaka ya baadaye ya maisha ya mtu;
   II. hudokeza mafanikio ya maisha ya mtu;
   III. hutoa maelezo ya kina ya kitu fulani kinachovutia au cha kushangaza kuhusu maisha ya mtu.

Sasa uko tayari kuanza somo!

**Waongoze wanafunzi wakati wanapoandika hadithi kuhusu maisha**

Wakati wanafunzi wanafanya kazi katika vikundi vyao, zungukia darasa ili kukagua kama wameelewa kazi hiyo na wanaweza kupata makala za kutumia. Ungeweza kuandika ‘orodha-kaguzi’ ubaoni ili kuwaongoza wanafunzi katika uandishi wao. Kwa mfano:

jina(ma) ya mtu huyo;

sehemu aliyozaliwa;

maelezo ya familia;

‘historia’ – siku za shule, mafanikio ya awali, mafanikio ya baadaye;

Vitu vya kuvutia/vya kuhuzunisha/vya kushangaza ambavyo vimetokea katika maisha ya mtu huyo.

Wahimize wanafunzi wafikirie kuhusu utaratibu watakaoutumia ili kuandika habari za mtu huyo na kutumia maneno yao wenyewe. Wasinakili tu kutoka kwenye makala.

**Hadithi ya maisha ya Freddy Macha (wasifu)**

Freddy Macha alizaliwa katika miteremko ya mlima Kilimanjaro nchini Tanzania. Yeye ni mwandishi wa nathari, ushairi, tamthiliya na nyimbo, na pia ni mpiga-ala mbalimbali, mwimbaji na mwigizaji.

Akiwa na umri wa miaka 13, Freddy alianza kuimba na kuigiza jukwaani. Katika miaka ya 1970 na 1980, alikuwa anaishi na kufanya kazi kama mwandishi wa habari jijini Dar es Salaam na alikuwa na vitabu vyake alivyochapisha vikiwemo *Twenzetu Ulaya* (mkusanyiko wa hadithi za Kiswahili ), wasifu wa mwana muziki maarufu Remi Ongala na mkusanyiko wa mashairi yanayoitwa *Papers! Papers! Papers!* Freddy alishinda tuzo ya BBC ya ushairi mwaka 1981 na mashairi hayo yalitokea katika mkusanyiko *Summer Fires*.

Mwaka1984, Freddy alifanya ziara iliyokuwa ya mafanikio katika nchi za Skandinavia ikiwa ni pamoja na Tamasha la Kimataifa la Thieta la Oslo pamoja na kikundi chake cka Kitanzania cha Sayari. Baadaye, kwa kipindi cha miaka mine tangu 1988, Freddy alikuwa anaongoza kikundi cha bendi cha rege kilichoitwa ‘reggae-afro-funk band Os Galas’, cha Brazili.

Freddy alikwenda Uingereza mwaka 1996 na alifanya miradi mingi ikiwa ni pamoja na warsha, drama na muziki. Kwa kutembelea sehemu nyingi, Freddy huzungumza na kuigiza kwa kutumia lugha mbalimbali. Tangu 1998 mpaka 2001, katika miji ya Stoke Newington na Brixton, Freddy amefanya tamasha maarufu katika Baa ya Lorca lililoitwa Usiku wa Muziki wa Dunia ambapo wanamuziki waliweza kukutana na kujaribu vifaa vipya. Hili lilijulikana kama 'the local WOMAD' na gazeti la ‘*The Hackney Gazette’* na ndiyo sababu muhimu kwa Freddy kuwa Mwakilishi wa Umoja wa Wanamuziki wa Dunia kwa upande wa sehemu ya muziki wa Jadi na wa Kimapokeo mwaka 1999–2001.

Hivi sasa, Freddy anaweza kuendesha warsha na matamasha mbalimbali mashuleni na katika kumbi za Uingereza. Alitunga kichekesho cha kitashtiti kinachoitwa ‘*News No News’,* ambacho wakati mwingine anakiigiza peke yake au na bendi yake ya Kitoto. Bendi ya Kitoto imeundwa na wanamuziki sita kutoka sehemu mbalimbali za Afrika, Karibiani, nchi za Uingereza na Amerika Kusini.

Nchini Uingereza, Freddy ametoa rekodi mbili: albamu inayoitwa *Constipation* (2000) yenye miziki 11 na wimbo mmoja unaoitwa *Kilimanjaro*. *Constipation* ina muziki, nathari na ushairi na inatumia lugha mbalimbali, ambayo imetengenezwa kutokana na utaalamu wa Freddy. Kwa mfano, kuna aina mbalimbali za nyimbo nzuri za Kiswahili na nyimbo za Kiingereza ambazo zinatoa mafunzo mazito kuhusiana na jamii. Freddy anafanya kazi sana za kutoa albamu mpya kwa ajili ya watoto wa shule. Matarajio ni kwamba albamu hiyo itakuwa bora kama *Constipation.*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Sehemu ya 5: Kubadilisha hadithi simulizi, mashairi na michezo kuwa vitabu

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kusaidia ujifunzaji wa lugha kwa kutunga na kusanifu vitabu?

**Maneno muhimu:** uandikaji; uchoraji wa vielelezo; usanifu; kitabu; gamba la kitabu (jalada la kitabu)

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Kutumia njia ya majadiliano kwasaidia wanafunzi kuelewa uhusiano na tofauti zilizopo kati ya matini simulizi na matini andishi;
- Kukuza njia ambazo wanafunzi wanaweza kuzitumia kubadilisha hadithi simulizi, mashairi, nyimbo au michezo kuwa katika maandiko na vielelezo;
- Kutalii jinsi ya kutoa vitabu vya hadithi, mashairi, michezo na nyimbo kwa ajili ya maktaba ya darasa.

## Utangulizi

Kipengele kimojawapo cha kufundisha ni kwa wanafunzi kuona lengo halisi la kazi unazowapa. Kwa kuwasaidia wanafunzi kutengeneza vitabu kwa ajili ya maktaba ya darasa, utakuwa umewapa sababu ya kuwa waangalifu katika maandishi na michoro yao. Hali hii itawasaidia kuthamini lugha zao za nyumbani na lugha ya mawasiliano darasani au lugha ya ziada. Vitabu vinaweza kuandikwa katika lugha yao ya nyumbani, lugha ya mawasiliano darasani au lugha ya ziada. Zaidi ya lugha moja inaweza kutumika katika kitabu kile kile. Vitabu wanavyoandika wanafunzi, kwa msaada wako, vitakupa matini zaidi kwa ajili ya shughuli za kusoma.

## Somo la 1

Wanafunzi wanaozungumza lugha ya nyumbani ambayo ni tofauti na wanayotumia darasani wanahitaji kujua kama unaithamini lugha yao ya nyumbani. Hii ni muhimu kwa kuwa lugha ya nyumbani ni sehemu ya mtu alivyo. Njia mojawapo ya kueleza hili ni kuwahimiza wanafunzi wako kutoa hadithi na vitendawili, kughani mashairi, kuimba nyimbo na kueleza michezo katika lugha za nyumbani na kisha kuziandika, ama kwa lugha zao za nyumbani au lugha nyinginezo.

Katika Shughuli 1, uwasaidie wanafunzi wako kugundua tofauti kati ya matini simulizi na andishi. Utawahimiza kufikiri kuhusu yaliyo na thamani katika utamaduni simulizi, kwa nini watu huandika na lugha zipi hutumika katika mazungumzo na katika maandishi.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kusimulia hadithi katika lugha za nyumbani; kuziandika katika lugha ya mawasiliano darasani

Hivi karibuni Bwana Okitikpi, mwalimu mzungumzaji wa lugha ya Kiyoruba, amehamishiwa Kaskazini mwa Nijeria katika jamii izungumzayo lugha ya Kihausa ikiwa lugha kuu, lakini baadhi ya wanafunzi wanazungumza lugha tatu za Kinijeria. Wazazi wachache na vijana watu wazima wamekubali kuwa walimu 'wasaidizi'. Wanafahamu Kihausa na Kiingereza kidogo na wanamsaidia Bwana Okitikpi kujifunza Kihausa ili aweze kwasiliana na wanafunzi vyema. Kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wake wanaweza kuzungumza lugha tatu za Kinijeria, Bwana Okitikpi amewahusisha wasaidizi hawa katika shughuli za utambaji wa hadithi ili kujenga kujiamini kwa wanafunzi katika uzungumzaji na kuwaonesha kuwa lugha zao za nyumbani zinathaminiwa.

Anataka wanafunzi kuandika hadithi, hususan katika lugha zao za nyumbani. Hata hivyo baadhi ya lugha hizo hazina mfumo wa maandishi, kwa hiyo ameamua waandike hadithi zao kwa kutumia lugha ya Kihausa.

Mmoja wa wasaidizi wake amejadiliana na wanafunzi kuhusu sababu za watu kuandika hadithi. Kisha, wanaandika hadithi wanayoipenda sana, kwa kutumia lugha ya Kihausa, ili waiweke katika kitabu kwa ajili ya maktaba ya darasa.

Bwana Okitikpi aliwaweka wanafunzi wake katika vikundi kwa ajili ya shughuli hii, akihakikisha kuwa angalau mwana-kikundi mmoja ni mzungumzaji mzuri wa lugha ya Kihausa na anaweza kuwasaidia wengine. Pia alimtaka msaidizi wake amsaidie kuangalia mchakato wa uandishi.

## Shughuli ya 1: Uandishi wa fasihi simulizi na michezo

Kwanza, soma Nyenzo-rejea 1: Jinsi hadithi zinavyoandikwa katika vitabu, na fikiria juu ya majibu ya maswali matano kwa ajili ya wanafunzi.

Watake wanafunzi wakueleze vichwa vya habari vya hadithi, mashairi, nyimbo na michezo katika lugha za nyumbani. Viandike ubaoni.

Jadili maswali haya na wanafunzi:

Je, matini hizi za lugha ya nyumbani zimeandikwa katika vitabu? Kwa nini watu huandika hadithi, mashairi, nyimbo na michezo katika vitabu?

Ungependa hadithi, mashairi, nyimbo na michezo ya lugha yako ya nyumbani kuandikwa katika vitabu? Kwa nini iandikwe au kwa nini isiandikwe?

Ni katika lugha ipi au zipi ambazo ungeandika mashairi, hadithi na michezo katika kitabu?

Vitabu vinaandikwaje na vinatolewaje? Waambie wanafunzi watakuwa wanaandika vitabu kwa ajili ya maktaba yao ya darasa.

Watake wanafunzi kila mmoja kuchagua hadithi aipendayo na kuandika mswada wa jaribio la kwanza katika lugha aipendayo.

Umefurahia majadiliano?

Wanafunzi wamefanyaje katika shughuli hii?

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Somo la 2

Baadhi ya ujifunzaji, kama kujifunza kucheza ala za muziki, kutumia kompyuta au kuendesha gari, huhitaji mazoezi mengi. Kama mwalimu, unahitaji kuwapa wanafunzi nafasi ya kurudia na kufanya mazoezi ya kile walichokwishafanya kabla ili waweze kufanya maendeleo katika juhudi zao za mwanzo. Wakati ambapo Shughuli 2 katika sehemu hii inafanana na Shughuli muhimu katika Sehemu 4, marudio haya ni muhimu. Wanafunzi watajifunza kuwa uandishi ni mchakato, na kuwa hadithi, mashairi na maelekezo yao ya michezo yaliyoandikwa yatawapa wengine furaha zaidi kama zitaandikwa kwa makini.

Kuandika, kuchora vielelezo na kusoma vitabu hivi yanaweza kuchukua masomo mengi, lakini kwa kuwa shughuli hizi huwezesha nafasi nyingi za kazi za lugha , muda utatumika vizuri. Unaweza kutumia Nyenzo-rejea 2: Orodha ya kupimia ya wanafunzi ili kuwasaidia kutathmini kazi zao. Uchunguzi-kifani unaelekeza jinsi walimu wanavyoweza kuandika vitabu pamoja na wanafunzi ambao hawajapata ujuzi wa kutosha wa uandishi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kuwasaidia wasomaji na waandishi chipukizi jinsi ya kuandika kitabu cha hadithi

Mwalimu Goodluck Nkini anawafundisha kwa pamoja wanafunzi 60 wa darasa la 1 na la 2, katika shule mojawapo karibu na mji wa Kigoma. Mwalimu mwenzake anafundisha wanafunzi 48 wa darasa la 3 na la 4. Mara kwa mara walimu hawa wawili huwakaribisha wazazi shuleni kusimulia hadithi kwa lugha ya Kiha.

Mwalimu Goodluck Nkini aliwataka wanafunzi kumsaidia kugeuza hadithi wanayoipenda, ambayo wamesaidia kuitunga, ili iwe kitabu.

Kwanza alitengeneza daftari kubwa lisiloandikwa chochote (Angalia **Nyenzo-rejea 3: Kubadilisha hadithi za wanafunzi kuwa 'kitabu kikubwa'** ).

Aliandika hadithi kwa kutumia vifungu na sentensi fupifupi. Halafu aliamua mahali ambapo kila kifungu au sentensi iwekwe wapi katika lile daftari kubwa. Alitumia rangi nyeusi pamoja na nta kuandika hadithi kwa herufi kubwa nzuri, akiacha nafasi kwa ajili ya picha.

Aliwaonesha wanafunzi kitabu darasani, na kusoma nao hadithi. Alijadiliana nao aina ya picha zilizotakiwa katika kila ukurasa. Aliwapa kila wanafunzi katika jozi vipande vya karatasi, na jozi mbili za wanafunzi walichora picha katika kila karatasi kati ya karatasi 15.

Aliwataka wanafunzi kutafuta ukurasa unaofaa kwa kila picha, na kuwasaidia kugundisha picha hizo katika kitabu.

## Shughuli ya 2: Ustadi wa kuandika rasimu ya kwanza na kusanifu vitabu

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Watake wanafunzi katika vikundi vya watu wanewane kusoma rasimu ya kwanza ya hadithi zao (kutoka Shughuli 1). Watake wachague rasimu mbili (kutoka katika zile nne) za kufanyia kazi katika jozi ili kuziboresha. Wanatakiwa kutumia orodha ya kupimia ya wanafunzi katika Nyenzo-rejea 2 ili kuwaelekeza jinsi ya kufanya kazi zao.

Hatua nyingine ni kuwataka waioneshe katika kundi la jozi nyingine ya wanafunzi kwa ajili ya kuiboresha.

Sasa kusanya kazi zao na sahihisha makosa ya tahijia, sarufi na vituo vya uandishi.

Halafu vipe vikundi kitabu chao kisichoandikwa kitu chochote (Angalia Nyenzo-rejea 3) na watake wafanye yafuatayo:

- wapange ni sentensi zipi ziwe katika kila ukurasa na michoro iwe wapi;
- waamue jinsi ya kugawa kazi za maandishi na michoro, ili kila mwana-kundi anashiriki.

Watake waoneshe mpango wao; jadiliana nao na watake watekeleze mpango wao.

Kwa wanafunzi wadogo, mnaweza kuandika hadithi pamoja katika kitabu kikubwa na baadaye wanafunzi wanaweza kuchora kwa kila ukurasa.

## Somo la 3

Mawasiliano sio kuhusu maneno tu. Siku hizi magazeti mengi yana picha nyingi kuliko zamani na vitabu vya siku hizi vina vielelezo vingi zaidi kuliko vitabu vya zamani. Watoa matangazo hutumia picha katika mabango, katika majarida na katika televisheni (luninga) ili kuuza bidhaa zao. Skrini za kompyuta huchanganya maneno na picha katika hali ya kusisimua. Wanafunzi wanahitaji kuandika na kusoma matini ambazo zinachanganya maelezo ya mazungumzo (maneno) na michoro (picha). Ukiwa mwalimu majukumu yako ni:

Kuwa na habari za sasa za mambo yanayowafurahisha wanafunzi;

Ukijumlisha na shughuli za michoro ya ubunifu (kwa mfano, ubunifu wa michoro ya vifurushi vya kuchukulia bidhaa za madukani, mabango ya matangazo, matangazo ya biashara) katika lugha na masomo ya kusoma na kuandika.

Sehemu hii inazingatia uchoraji wa gamba la vitabu vya watoto vinavyohusu hadithi, mashairi, nyimbo na michezo.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kujadili na kutengeneza magamba ya vitabu

Mwalimu Malaitji anawahimiza wanafunzi wake wa somo la Kiingereza wa darasa la 6 kuuliza maswali wakati wa somo lao la kusoma kuhusu maneno na misemo ambayo wanaisikia au kuisoma lakini hawaielewi. Siku moja asubuhi, mwanafunzi aliliambia darasa kuwa amesikia mhusika mmoja wa mchezo wa kuigiza katika televisheni akimwambia mwenzie kuwa 'Usihukumu kitabu kwa kuangalia gamba lake.' Mwalimu Malaitji aliwauliza wanafunzi wake mawazo kuhusu msemo huo una maana gani na kwa nini ulitumika katika mchezo huo wa kuigiza. Baada ya muda mfupi wa majadiliano, wanafunzi walielewa kuwa uchoraji wa gamba la kitabu unaweza au usiweze kutoa wazo zuri kuhusu yaliyomo katika kitabu. Kwa mtazamo huo, mtu aonekanavyo au asemavyo inaweza isiwe kielelezo cha jinsi mtu huyo alivyo 'ndani mwake'.

Mwalimu Malaitji aliamua kuendeleza majadiliano. Aliwataka wanafunzi darasani kufikiri kuhusu shabaha za gamba la vitabu, halafu waangalie gamba la kitabu cha hadithi ambacho alileta darasani. Wanaweza kueleza kuhusu hadithi inahusu nini kwa kuangalia gamba la kitabu? Wamependa nini au ni kitu gani ambacho hawakukipenda kuhusu gamba hilo la kitabu? Gamba hilo linaweza kuboreshwa, na kama jibu ni ndiyo, linaweza kuboreshwaje? Baada ya mjadala hai na kusoma hadithi kwa wanafunzi, aliwataka wafanye kazi katika vikundi vya wanafunzi wanewane kutengeneza gamba jipya kwa ajili ya kitabu hiki na aliwapa makaratasi ya kufanyia kazi. Walipomaliza, mwanafunzi mmoja kutoka kila kikundi alitoa maelezo darasani kwa nini wamechora gamba la kitabu katika namna waliyochagua. Mwalimu Malaitji aliyabandika magamba ya vitabu katika ukuta wa darasa.

## Shughuli muhimu: Kuandika vitabu na kutayarisha gamba la vitabu

Baada ya kumaliza kuandika na kuchora kwa ajili ya vitabu vya hadithi, wanafunzi sasa wako tayari kutayarisha gamba la kitabu. Unaweza kutumia migongo ya mabango, karatasi za maboksi na vifaa vingine 'vilivyotupwa', hasa kama vifaa havitoshi shuleni kwenu. Tazama **Nyenzo-rejea muhimu: Kuwa mwalimu mwenye msaada katika hali zenye changamoto kwa mawazo zaidi.**

Waoneshe watoto magamba ya vitabu na waulize sifa nzuri za gamba hilo (Tazama Nyenzo-rejea: Sifa za matayarisho ya gamba la vitabu).

Watake kila kikundi kutayarisha gamba la kitabu chao. Wanapaswa kukubali kuhusu maneno watakayotumia, michoro na sehemu watakapoiweka na kuamua waamue nani ataandika au kuchora kila sehemu ya gamba.

Zungukia vikundi kujadiliana matayarisho yao na wasaidie na kuwaongoza wanapotengeneza gamba lao la kitabu

Vipe muda vikundi kukamilisha vitabu vyao.

Mtake mwanafunzi mmoja wa kila kikundi kuonesha kitabu chao na wahimize wanafunzi wengine katika vikundi kukisoma.

Viweke vitabu katika maktaba ya darasa.

Unafikiri wanafunzi wako wamejifunza nini katika shughuli hii?

Je, vitabu hivyo vilisomwa na wanafunzi wengine vilipowekwa katika maktaba ya darasa?

Kwa watoto wadogo, soma hadithi au mashairi na watake wachore picha kwa ajili ya gamba la kitabu au ndani ya kitabu.

## Nyenzo-rejea 1: Jinsi hadithi zinavyoandikwa kuwa vitabu

**Usuli wa welewa kwa ajili ya mwalimu**

Uandishi wa kitabu kwa ajili ya darasa lako sambamba na shughuli zao za kawaida ili za usomaji na uandishi huwapa wanafunzi welewa wa umuhimu wa kuweza kusoma kupata taarifa na hadithi mpya. Mchakato huu unaweza kuwahimiza wanafunzi wako kutaka kusoma zaidi kwa kuandika kitabu kwa ajili ya darasa kwa kutumia michoro/picha zao na maneno yao wenyewe kadiri wanavyokuwa waandishi hodari.

**Hatua ya 1: Vitabu huanza na wazo kuu**

Mwandishi huandika hadithi. Huenda mwandishi ataandika rasimu kadhaa za hadithi, akijaribu kuiboresha kila mara. Mara nyingi waandishi hufanya uchunguzi kwa ajili ya hadithi zao kuhakikisha kuwa wanaandika maneno kwa tahijia sahihi na uhakika wa mambo wanayoyaandika. Wakati mwingine inamchukua mwandishi majuma kadhaa kabla ya kupata njia sahihi ya kuandika hadithi yake. Mwandishi anaporidhika, ataandika maneno yake katika muswada, ambayo ataituma kwa mhariri wake katika jumba la uchapishaji

**Hatua ya 2: Wahariri wana majukumu mengi, na wanapaswa kusoma SANA.**

Miswada hupokelewa kila siku kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Wahariri wanapaswa kuichambua na kuamua ni hadithi zipi wanazofikiria kuchapisha. Wahariri hufurahia kuwaambia waandishi kuwa wanataka kuchapisha hadithi zao. Na bila shaka mwandishi husisimka! Mhariri huamua pia nani atachora michoro ya muswada. Si kawaida kufikiri kuwa kwa baadhi ya vitabu mhariri na mchoraji hawakubaliani! Wakati mwingine mhariri husaidia mawasiliano.

**Hatua ya 3: Kuanza kazi kwa msanii.**

Kabla ya mwandishi kuanza kuandika hadithi, hufikiria ukubwa wa kitabu utakuwaje, halafu hupanga karatasi. Hutengeneza mfano wa kitabu, kikiwa na vielelezo vya awali, ili kumuonesha mhariri na msanii wa kitabu. Katika hatua hii, mhariri anaweza kufanya mabadiliko katika matini ya hadithi. Wahariri ni wazuri katika kuwasaidia waandishi kupata namna bora ya kujieleza.

**Hatua ya 4: Kuhusika kwa msanifu wa kitabu.**

Msanifu huangalia kitabu cha mfano, na hutoa mapendekezo kwa ya michoro. Hutafuta pia aina za maandishi za kutumia katika kitabu. Mtindo na ukubwa wa herufi unaweza kuleta tofauti kubwa katika muonekano wa kitabu. Msanii anaweza pia kumsaidia mchoraji kuamua jinsi maneno ya hadithi yatakavyofaa katika muono wa kitabu. Halafu hadithi inapelekwa kwa mhariri ili ahakiki tahjia, sarufi, na uandishi wa vituo. Mwandishi anapewa nafasi nyingine ya kubadilisha sehemu yoyote ya hadithi.

Wakati huohuo…..

**Hatua ya 5: Msanii anashughulika sana kutunga kazi za mwisho**

Hutumia kitabu chake cha mfano kama kiongozi. Lazima karatasi zipimwe kwa usahihi ili achore michoro katika sehemu husika. Huchora alama katika mchirizi ambapo karatasi zitakaposhonwa na kubanwa, na huweka alama katika mikunjo ambapo karatasi zitakatwa.

Sio rahisi! Anahitaji kutengeneza usanii kwa namna itakavyoonekana katika kitabu kilichochapishwa. Inahitajika kuwa kazi nzuri. Mistari inahitajika kuwa nyoofu, na panahitajika kuwepo na nafasi kwa ajili ya maneno ya hadithi.

Wakati kazi hii inapomalizika, anaipeleka kwa mhariri katika shirika la uchapishaji.

Kule, kazi inakaguliwa ili kuhakikisha kuwa hamna makosa, na mkurugenzi wa uzalishaji anafanya makadirio ya gharama itakayotumika kutengeneza kitabu. Anaamua muda wa uchapishaji wa kitabu na kuagiza karatasi.

**Hatua ya 6: Kitabu kinapelekwa uzalishaji!**

Msanii anaonesha jinsi maneno na michoro itakavyowekwa. Prufu za rangi zinatengenezwa, na kila mmoja anakagua kuhakikisha kuwa rangi zilizochapishwa zinaoana na michoro ya msanii. Hii ndicho kitu wanachokiangalia katika picha hii.




Kila mmoja akisharidhika na jinsi michoro inavyoonekana katika kurasa, visahani vya maandishi ya kuchapisha vinatengenezwa. Visahani hivyo vitatumika katika usindikaji wa uchapishaji kuchapisha kurasa.

**Hatua ya 7: Mwisho! Ni wakati wa kuchapisha kitabu**

Baada ya miezi ya matayarisho uchapishaji huchukua siku moja tu.

Vijisahani vyembamba (vyenye chapa ya kitabu) vinafungwa kuzunguka silinda kubwa ambayo hupelekwa kwenye mathaa. Kila silinda inachapisha rangi mojawapo kati ya rangi nne za kitabu - ya kwanza ni ya njano, halafu bluu, halafu nyekundu, halafu nyeusi. Rangi nyingine zinatengenezwa kutokana na mchanganyiko wa rangi hizo nne.

kikamatiyo maalum na mikanda wa kuchukulia husaidia kusogeza karatasi kupitia katika mtambo wa kusindika.



**Hatua ya 8: Hongera! Dakika ambayo kila mmoja alikuwa akiisubiri imefika**

Kitabu kimechapishwa na kimetoka vizuri sana!

Ulijua kuwa karatasi zote za kitabu zimechapishwa katika karatasi moja KUBWA! Nusu ya kurasa zimechapishwa katika sehemu moja ya kurasa za kusindika na nusu nyingine imechapishwa katika kurasa iliyopo kinyume chake. Baada ya karatasi hizi kuchapishwa, zinakunjwa, kukatwa na kufungamanishwa katika kitabu.

**Hatua ya 9: Vitabu vipya vinasambazwa!**

Vitabu vilivyofungamanishwa vinachukuliwa ghalani, ambapo hutunzwa hadi vinapouzwa katika maktaba na maduka ya vitabu.

Wakutubi na wauzaji wa vitabu wanajuaje kuwa vitabu vizuri vipya vimechapishwa? Watu wengine katika ofisi za uchapishaji huuza na kutangaza vitabu. Wakati mwingine mabango na maonesho maalum hufanywa. Wachapishaji hupeleka nakala za mapitio ya vitabu kwa watu waandishi wa habari. Waandishi mara nyingi husailiwa na waandishi wa habari magazetini na katika televisheni.

Watu wengi hufanya kazi kwa bidii wakijua kuwa siku moja...

**Hatua ya 10: …umesoma kitabu!**

Watu wote uliokutana nao wanakufikiria na kama utakipenda au hutakipenda kitabu. Mwandishi na wasanii wanakufikiria wakati wanabuni hadithi na michoro. Mhariri na mchoraji vielelezo wanakufiria, pia, wakati wanapotayarisha kitabu. Na WEWE ndiye sababu mtambo wenye kelele wa kusindika vitabu unachapa vitabu kwa ajili yako ili uvisome.

Usomaji mwema!

*Imerekebishwa kutoka: How a book is made: Harper Childrens; Website. ThinkQuest, Website. Fact Monster, Website.*

## Nyenzo-rejea 2: Orodha ya kuhakiki kwa ajili ya wanafunzi - ili kutumika wakati wanapohariri kazi zao kwa ajili ya kitabu

**Kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi**

| **Orodha ya kuhakiki hadithi** | ✓ |
|---|---|
| Hadithi ina kichwa cha habari? | |
| Je, Kichwa cha habari hicho kitawafurahisha wasomaji wa hadithi? | |
| Je, wasomaji wataweza kufuata mtiririko wa matukio katika hadithi (ilitokea nini kwanza halafu kilichofuata ni nini)? | |
| Je, Wahusika na mandhari katika hadithi vimeelezwa vizuri ili wasomaji waweze kupata taswira yavyo? | |
| Je, hadithi inafikia upeo/mwisho? | |
| **Orodha ya kuhakiki mashairi** | ✓ |
| Shairi au wimbo una kichwa cha habari? | |
| Je, kichwa cha habari hicho kitawafurahisha wasomaji wa mashairi au wimbo? | |
| Je, shairi au wimbo una wizani au vina (au vyote viwili) ambavyo vinawafanya wasomaji wafurahie? | |
| Maneno yameteuliwa vyema kuelezea watu, wanyama, vitu, matendo au hisia? | |
| **Orodha ya kuhakiki michezo** | ✓ |
| Je, mchezo una jina? | |
| Je, maelekezo yana mtiririko sahihi? (kwanza fanya hili ……) | |
| Je maelekezo yako wazi? | |
| Iwapo vitu (kama changarawe au karatasi) vinahitajika katika mchezo, je, vimeorodheshwa? | |

# Nyenzo-rejea 3: Kubadilisha hadithi za wanafunzi kuwa ‘kitabu kikubwa’

**Nyenzo ya Mwalimu kwa ajili ya kupanga/kurekebisha na kutumia na wanafunzi**

| |
|---|
| Utakavyohitaji |
| Makaratasi makubwa ya ‘kuchapia habari’ (karibu 60 sm x 85 sm) |
| Penseli kubwa ya nta |
| Penseli |
| Peni kubwa zenye ncha kali |
| Sindano kubwa ya kushonea |
| Kamba nyembamba |
| Gundi |
| Vipande vidogo vya karatasi zisizo na maandishi |
| Karatasi kubwa ya bango au chati |
| Mwanzo wa hadithi uliowaambia wanafunzi wako |
| Sehemu iliyobaki ya hadithi, ambayo wanafunzi wamekusomea |

**Jinsi ya kutengeneza kitabu kikubwa**

Kuandika vitabu kunaweza kuwahamasisha watoto kutaka kusoma na kujiandikia zaidi. Kwa watoto wadogo, unahitaji kufanya matayarisho kabla, ukifupisha kazi wanazohusika nazo kwa kuzingatia vipengele maalum (angalia hapa chini). Kwa watoto wakubwa na kwa kuzingatia ujuzi wao, wanaweza kujifanyia kazi zaidi (kama katika **Shughuli 2**).

1. Kwanza soma hadithi yote kwa makini na hakikisha ni kamili na vituo vya uandishi vimewekwa kikamilifu.
2. Amua ni urefu wa matini kiasi gani unaotaka kuandika katika kila ukurasa wenye sehemu mbili. Kama una madarasa ya darasa la kwanza na ni mwanzo wa mwaka wa masomo, utapenda kuhakikisha kuwa hakuna zaidi ya sentensi mbili au tatu kwa kila ukurasa wenye sehemu mbili. Katika baadhi ya sehemu za hadithi huenda ukapenda kuandika aya moja. Kama unafanya kazi na wanafunzi wakubwa, unaweza kuandika zaidi.
3. Fikiria michoro au vielelezo ambavyo unataka viambatane na matini. Hii itakusaidia kuamua ukubwa wa kitabu, na kitakuwa na kurasa ngapi.
4. Chukua kadi yako nyembamba, na ikunje katikati. Hili litakuwa gamba la kitabu chako. Kama kitabu kilichotengenezwa na karatasi za uchapishaji kina gamba gumu, kinadumu kwa muda mrefu.
5. Andika hadithi yote katika karatasi zenye mistari za ukubwa wa A4 na weka matini kwa kila kurasa yenye sehemu mbili katika mstari mpya.
6. Kunja kila karatasi mara mbili. Ziweke karatasi pamoja na hakikisha kuwa ni safi, na zinabana vizuri. Usizifungamanishe karatasi pamoja kwanza.

7. Sasa amua utakapotaka kuweka matini. Utaiweka kushoto kwa kila ukurasa wenye sehemu mbili zilizotandazwa? Au utaiandika kulia mwa ukurasa? Utaiandika juu ya ukurasa? Au utaiandika chini ya ukurasa? Kila ukurasa wa sehemu mbili utaonekana tofauti? Labda utaamua kuandika toka upande mmoja hadi mwingine katika ukurasa wenye sehemu mbili? Unapaswa kuamua kuhusu hili.
8. Sasa chukua karatasi zilizokunjwa. Fanyia kazi katika meza kubwa. Tumia kalamu ya nta ya rangi nene na andika kwa unadhifu kipande cha hadithi sehemu ya nje ya karatasi ya kwanza. Andika sehemu ndogo kwa jinsi itakavyoonekana katika ukurasa wa kwanza katika kitabu ambacho ungenunua dukani. Unahitaji kitabu chako kuonekana kimeandikwa na bingwa.
9. Chini, kwa herufi ndogo andika majina ya wanafunzi wote ambao walishiriki kuandika hadithi, au darasa lako. (Kama ni darasa zima, itakuwa vigumu kuandika majina ya wanafunzi 50 au zaidi, kwa hiyo taja darasa kama majina yote hayawezi kuenea!)
10. Halafu, fungua ukurasa wa kwanza wa karatasi za magazeti. Huu utakuwa ukurasa wako wa kwanza ulioandikwa sehemu zote mbili. Andika sentensi au aya ya kwanza katika ukurasa huu ulioandikwa sehemu zote mbili, ukitumia kalamu ya rangi nene yenye nta. Unapaswa kuacha nafasi ya kutosha kwa ajili ya vielelezo au michoro.
11. Unapokuwa umekwisha andika matini katika ukurasa ulioandikwa sehemu mbili, geuza ukurasa mwingine ulioandikwa sehemu mbili, na andika sentensi au virai kwa kalamu y nta ya rangi nyeusi. Endelea hivyo hadi kumalizia kuandika hadithi yote.
12. Chukua ‘gamba’ la kitabu chako. Unahitaji kuamua ni mahali gani pa kuandika kichwa cha habari. Ni wazo zuri kuacha nafasi kwa ajili ya vielelezo. Utaandika kichwa cha habari juu, au chini? Ukifurahia jinsi kazi ilivyo, rudishia tena maandishi yaliyoandikwa kwa penseli.
13. Ingiza vizuri karatasi za magazeti ndani ya ‘gamba’.
14. Sasa shona karatasi pamoja na gamba la kitabu pamoja. Kuna njia tofauti ambazo unaweza kutumia kufanya jambo hili, lakini njia zifuatazo ni bora zaidi:
15. Fungua kitabu chako ili gamba la kitabu liwe liko chini, na katikati ya kurasa zilizoandikwa sehemu mbili ziko juu. Kwa kitabu kikubwa, ni wazo zuri kuweka alama katika nafasi mbili kwenye mkunjo katikati, ambapo unaweza kushona
16. Weka alama juu katika nusu ya mkunjo, na weka alama ya pili katika nusu ya chini. Katika kila sehemu, tengeneza alama tatu. Alama hizi ziwe na nafasi ya sentimita 4.
17. Tunga uzi mwembamba katika sindano wenye urefu wa sentimita 50. Ingiza ncha ya sindano katikati ya seti ya alama zile tatu, katika kurasa zote pamoja na gamba lake. Vuta uzi , lakini acha kipande cha uzi chenye urefu wa kama sentimita 7 kikining’inia na fuata chati. Kata uzi ulioshikizwa katika sindano, karibu sentimita 7 kutoka mahali ulipopenyeza kwenye karatasi. Sasa funga kwa uthabiti nyuzi za sehemu zote mbili za urefu wa sentimita 7.
18. Rudia mchakato huu nyuma ya mkunjo.
19. Tengeneza orodha ya vielelezo unavyotaka. Amua kama unawataka wanafunzi fulani kutengeneza vielelezo, au unataka darasa lako zima kuhusishwa. Wanafunzi wanaweza kufanya vizuri wakiwa wawiliwawili kutengeneza picha. Panga jinsi ya kutengeneza michoro.

20. Uchaguzi wa picha. Soma , pamoja na wanafunzi wako matini yote. Fungua kurasa na soma hadithi kwa sauti. Isome hadithi kwa namna ambayo itafurahisha.
21. Waeleze wanafunzi wako kuwa unawataka kuchora picha. Usomapo hadithi kwa mara ya pili, sita kwa muda kwa kila kurasa zenye sehemu mbili na jadili kuhusu picha inayotakiwa. Wewe na darasa lako mnapofanya uamuzi kuhusu picha inayotakiwa kwa kila ukurasa, gawia kila kielelezo kwa mwanafunzi fulani, au wanafunzi wawiliwawili.


Wape muda kutengeneza picha vizuri. Wahusishe wanafunzi kushughulikia yaliyomo kwenye kitabu. Hata wanaoanza kusoma wanaweza kukariri hadithi, na wana taarifa ya kila picha inapopaswa kuwekwa. Chini ya picha hiyo, andika majina ya wanafunzi walioichora. Endelea kwa njia hii hadi picha zote zigandishwe na kuwekewa jina.

Wakati ambapo vielelezo vyote vimekwishagundishwa, soma kitabu pamoja na wanafunzi wako. Tuna hakika kuwa wewe na wanafunzi wako mtajivunia juhudi zenu.

*Imerekebishwa kutoka: Umthamo 2, University of Fort Hare Distance Education Project*

## Nyenzo-rejea 4: Sifa za usanifishaji wa gamba la kitabu

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**




*Imetolewa kutoka: Nancy Keane, Website.*

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kinachovutia machoni – msomaji huvutiwa na ‘sura’ ya gamba la kitabu

Kichwa cha habari kinawekwa mahali pazuri na kinaonekana waziwazi

Kichwa cha habari kinawahimiza wasomaji kukifungua

Maneno ya kichwa cha habari na majina ya waandishi ni rahisi kusomeka.

Matumizi ya rangi yanamvutia msomaji.

Matumizi na sehemu za kurasa zilipowekwa sanamu (michoro au picha) zinavutia msomaji na sanamu hizi ‘zinahusishwa’ na kitabu.

Kuna nafasi wazi katika gamba la kitabu ili michoro isiwe imejazana.

*Chanzo: Two Bookmark; Website.*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

TESSA

Teacher Education in Sub-Saharan Africa

www.tessafrica.net

Rasilimali za Msingi

# Kujua kusoma na kuandika

## **Namba ya moduli 3** Uhamasishaji wa mawasiliano katika lugha ya ziada

**Sehemu ya 1** Kuandaa mazingira asilia kwa ajili ya mazoezi ya lugha

**Sehemu ya 2** Njia zijengazo ufasaha na usahihi

**Sehemu ya 3** Kuunda Fursa za Mawasiliano

**Sehemu ya 4** Namna ya kujenga juu ya ujuzi wa lugha ya nyumbani

**Sehemu ya 5** Kusaidia ujifunzaji wa lugha ya ziada

**KISWAHILI**

*TESSA (Teacher Education in Sub-Saharan Africa) inalenga kuboresha utekelezaji darasani wa walimu wa msingi na walimu wa sayansi wa sekondari barani Afrika kupitia matoleo ya Rasilimali Huria za Elimu (OERs) ili kuunga mkono walimu kuunda njia zinazowalenga wanafunzi na kuwashirikisha. OER ya TESSA huwapa walimu kitabu cha kurejea pamoja na vitabu vya shule. Zinatoa shughuli kwa walimu kujaribu madarasani pamoja na wanafunzi wao, pamoja na masomo ya utafiti inayoonyesha jinsi walimu wengine wamefunza mada hiyo, na rasilimali husishi za kuwaunga mkono walimu katika kukuza mipango ya masomo yao na ufahamu wa somo.*

OER ya TESSA imeandikwa kwa ushirikiano wa waandishi wafrika pamoja na wa kimataifa *ili kushughulikia mtalaa na muktadha. Zinapatikana kwa matumizi ya mtandaoni na chapa (*http://www.tessafrica.net*). OER Msingi zinapatikana katika matoleona lugha kadhaa (Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu na Kiswahili). Mara ya kwanza, OER ilitolewa kwa Kiingereza na kupatikana Afrika nzima. OER hizi zimebadilishwa na washirika wa TESSA ili kufaa Ghana, Nijeria, Zambia, Rwanda, Uganda, Kenya, Tanzania na Afrika Kusini, na kutafsiriwa na washirika nchini Sudani (Kiarabu), togo (Kifaransa) na Tanzania (Kiswahili) OER ya Sayansi ya Sekondari zinapatikana kwa Kiingereza na zimebadilishwa ili kufaa Zambia, Kenya, Uganda na Tanzania. Tunakaribisha maoni kutoka kwa wale wanaosoma na kutumia rasilimali hizi. Leseni ya uundaji wa ubunifu huwawezesha watumiaji kuchukua na kujanibisha OER zaidi ili kutimiza mahitaji na muktadha wa kindani.*

*TESSA inaongozwa na Open University, Uingereza, na inafadhiliwa kwa sasa na ruzuku za ufadhili kutoka kwa Wakfu wa Allan and Nesta Ferguson, Wakfu wa William and Flora Hewlett na Open University Alumni. Orodha kamili ya wafadhili inapatikana kwenye tovuti ya TESSA (*http://www.tessafrica.net*).*

*Pamoja na rasilimali kuu za mafundisho za kuunga mkono mafunzo katika masomo maalum, ni chaguo za rasilimali za ziada ikiwa ni pamoja na sauti, rasilimali kuu ambazo zinafafanua utendakazi, vitabu na zana maalum.*

**TESSA Programme**
**The Open University**
**Walton Hall**
**Milton Keynes, MK7 6AA**
**United Kingdom**

**tessa@open.ac.uk**

Copyright © 2017 The Open University
Except for third party materials and otherwise stated, this content is made available under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 licence: http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0/. Every effort has been made to contact copyright holders. We will be pleased to include any necessary acknowledgement at the first opportunity.

***TESSA_SwPA_LIT_M3 August 2017***

*This work is licensed under a Creative Commons Attribution-Share Alike 4.0 License*

# Contents


Sehemu ya 1: Kuandaa mazingira asilia kwa ajili ya mazoezi ya lugha 5
Utangulizi 5
Somo la 1 5
Somo la 2 7
Somo la 3 8
Nyenzo-rejea ya 1: Mjumuisho wa mwitikio wa vitendo 9
Nyenzo-rejea 2: Mapishi 12
Sehemu ya 2: Njia zijengazo ufasaha na usahihi 15
Utangulizi 15
Somo la 1 15
Somo la 2 17
Somo la 3 18
Nyenzo-rejea ya 1: Miundo mbadala ya somo – iliyotumiwa na Bwana Gasana 20
Nyenzo-rejea 2: Tangazo la mauzo 21
Nyenzo-rejea 3: Chati za njeo za kitenzi 22
Nyenzo-rejea 4: Shairi la kusifu 23
Nyenzo-rejea 5: Vitenzi na vielezi katika shairi – Ngoma Yangu na Francis Faller 25
Sehemu ya 3: Kuunda Fursa za Mawasiliano 27
Utangulizi 27
Somo la 1 27
Somo la 2 29
Somo la 3 30
Nyenzo-rejea ya 1 : Shughuli zaidi zihusuzo tofauti za taarifa 32
Nyenzo-rejea 2: Madokezo kwa ajili ya picha 33
Nyenzo-rejea 3: Maneno na maana – mifupa katika mwili 34
Nyenzo-rejea 4: 34
Nyenzo-rejea 5: Kuunda maana 35

Sehemu ya 4: Namna ya kujenga juu ya ujuzi wa lugha ya nyumbani 37
Utangulizi 37
Somo la 1 37
Somo la 2 39
Somo la 3 40
Nyenzo-rejea ya 1: Shairi 42
Nyenzo-rejea 2: Mfano wa somo 43
Nyenzo-rejea 3: Usalama 45
Nyenzo-rejea 4: Kauli za Dira na Malengo - mifano 46
Sehemu ya 5: Kusaidia ujifunzaji wa lugha ya ziada 48
Utangulizi 48
Somo la 1 48
Somo la 2 50
Somo la 3 52
Nyenzo-rejea ya 1: Marafiki wa kalamu 53
Nyenzo-rejea 2: Uandishi wa barua 54
Nyenzo-rejea 3: Kutathmini barua za urafiki wa kalamu 55
Nyenzo-rejea 4: Nyimbo na hadithi kuhusu michakato 56

# Sehemu ya 1: Kuandaa mazingira asilia kwa ajili ya mazoezi ya lugha

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuwasaidia wanafunzi kufanya mazoezi ya muundo wa lugha katika mazingira asilia?

**Maneno muhimu:** usimamizi wa darasa; michezo; mapishi; maelekezo; mchakato

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- Kutumia uongozi/utawala wa darasa kuwasaidia wanafunzi kujifunza lugha ya ziada;
- Kutumia michezo na shughuli za kila siku kuimarisha wanafunzi kuhusu stadi za lugha na msamiati.

## Utangulizi

Wanafunzi wako wana fursa gani kupitia –redio, vitabu, magazeti, wazungumzaji wa lugha na televisheni kwa lugha ya ziada ukilinganisha na ile inayotumika nyumbani?

Jawabu linaweza kuwa ni 'fursa ndogo'. Wanaisikia na kuitumia kila siku darasani shuleni. Hii ina maana kuwa unawajibika kuwapa fursa ya kutumia lugha ambayo itawasaidia wanafunzi:

Kuitumia na kuwa wazungumzaji hodari katika matumizi ya msamiati mpya na muundo wa sarufi;

Kuwasiliana kwa kutumia lugha ya mazungumzo katika mazingira ya kijamii;

Kuimarisha na kuendeleza stadi zao za kusoma na kuandika.

Yote haya yanahitaji tafakuri ya hali ya juu, na upangaji na stadi makini. Sehemu hii itakupatia mikakati na mbinu za kukusaidia.

## Somo la 1

Ukiwa mwalimu, utatoa maelekezo ya aina mbalimbali kwa wanafunzi wako.

Unaweza kutumia maelekezo ya kila siku kukuza msamiati mpya na stadi ya usikilizaji katika lugha ya ziada. Maelekezo hutumia muundo wa amri wa kitenzi. Wakiona muundo wa kuamuru katika kitenzi mara kwa mara katika mazingira yanayoleta maana, wanafunzi wataanza kuelewa na kujifunza muundo huo.

Wanafunzi wanapojifunza lugha mpya, usikilizaji huendelea haraka kuliko mazungumzo. Wanahitaji nafasi kubwa ya kusikiliza na kujibu katika lugha mpya. Katika hatua za mwanzo za ujifunzaji lugha (na baadaye pia), unaweza kutumia shughuli ambazo zinawahitaji kujibu kwa vitendo lakini haiwahitaji kujibu (kwa maneno) hadi wanapojisikia kuwa na uhakika zaidi. (Hii mara nyingi huitwa 'mawazo ya mbinu jumuishi'- Angalia **Nyenzo-rejea 1: Mawazo ya mbinu jumuishi** .)

## Uchunguzi kifani ya 1: Uongozaji wa darasa katika Kiingereza

Bibi Mujawayo anafundisha darasa la kwanza mjini Kigali, Rwanda. Anatumia Kiingereza katika uendeshaji wa darasa.

Asubuhi husalimiana na wanafunzi katika lugha zao za nyumbani, na huwauliza habari zao za nyumbani katika lugha zao.

Baada ya baraza, huanza kutumia Kiingereza darasani, 'Pangeni mstari wanafunzi' na huwaelekeza barazani, mahali ambapo wanapaswa kujipanga. 'Ingia darasani' husema huku akiwaonesha vitendo vya kuwaelekeza kuingia ndani. 'Simameni karibu na madawati yenu.

Mwalimu na wanafunzi husalimiana kwa kutumia Kiingereza. Husema 'Kaeni chini.

Hurejea tena katika lugha yao ya nyumbani ili kuanza kusimulia hadithi hadi anapowaweka katika vikundi, kwa ajili ya shughuli mbalimbali.

Kila kikundi kina alfabeti. Husema kwa Kiingereza kwa kunyoosha mikono A na B nyosheni mikono. Kwa kuonesha katika kisanduku huwaambia 'Chukueni vitabu kutoka katika kisanduku.' 'Kaa chini, na msomee mwenzio.' Kama wanaonekana kutoelewa, wanaigiza wanachopaswa kufanya.

Baadaye hutoa maelekezo zaidi kwa Kiingereza, bila kutafsiri. Vikundi viwili vinapaswa kuonesha hadithi yao na kikundi kingine watasoma pamoja naye katika lugha yao ya nyumbani kutoka katika kitabu kikubwa.

Bibi Mujawayo anagundua kuwa wanafunzi wake wanaanza kuelewa haraka maelekezo katika Kiingereza, na mara huanza kusema maneno.

## Shughuli ya 1: Simple Simon husema

Katika mchezo huu unaojulikana sana, wanafunzi hufuata kwa vitendo maelekezo. Unaweza kutumia njia hii kuongeza msamiati na stadi ya usikilizaji katika maeneo mbalimbali ya masomo.

Kiongozi hutoa amri na kuonesha vitendo wakati huohuo. Wanafunzi wanapaswa kufuata amri hiyo kutoka kwa Simple Simon. (Unaweza kubadilisha jina hili kwa kutumia jina la mtu ambaye ni mashuhuri kijijini.) Mchezo huchezwa kama hivi:

Kiongozi: Simple Simon anasema , 'Ruka!' (Kiongozi anaruka.)

Wanafunzi wanaruka.

Kiongozi: Simple Simon husema, 'Shika vidole vya miguu !' (Kiongozi anashika vidole vya miguu)

Wanafunzi wanashika vidole vya miguu.

Kiongozi: 'Kuna pua yako!' (Kiongozi anakuna pua yake.)

Baadhi hukuna pua zao. Wengine hawafanyi hivyo. Wale ambao wamekuna pua zao wanatoka (kwa sababu amri haikutoka kwa Simple Simon Na kuendelea hivyo….. Tumia maelekezo rahisi kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ngeni, maelekezo magumu kwa wale ambao ni wanaielewa lugha zaidi. Anza polepole, lakini endelea kwa kasi zaidi. Mshindi ni yule aliyebaki.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Somo la 2

Ni jambo muhimu kuwapa wanafunzi nafasi ya asilia ya kuendeleleza stadi zao katika lugha ya ziada. Hapa tunapendekeza njia ambazo unaweza kuzitumia kushirikisha jamii na kutumia stadi za asilia na busara kama njia ya Nyenzo-rejea ya shughuli za darasani.

Umeona, katika **Uchunguzi-kifani 1** na **shughuli 1**, namna maelekezo ya kila siku yanavyoweza kuleta muktadha asilia wa ujifunzaji lugha. Wanafunzi walisikiliza na kuonesha uelewa kwa vitendo. Katika sehemu hii tunashauri utumie mapishi ya asilia na mchakato kama njia ya muktadha wa mafunzo, ukiwapa nafasi wanafunzi kuzungumza (na kuandika) na vilevile kusikiliza.

Shughuli zilizotumika hapa zitaendelezwa mbele katika sehemu ya 5, ambapo darasa lako litaanza kutayarisha kitabu cha mapishi.

### Uchunguzi kifani ya 2: Wanafunzi watu wazima hujifunza kwa vitendo

Baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili walitumia muda wa siku nzima mjini kama sehemu ya kozi yao. Kila mwanafunzi alikuwa akifuatana na msaidizi wa lugha ambaye alikuwa mzungumzaji wa Kiswahili. Wasaidizi waliwasaidia wanafunzi walipokuwa wakijaribu lugha waliojifunza; wakinunua mboga kutoka kwa wauzaji wa barabarani na kuzungumza na familia zilizokuwa zinawasaidia.

Sehemu muhimu ya siku hiyo ilitumika kupika chakula. Mwanafunzi alipaswa kupika chakula, akielekezwa na msaidizi wa lugha. Upikaji ulikuwa umefanyiwa mazoezi na kuigizwa, na mara nyingi kuandikwa au kurekodiwa katika kinasa sauti, wiki moja kabla darasani. Wanaume walipewa maelekezo ya kutayarisha moto, wakati wanawake walitakiwa kupika chakula kama ugali, ndizi na nyama na kabichi. Walizungumzia pia jinsi ya kubadilishana nafasi ili kuwasaidia kujifunza lugha.

Wakati chakula kilipokuwa tayari, nyimbo za Kiswahili ziliimbwa, na wanafunzi walijifunza michezo ya asili ya Kiswahili ya watoto. Baada ya vyombo kusafishwa, kundi la wanafunzi wenye furaha na uchovu walijipakia katika teksi na kurudi nyumbani.

### Shughuli ya 2: Kujifunza kwa vitendo vya shughuli za kijamii

Waambie wanafunzi wako kwamba watakwenda kutafuta jinsi shughuli za nyumbani zinavyotekelezwa na kueleza njia za mchakato katika lugha ya ziada. Watake wanafunzi kuleta taarifa kutoka nyumbani au mkaribishe mwenyeji shuleni kutoka katika jamii ili kuonesha stadi.

Wagawane wanafunzi katika jozi au katika vikundi (vikundi hivi vinaweza kuwa vya mchanganyiko wa uwezo tofauti), kufanya kazi, na ikiwezekana kuandika hatua za moja ya mchakato katika lugha ya ziada. Zungukia darasa na kuwasaidia msamiati mpya ambao watuhitaji.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Vipe vikundi muda wa kukariri na kufanya mazoezi ya hatua zinazotumika, katika kujitayarisha kuwasaidia wengine. Wanaweza kukusanya toka nyumbani vitu vinavyohitaji katika mchakato huo.

Siku inayofuata, mpe nafasi mwanafunzi mmoja kutumia lugha ya ziada kuelekeza mjumbe wa kikundi kingine, wakati huohuo darasa likiangalia k.m. kusafisha nyumba.

Wanafunzi wamefanyaje katika shughuli hiyo?

Unaweza kuitumia njia hiyo katika mchakato mwingine ili kukuza msamiati wao?

Kama jibu ni ndiyo, vipi?

## Somo la 3

Lugha hutumika kwa mawasiliano, na ni muhimu uwe na sababu za wanafunzi kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika katika lugha ya ziada. Hii si rahisi ukiwa katika mazingira ambapo lugha ya ziada haizungumzwi. Hata hivyo, lugha ya ziada inaweza kuwa lugha ya vitabu na ya mawasiliano ya maandishi.

Duniani kote watu hubadilishana mawazo kuhusu ‘jinsi ya kufanya shughuli’; kwa mfano wanapeana maelezo ya upishi au sulubu ya utengenezaji wa nguo. Umekwisha kulifanya hili kwa mazungumzo; sasa wanafunzi wanaweza kufanya kwa maandishi. Waoneshe wanafunzi wako muundo wa kawaida wa maandishi ya maelezo ya upishi, katika lugha ya ziada. Maelezo ya upishi huandikwa kama mfululizo wa maelekezo.

Tunapoandika maelezo ya upishi, au kuelezea mchakato wake, hatujali nani atatenda, bali tunajali kuwa tendo linatendeka.

## Uchunguzi kifani ya 3: Kuchora na kuandika maelezo ya upishi

Katika shule iliyopo Njombe, kusini mwa Tanzania wanafunzi wamekuwa wakibadilishana maelezo ya upishi. Walitaka kuchora maelezo ya upishi katika michoro na kubadilishana na marafiki zao. Bibi Masawda, mwalimu wao, alifikiri kuwa itakuwa vizuri kwao kujua njia mbalimbali za kuwasilisha taarifa. Aliwaonesha jinsi ya kuchora michoro ya kuonesha mifumo. Mara wanapokuwa wamekwisha chora na kuweka maelezo katika mchoro wa mfumo, waliandika mchakato kama pia maelezo (angalia kwa mfano **Nyenzo-rejea 2: maelezo ya upishi**).

Bibi Masawda alijadiliana na wanafunzi wake ni kipi walichokiona ni rahisi kufanya, na kwa nini. Zaidi ya theluthi mbili za darasa waliona kuwa chati ya mfumo ilikuwa inafurahisha na ilikuwa rahisi kutengeneza  kwa sababu waliweza kubadilisha maelezo ya upishi katika hatua na mchoro uliwasaidia kukumbuka na kuelewa maneno.

Bibi Masawda alitumia wazo hili la chati za mifumo katika masomo mengine, kwa kuwa hili lilionekana kuwasaidia wanafunzi wake kukumbuka zaidi.

Kwa mfano, katika somo la jiografia, alitumia chati ya mfumo kuandika kuhusu maelekezo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine, na wanafunzi walichora picha za alama za mipaka ili kuifanya iwe rahisi kukumbuka maneno.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Shughuli muhimu: Kuandika maelezo ya upishi na mchakato wa maelezo

Watake wanafunzi kutafuta jinsi ya kupika vyakula vyao wanavyovipenda sana kutoka nyumbani na shirikiana mawazo hayo na darasa.

Wajulishe wanafunzi wako muundo wa maandishi ya mapishi kabla hawajafanya mfano wao (Angalia **Nyenzo-rejea 2**)

Watake wanafunzi kuandika maelezo ya mapishi vizuri, kila mmoja akijiandikia maelezo, na mwingine akitumia maelekezo ya mapishi ya kitabu cha darasani. Maelezo ya pili yanaweza kutumia muundo tofauti na ule wa kwanza (angalia Nyenzo-rejea 2 kwa ajili ya mitindo).

Watake wanafunzi wako wabadilishane kazi zao na kujadili maelezo ya mapishi.

## Nyenzo-rejea ya 1: Mjumuisho wa mwitikio wa vitendo

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

**Kwa toleo la mtandaoni:**

http://www.tpr-world.com/

Webu inatoa taarifa kuhusu mjumuisho wa mwitikio wa vitendo kama njia ya kufanya kazi katika ujifunzaji lugha. Kuna maelezo mengine ambayo unaweza kufuatilia.

**Kwa ajili ya kuhariri matini**

Unaweza kuwajulisha wanafunzi wako muundo wa lugha mbalimbali kutokana na vitendo vya kimchezo ambavyo vinawahitaji kufuata maelekezo kwa vitendo (mjumuisho wa mwitiko wa vitendo). Hapa kuna mifano ya namna ya maelekezo ambayo unaweza kuwapa wanafunzi. Weka mkazo katika aina moja ya maelekezo kwa wakati mmoja, ili wanafunzi waelewe jinsi lugha inavyofanya kazi

**Mtingishiko wa mwili**

Simama.

Cheka.

Kohoa.

Lia.

Gonga meza.

**Vitendo na vifaa**

Onesha mlango.

Okota kalamu.

Funga dirisha.

Nusa ua.

Onesha mlima.

Onesha mwanamke anayetengeneza keki.

**Vitendo, vifaa na watu**

Chukua kalamu na umpe Nuru

Tafuta kitabu na unipe

Okota karatasi na mpe Thimba.

**Ongeza vimilikishi**

Mpe Aida kitabu cha Thimba.

Leta peni ya Nuru kwangu

Mpe Kito kitabu chake.

Mpe Eshe miwani yake.

**Hiki na kile; hapa na pale**

Mpe hiki Adia.

Tafuta kile kutoka kwake.

Tafuta kalamu na iweke hapa.

Tafuta kitabu na kiweke pale.

**Kuhusisha nafasi**

Weka kalamu katikati ya vitabu viwili.

Weka kalamu karibu na rula.

Weka kifutio ndani ya kisanduku.

Weka rula juu ya kisanduku.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Jumlisha namba, ziweke rangi na ukubwa**

Weka kalamu mbili ndani ya kisanduku.

Chukua mawe matatu nje ya kisanduku.

Okota kalamu nyekundu na mpe Thimba.

Weka kitabu cha kijani mezani.

Chukua kitabu kidogo na mpe Nuru.

Weka kitabu kikubwa ndani ya kisanduku.

**Maelekezo na maelezo, pamoja mazungumzo kiasi**

**Fanya na kusikiliza**

Wanafunzi wanafanya tendo. Mwalimu (au mwanafunzi mwingine) husema wanachofanya (k.m. 'Umesimama.')

**Sikiliza na kufanya**

Mwalimu (au mwanafunzi mwingine) anamuelekeza mwanafunzi (k.m. Simama.' Mwanafunzi anafuata amri, kwa kufanya tendo.

**Sahihi au si sahihi**

Mwanafunzi anajifunza kusema 'sahihi' na 'si sahihi'. Mwalimu (au mwanafunzi mwingine) anatenda tendo, na kutoa tamko 'lililo sahihi' au 'lisilo sahihi' kuhusu anachofanya (k.m. 'Nimekaa.') Wanafunzi wanasema 'kweli' au 'si kweli'

**Sikiliza, igiza na tenda**

Mwalimu (au mwanafunzi mwingine)anamuelekeza mwanafunzi. Mwanafunzi anarudia yaliyosemwa na halafu anatenda amri hiyo.

**Eleza, sikiliza na igiza**

Mwanafunzi hutenda na kueleza wanachofanya (k.m. 'Nimesimama.') Mwalimu ( au mwanafunzi mwingine) anaeleza kile kilichosemwa na mwanafunzi na anatekeleza kitendo.

**Kwenda nje au kutumia picha ili kuongeza msamiati**

Mwanzoni, unahitaji kutumia maneno yanayojulikana na maelekezo mapya. Baada ya msamiati wa darasa kujulikana, unaweza kutumia msamiati wa nje ya darasa, k.m.:

Gusa jani.

Onesha mbingu.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Unaweza pia kuongeza msamiati kwa kutengeneza kadi zenye maneno au picha, k.m. picha za aina ya chakula:

Chukua nyama na mpe Nuru.

Tafuta mkate wa Kapuki na unipe.

*Zimetolewa kutoka: Total Phsyical Response Worldwide, Website*

## Nyenzo-rejea 2: Mapishi

**Nyenzo ya Mwalimu ya kutumia na wanafunzi kwa ajili ya kupanga/kurekebisha**

Hapa kuna njia tatu za kuonesha mapishi ya aina moja

Kutengeneza supu ya pilipili (mchoro mfumo)

Osha na kata nyama katika vipande vidovidogo

Pika/Chemsha nyama katika maji ya moto

Kata vitunguu, nyanya na pilipili

Weka vitunguu vilivyokatwa, nyanya na pilipili kwenye nyama na koroga

Tia maji mengi ya kutosha kiasi cha kufunika mchanganyiko na iache ichemke katika moto mdogo

Safisha, osha, katakata na kuongeza mboga nyinginezo

Iache ichemke polepole hadi nyama inapokuwa laini

Kula kwa wali

**Kutengeneza supu ya pilipili (maelezo ya mchakato)**

Wakati supu ya pilipili unapotayarishwa, 0.5 ya nyama inasafishwa na kukatwa katika vipande vidogo vidogo. Nyama inapikwa katika maji moto, na vitunguu, nyanya, mboga na pilipili zinaongezwa. Zinachemshwa hadi zinakuwa laini; halafu zinaliwa kwa wali.

**Kutengeneza supu ya pilipili (viungo na mbinu)**

Viungo:


0.5 kg ya nyama (iliyooshwa na kukatwa katika vipande vidogo)



Vitunguu 4



Nyanya 8



Pilipili zilizokaushwa 4 hadi 5



Mboga nyinginezo, zinazopatikana









Lita 1.5 ya maji



Mbinu: Weka maji katika sufuria na yachemshe Ongeza vipande vya nyama na chemsha Ongeza vitunguu vilivyokatwa, nyanya, pilipili na mboga nyinginezo, koroga na acha ichemke.

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Sehemu ya 2: Njia zijengazo ufasaha na usahihi

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuwasaidia wanafunzi kujenga hali ya kujiamini katika utumiaji wa miundo ya lugha mahsusi?

**Maneno muhimu:** vitenzi; vielezi; urudiaji; mashairi; nyimbo; uhariri

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- umewaongoza wanafunzi wako katika kuwapa ujuzi wa kudhibiti miundo ya lugha ya ziada;
- umetumia urudiaji, nyimbo, mashairi na hadithi katika kufundisha miundo ya lugha;
- umewasaidia wanafunzi wako kusimamia kazi yao wenyewe kadri wanavyotafuta maana na matumizi sahihi ya vitenzi.

## Utangulizi

Ukiwa mwalimu wa lugha ya ziada, mara zote unatakiwa utafute mbinu mpya za kuwapa wanafunzi wako uzoefu wa lugha hiyo. Kama wanapewa fursa za kujizoeza lugha hiyo, matumizi yao ya lugha hiyo yatakuwa fasaha na sahihi zaidi.

Sehemu hii inakupatia mazoezi yanayofaa ambayo yanalenga katika kauli na miundo mahsusi.

Kumbuka kwamba vitendo utakavyovichagua ni lazima viwe vinafahamika kwa wanafunzi, ama kitendo chenyewe, au katika maisha yao (inapendelewa viwe vinavyohusu sehemu zote mbili).

## Somo la 1

Kuwapatia wanafunzi wako fursa za kutumia miundo ya lugha mahsusi tena na tena ili waweze kuimudu, kunahitaji kuwa tendo la kufurahia.

Kuna nadharia isemayo kwamba watu hujifunza lugha kwa kuiga na urudiaji. Hapo zamani, kozi nyingi za lugha zilitumia sehemu kubwa ya urudiaji (mazoezi ya kurudiarudia). Siku hizi inadhaniwa kwamba vitendo vinavyowahusisha wanafunzi katika mawasiliano ‘halisi’ vinawasaidia zaidi kuliko urudiaji usiokuwa na maana. Hata hivyo, urudiaji bado unaweza kuwa wenye manufaa endapo wanafunzi watachomeka maana halisi katika sentensi. Inasaidia kama watawekewa urudiaji katika muziki.

Jaribu mawazo yaliyomo katika **Uchunguzi-kifani 1** na **Shughuli 1** kupima nadharia hizi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Urudiaji katika lugha unaohusu hadithi kutoka gazetini

Bwana Gasana anafundisha Kiingereza Darasa la 4 huko Butare, Rwanda. Mauaji yalitokea katika jiji lao, saa 2 usiku, siku mbili zilizopita. Aliwaonesha wanafunzi wake ripoti ya mauaji hayo kutoka kwenye gazeti. Alizungumza na wanafunzi wake (kwa lugha ya nyumbani) kuhusu jinsi askari wa upelelezi wanavyouliza watu wanapojaribu kutafuta mhalifu. Halafu akaweka sampuli ya swali na jibu ubaoni, kwa Kiingereza:

Q: Ulikuwa unafanya nini Jumanne saa 2 usiku, Kigeri?

A: Nilikuwa ninatazama runinga.

Aliwauliza wanafunzi wachache swali hilo hilo, ili kuhakikisha watatoa majibu yao wenyewe kwa utaratibu sahihi. Kisha, aliwaweka wanafunzi katika makundi ya wanafunzi sita sita. Kila mwanafunzi alitakiwa kuuliza swali kwa wanakikundi wake wengine watano, ambao kila mmoja atatoa jibu lake. Bwana Gasana aliwahimiza wanafunzi kusahihishana, na alitembea kuzunguka darasa, kusikiliza na kuongoza makundi.

Alimwambia kila mwanafunzi aandike 'ripoti ya askari wa upelelezi' kuhusu kundi lake. Kila moja kati ya sentensi sita zilionekana katika muundo ufuatao:

Saa 2 usiku Muteteli alikuwa anacheza na kaka yake.

Saa 2 usiku Erisa alikuwa anaandaa chakula.

Nyenzo-rejea 1: Miundo mbadala ya somo inatoa sampuli zilizotumiwa na Bwana Gasana akiwa na wanafunzi wake wakubwa wa Darasa la 5.

## Shughuli ya 1: Urudiaji katika bei mbalimbali

Tafuta au tengeneza tangazo la mauzo au orodha ya bei za mbogamboga za mahali hapo, ukionesha mapunguzo ya bei (angalia Nyenzo-rejea 2: Tangazo la bei kwa mifano). Kabla ya somo, tengeneza nakala kubwa ya tangazo au orodha ya bei ubaoni, au tayarisha tangazo moja au orodha ya bei kwa kila kundi katika darasa lako.

Andika mfuatano ufuatao wa swali na jibu ubaoni.

Q: ….. ni bei gani ?

A. Kabla ilikuwa shilingi …., lakini sasa ni shilingi …. tu.

Q: Hizo …. ni bei gani?

A: Kabla zilikuwa shilingi …., lakini sasa ni shilingi …. tu.

Wakati wa somo, onesha baadhi ya bidhaa, huku ukiuliza swali kulingana na bidhaa, na kuwaambia wanafunzi wachache wajibu.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kisha, waweke wanafunzi katika makundi, ili waulizane na kujibizana kwa utaratibu huo huo.

Waambie kila kundi watunge na kuigiza wimbo wenye mistari yenye muundo huu: Kabla, hiyo …. ilikuwa shilingi …., lakini sasa ni shilingi …. tu.

Wanafunzi wako wamejifunza nini kutokana na shughuli hizi? Unajuaje? Je, utatumia aina hii ya zoezi tena?Kwa nini utalitumia tena, au kwa nini hutalitumia tena?

## Somo la 2

Katika ufundishaji wa lugha ni muhimu kuzingatia maana ya lugha, kwa kukazia umuhimu wa mawasiliano, lakini wakati huohuo, kukazania ukuzaji wa uwezo wa kisarufi wa wanafunzi. **Shughuli 2** inatoa mfano wa jinsi ya kutumia shairi la kusifu lililoandikwa kwa Kiingereza kufanyia kazi na wanafunzi kwa upande wa vitenzi na vielezi. Aina hii ya kazi inaweza kufanywa kwa kutumia matini za viwango mbalimbali, kwa kuzingatia viwango vya miundo mbalimbali. Vilevile, hakikisha kwamba unazingatia maana ya kipande cha maandishi, ingawa usitumie maana hiyo kwa urahisi tu kama nyenzo ya kufundishia sarufi. Ukiwa na wanafunzi wa umri mdogo, mkazo uwe kwenye maana na ufurahishaji.

Kwa kawaida hadithi hutumia njeo iliyopita, wakati maelezo aghalabu hutumia njeo iliyopo. Haya ni mazingira mazuri ya kuwapatia wanafunzi wako mazoezi ya njeo.

Kama hufundishi Kiingereza, fikiri kuhusu mada ya kisarufi ya lugha unayofundisha iliyo ngumu kwa wanafunzi, na utumie **Shughuli 2** kulingana na lugha hiyo.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kujadili sarufi katika warsha ya walimu

Katika warsha iliyofanyika Tanga, walimu walikuwa na majadiliano changamfu kuhusu sarufi. Bwana Thomas Changae alishuhudia kuwa alisoma kwamba sarufi ni mifupa au kiunzi cha lugha na maneno mengine ni nyama. Vyote viwili mifupa na nyama vinachangia katika maana. Walimu walikubaliana kwamba wanafunzi wanahitaji kuendeleza welewa wao wa jinsi miundo ya lugha inavyofanya kazi, lakini pia walilalamika kuhusu wanafunzi kutopenda masomo ya sarufi.

Bi Susan Mkari alisema alijaribu kuhusisha shughuli ambazo zilikazia kwenye miundo ya lugha wakati wanafunzi wake wa Darasa la 6 wanaposoma hadithi na mashairi ya kuvutia. Kwa mfano, baada ya kufanya marudio ya njeo kuu za kitenzi cha Kiingereza, aliwaambia wanafunzi kutoa maoni yao kuhusu sababu za mwandishi wa hadithi au shairi kutumia njeo iliyopita, ya sasa au ya wakati ujao. Kisha, aliwaambia wanafunzi kuamua njeo ipi ya kitenzi au njeo zipi wanazihitaji katika kuandika hadithi au shairi lao wenyewe ili kuleta mvuto zaidi kwa wasomaji wao.

Kwa kuwa Kiingereza ni lugha ya ziada kwa wanafunzi, Bi Mkari hutengeneza chati kubwa nyuma ya kalenda za zamani. Hii huwapa wanafunzi taarifa kuhusu njeo mbalimbali za vitenzi kuhusu wakati uliopo, uliopita na ujao. (Angalia **Nyenzo-rejea 3: Chati za njeo za kitenzi** kwa mfano rahisi ambao unaweza kutumia na wanafunzi wako.) Anawahimiza wanafunzi wake kusoma chati hizi wanapoandika.

## Shughuli ya 2: Mchezo wa ugunduzi wa kitenzi na kielezi

Toa nakala za **Nyenzo-rejea 4: Shairi la kusifu** . Mahali ambapo mashine za kutolea nakala hazipo, nakili shairi ubaoni au sehemu ya nyuma ya kalenda.

Mara wanafunzi watakaposoma shairi na kulielewa, waache wafanye kazi kwenye makundi kwa kutafuta vitenzi vyote vilivyomo katika shairi. Wakumbushe wanafunzi kwamba vitenzi vingi ni maneno 'yanayoonesha kutenda'. Waambie kila kundi kuripoti mbele ya darasa kuhusu vitenzi katika ubeti mmoja (angalia **Nyenzo-rejea 5: Vitenzi na vielezi katika shairi**).

Waulize wanafunzi vitenzi viko katika njeo gani. Katika ubeti wa 1 na 2, vitenzi viko katika njeo iliyopo; baadhi ya vitenzi katika ubeti wa 3 viko katika njeo ijayo na vingine katika ubeti wa 4 viko katika njeo iliyopita. Kwa wanafunzi wa kiwango cha juu zaidi, jadili kwa nini njeo hizi zilitumika.

Waulize kuna tofauti gani kwenye maana inayosababishwa na utumiaji wa njeo tofauti na athari yake kwa shairi?

Unaweza kutumia mashairi na hadithi nyingine kwa njia zinazofanana na hizi.

## Somo la 3

Yumkini utakuwa umegundua kwamba ni vigumu, wakati mwingine, kusahihisha kazi zilizoandikwa na wanafunzi, kwa sababu kuna makosa mengi sana ya lugha ndani yake. Hutakiwi kuwavunja moyo wanafunzi wako kwa kufanya masahihisho mengi kupita kiasi. Lakini pia hutakiwi kuwaacha waendelee na tabia mbaya. Tutatatuaje tatizo hili?

Njia mojawapo ni kuunganisha maana na miundo ya lugha. Andaa zoezi la kuandika ambalo lina maana kwa wanafunzi. Wahimize wahariri kazi zao kabla hawajazikusanya. Unaweza kuwaambia, wawili wawili, waandike ili waweze kusaidiana. Kisha wanaweza kurudishiwa kazi zao bila kuwa na maoni mengi ya kiusahihishaji.

Unaposahihisha kazi zao, zingatia kwenye maana na jambo linalopendelewa. Uzingativu wa pili, kazia kwenye kipengele kimoja cha muundo wa lugha –tahajia au pengine njeo za kitenzi au viunganishi. Kwa njia hii, maoni ya kiusahihishaji huwa si mengi na huelekeza sehemu maalum, na wanafunzi wana uwezekano mkubwa wa kuyaona na kuyazingatia.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 3: Kubadilishana uzoefu katika 'Gurudumu la Waandishi'

Kozi ya kundi la walimu waliomo kwenye mafunzo kazini mjini Tabora walikuwa wakijaribu kuboresha uandikaji wao wenyewe. Wakufunzi waliwahimiza kuunda 'Gurudumu la Waandishi', ambako watasomeana kazi zao na kupeana maoni. Waliandika kuhusu uzoefu wao –kumbukumbu za utotoni, watu na mahali pa ajabu wanapopakumbuka, mambo ambayo hawatayasahau.

Wakufunzi waliwaongoza katika utoaji wa maoni, kwa kutumia vigezo mbalimbali kutegemeana na kitu kilichokuwa kimeandikwa. Hii hapa ni mifano:

Je, mwandishi anakisema akitakacho kwa ufasaha? Je, kuna sehemu ambazo zinahitaji kufafanuliwa?

Sehemu zipi zinavutia? Kitu gani kinazifanya zivutie? Sehemu gani zinachusha? Zinawezaje kuboreshwa?

Je, kila aya ina wazo kuu? Je, kuna baadhi ya mawazo makuu yanayohitaji kuendelezwa zaidi? Je, aya zinahitaji kupangwa tena?

Je, sentensi ni kamilifu? Je, ni ndefu sana au fupi sana? Je, zimewekewa alama za uandishi kwa usahihi? Je, tahajia za maneno ni sahihi?

Kazi hiyo imeandikwa kwa kutumia njeo ipi? Kagua ili kuhakikisha kwamba kila kitenzi kiko katika njeo stahili au kama kuna sababu ya msingi ya kutumia njeo nyingine.

Kitabu kiliwekwa pamoja kwa kujumuisha maandiko ya walimu hawa ambacho kilshirikishwa kwa familia na rafiki. Walimu waliamua kwamba baadhi ya mawazo haya yanaweza kutumika darasani, vikabadilishwa kulingana na umri na uwezo wa wanafunzi wao.

## Shughuli muhimu: Uhariri wa kujifanyia mwenyewe na wa kubadilishana na wanadarasa kwa lengo la kuboresha uandishi

Waambie wanafunzi wako waandike kuhusu jambo linalotokana na uzoefu wao wenyewe. Jadili mawazo yatakayojitokeza ili kusisimua ubunifu wao. Kwa mfano, wanaweza kueleza kitu ambacho ni mali yao au mtu wa kuvutia wanayemfahamu. (Kwa kuwa uandishi huu ni wa kutoa maelezo, ni yumkini wakatumia njeo iliyopo.) Wanaweza kusimulia hadithi ya kutisha au tukio la kusisimua, au jambo la kijumuiya. (Kwa vile uandishi huu unajumuisha hadithi au masimulizi, ni yumkini wakatumia njeo iliyopita.) Wanafunzi wengine wanaweza kuona inasaidia zaidi kufanya kazi hii wawili wawili.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kisha, waambie wafanye kazi katika makundi madogo madogo, kwa kusomeana maandishi yao. Watake watumie mojawapo au zote mbili kati ya seti za maswali zifuatazo ili kutoa maoni kwa kila kundi:

A. Sehemu zipi zinavutia? Kitu gani kinazifanya zivutie? Sehemu zipi zinachusha? Hizi zinawezaje kuboreshwa?
B. Uandishi huu umetumia njeo gani? Kagua ili kuhakikisha kwamba kila kitenzi kiko katika njeo stahili AU hakikisha kuwa kuna sababu ya msingi ya kutumia njeo nyingine.

Baada ya kupata maoni kutoka kwenye makundi, kila kundi liandike tena kazi yao. Kusanya kazi hizo, na tumia vigezo sawa kusahihisha kazi zote.

Utaratibu huu ulifanikiwa kwa kiasi gani? Je, utaurudia tena?

Je, hali ya uandishi wa wanafunzi wako ilipata ubora? Unajuaje?

## Nyenzo-rejea ya 1: Miundo mbadala ya somo – iliyotumiwa na Bwana Gasana

**Usuli/taarifa ya mwanzo/uelewa wa mwalimu**

**Mfuatano wa swali na jibu**

S: Je, Bibi Yuhi, ulisikia mlio wa bunduki?

J: Ndiyo, wakati huo tulikuwa tunakula cha jioni.

au

S: Je, Bwana Mulifi, ulisikia mlio wa bundukit?

J: Hapana, wakati huo nilikuwa ninasafiri kwenda Nyanza.

**Miundo ya ripoti ya askari wa upelelezi**

Bibi Yuhi alisikia mlio wa bunduki wakati walipokuwa wakila chakula cha jioni.


au

Bwana Mulifi hakusikia mlio wa bunduki kwa sababu alikuwa safarini kwenda Nyanza.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Nyenzo-rejea 2: Tangazo la mauzo

**Nyenzo ya Mwalimu ya kutumia na wanafunzi kwa ajili ya kupanga/kurekebisha**




Kwa wanafunzi wenye umri mkubwa, unaweza kutumia mfuatano wa kiwango cha juu zaidi, kama vile:

S: Tazama shati ile! Hiyo ni bei rahisi.

*J: Ndiyo, walikuwa wanaliuza kwa ShzT …. wiki iliyopita!*

*au*

*S: Ninakuonea huruma ulinunua hizo jeans wiki iliyopita!*

J: Ndiyo, natamani ningesubiri punguzo la bei. Nimepoteza ShzT ….

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

**Orodha ya bei za mboga mboga**

Onesho hili linaweza kuwa lenye manufaa kama uko eneo la vijijini ili kuunda mazingira kwa ajili ya **Shughuli 1**.



*Chanzo: Decade Volcano Photograph, Website.*

BEI POA KABISA ZA LEO –NJOO UNUNUE!

MUHOGO siyo ShzT 2500 SASA ShzT 2000!

NYANYA siyo ShzT 1500 SASA ShzT 1200!

VITUNGUU siyo ShzT 1500 SASA ShzT 1100!

NDIZI siyo ShzT 1500 SASA ShzT 1000!

## Nyenzo-rejea 3: Chati za njeo za kitenzi

**Nyenzo ya Mwalimu ya kutumia na wanafunzi kwa ajili ya kupanga/kurekebisha**

| Njeo iliyopo | Njeo iliyopita | Njeo ijayo |
|---|---|---|
| Natembea | Nilitembea | Nitatembea |
| Nang'ata | Niling'ata | Nitang'ata |
| Nachagua | Nilichagua | Nitachagua |
| Nalima | Nililima | Nitalima |
| Nachora | Nilichora | Nitachora |
| Nakula | Nilikula | Nitakula |
| Nasahau | Nilisahau | Nitasahau |
| Nafahamu | Nilifahamu | Nitafahamu |
| Naona | Niliona | Nitaona |
| Nalala | Nililala | Nitalala |
| Naogelea | Niliogelea | Nitaogelea |
| Naandika | Niliandika | Nitaandika |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Nyenzo-rejea 4: Shairi la kusifu

**Kwa matumizi ya wanafunzi**

*Ngoma Yangu* na Francis Faller

Inapiga
kwa uvumilivu
kama maji
yadondokayo
toka kwenye
bomba la
mfereji
au kwa majivuno
kama sauti ya mapigo ya maji ya bahari.
Ngoma yangu. Ngoma yangu.
Inaita upendo.
Inatwanga hasira.
Inahubiri uhuru.
Haisimami kamwe
Hata wakati hakuna mtu
anayesikia ngoma yangu
isipokuwa mimi.
Ngoma yangu inasalimia
kila kitu

kipitacho njia:
jua linalochomoza
mvua inayogongagonga
upepo unaovuma
familia ya korongo
makazi pote angani.
Inamsalimia chenene
Anayelia mlio mwembamba kwa sababu ya raha yake.
Inawasalimia wafanyakazi
ambao vifaa vyao vya kutobolea na kupasulia
vinachimba mashimo
kwa kuchosha.

Ninaifuatilia
katika kicheko
Ninaiongoza kuvuka
maumivu yanayopwita.
Ni shorewanda anayedonoa mbegu
ni ufito kando ya ukingo
ni risasi iendayo kasi.
Ngoma yangu. Ngoma yangu.
Inapiga kwa kiherehere
makaribisho
kwa ajili yako.
Je, utaisikia
kwa furaha?
Je, utakimbia kwa hofu?
Ngoma ni
ngozi na mbao tu
kwa hiyo utakuja?
Ni lazima uje.
Ni lazima uje.
Ngoma yangu kipenzi
ilikuwa jana dhaifu sana.
Leo inapiga.
Kwa nguvu.
Hakika haikutumika zaidi
duniani kote
kupiga bure.
Ingawa kamwe
haipati jibu
Nafikiri
sitaweza kuishi
kama wimbo
wa ngoma yangu
utakufa.

*Chanzo asilia: My Drum – Meyerowitz, B., Copans, J. & Welch, T. (watunzi)*

# Nyenzo-rejea 5: Vitenzi na vielezi katika shairi – Ngoma Yangu na Francis Faller

**Taarifa za msingi / welewa wa somo wa mwalimu**

Katika tafsiri hii ya shairi vitenzi vimepigiwa mstari na vielezi vimewekewa wino uliokolezwa.

| | |
|---|---|
| Inapiga<br>**kwa uvumilivu**<br>kama maji<br>yadondokayo | Dokezo 1: patiently ni kielezi cha namna, ambacho kinaeleza jinsi ngoma inavyopiga/lia: kwa utulivu, kwa kurudiarudia pasipo kuudhika au kuwa na hasira. |
| toka kwenye<br>bomba la<br>mfereji | Dokezo 2: dripping ni sehemu ya kitenzi kamili 'is dripping': kama maji [that is/ambayo] inadondoka – mshairi ameamua kutotumia 'that is'. |
| au **kwa majivuno**<br>kama sauti ya mapigo<br>ya maji ya bahari.<br>Ngoma yangu. Ngoma<br>yangu.<br>Inaita upendo.<br>Inatwanga hasira. | Dokezo 3: proudly vilevile ni kielezi ambacho kinaeleza jinsi ngoma inavyolia: kwa kujipenda, kama kwamba inajifurahia sana. |
| Inahubiri uhuru.<br>Haisimami **kamwe**<br>Hata wakati hakuna<br>mtu<br>anayesikia ngoma<br>yangu<br>isipokuwa mimi. | Dokezo 4: never ni kielezi cha wakati ambacho kinaongezea taarifa kwenye kitenzi 'stops': ngoma haiwezi kusimama hata mara. |
| Ngoma yangu<br>inasalimia<br>kila kitu<br>kinachopita njia: jua | Dokezo 5: battering ni sehemu ya kitenzi kamili 'is battering': mvua [that is/ambayo] inagongagonga. |
| linalochomoza mvua<br>igongayo upepo<br>unaovuma familia ya<br>korongo makazi | Dokezo 6: monotonously ni kielezi cha namna ambacho kinaeleza jinsi kazi ya kuchimba inavyoendelea kwa namna inayochosha na ya kurudiarudia |
| pote angani.<br>Inamsalimia chenene<br>Anayelia mlio<br>mwembamba kwa<br>sababu ya raha yake. | Dokezo 7: It's ni kifupi cha It is na 'is' ni kitenzi, ingawa si kitenzi kinachoonesha tendo. |
| Inawasalimia<br>wafanyakazi<br>ambao vifaa vyao vya<br>kutobolea na kupasulia<br>vinachimba mashimo | Dokezo 8: Nervously ni kielezi cha namna ambacho kinaeleza jinsi ngoma inavyolia: kama kwamba ngoma ina hamu au ina woga kidogo. |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

| | |
|---|---|
| **kwa kuchosha**. | Dokezo 9: ‘will come’ ni iko katika njeo ijayo lakini iko katika muundo wa swali, ‘will you come?’ |
| Ninaifuatilia katika kicheko Ninaiongoza kuvuka maumivu yanayopwita.<br>Ni shorewanda anayedonoa mbegu | You should ni muundo uliofupishwa wa You should come – vilevile ni tendo katika njeo ijayo. |
| ni ufito kando ya ukingo | Dokezo 10: was ni njeo iliyopita ya ‘is’. |
| ni risasi iendayo kasi. Ngoma yangu. Ngoma yangu. | Dokezo 11: Strong kwa kawaida ilitakiwa iandikwe ‘strongly’: hiki ni kielezi ambacho kinaeleza jinsi ngoma inavyolia. |
| Inapiga **kwa kiherehere** makaribisho<br>kwa ajili yako. | Dokezo 12: wasn’t stretched ini kitenzi kilicho katika njeo iliyopita. |
| Je, utaisikia<br>kwa furaha?<br>Je, utakimbia kwa hofu? | Dokezo 13: never ni kielezi cha wakati (tazama Dokezo 4). |
| Ngoma ni<br>ngozi na mbao tu<br>kwa hiyo utakuja?<br>Ni lazima uje.<br>Ni lazima uje. | Dokezo 14: could not live na should die ni vitenzi ambavyo vinarejelea katika wakati ujao kwa sababu vinaashiria kwamba mshairi hataweza kuishi hapo baadaye bila ngoma. |
| Ngoma yangu kipenzi ilikuwa jana dhaifu sana. Leo inapiga.<br>**Kwa nguvu**.<br>Hakika haikutumika zaidi<br>duniani kote<br>kupiga bure.<br>Ingawa **kamwe** | Dokezo 15: Wanafunzi wanaweza kukanganywa na maneno yanayoishia na ‘ing’. Wakati mwingine maneno haya ni sehemu ya kitenzi, mfano: ‘I am *singing*. Pengine maneno haya ni nomino, mfano: ‘The *singing*’ of the choir was excellent. Pengine, ni vivumishi ambavyo vinafafanua nomino, mfano: ‘The *singing* canaries’ flew to the top of their cage. Katika shairi hili dripping, battering, chirping, digging, pecking, beating ni sehemu za vitenzi. The pounding ni nomino. Throbbing ni kivumishi kinachofafanua pain. |
| haipati jibu<br>Ninafikiri<br>sitaweza kuishi<br>kama wimbo<br>wa ngoma yangu<br>**utakufa**. | Everything ni kiwakilishi ambacho kinasimama mahali pa nomino ambazo zinakifuatia katika ubeti wa 2. For nothing ni msemo ambao unamaanisha ‘without payment/bila malipo’ au ‘for no reason/bila sababu’. |

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 3: Kuunda Fursa za Mawasiliano

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kuunda shughuli za kukuza mawasiliano katika lugha ya ziada?

**Maneno muhimu:** tofauti katika taarifa; maingiliano ya kimawasiliano; umaanifu; kuunda shughuli; makundi

| Matokeo ya ujifunzaji |
|---|
| Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:<br>• umeunda shughuli za mawasiliano halisi katika darasa lako la lugha ya ziada;<br>• umeendeleza 'maktaba' ya nyenzo za kuchochea mazungumzo asilia;<br>• umetumia kazi za vikundi na za wanafunzi wawili wawili ili kukuza mawasiliano ya lugha ya ziada. |

## Utangulizi

Ukiwa mwalimu, unapaswa kutumia matokeo ya tafiti kuhusiana na kitu unachokifanya. Tafiti za hivi karibuni zinaonesha kwamba watu hujifunza lugha kutokana na kushiriki katika mawasiliano yenye maana ya lugha husika, katika mazingira asilia. Hoja hii inamaanisha nini?

'Kushiriki': Kila mwanafunzi lazima ashiriki –au ahusishwe kikamilifu.

'Umaanifu': Shughuli lazima iwe inalandana na mazingira halisi na ilete maana kwa wanafunzi.

'Maingiliano': Mawasiliano lazima yahusishe njia-mbili (au njia tatu au nne).

'Mazingira asilia': Lugha inayotumiwa lazima iwe lugha ya kawaida ya mawasiliano ya kila siku.

Katika sehemu hii, tunaangalia jinsi ya kuchochea maingiliano ya kimawasiliano ya aina hii darasani kwako, hususan kwa kutumia picha. Tunashauri kwamba uunde uteuzi wa zana.

Kwa kawaida, darasa lenye kazi za maingiliano ya kimawasiliano hufanywa katika makundi madogo madogo. Itasaidia kusoma **Nyenzo-rejea Muhimu: Kutumia kazi za vikundi katika darasa lako** .

## Somo la 1

Kuwatia hamasa wanafunzi ili wawasiliane miongoni mwao kunahusu uandaaji wa shughuli wanazoweza kuzifanya pamoja, na ambazo ni 'halisi'. Makundi yanasaidia kutiana moyo na yanawawezesha wanafunzi kujaribu lugha mpya.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Mawasiliano ‘halisi’ huhusisha ‘tofauti za taarifa’; kwa maneno mengine, wanafunzi hugundua kitu ambacho hawakukifahamu awali kutoka kwa wenzao. Zamani, wanafunzi wangeweza kuagizwa kumwuliza mwanadarasa mwenzao, ambaye jina lake wanalifahamu vizuri, ‘Jina lako nani?’ Hapa hakuna tofauti ya taarifa, kwa hiyo mawasiliano haya si ‘halisi’.

**Uchunguzi-kifani 1** na **Shughuli 1** zinaonesha jinsi utafutaji wa taarifa zinazokosekana unavyoweza kutumika kwa lengo la kuunda makundi au kazi za watu wawili wawili. Vile vile, angalia **Nyenzo-rejea 1: Mifano zaidi kuhusu Shughuli za tofauti za taarifa** .

## Uchunguzi kifani ya 1: Shughuli za tofauti za taarifa katika kuunda makundi

Liz Botha wa East London, Afrika ya Kusini, alitaka kugawanya kundi la walimu 40 katika makundi manne, kwa namna ambayo ingewasaidia kuwasiliana miongoni mwao.

Alitafuta jumla ya picha 16 zote katika ukurasa mmoja wa kitabu (angalia **Nyenzo-rejea 2: Mawazo katika picha** ). Alitengeneza nakala nne za ukurasa huo na kukata picha kumi kutoka katika kila ukurasa ili apate makundi kumi yenye picha nne nne: viatu; bendera, nk. Kisha alizichanganya picha.

Walimu walipofika, alimpatia kila mmoja picha moja, na kuwaambia wasiioneshe kwa mtu yeyote. Kisha akawaagiza watembee kuzunguka darasa, wakiuliza maswali ya aina hii:

Swali: Una picha ya (n) …. ?

Jibu: Hapana, sina./Ndiyo, ninacho.

Waliendelea namna hii mpaka wakaunda kundi la watu wanne wenye picha zinazofanana.

Baada ya makundi kuundwa, wanavikundi wakaanza kusemezana, na wakagundua, kwa njia ya majadiliano, kwamba wana kitu kimoja kilicho sawa kwa wote: labda wote wanne wana dada wadogo, au wanapenda au hawapendi aina fulani ya chakula au muziki, nk.

Walifurahia mno shughuli hii, na waliikamilisha kwa kufahamiana zaidi miongoni mwao.

Ni kwa jinsi gani unaweza kufanya shughuli kama hii katika darasa lako?

## Shughuli ya 1: Tafuta mwenzi wako

Andika orodha ya maneno yanayohusiana na somo la hivi karibuni (angalia **Nyenzo-rejea 3: Maneno na maana** ili kuona baadhi ya maneno).

Wape kila wanafunzi wawili wawili neno moja kutoka kwenye orodha na vipande vidogo viwili vya karatasi. Waambie waligawe neno lao katika sehemu mbili/nusu, na waandike nusu moja katika kila kipande miongoni mwa vipande hivyo vidogo vya karatasi.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Kusanya na changanya vipande vyote vya karatasi. Sasa mpe kila mwanafunzi nusu-neno.

Waambie wanafunzi wamtafute mwanafunzi ambaye ana nusu nyingine ya neno lao, na kisha wasimame naye.

Kundi la wanafunzi wawili wawili lisome maneno yao mbele ya darasa.

Kisha, kila kundi la wanafunzi wawili wawili liandike maana ya neno lao katika kipande kingine cha karatasi. Kusanya maana hizo na maneno yaliyo nusu.

Wape tena maneno yaliyo nusu na rudia mchakato wa kuoanisha.

Baadaye, taja kila maana kwa zamu na liambie kundi la wanafunzi wawili wawili likae chini litakaposikia maana ya neno lao. Mtu yeyote asiseme kama wamekaa chini kwa kukosea au kwa usahihi. Mwishoni maana zitafafanuliwa.

Jaribu mchezo huu tena na angalia kama wanaweza kuucheza kwa haraka na kwa usahihi zaidi.

Je, shughuli hii iliwasaidia wanafunzi wako kuelewa maana za maneno? Unajuaje?

## Somo la 2

Ukiwa mwalimu, mara zote unapawa kutafuta shughuli ambazo zinakuza ujuzi wa kusikiliza kwa kuelewa.

Hapa, **Shughuli 2** inahusisha kusikiliza na kuchora, au kubadili lugha ya taarifa kwenda katika kielelezo cha taarifa. Ina faida inayofanana na *mwitikio wa mwili wote* (total physical response); kwa sababu wanafunzi hawalazimiki kutumia lugha katika kuonesha welewa wao. Hata hivyo, inatakiwa yule anayeelezea awe fasaha na sahihi sana –vinginevyo, athari zinaweza kuonekana kwenye picha ya mwanafunzi mwenza.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kueleza na kupanga mawasiliano yasiyofahamika kwa njia ya posta

Aghalabu, Lulu alikuwa akipata 'mawasiliano asiyoyafahamu' yaliyowekwa kwenye sanduku lake la barua: matangazo kutoka kwenye maduka mbalimbali yanayoonesha picha za bidhaa zao. Siku moja aliamua kuyaweka, badala ya kuyatupa kwenye pipa la taka.

Alikata sehemu tofauti tofauti za bidhaa za nyumbani: pakiti za vyakula, sukari na unga; maboksi ya sabuni za unga na nafaka, nk. Alikuwa na nakala nyingi.

Alichora picha sita za vinafasi vya kabati la jikoni, na kuchomeka bidhaa za nyumbani katika vijinafasi vitatu ( Nyenzo-rejea 4: Eleza na panga sinaonesha mifano). Kila moja kati ya picha hizo tatu ilikuwa tofauti na nyingine. Kisha alikata nakala za bidhaa zote kwenye vijinafasi vya kabati la jikoni. Bado alibakiwa na vijinafasi titatu visivyo na kitu.

Siku iliyofuata, kwenye Darasa lake la 4, makundi matatu ya wanafunzi sita sita au saba saba yalipewa picha za vijinafasi vya kabati vilivyojaa vitu. Vile

vilivyokuwa vitupu, viligawiwa kwa makundi mengine matatu, na wanafunzi tofauti katika makundi haya walipata nakala za bidhaa.

Aligawa makundi hayo katika sehemu mbili, na kulifanya sehemu ya 1 (ililo na picha zilizokamilika) kukaa karibu na sehemu ya 2 (yenye vijinafasi visivyo na kitu na bidhaa tofauti). Wanakundi la sehemu 1 walieleza jinsi bidhaa zilivyopangwa kwenye vijinafasi, na wanakundi la sehemu 2 walizipanga katika vijinafasi vilivyokuwa vitupu. Waliuliza maswali pale ambako hawakuwa na uhakika. Mchezo huu uliwapa zoezi la kutumia maneno kuhusu nafasi mbalimbali katika mazingira 'halisi'.

Somo lilikwenda vizuri. Lulu aliamua kwamba wakati mwingine atakuza msamiati wa wanafunzi wake kwa kuwaambia wachambue na kueleza taswira za –au, kama itawezekana, ngoma-halisi na vitu vilivyobuniwa kutoka katika jumuiya ya mahali hapo.

## Shughuli ya 2: Eleza na chora

Shughuli hii hufanywa katika makundi au na watu wawili wawili. Mtu mmoja anaeleza na mwingine/wengine anachora/wanachora. Darasa lenye wanafunzi wa viwango mbalimbali, wanafunzi wakubwa wanaweza kutoa maelezo, na wadogo wachore.

Tafuta picha au michoro rahisi sana au chora ya kwako, m.f. mchoro wa vistari wa picha ya nyumba au mti. Utahitaji picha moja kwa kila jozi au kundi la wanafunzi. Picha zinaweza kuwa sawasawa au tofauti.

Anza kuwafundisha wanafunzi msamiati na aina za sentensi ambazo watahitaji kuzitumia, mfano, 'Chora mraba katikati ya ukurasa'. 'Chora kuku wawili kando ya nyumba.'

Toa picha moja kwa kila jozi (au kundi) la wanafunzi, huku ukiwaambia 'watoa maelezo' kutowaonesha wenzao picha hizo. Mwanafunzi aliyeshika picha anaielezea picha hiyo kwa wanafunzi wengine/mwanafunzi mwingine, ambaye anajaribu kuchora kitu kinachotolewa maelezo. Hawatakiwi kusema picha hiyo ni nini.

Mwishoni, mtoa maelezo na mchoraji wanalinganisha picha zao. Anza mjadala wa darasa zima: Duara la 'Asanda' ni dogo kuliko lililoko katika picha'. Kuku wa Amina wana vichwa vikubwa, lakini kuku walioko katika picha wana vichwa vidogo.' Wakiwa wanafanya mazoezi, wataifanya vizuri zaidi shughuli ya aina hii.

**Nyenzo-rejea Muhimu: Kufanya kazi katika madarasa makubwa/madarasa ya mchanganyiko** kunatoa mawazo zaidi kuhusu mbinu za kufanya kazi.

## Somo la 3

Ukiwa mwalimu, unapaswa kukumbuka kwamba aghalabu, binadamu (pamoja na wanafunzi) hutaka kujua maana ya kitu wanachokifanya. Kila shughuli unayowapa wanafunzi lazima iwape fursa ya kutafuta maana.

**Uchunguzi-kifani 3** na **Shughuli Muhimu** vinatalii njia za kutafuta maana katika aya au matini. Wanafunzi wafanye mazoezi ya baadhi ya maarifa muhimu yaliyomo katika maandishi hayo: utabiri na utazamiaji (kukisia kitu gani kitatokea baadaye). Walitakiwa pia kuwasiliana miongoni mwao ili kutatua tatizo. Kila mmoja alikuwa na nafasi ya kuchangia ili kutatua 'fumbo' na kutafuta maana.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 3: Hadithi: kutoka vyanzo tofauti na kuwekwa pamoja

Darasa la 6 la Bibi Ndaba lilileta hadithi kutoka majumbani na kuzieleza kwa ufafazi. Katika kila ukurasa, waliandika sentensi na kuchora picha inayoona na sentensi husika. Kurasa hizo zilipachikwa kwenye magamba ya plastiki ya kurekodia na kuunda jarida ambalo ili kutengeneza kitabu.

Mfanyakazi mwenzie, Bibi Mapande, ambaye anafundisha darasa la 3 aliziona hadithi zilizofafanuliwa, na akaomba kuziazima kwa ajili ya shughuli ya kusoma katika darasa lake. Bibi Ndaba alifika kuangalia darasa la mwenzie.

Bibi Mapande aliligawa darasa lake katika makundi matano. Alilipa kila kundi hadithi lakini alizitoa kurasa kutoka kwenye jarida na kuliweka jarida hilo katikati ya meza. Alimpa kila mwanafunzi katika kundi ukurasa mmoja wa hadithi, huku akihakikisha kwamba amechanganya mpangilio wa kurasa hizo. Kila mwanafunzi alitakiwa kusoma sentensi iliyo kwenye ukurasa wake mbele ya kundi lake. Kwa njia ya majadiliano, kundi liliamua sentensi ipi ikae mwanzo wa hadithi, na kuweka sentensi nyingine zote katika mpangilio unaostahili; na kurudishia kurasa katika jarida kwa mpangilio sahihi.

Bibi Mapande alimwambia mwanafunzi mmoja kutoka katika kila kundi, asome hadithi ya kundi lake mbele ya darasa; na wanadarasa walitoa maoni kuhusu mpangilio wa sentensi. Wakiwa katika darasa, walichagua hadithi waliyoipendelea zaidi, na igizo la dakika tano likaandaliwa kuonesha hadithi hiyo.

## Shughuli muhimu: Sehemu za kitu kizima

Unaweza kutumia shughuli ya aina hii kwa darasa la kiwango chochote

Chagua hadithi fupi, iliyoandikwa vizuri, au aya ambayo wanafunzi wako wanaweza kuielewa na kuihusisha na ukweli. Unaweza kutumia hadithi, hadithi au aya za/ya picha kama zile zilizoko katika **Nyenzo-rejea: Kuunda maana** , au aya ambayo ni changamano zaidi ya lugha au mada yoyote. Kila kundi linaweza kuwa na hadithi hiyo hiyo au tofauti ya kushughulikia.

Ikate hadithi katika vipande sita au saba. Vipande vyaweza kuwa aya, sentensi au kundi la sentensi, kulingana na umri na uwezo wa wanafunzi wako. Pachika kila kipande kwenye kadi.

Lipe kila kundi seti ya sehemu za aya zilizokatwa.

Kila mwanakikundi ana kipande cha aya, na anawasomea wengine kipande chake. Wakiwa kama kundi, wanaziweka aya zao pamoja katika mpangilio wake sahihi.

Kwa wanafunzi ambao wana uwezo au uzoefu zaidi, waambie waeleze jinsi walivyofanya mpaka kupata mpangilio sahihi.

Soma aya au hadithi hizo mbele ya darasa.

# Nyenzo-rejea ya 1 : Shughuli zaidi zihusuzo tofauti za taarifa

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**

**Kufanana ni nini ?**

Chagua seti za picha sita au nane. Kila seti ya picha lazima iwe na kitu kinachofanana kwa picha zote. Kwa mfano, unaweza kuwa na picha sita ambazo zote zina kitu kimoja ambacho kimetengenezwa kwa kioo, au seti ya picha sita ambazo katika kila picha kuna mtu anakula. Pengine una picha sita ambazo zinaonesha mtoto, au zinaonesha umaskini, au ukarimu.

Gawa darasa lako katika makundi ili kila kundi linaweza kuwa na seti ya picha kadhaa. Hakikisha kwamba una baadhi ya picha za akiba, kwa ajili ya kundi lolote litakalomaliza kazi haraka. Mara kundi linapomaliza, unaweza kukusanya seti za picha zao na kuzigawa kwa kundi lingine ambalo limemaliza.

Wanakikundi wasioneshane picha zao. Wanatakiwa kuulizana na watu wengine katika kundi aina ifuatayo ya maswali :

Je, kuna (kitu)…. Katika picha yako ?

Je, kuna (vitu)…. Katika picha yako ?

Je, picha yako inaonesha …. ?

Wanakikundi wengine wanajibu:

Hapana, hakuna. Au, Ndiyo, ipo/zipo.

Hapana, haioneshi. Au, Ndiyo, inaonesha.

Mtu ambaye anabainisha sifa ya ufanano ndiye mshindi.

Mchezo huu ni rahisi au mgumu zaidi kutegemeana na kiwango cha udhahania kilichomo kwenye sifa ya ufanano.

**Unafanya nini ili kujipatia kipato?**

Andika orodha ya kazi ubaoni, kama hii iliyopo hapa chini.

| | | |
|---|---|---|
| Daktari | Daktari wa Meno | Mwalimu |
| Muuza duka | Muuguzi | Meneja |
| Karani | Rubani | Mhandisi |
| Mtunza Bustani | Mkutubi | Askari polisi |
| Mkulima | Mchuuzi wa samaki | Fundi wa ngamizi |
| Mhudumu katika ndege | Mfamasia | Mama Ntilie/Lishe |
| Mtaalam wa maua | Mwanasayansi | Mwanamuziki |
| Mtaalam wa ngamizi | Mhudumu wa dukani | Fundi gereji |

Waambie wanafunzi waseme wangependa kufanya nini watakapomaliza masomo yao. Wanaweza kuongeza kazi nyingine katika hizo zilizoorodheshwa.

Toa kadi kwa jozi za wanafunzi na waambie waandike jina la kazi kwenye kadi hiyo. Kwenye kadi nyingine, wanatakiwa waandike fasili ya kazi hiyo.

Mwambie mwanafunzi mmoja kutoka katika kila jozi kutoa ripoti mbele ya darasa kuhusu kazi waliyonayo, na fasili yake. Wanafunzi wengine lazima watoe maoni kama wanadhani fasili ni sahihi.


Kusanya kadi za kazi na maana zake, zisambaze kwa wanafunzi bila kufuata utaratibu wowote. Waambie wanafunzi wazunguke darasani na kutafuta mwenza ambaye ana fasili au neno sahihi.

Wenza wanapopatana, wanatakiwa wasimame pamoja mpaka kila mmoja hapo darasani amalize shughuli hiyo.

Kisha waambie waunde sentensi kwa kutumia kazi walizozifasili.

## Nyenzo-rejea 2: Madokezo kwa ajili ya picha

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**



*Chanzo asilia: Books on display: New Day-by-Day English Course*

*Line drawings: Modern English Teacher, 10*

# Nyenzo-rejea 3: Maneno na maana – mifupa katika mwili

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**

| Neno | Maana |
|---|---|
| Muungabega/Humerus | Aina ya mfupa iliyopo sehemu ya juu ya mkono |
| Fuu la kichwa/Cranium | Fuvu, ambalo huhifadhi ubongo |
| Fibula/goko | Mfupa mdogo kati ya mifupa miwili iliyopo sehemu ya chini ya mguu |
| Radias/Radius | Mmoja kati ya mifupa ya kwenye kiwiko ambao huzunguka kadri unavyouzungusha mkono wako |
| Fema/Femur | Mfupa mmoja uliopo juu ya mguu na ulio mrefu kuliko yote mwilini |
| Pingilimgongo/Vertebrae | Mifupa ambayo huunda uti wa mgongo na inayoshikilia neva zipitazo sehemu hiyo |
| Kifupakono/Metacarpals | Mifupa iliyopo kwenye mkono |
| Kifupakidari/Ster num | Mfupa wa kwenye kidari, ambao unahifadhi moyo |
| Skapula/Scapula | Mfupa ambao unajulikana kama bapa la bega sehemu ya nyuma |
| Muundi goko/Tibia | Mifupa mikubwa miwili iliyopo sehemu ya chini ya mguu |
| Tarisas/Tarsus | Mkusanyiko wa mifupa inayounda sehemu ya juu ya kiwiko na goti |

## Nyenzo-rejea 4:

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**





Unaweza kuandaa michezo kama hii kwa kutumia mpangilio wa nyumbani na picha za samani. Viweke katika sanduku lako la zana kwa matumizi ya baadaye, au ili wanafunzi watumie wakati watakapokuwa na nafasi kwa ajili ya shughuli za kujisomea na ujifunzaji binafsi, na kufanya mazoezi ya msamiati. Unaweza kuhitaji kutumia vitu na bei za mahali hapo.

## Nyenzo-rejea 5: Kuunda maana

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**

**Aya kwa ajili wanafunzi wa madarasa ya juu: Wafalme wa Zulu**

Wafalme wa Zulu walianzisha utawala wa kinasaba wenye nguvu kuliko tawala zote za watu weusi katika Afrika. Mkuu Shaka, ambaye alianzisha utawala wa kinasaba mwanzoni mwa karne ya 19, aliunganisha taifa la Wazulu na kuunda kikosi cha kijeshi kilichokuwa cha kuogopesha. Kufuatia kujulikana kwake kama ‘Napoleon Mweusi’, mfalme huyu wa kwanza wa Wazulu alikuwa katili, ingawa pia alikuwa kiongozi mwerevu sana. Kutokana na sifa yake ya kuwa mshindi na asiye na huruma katika vita, aliongoza watu wake kujipatia umashuhuri na aliwatawala kwa nidhamu ya ukali. Mauaji aliyomtendea nduguye aliyechangia naye mzazi mmoja ambaye alimsaliti, Dingane, hayakusaidia kupunguza utawala wa kigaidi. Lakini Dingane, aliyejiingiza matatani, ijapokuwa alikuwa katili na dikteta, hakuwa mwanajeshi, na utawala wake uliishia katika maafa. Baada ya kuzidiwa nguvu na Makaburu katika vita ya Mto wa Damu, hatimaye Dingane alilazimika kuikimbia nchi ya Zulu, na alifia uhamishoni. Baada ya kifo chake eneo la jirani la Natal likawa makazi ya wazungu, na mkondo wa historia ya Zulu ukabadilika.

*Vyanzo asilia:*

*Matini iliyoandikwa – imetoholewa kutoka ‘The Zulu Kings’, na Brian Roberts, Hamish Hamilton, 1974. imekaririwa katika Rodseth, V. na wengine. 1992. Think Write: A writing skills course for students, teachers and business people. Randburg: Hodder and Stoughton Educational. ISBN 0 947054 87 1*

*Hadithi ya picha – Standard 2 Language Book, Maskew Miller Longman*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 4: Namna ya kujenga juu ya ujuzi wa lugha ya nyumbani

**Swali Lengwa muhimu:** Utawezaje kukuza umilisi katika lugha ya ziada kwa kutumia ujuzi wa lugha ya nyumbani?

**Maneno muhimu:** kujenga; msamiati; dhana; uwili-lugha nyongeza

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- kutumia lugha ya nyumbani kupeusha ubunifu, welewa na ukuzaji wa mawazo;
- kuelewa umuhimu wa mwingiliano baina ya lugh aya nyumbani na lugha ya ziada.

## Utangulizi

Ukiwa mwalimu, unahitaji kupeusha ujifunzaji na stadi katika lugha ya ziada na kwa hiyo unahitaji kufanya maamuzi kuhusu lini na jinsi ya kutumia lugha ya nyumbani. Uchaguzi wako wa lugha unapaswa kutegemea jinsi lugha hiyo itakavyowasaidia wanafunzi katika kujifunza, na sio urahisi wa lugha wa lugha kwa mwalimu.

Katika shule nyingi, lugha za nyumbani za wanafunzi zinatumika nyumbani, na tena katika miaka michache ya mwanzoni ya shule tu. Hali hii husababisha watu wawe na fikira kwamba lugha ya nyumbani haina thamani kubwa. Walimu na wazazi husahau kwamba ni muhimu kutumia ujuzi na stadi za lugha ya nyumbani ya wanafunzi na kutumia lugha zote mbili.

Sehemu hii inaonesha jinsi kutumia lugha ya nyumbani inavyoweza kupeusha ubunifu, welewa na ukuzaji wa mawazo, kadhalika ukuaji wa lugha ya ziada.

## Somo la 1

Wanafunzi wako huja shuleni wakiwa tayari na usuli tajiri wa mitagusano ya kibinadamu na tajiriba za ulimwengu. Wanayo pia lugha ya kuelezea ulimwengu wao. Wanapotumia lugha yao ya nyumbani wanaweza kutumia tajiriba yao kusheheneza uneni na uandishi wao kwa maelezo makini na jazanda. Ukiwa mwalimu, unahitaji kuwahimiza wafanye hivi, na kuwafanya watumie maarifa waliyo nayo.

Kuhusu kusema au kuandika katika lugha ya ziada, wanafunzi mara nyingi hawatang’amua kuwa wanaweza kutumia maarifa hayo. Walimu, pia, wanaweza kusahau kwamba kazi yao ni kuwasaidia wanafunzi wahamishe maarifa yao katika/kwa lugha yao ya nyumbani ili yawe katika lugha ya ziada, na sio kuanza na bure.

Katika kisehemu hiki, tunapendekeza kuwa uwasaidie wanafunzi kueleza wanayofahamu na kubuni/kufikiria kwa lugha yao wenyewe, na kisha kufikiria njia za kuhamishia maana hiyo kwenye lugha ya ziada.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

## Uchunguzi kifani ya 1: Kuandika katika isiZulu kutajirisha Kiingereza

Bi Nonhlanhla Dlamini anafundisha Kiingereza kwa wanafunzi 64 wa darasa la 6 wanaosema isiZulu katika wilaya ya Nongoma katika KwaZulu-Natal, Afrika ya Kusini.

Siku moja, alisoma na kujadili mifano ya mashairi ya sifa na hadithi na wanafunzi wake na kupendekeza kuwa nao waandike yao. Walifurahi sana, lakini jitihadi zao katika Kiingereza hazikuridhisha; kwa hiyo aliamua kuchukua mkabala tofauti.

Bi. Dlamini aliwataka wanafunzi wake kufanya kazi wawiliwawili waelezane kitu wanachotaka kukiandika na kusaidiana waandike hadithi na shairi kwa isiZulu.Kisha wakafanya kazi wawiliwawili kuandika nakala za Kiingereza.

Aliwakumbusha wasifanye tafsiri za neno kwa neon kwa sababu sarufi na msamiati wa lugha mbili hizi vimejengwa kwa namna tofauti.

Jitihadi zilizofuata katika uandishi katika Kiingereza zilivutia zaidi, ingawa hazikusheheni maelezo yenye undani na mvuto kama nakala za Kizulu.

Bi. Dlamini alifanya kazi ya kukuza msamiati na wanafunzi kupanua masafa yao ya vitenzi na vielezi katika lugha ya ziada, kwa kuwa aliona kuwa eneo hili lilikuwa na upungufu. Kisha, akawataka wanafunzi warekebishe uandishi wao, kwa kutumia vitenzi na vielezi vingi zaidi.

Baada ya kuandika majina kwenye kazi zao, wanafunzi waliweka mashairi na hadithi zao kwenye meza nyuma ya darasa. Walifurahia kusomeana kazi zao.

Bi. Dlamini aliona jinsi vitenzi na vielezi vingi zaidi vilivyokuwa sehemu ya msamiati wa kawaida wa wanafunzi kutokana na zoezi hili.

## Shughuli ya 1: Picha za maneno katika lugha mbili

Andika ubaoni shairi la matusi ‘Wewe’. Andika ubaoni shairi la ‘matusi’ ‘Wewe’, lililo katika **Nyenzo-rejea 1: Shairi** .

Lisome na wanafunzi na mjadiliane kila ulinganishi, k.m. ‘kichwa ni kama ngoma tupu’ humfanya mtu afikiri kuwa ni kikubwa na kitupu, n.k.

Watake waandike shairi la sifa, kama darasa, juu ya mtu anayefahamika sana wanayemheshimu.

Amua kwa kushirikiana nao sifa au vipengele ambavyo wataeleza. Kama mtu ni mwanariadha, wanaweza kuchagua sifa za kimwili, miguu, umbo, jinsi anavyotembea, n.k.

Sasa vigawie sifa hizi vikundi au mtu mmojammoja, na watake wafikirie vilinganishi katika lughaya nyumbani.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Watakapotaja vilinganishi vyao, amua, kama darasa, kuhusu kilinganishi bora kwa kila sifa, na viandike katika lughaya nyumbani.

Sasa jadili jinsi wanavyoweza kusema hayo katika lugha ya ziada. Tafsiri ya moja kwa moja (tafsiri sisisi) haifai, lakini jaribu kujenga taswira inayolingana na iliyo katika lugha ya nyumbani.

Kwa njia hii, lijenge shairi lako na darasa lako katika lugha ya ziada.

Watake watunge shairi lao wenyewe –'matusi' au 'sifa'. Wanafunzi wahahakikishe wasisababishe chuki ya kweli. Je, mkabala huu umefaulu kuwasaidia wanafunzi kukuza msamiati katika lugha ya ziada?

## Somo la 2

Mara nyingi watu huwaza kwamba mwalimu lazima atumie lugha ya ziada tu darasani ili wanafunzi waweze kuwa na ufasaha katika lugha hiyo. Hili si wazo baya na linatekelezeka vizuri katika hali fulani. Hata hivyo, hali halisi katika madarasa mengi hapa Afrika ni kwamba:

hakuna wasemaji wazawa au wasemaji wajuzi (walimu au walimu) wa lugha ya ziada shuleni;

wanafunzi wana nafasi finyu sana kutumia lugha ya ziada nje ya darasa;

walimu wengi zaidi hubadilisha msimbo kwa kiasi kingi (hutumia lugha hizi kwa kuzichanganya wanapozungumza);

iwapo lugha ya ziada tu ikitumika wanafunzi hawaelewi wakati mwingi, hasa katika miaka ya mwanzo ya kujifunza lugha mpya.

Wanafunzi wanapojifunza lugha ya ziada kwa miaka michache tu, na kama hawana nafasi ya kuitumia nje ya darasa, wanaweza tu kuelewa na kutunga sentensi zinazohusiana na mambo ya kawaida ya kila siku. Aghalabu hawajawa tayari kuitumia kujadili fikira na dhana. Ili kupanua ujifunzaji ujumuishe kujadili fikira, inafaa kutumia mkabala wa utumizi wa lugha mbili.

### Uchunguzi kifani ya 2: Kujadili mawazo katika lugha ya nyumbani

Huko Kibaha, Zawadi Nyangasa aliongoza darasa la 7,kipindi cha Kiingereza, katika somo lililojikita kwenye hadithi juu ya mfalme na mshona-viatu. Alitaka wafikiri juu ya hulka ya busara ya kweli na ujanja, na madhumuni ya elimu.

Alisoma hadithi kwa sauti kwa wanafunzi, akisita mara kwa mara kuuliza maswali kuona kama wameelewa.

Maswali na majibu mengi yalikuwa katika Kiingereza, lakini kulikuwa na nyakati ambapo alitumia lugha ya kwanza kuelezea dhana au kuhusisha na maisha ya wanafunzi (taz. Nyenzo-rejea 2: Mfano wa somo .)

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Baada ya kusoma hadithi, aliwataka wanafunzi kujadili maswali yafuatayo, katika vikundi vidogo vya watu wanne hadi sita. Aliwahimiza kutumia lugha yao ya mama.

Unafikiri mshona-viatu alikuwa mtu mwenye elimu? Alikuwa mwenye busara? Mjanja? Mwenye furaha? Ni sababu zipi zimekufanya useme hivyo?

Ni mambo yapi muhimu tunayojifunza shuleni? Kwa nini ni muhimu?

Walitoa taarifa baadaye katika lugha yao ya mama, na walikuwa na mjadala wa kijumla juu ya maswali. Aliandika madondoo ubaoni, pia katika lugha ya mama.

## Shughuli ya 2: Watu wazima ninaoheshimu

Soma Nyenzo-rejea 3: Usalama na fikiria juu ya vipengele vya usomaji ambavyo vinaweza kusababisha matatizo kwa darasa lako.

Soma kara na wanafunzi wako, huku ukijadili maneno au dhana zisizo za kawaida.

Waulize juu ya mienendo ya watu wazima.

Je, wanatenda kama wale walioelezwa katika aya tatu za kwanza za kara, au kama wale walioelezwa katika aya ya nne?

Mienendo ya watu wazima inawasaidia kama vijana? Kama inawasaidia au haiwasaidii kwa nini?

Fanya majadiliano haya katika lugha ya nyumbani/lugha mama. Kama itahimiza mjadala mzito zaidi, waruhusu wanafunzi wafanye majadiliano katika vikundi vidogo na kisha watoe taarifa baada ya kama dakika 15.

Watake wachague mtu mzima wanayemfahamu na kumheshimu na kuandika maelezo ya mtu huyu, kwa kutumia lugha watakayoiteua. (Taz. **Nyenzo-rejea 4: Baba yangu ni nani** ?) Wanaweza kufanya kazi wawiliwawili au vikundi vya watu watatu ay wanne.

Kusanya kazi zao na uwape mrejesho. Wanaweza kuwa na hisia-bia zilizo nzito, kwa hiyo uwajibu kwa uungawana kuhusiana na maudhui, badala ya kulenga makosa ya kisarufi, n.k. (Taz. **Nyenzo-rejea muhimu: Kutathmini kujifunza**.)

# Somo la 3

Baada ya stadi na welewa kuimarishwa katika lugha inayofahamika vizuri, ni rahisi zaidi kuvihamishia kwenye lugh aya ziada. Wataalamu wengi huamini pia kuwa kama mtu ataliangalia somo kutumia mitazamo ya lugha mbili, stadi zao za kufikiri huwa bora. Ni muhimu uhakikishe wanafunzi wako wanajiona kuwa tajiri –badala ya fukara –kwa kuwa na lugha mbili au zaidi.

Wanafunzi wako wanapojadili mawazo katika lugha ya nyumbani au lugha ya mawasiliano mapana, inafaa kutafuta and kujifunza njia za kueleza mawazo haya katika lugha ya ziada. Unapaswa daima kufikiria njia kuwasaidia kufanikisha hili. Kisehemu hiki kinakupatia mawazo kadhaa.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

# Uchunguzi kifani ya 3: Kueleza mawazo kwa Kiingereza

Zawadi alihakikisha kuwa tini katika Kiswahili juu ya somo la mfalme namshona-viatu hazikufutwa ubaoni.

Katika somo lililofuata la darasa la 7, alianza kujadiliana na wanafunzi jinsi ya kujibu, kwa Kiingereza, maswali aliyokuwa ameuliza.

Walizungumzia baadhi ya maneno au mafungu muhimu waliyokuwa wametumia, mathalani tabia, maumbile. Ni mtu au sifa ya namna gani iliyorejelewa na kila neno? Walifahamu watu wenye sifa hizo?

Walijadili pia, kwa njia hiyo hiyo, baadhi ya maneno muhimu ya Kiingereza katika maswali: educated (mwenye elimu); wise (mwenye busara); clever (mjanja); happy (mwenye furaha); learned (msomi). Aliwakumbusha kuwa hakuna tafsiri sisisi wakati wote kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili au kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Hata hivyo walipata njia za kueleza mawazo yaliyokuwa ubaoni kwa Kiingereza. Katika kufanya hivyo, walijifunza miundo mipya ya lugha na msamiati mpya.

Zawadi aliyaandika haya ubaoni, na akawataka wafanye kazi katika vikundi na kuandika majibu ya maswali yake mawili kwa Kiingereza. Kikundi kingeweza kuandaa majibu pamoja, lakini kila mwanafunzi alipaswa kuandika majibu yake mwenyewe.

Zawadi aligundua kuwa mbinu ya kubadili msimbo iliwasaidia wanafunzi wake kukuza Kiingereza chao zaidi.

## Shughuli muhimu: Mtu mzima ambaye ningetaka niwe: Kauli ya Dira

Watake baadhi ya wanafunzi wako kuwasilisha maelezo ya watu wazima wanaowaheshimu darasani. Litake darasa kubainisha watu wazima wawili wanaowaheshimu katika jumuiya yao, na panga ili watu wazima hawa wazungumze na wanafunzi.

Amua kuhusu maswali ya kuuliza, k.m.:

Ni jambo lipi ni muhimu kabisa katika maisha?

Ni tajiriba zipi za maisha zilizokufanya uwe imara zaidi?

Nani aliyekuwa na athari kubwa kabisa kwako katika makuzi yako?

Kubalianeni nani atauliza maswali, na jinsi ya kurekodi yanayosemwa. Wanafunzi na watu wazima yumkini watatumia lugh aya nyumbani.

Baada ya ugeni, jadilianeni wanafunzi walichojifunza.

Waulize wanafunzi: Ni sifa na maadili yapi ungependa kuyajenga ili uwe nayo ukiwa mtu mzima?

Tafuta maneno ya lugha ya nyumbani na lugha ziada yanayotaja sifa na maadili haya, na uyaandike.

Watake waandike kauli za dira na/au malengo yao katika lugha ya ziada. (**Nyenzo-rejea 5: Kauli za dira na lengo** inatoa mifano.)

# Nyenzo-rejea ya 1: Shairi

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**

Wewe!

Kichwa chako ni kama ngoma tupu.

Wewe!

Macho yako ni kama mabonge ya moto.

Wewe!

Masikio yako ni kama pepeo za kuchochea moto.

Wewe!

Tundu la pua yako ni kama shimo la panya.

Wewe!

Mdomo wako ni kama bonge la tope.

Wewe!

Mikono yako ni kama mikwiro.

Wewe!

Tumbo lako ni kama chungu cha maji machafu.

Wewe!

Miguu yako ni kama nguzo za miti.

Wewe!

Mgongo wako ni kama kilele cha mlima.

Ibo

**Tini za Mwalimu**

Shairi hili limeundwa kwa mfuatano wa tashibiha. (Katika mfano huu, mfuatano wa tashibiha ni mfuatano wa matusi pia!). Tashibiha ni ulinganishi, unaotumika kusisitiza sifa fulani alizo nazo mtu au kitu kinachoelezwa. Unaposoma au unaposikia tahsibiha unapiga taswira ya ‘shimo la panya’ (kwa mfano), nah ii inakusaidia kujua jambo fulani kuhusu tundu la pua. Katika kuchambua tashibiha hii zaidi, unajiuliza: ‘tundu la panya li vipi? Ni kubwa kabisa (kulinganisha

na tundu la pua). Kuna giza ndani. Kumejaa viota vilivyokaa ovyoovyo na ni kuchafu. Hapo tutaweza kuona waziwazi zaidi mshairi anavyofikiri kuhusu pua ya mtu aliyelengwa.

Tashibiha ni ulinganishi wa wazi. Kwa maneno mengine, mwandishi au msemaji yuko wazi kuhusu ukweli kwamba huu ni ulinganishi. Baadhi ya maneno yanayoashiria tashibiha ni 'kama', mathalani: 'Tundu la pua yako ni kama shimo la panya' au ' Katika shimo la chini kwa chini, kulikuwa ni kweusi kama usiku'.

Kama mshairi angeandika 'Tundu la pua yako ni shimo la panya', hii ingekuwa na athari inayofanana nayo, lakini ulinganishi wa namna hii unaitwa sitiari. Hapa ulinganishi ni wa mdokezo. Hatuambiwi kuwa ulinganishi unafanyika. Tundu la pua linaelezwa kama kwamba ni tundu la panya.

*Chanzo cha awali: Machin, N. African Poetry for Schools: Book 1*

## Nyenzo-rejea 2: Mfano wa somo

**Taarifa ya usuli / maarifa ya somo kwa mwalimu**

**Mwalimu (M) anawafundisha wanafunzi (W) wa darasa la 7 Kiingereza (somo la kusoma) (Mwanafunzi = Mw)**

M: Ninalotaka kufanya sasa ni kwamba nitasoma kwanza, na nitawaomba mnifuate. Sawa?

W: Ndiyo.

M: *Hapo zamani za kale, Mfalme wa Misri alitaka kufahamu jinsi watu wake walivyoishi*. Misri iko wapi?

Mw: Kaskazini mwa Afrika.

M: Mnakubali? Mnakubali?

W: Ndiyo (Kwa pamoja).

M: Sawa*. Usiku mmoja alivaa kama mtu fukara na kuenda jijini.* Jiji ni nini?

**Mw: Mji…**

M: Aliwasikiliza watu wake wakilalamika. Watu wake walikuwa wakilalamika. Unapolalamika … ni kwamba huwa hujaridhika na hali ilivyo…

Mw: Kutoridhika…

M: Ndiyo, kutoridhika…niendelee na hadithi?

W: Ndiyo.

M: Basi watu walisema kuwa walikuwa masikini na chakula kilikuwa ghali…Walilalamika… Hakuna aliyecheka katika jiji hili. Hakuna aliyeimba nyimbo, na hakuna aliyekuwa na furaha. Kila mtu alikuwa na huzuni… Mfalme alipokuwa akirejea kwenye ikulu yake… Ikulu ni nini?

Mw: Ikulu ni mahali anapokaa mfalme.

**M: Vyema. Hadithi inaendelea…**

Alipita karibu na kijiduka. Akasikia mtu akiimba. Ndani ya kijiduka. Aliingia ndani. Kijana mwanamme alikuwa amekaa sakafuni, akishona viatu, huku akiimba.

Mshona-viatu alipoona kwamba kuna mgeni, alisimama na kumsalimu. Kisha akampa mfalme mkate na maji. Alimpa nini?

W: Mkate na maji.

M: Je, mshona-viatu alifahamu kuwa huyu alikuwa mfalme? Kwa hakika, hakufahamu. Kwa nini hakufahamu?

**Mw: Alivaa kama mtu fukara.**

M: Turudi kwenye hadithi. Hebu fikiria picha ya Madiba akiwa amevaa nguo kuukuu.… Unapata picha ya jambo ninalozungumzia?

W: Ndiyo.

M: Je, utamfahamu Madiba akitokea mlangoni hapo?

W: La.

M: La, hakuna anayeweza kumjua?

Mwalimu aliendelea kusoma hadithi na wanafunzi, akiwauliza maswali kuhusu hadithi hiyo. Maswali mengi yalikuwa yanafanana na hayo ya juu. Wanafunzi waliyajibu kwa ufupi, kwa Kiingereza. Kisha somo liliendelea kama lilivyoelezwa katika **Uchunguzi-kifani 2**.

*Imetoholewa kutoka: Umthamo 3, Mradi wa Elimu-Masafa wa Chuo Kikuu cha Fort Hare*

# Nyenzo-rejea 3: Usalama

**Nyenzo za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**

**Kaka yangu**

Kaka yangu ni Ipyana Mwakipesile. Ana umri wa miaka 18, na ni kama baba kwangu. Baba yangu alikufa zamani sana. Ana nafasi muhimu sana katika maish ayetu, ingawa bado ni kijana anayesoma kidato cha tano Shule ya Sekondari Azania. Ni muwajibikaji. Anatutunza. Anapika chakula na kusafisha nyumba. Anamlea mtoto mchanga kwa sababu mama yetu aliaga dunia miezi michache iliyopita. Kila adhuhuri hufunga lango la ua ili tuwe salama ndani. Anatusaidia kwa kila njia. Hatujihisi kuwa mama yetu pia hayupo nasi. Kaka yetu hutupatia upendo ambao tulizoea kuupata kutoka kwa wazazi wetu. Kila Jumamosi, anaoka keki, anafanya manunuzi kama mama alivyokuwa akifanya. Kaka yangu ni kama baba kwetu. Tunamwamini, tunampenda.

**Baba yangu**

Baba yangu alizaliwa na kukulia Mbeya; baadaye akahamia Dar. Alisomea Shule ya Sekondari ya Minaki; mama yake alikufa baada yamiaka miwili. Baba yake alimwacha na wadogo zake wawili wa kike. Aliishi na babu na bibi, kisha akaishi na shangazi yake, kabla kuhamishiwa kwenye kituo cha watoto yatima.

Wakati akiwa katika kituo cha watoto yatima, alikabiliwa na shida nyingi na alijifunza mengi. Alipambana na watu wajeuri na mara nyingi ilimpasa kuwalinda dada zake. Ingawa alionekana kuwa na muda mgumu, alithamini yote aliyopata kituoni. Jambo gumu kuliko yote lilikuwa kutokuwa na familia yake.

Kutokana na malezi katika kituo cha mayatima, alijifunza kujikimu.

Akiwa ngazi ya juu ya Shule ya Sekondari, alifanywa kuwa kiranja mkuu. Alikuwa maarufu pia, na alishiriki katika shughuli mbalimbali za kitamaduni na riadha pia.

Alipomaliza shule, alijiunga na jeshi la kujenga taifa, na kuona sehemu nyingi za Tanzania. Mara nyingi husimulia hadithi na matukio aliyoshiriki wakati akiwa jeshini. Tajiriba zake katika kituo cha mayatima zilimsaidia kuyamudu maisha ya jeshini, na alikuwa kwenye kundi la viongozi, na akawa mkufunzi. Baba yangu daima amekuwa na marafiki wema na maalumu, na daima amekuwa katika nafasi fulani ya uongozi. Baada ya kumaliza mafunzo na huduma ya kijeshi, alikwenda kuchukua mafunzo ya ualimu.

Akiwa chuoni, alikutana na msichana ambaye baadaye alikuwa mtu muhimu sana katika maisha yake. Baada ya kumaliza masomo, alimposa. Uhusiano huu haukuendelea. Ni wakati huu ambapo mama alikuja kufanya kazi shule moja na baba. Walishikana urafiki na baadaye akamwoa.

Mwaka 1990 nilizaliwa, na tangu hapo nimekuwa karibu naye sana.

Baba yangu amekuwa na nafasi muhimu katika maisha yangu, na ninataka siku moja kurithisha tuzo aliyonipa. Amekuwa mwalimu wangu, kocha wangu wa michezo ya riadha, mshauri wangu, na juu ya yote, rafiki yangu wa karibu.

*Imetoholewa kutoka ‘Children First’ Nov/Dec 2004/ Vol 8 No 58, ukurasa wa 5, 6, na 7*

# Nyenzo-rejea 4: Kauli za Dira na Malengo - mifano

**Taarifa ya usuli / maarifa ya somo kwa mwalimu**

Kauli ya dira kwa kawaida in fupi. Inalenga siku za usoni na unachotaka kuwa siku za usoni.

Kauli ya lengo kwa kawaida ni ndefu zaidi, na inatoa maelezo zaidi kuhusu mambo ya kufanya ili kutimiza dira.

Hapa kuna mifano miwili:

Kauli ya dira ya shule ya Mtakatifu Jude, Kaskazini mwa Tanzania

Kuwa asasi ya kisasa, ya mfano na yenye kujiendeleza yenyewe, inayoibua badiliko la kimwelekeo katika mfumo wa elimu wa Tanzania kwa kuwawezesha Watanzania kuendesha shule zenye mafanikio na maadili, na kwa hiyo kupunguza umaskini na kuvunja mzunguko wa utegemezi kwenye misaada ya nje.



*Chanzo cha awali: School of St. Jude, Website*

Kauli ya lengo la maisha la mtu asiyefahamika

Kuwa mtu ambaye watoto wangu watajivunia wanaposema, 'Huyu ni babangu".

Kuwa mtu ambaye watoto wangu watakuja kupata upendo, faraja na welewa.

Kuwa rafiki wanayemfahamu kwa kujali na daima kuwa tayari kusikiliza matatizo yao kwa makini.

Kuwa mtu asiye tayari kushinda kwa gharama ya kuumiza wengine kiroho.

Kuwa mtu anayeweza kusikia maumivu na asiyetaka kuumiza wengine.

*To be the person that speaks for the one that cannot, to listen for the one that cannot hear, see for the one without sight, and have the ability to say, 'You did that, not I.'*

Kuhakikisha vitendo vyangu vinalandana daima na maneno yangu kwa neema ya Mungu.

*Chanzo cha awali: Covey, S. et al. First Things First*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

# Sehemu ya 5: Kusaidia ujifunzaji wa lugha ya ziada

**Swali Lengwa muhimu:** Unawezaje kujenga mahusiano ya kusaidiana katika lugha ya ziada?

**Maneno muhimu:** mawasiliano ya mtu binafsi; marafiki wa kalamu; kupeana taarifa za ndani.

## Matokeo ya ujifunzaji

Mwishoni mwa sehemu hii, utakuwa umeweza:

- kuanza kukuza mahusiano baina ya wanafunzi ambayo yatasaidia ujifunzaji wao wa lugha ya ziada na kuwasaidia katika kutafakari juu ya ujifunzaji wao wenyewe;
- kutoa nafasi kwa wanafunzi kuwasiliana kwa kutumia maarifa ama wazungumzaji wa lugha ya ziada amabao kwao hiyo ni lugha mama kuweka nafasi kwa ajili ya mawasiliano na wanafunzi nje ya shule yako.

## Utangulizi

Wanafunzi wengi Afrika wana nafasi chache za kushirikiana na wazungumzaji wa lugha yao ya ziada ambao kwao hiyo ni lugha mama.

Mara nyingi welewa kwenye lugha unapatikana kwa njia za kusoma, kusikiliza redio na kutazama televisheni.

Hata hivyo, zipo njia zitakazowasaidia wanafunzi wako kuzungumza na kuandika kwa watu wenye ufasaha katika lugha ya ziada. Unaweza pia ukawasaidia wanafunzi wako kuwasiliana kwa kutumia lugha ya ziada na wanafunzi wa shule nyingine

Sehemu hii inaangalia njia zitazotumika kufanikisha jambo hili.

## Somo la 1

Kwa watu ambao hujifunza lugha katika mfumo wa kawaida wa darasani, misemo ambayo watu hutumia kila siku katika maingiliano yao mara nyingi huwa ni kitu cha mwisho kujifunza.

Zipo njia ambazo zinaweza zikatumika kuwasaidia wanafunzi wako kupata ustadi katika misemo na sentensi ambazo wanaweza kuzitumia pindi wanapokutana na watumiaji stadi wa lugha ya ziada. Kila seti ya misemo au sentensi zinatakiwa:

ziwe fupi na rahisi kujifunza;

ziseme kitu ambacho wanafunzi wanataka;

ziwe zinatumiwa na watu wengi;

ziwaruhusu wanafunzi kuanza majibizano na kujenga mahusiano;

ziwaruhusu wanafunzi kujifunza zaidi kuhusu lugha kutoka kwa watu wanaozungumza nao;

zisichochee majibu marefu toka kwa watu wengine.

## Uchunguzi kifani ya 1: Kujifunza kiZulu kupitia katika mahusiano

Liz Botha aliyepo Mashariki mwa London, Afrika Kusini, alijifunza kiZulu kama lugha ya ziada kupitia mradi wa lugha za ndani uitwao TALK. Kauli-mbiu ya mradi wa TALK ilikuwa, 'Jifunze kidogo, na utumie SANA!'

Alianza kwa kujifunza namna ya kusalimia kwa kiZulu, na kuwaeleza watu kuwa alikuwa anajifunza kiZulu. Alijifunza pia kuwataka wao wamsemeshe kwa kiZulu na kumsaidia katika zoezi lake la kujifunza lugha hiyo.

Aliwatafuta watu ambao anaweza kuzungumza nao kiZulu, na kubaini kuwa kuna idadi kubwa ya wazungumzaji wa kiZulu wanaofanya biashara ya kutembeza matunda na mbogamboga katika mtaa wa karibu na nyumbani kwake. Alifanya mazoezi ya sentensi zake kwao na kuanza kuwaelewa.

Alikuwa na rafiki aliyekuwa anamfundisha misemo mipya, na kujifunza kutoka kwake namna ya kuuliza bei ya kitu fulani na kukinunua. Hizi ndizo sentensi alizozitumia wakati uliofuata alipowaona rafiki zake wanaotembeza biashara.

Kadiri muda ulivyozidi kwenda, alijifunza kujieleza kwao kuhusu yeye mwenyewe na familia yake. Baadaye aliwasimulia hadithi fupi kuhusu nini kilichotokea kwake siku moja kabla, au mwisho wa wiki. Mmoja wa watembeza biashara aliyeitwa Jabu, akawa rafiki yake wa karibu sana na kumfundisha maneno na sentensi nyingi. Mwishowe akawa anawasaidia watu wengine kujifunza kiZulu katika mradi wa TALK.

## Shughuli ya 1: Kujenga mahusiano ya kujifunza lugha

Waulize wanafunzi wako ni wapi wamesikia lugha ya ziada ikizungumzwa. Ni watu gani pia wanaowafahamu kuwa wanaitumia vizuri? Ni nani wanaweza kuzungumza naye lugha ya ziada? Zingatia watu waliopo nje na ndani ya shule na pia watu ambao unaweza ukawaalika katika darasa lako. Fikiria ushirikiano na shule ya karibu kama unaweza kukuza mtagusano katika lugha ya ziada.

Sasa wanafunzi wako wanafahamu ni akina nani wanataka kuzungumza nao, pangilia mambo wanayotaka kusema nao.

Kwa utaratibu maalum, wasaidie kujifunza msamiati kama mradi wa muda mrefu. Weka uzito katika sauti na matamshi bayana.

Waache wafanye mazoezi wawiliwawili.

Mawazo juu ya vitu vya msingi vya kujifunza yanajumuisha:

salamu na kuagana;

kutaja na kuuliza majina na taarifa binafsi na za familia;

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

kueleza kuwa wao ni watu wanaojifunza lugha na kuwa wanahitaji msaada wa kujifunza;

kununua vitu;

kuzungumzia kuhusu hali ya hewa;

kuelezea mambo yalitokea jana;

kuomba radhi, kuomba kitu au jambo, kusifu, n.k

Wahimize wafanye mazoezi na watu waliowapendekeza (hapo juu).

Tenga muda fulani kila wiki ili kufuatilia maendeleo yao.

Je kuna mafanikio na matatizo gani wamekumbana nayo? Ni lugha ipi mpya wamejifunza?

Nini kingine walichojifunza?

## Somo la 2

Katika sehemu hii,tunapendekeza kuwa uwahamasishe wanafunzi waandike barua kwa kutumia lugha ya ziada. Hii inaweza kuwa na maana ya kuweka mhusiano ya mbali na wazungumzaji wa lugha ya ziada, ama wanaweza kuwaandikia rafiki zao wa karibu.

Unaweza kuanzisha utaratibu wa rafiki wa kalamu na darasa lingine (tazama **Nyenzo-rejea 1: Marafiki wa kalamu** ). Hili linaweza kuwa darasa katika nchi yako au nchi nyingine.

Kama wanafunzi watakuwa waandishi na wasomaji wanaojiamini wakingali shule ya msingi, kuna uwezekano mkubwa kuwa waandishi wa barua wenye mafanikio hapo baadaye katika maisha yao. Kadiri wanavyoandika barua binafsi kwa marafiki zao, unaweza pia ukafundisha mtindo mwingine wa uandishi wa barua. Hili litawaandaa kwa ajili ya mahitaji ya baadaye, kama vile, kuomba kazi, barua kwenda magazetini, barua za pongezi au rambirambi.

## Uchunguzi kifani ya 2: Kuandika kwa ajili ya kufariji au kulalamika

Wanafunzi wa darasa la 5 la Bibi Linda Shigeka walikuwa katika mfadhaiko na hawakuweza kushiriki vema katika kazi zao za shule. Mwanafunzi mwenzao mmoja, Mandisa, alifariki katika ajali ya basi. Walimkumbuka sana rafiki yao.Walikuwa pia na hasira kwa sababu walisikia kuwa basi halikuwa na breki.

Bibi Shigeka aliwahimiza wanafunzi kueleza namna wanavyojisikia. Alibaini kuwa wanataka kufanya jambo fulani, akawauliza kama wanataka kuiandikia familia ya Mandisa barua. Akapendekeza kuwa waandike barua mbili, moja kwa Kiswahili kwa ajili ya wazazi na wazee (babu na bibi) na nyingine kwa Kiingereza kwa ajili ya kaka na dada ambao wamekulia London wakati wazazi wao walipokuwa uhamishoni. Wanafunzi walisema kuwa wanataka kuieleza familia ya Mandisa kuwa wapo pamoja nao na pia wanataka kuwaeleza mambo mazuri kuhusu Mandisa.

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Bibi Shigeka aliwasaidia kwa kuwapa dondoo za maandishi yao. Wanafunzi waliandika barua binafsi kwa Kiswahili. Katika somo lililofuata, Bibi Shigeka aliwasaidia kuandika barua moja kwa Kiingereza kwa ajili ya darasa zima na kisha kila mwanafunzi aliweka saini yake

Kwa msaada wa Bibi Shigeka, waliandika pia barua kwa Kiingereza kwenda kwenye kampuni ya basi wakiomba kuwa mabasi yakaguliwe vema kuhakikisha kuwa ni salama na yanafaa kutembea barabarani.

Wanafunzi walipata majibu ya barua zote mbili walizoandika. Bibi Shigeka akazibandika barua hizi kwenye ubao wa matangazo uliopo darasani.

Bibi Shigeka alibaini ni kwa namna gani suala hili limewahamasisha wanafunzi na kuwapa stadi muhimu ya kijamii. Imewasaidia pia kuona lengo la kujifunza lugha ya ziada.

## Shughuli ya 2: Barua ya kwenda kwa rafiki au rafiki wa kalamu

Soma **Nyenzo-rejea 1 kwanza**, na anzisha uwenza na shule jirani.

Mpe kila mwanafunzi darasani mwako jina la rafiki wa kalamu ambaye wanaweza kuanzisha uhusiano. (Kama haitawezekana, jaribu kumfanya kila mwanafunzi kumtambulisha mwanafunzi wa darasa lingine au jamaa au rafiki wa mbali na nyumbani ambao wangependa kuandikiana barua). Kama una shule nyenza tayari au ndiyo unaiasisi ( **angalia Nyenzo-rejea 1 kwa namna ya kulitekeleza hili** ), dumisha mawasiliano ya karibu na mwalimu mwenza wako, kujadili matatizo nyeti na kuyatafutia suluhisho kwa pamoja.

Jadili na darasa lako juu ya vitu ambavyo wangependa kuzungumzia katika barua yao ya kwanza. Wakati huo huo wanaweza kubadilishana habari juu ya maisha yao, familia zao, rafiki zao, mambo wayapendayo na matarajio yao.

Ridhia muundo wa barua (angalia **Nyenzo-rejea 2: Kuandika barua** ), na waache waanze kuandika. Zungukazunguka ukiwasaidia maneno na virai wanayohitaji.

Waache wapitie na kuhariri barua zao katika jozi. (angalia **Nyenzo-rejea 3: Kupima ubora wa barua za marafiki wa kalamu** ). Zichukue barua, na toa mrejesho saidizi na wenye kujenga.

Waache wanafunzi waandike toleo la mwisho la barua yao, andika anuani juu ya bahasha na uitume (kwa njia ya posta).

Kwa wanafunzi wadogo, hii yaweza kuwa shughuli ya darasa zima na andika wanayotaka kusema. Wanaweza kuwaandikia darasa jingine hapo shuleni.

Je, unawezaje kusaidia maendeleo ya huu uhusiano wa kuandikiana barua?

Je, unawezaje kusaidia pale unapohitajika, wakati wa kutoa nafasi kwa mahusiano kukua?

## Somo la 3

Kuzalisha vitabu ambavyo wanafunzi wameandika na kuvitengeneza, sio tu kunawaongezea kujisifu, lakini pia kunakupatia **Nyenzo-rejea nzuri darasani.**

Sehemu hii hujengwa na mawazo ya Kitabu Kikubwa katika Moduli 1, Sehemu 5. Inapendekeza kuwa uwape moyo wanafunzi wako kuyaleta maandishi na michoro yao katika hatua ya mwisho kwa kutengeneza kitabu. Hii wanaweza kushirikiana darasani, au na watu, kikundi au shule nyingine.

Unatakiwa ufikirie ni kwa jinsi gani unaweza kupanga na kuendesha zoezi kama hili. Utatakiwa kufikirikiria juu ya aina ya kitabu cha kutengeneza (mfano kitabu cha kukunja), vielelezo na mpangilio wa kitabu, na aina ya kitabu (k.m kitabu cha nyimbo, kitabu cha hadithi au kitabu cha hadithi isiyo ya kubuni).

Utapaswa kufikiria juu ya nyeno rejea zitakiwazo na wapi pa kuzipata. Uanweza kuwashirikisha wanafunzi katika kukusanya baadhi yake kabla hujaanza kabisa kazi darasani. Aina hii ya upangaji na uandalizi ni muhimu kama darasa lako ni kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi kujifunza (angalia **Nyenzo-rejea muhimu: Kuwa mwalimu mwerevu katika mazingira (hali) yenye changamoto** .)

## Uchunguzi kifani ya 3: Kutengeneza kitabu cha darasa

Bibi Ndekule, ambaye anafundisha wanafunzi 44 wa darasa la 5 huko Zanzibar, alitaka kuwatia moyo kama waandishi na wasomaji na aliamua kutengeneza nao kitabu kwa kutumia lugha yao ya ziada ya Kiingereza.

Aliwambia kuwa alitamani kuanzisha hifadhi ya vitabu kwa ajili ya darasa, na ingestawi tu kama wangezalisha baadhi ya vitabu vyao wenyewe. Walijadili aina gani ya vitabu walipenda kusoma na aliviorodhesha ubaoni. Orodha ilijumuisha, riwaya, mashairi na vitabu juu ya michezo na mavazi. Halafu aliwambia wanafunzi waunde makundi madogo yasiyozidi watu sita wenye kupenda aina fulani ya kitabu.

Bibi Ndekule ailjadiliana na kila kundi juu ya aina ya kitabu watakachoandika. Kundi moja liliamua kujigawa katika makundi mawili ya watu watatu kutengeneza vitabu viwili vya michezo, kimoja cha mpira wa miguu na kingine cha riaadha. Kundi jingine lilitaka kuandika kitabu cha hadithi juu ya hadthi za mapokeo. Bibi Ndekule aliyapa makundi muda kupanga dondoo zao kabla hajawaambia wajadiliane na wengine. Darasa lilitoa mwitikio kwa kila kundi. Katika wiki iliyofuata, aliwapa muda wa darasani na wa kazi za nyumbani kuadika kazi zao.

Walipomaliza rasimu zao za mwanzo, Bibi Ndekule alizipitia na kutoa mwitikio juu ya njia za kuboresha vitabu vyao. Rasimu zao za mwisho zilikuwa ziameisha katika wiki iliyofuata na ziliwekwa kwenye maonesho kwa ajli ya darasa zima kuvisoma.

## Shughuli muhimu: Kutengeneza kitabu cha ubia

Pendekeza kwa darasa lako watengeneze kitabu kwa ajili ya shule nyenza (au kwa lengo jingine) kikiwa na nyimbo, mapishi na habari nyingine za nyumbani. Kama una kitabu cha mapishi, waoneshe. Baadhi ya vitabu vya mapishi huwa na picha , habari na hadithi juu ya mahali na watu wanaohusiana na mapishi.

Amua ni nyimbo zipi au mapishi yapi yatajumuishwa na jinsi yatakavyo wasilishwa. (angalia **Sehemu 1**).

Amua kwa pamoja ni mambo gani zaidi yatakuwemo ndani ya kitabu. Angalia **Nyenzo-rejea 4: Nyimbo na hadithi kuhusu michakato** –nyimbo hizo hizo na hadithi zinaweza kujumuishwa. Mashairi na maelezo kutoka kwenye shughuli zilizopo katika **Sehemu 2 na 4 zinaweza kuhusishwa.** Fikiria kuhusu vielelezo(michoro), picha, maelekezo ya michezo ya asili, riwaya au mashairi.

Panga na wanafunzi wako ambao watafanya kila sehemu ya kazi, nani atahariri kazi na lini kila sehemu ya kazi itakuwa iimekamilika. (Moduli 1, Sehemu 5, **Nyenzo-rejea 1**: Jinsi hadithi zinavyotengenezwa kitabu. Huonesha jinsi kitabu kinavyoandaliwa na watu tofauti.)

Andaa mpango. Kama inawezekana, toa nakala ya kitabu ili kimoja ubaki nacho na kingine ukipeleke katika shule nyenza. Waombe pia shule nyenza kama wanaweza kukutumia kitabu walichotengeneza.

Pale nyenzo zinapokuwa chache, karatasi zilizotumika, kalenda za zamani, magazeti ni vifaa ambavyo unaweza kuvikusanya kirahisi kutengenezea kitabu. Kwa mawazo zaidi, angalia Rejea muhimu: Kuwa mwalimu mwerevu katika mazingira yenye changamoto.

## Nyenzo-rejea ya 1: Marafiki wa kalamu

**Taarifa ya usuli / maarifa ya somo kwa mwalimu Wewe!**

Kama unapenda kuwa na mawasiliano na shule katika nchi yako au nchi nyingine ambayo pia hutumia vifaa vya TESSA , tafadhali wasiliana na Jane Devereux wa Open University, kwa kutumia j.b.devereux@open.ac.uk au tumia anuani ifuatayo: The Open University, P O Box 77, Walton Hall, Milton Keynes MK7 6BT, UK.

Pia unaweza kuasisi uhusiano kati ya darasa lako na darasa la rika sawa kutoka shule nyingine na panga kila mmoja wa wanafunzi wako kuwa na rafiki wa kalamu. Hii itawapa wanafunzi wako faida ya kuwa na rafiki wa kumwandikia na kupokea majibu kutoka kwake, juu ya maswala yanayowapendeza, kutumia lugha ya ziada au lugha ya biashara/maasiliano. Watapata mazoezi katika kusoma na kuandika kwa lengo maalum, na kujifunza zaidi juu ya watu wengine, familia zao, shule, nchi na mtindo wa maisha.

Kabla hujawaingiza wanafunzi wanafunzi wako kwenye mpango/mradi, hakikisha umeshachanganua vizuri mambo kama ville mgawo na malipo ya bahasha na stampu. Unaweza ukaweka barua zote kwenye bahasha kubwa na kuituma kwa mwalimu.

# Nyenzo-rejea 2: Uandishi wa barua

### Taarifa ya usuli / maarifa ya somo kwa mwalimu

Wanafunzi wana mwelekeo wa kufurahia zaidi uandishi wa barua (katika ama lugha ya mama au lugha ya ziada) kama wanahisi kuna sababu halisi ya kuandika na kwamba watu wengine watavutiwa kuzisoma. Kutakuwa na hali kadhaa ambapo utumizi wa lugha ya ziada utakuwa ni mwafaka zaidi. Kwa kila hali, unapaswa kujadili lugha ipi ya kutumia.

Unaweza kupanga na walimu katika shule nyingine ili wanafunzi wa shule moja wawaandikie barua wanafunzi wa shule nyingine (taz. Nyenzo- rejea 1). Unaweza pia kuwasaidia wanafunzi kuandika barua kwenye kampuni kuomba mchango wa fedha, vitu au huduma kwa ajili ya shule. Kama umewapeleka kwenye ziara katika jumuiya yako kwa mfano kliniki, mradi wa kilimo au kiwanda, unaweza kuwasaidia kuandika barua ya shukurani. Kunaweza kuwepo matukio ya furaha au huzuni ambapo ingekuwa vyema kwao kumwandikia mtu barua ya pongezi/hongera au rambirambi.

Kwa aina yoyote ya barua utakayotaka kushughulikia, kwanza jadiliana na wanafunzi kwa nini watu huandika barua na mambo wanayotaka kusema katika aina hiyo ya barua. Andika mawazo yao ubaoni, na uwasaidie kuyapanga katika aya. Ukitaka unaweza kutumia vidokezo vilivyo hapa chini.

Pindi wanafunzi wamalizapo barua zao, zitume kwa mtu au shirika lililolengwa. Unaweza kukusanya barua zote na kuziweka kwenye bahasha moja kubwa ikiwa na anwani husika. Kama wewe na wanafunzi mna bahati, mtapata jibu!

**Vidokezo vya barua kwa ‘rafiki wa kalamu’ katika shule nyingine (au nchi nyingine).**

Mpendwa ……………….

Nimefurahi sana kwamba tutakuwa marafiki wa kalamu. Katika barua hii lengo langu ni kujitambulisha kwako.

Jina langu kamili ni ………………………………. Nina umri wa miaka …... Kwa kuwa sina picha ya kukutumia sasa hivi, nitaeleza ninavyoonekana. [ikifuatwa na sentensi zenye maelezo haya]

Ningependa kukuambia juu ya familia yangu [ikifuatwa na sentensi kuhusu familia]

Tunaishi ………………… [ikifuatwa na sentensi juu ya mahali ]

Haya ni baadhi ya mambo ninayopenda. Chakula ninachokipenda ni….muziki ninaoupenda ni ……………. Somo ninalolipenda zaidi shuleni ni ……..

Wakati wa wikendi mimi hupendelea………

Nitakapomaliza shule ninatarajia ……………….

Ninatarajia kupata jibu kutoka kwako hivi karibuni…………..

Ninakutakia kila la heri,

Wako,

[Jina na saini]

**Vidokezo vya barua ya shukurani baada ya ziara ya shule**

Mpendwa ……………….

Kwa hakika nilifurahia ziara yetu hapo……………….

Kilichonivutia kuliko vyote kilikuwa ……………………………

Nilifikiri hili lilikuwa na mvuto kwangu kuliko vitu vingine kwa sababu……………………

Kama shule yetu itapata nafasi ya kufanya ziara nyingine, ningependa ……………….

Ninakushukuru sana kwa ……………………………………………

Wako mwaminifu,

[Jina na saini]

**Vidokezo vya barua kwa kampuni kuomba mchango**

Bw./Bi ……… [jina la mtu]

Ninaandika barua kuomba msaada wako. Shule yetu inahitaji …………………

Tunahitaji hili kwa sababu ……………………………………………………

Ninakuandikia kwa sababu ………………… [sababu kwa nini kampuni hii inaweza kusaidia]. Ninatumaini utaweza kutusaidia. Wako mwaminifu

[Jina na saini]

## Nyenzo-rejea 3: Kutathmini barua za urafiki wa kalamu

**Kwa matumizi ya mwanafunzi**

| |
|---|
| Je, barua inaunda picha hai na ya kuvutia ya mwandishi? Taarifa gani zinatakiwa kuongezwa ili kuifanya ivutie zaidi? |
| Je, maelezo yametolewa kwa ufasaha? Je, barua inasomeka kwa urahisi? |
| Je, mada tofauti zimeshughulikiwa katika aya tofauti? |

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

| |
|---|
| Je, barua iko katika njeo sahihi? (Maelezo yanaweza kuwa katika njeo iliyopo.) Je, kila kitenzi kiko katika njeo iliyopo au, kama si hivyo, kuna sababu ya msingi ya kutumia njeo tofauti? (Unaweza kuamua kuhusu aina za miundo unayotaka kukazia katika shughuli hii.) |
| Je, barua inaonekana ni nzuri? (Safi, imepangiliwa vizuri.) |

## Nyenzo-rejea 4: Nyimbo na hadithi kuhusu michakato

**Nyenzo-rejea za mwalimu kwa ajili ya kupanga na kutumia na wanafunzi**

Hapa kuna wimbo wa kijadi wa Kiswahili unaofafanua michakato mbalimbali ambamo nafaka hupitia kabla ya kuliwa. Uliambatishwa katika kijitabu cha ‘Michakato na Uchakataji’. Wimbo huo unaweza kuingizwa kwenye kitabu cha mapishi. Hadithi zinafuatia, ambazo nazo zinatoka kwenye chanzo hicho hicho, zinaweza pia kujumuishwa kwenye kitabu hicho cha mapishi au cha mchakato.

Ninakipenda chakula

Chakula cha asubuhi,

Makande, uji na viazi

**Ugunduzi wa mtama**

Hapo zamani za kale palikuwa na mwanaume aliyekuwa na wake wawili. (Katika baadhi ya sehemu za Afrika, wanasema, ‘Mke mmoja – tatizo moja. Wake kumi na mbili – matatizo kumi na mbili!’) Mke mkubwa hakuweza kuwa na watoto, kwa hiyo alipogundua kuwa mke mdogo alikuwa mjamzito, aliona wivu sana. Lakini hakuwa na la kufanya.

Mume na mke mdogo wakapendana sana. Na hili likamfanya mke mkubwa aone wivu zaidi. Kwa hiyo mke mkubwa aliamua kusubiri mpaka baada ya mke mdogo kujifungua.

Lakini mtoto alipozaliwa, alikuwa ni mtoto wa kiume. Kwa mujibu wa mila, mke mkubwa alitakiwa kuwatunza mtoto mchanga na amariya (mke mdogo) kwa miezi michache. Mke mkubwa aliamua kwenda msituni kutafuta kitu cha kumpikia mke mdogo ambacho kingemdhuru. Alitarajia kwamba mke mdogo angekufa, na hapo angeweza kumlea mtoto mchanga kama mtoto wake mwenyewe.

Kule msituni, mke mkubwa aliona mmea ambao ulikuwa na vichwa vyenye punje zikuazo juu yake. Hajawahi kuona kitu kama hiki hapo awali. ‘Hii itamfanya alale, usingizi mzito hasa, kiasi kwamba hataweza kuamka siku itakayofuata. Kisha nitaandaa mazishi mazuri sana.’

Creative Commons Attribution-Share Alike - www.tessafrica.net

Alipika mtama na kumlisha amariya. Alipata mshangao, amariya hakulala usingizi mzito wala kufa. Badala yake, alinenepa na kuonekana mwenye afya na kupendeza kila uchao. Vilevile, mtoto mchanga alinawiri.

Mke mkubwa alipoona matokeo ya kitu alichokuwa anakipika na kumlisha mke mdogo, aliamua kukionja yeye mwenyewe. Aliipenda ladha yake, na aliendelea kukipika na kukila kitu hicho kipya. Yeye pia, alianza kunenepa na kuwa na afya zaidi.

Sawa, mume alishindwa kujizuia kuona kuwa wake zake wawili walipendeza sana, na mtoto alikuwa na afya. Alitaka kukionja, kwa vyovyote kilivyo kitu hicho, ambacho wakeze walikuwa wanakula. Kwa hiyo, wote wakawa wanene na wenye afya.

Na, kwa hakika, katika kijiji, neno husambaa kwa haraka sana, Kabla muda haujapita, wanakijiji wote waliobaki walitaka kujua kitu ambacho familia hii ilikuwa inakula. Na ndivyo ikawa kwamba mtama ukagunduliwa.

**Ugunduzi wa jibini**

Hapo kale palikuwa na wanandoa vijana waliokuwa na kundi kubwa la ng’ombe na kundi kubwa la kondoo. Mume aliilisha familia yake kwa kukamua ng’ombe. Nyakati hizo, walihifadhi maziwa kwenye vibuyu.

Wanandoa hao wakati mwingine waligombana; na mke alionekana akikimbilia kwa mama yake, huku mumewe akikimbia kumfuata, kwa kufoka na kupiga ngumi hewani.

Siku moja wakati walipokuwa wakigombana, mume alikuwa ameshika kimojawapo kati ya vibuyu vyenye maziwa mazito yenye malai. Wakati mke wake alipokimbia, mume alimkimbiza, kama kawaida. Lakini safari hii alisahau kuweka chini kibuyu cha maziwa mazito yenye malai. Kadri alivyokuwa akikimbia na kumfokea mkewe, alikunja ngumi yake huku akiwa amekishika kibuyu hewani. Kwa hakika, mume alikimbia upesi sana kiasi kwamba kibuyu cha maziwa kilitikisika kwa nguvu hasa.

Aliposhindwa kumkamata mkewe, hali ya kuwa ameishiwa na pumzi, mwanaume alikaa chini. Alikuwa anasikia joto na kiu baada ya kumkimbiza mke wake na kumfokea. Kwa hiyo aliweka kibuyu mdomoni ili anywe kinywaji cha maziwa mazito yenye malai. Lakini hayakuwa maziwa yaliyomwagika toka kwenye kibuyu. Yalikuwa vitu kama maji! Haya yote yalikuwa ni makosa ya mke wake!

Mume alipigwa na butwaa. Alikaa chini na kuangalia ndani ya kibuyu. Kitu gani kimetokea kwenye maziwa mazito yenye malai? Kwa nini yamegeuka kuwa kitu cha majimaji? Akajaribu kuweka funda lingine mdomoni. Ikawa hivyo hivyo. Akaweka mkono wake ndani ya kibuyu na kugundua kwamba kulikuwa na bonge fulani. Nina hakika unaweza kukisia kitu alichokiona. Ndiyo, ni sawa, ilikuwa ni bonge la jibini laini yenye mafuta. Wakati mume aliporamba vidole vyake, aliona kwamba bonge la kitu hicho lilikuwa na ladha nzuri. Ilikuwa kama mafuta.

Alirudi nyumbani kwake haraka, akatafuta mkate wa mahindi, na kuupaka kiasi cha mafuta toka kwenye kibuyu kwenda kwenye kibonge cha mkate. Mkate ulikuwa na ladha nzuri zaidi kuliko kawaida. Hasira yake ikayeyuka. Wakati mkewe aliporudi baada ya kitambo kidogo, alimwonesha kilichotokea, na alimpa kiasi cha mafuta ili ajaribu kukionja kwenye mkate.

Kwa muda mrefu baada ya hapo, kila jibini inapokuwa imemalizika, mume alianzisha ugomvi na mkewe ili aweze kuchukua kibuyu cha maziwa mazito yenye malai anapomkimbiza. Alielewa kwamba kwa namna hiyo, maziwa mazito yenye malai yatatengeneza jibini.

Siku moja wakati jibini kidogo sana ilikuwa imebakia, mke alichukua kibuyu cha maziwa mazito yenye malai na kukitikisa kwa nguvu kadri alivyoweza. Alikitikisa, na kukitikisa. Alipoacha kukitikisa zaidi, alikiweka chini. Unaweza kukisia alichokiona ndani ya kibuyu, huwezi? Aliona jibini, na kiasi cha majimaji ya maziwa.

Jioni hiyo mume aliporudi nyumbani, mkewe alimgeukia na kusema, ‘Labda kama tutatingisha kibuyu kilichojaa maziwa mazito yenye malai kwa nguvu, tutatengeneza jibini nyingi zaidi. Hivyo hatutalazimika kugombana tena.’

Na hivyo ndivyo ilivyokuwa, kwamba waliishi kwa raha mustarehe, na kuwa familia yenye afya kwa kupiga maziwa mazito yenye malai kutoka kwenye mifugo yao, na jibini, ambayo wamejifunza kuitengeneza.

*Imetoholewa kutoka: Ngtetu, C. & Lehlakane, N., Inqolowa, The Discovery of Amazimba and The Discovery of Butter, Umthamo 3, University of Fort Hare*

Kurudi Kujua kusoma na kuandika ukurasa

TESSA

Teacher Education in Sub-Saharan Africa

www.tessafrica.net